Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 20 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne. S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 268

**Fedha za Ukarabati wa Barabara – Manispaa ya Kinondoni**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali hutenga wastani wa shilingi ngapi kwa ajili ya ukarabati ndani ya Manispaa ya Kinondoni, na ni utaratibu gani unatumika kufuatilia toka kwa Wahandisi wa Manispaa kuhakikisha kwamba barabara zote za Manispaa zinapatikana nyaraka zote?

(b) Je, kuna utaratibu gani wowote wa kuthaminisha gharama zilizotumika na uhalisi wa kila kilichotengewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee Mbunge wa Kawe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni hupata fedha kwa ajili ya miradi ya barabara, Madaraja na Makalvati kutoka katika Mfuko wa Barabara, ruzuku za fedha za maendeleo ya Serikali za mitaa na vyanzo vya mapato ndani ya Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Manispaa kupitia vyanzo hivyo ilipata jumla ya shilingi bilioni 4.3. Fedha hizi zilitumika kufanya matengenezo ya barabara za lami kilomita 1.65, kufanya matengenezo ya changarawe kilomita 48, kuziba viraka katika barabara za udongo kilomita 23.5 matengenezo ya madaraja ya madaraja 11, kujenga kalvati 1 na ununuzi wa *Motor Grader 1*.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) hutuma utaratiu wa kutumia Wahandisi na Wataalam wengine kutoka ofisi zao kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji au kuhakiki kazi hizo *(Physical and Financial Audit).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepanga kutumia shilingi bilioni 3.2 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Manispaa shilingi milioni 350 kama Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa *(LGCDG)* kwa ajili ya kujenga daraja la Makongo maeneo ya Goba na shilingi bilioni 5.6 kutoka vyanzo vya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya kujenga barabara kiwango cha lami, changarawe na madaraja.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Makaguzi wa ndani, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*, Kamati ya Kudumu ya Bunge Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na kitengo cha ufuatiliaji na tathimini *(M&E)* katika Halmashauri, Mkoa na OWM-TAMISEMI hufanya ukaguzi wa Miradi inayotekelezwa ili kuona kama fedha hizo zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha katika miradi hiyo *(Value for Money).*

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nina swali moja tu la nyongeza. Kufuatia mvua kubwa sana zilizonyesha Mkoa wa Dar es Salaam, karibu asilimia 80 za Barabara za Manispaa ya Kinondoni ni mbovu sana; na kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam na husasan Manispaa ya Kinondoni ndiyo inatoa mchango mkubwa sana katika Road Toll, karibia asilimia 80.

Je, Serikali haioni sasa Dar es Salaam inatakiwa iangaliwe kwa jicho la pekee linapokuja suala la mgao wa fedha za barabara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kitu ambacho Mheshimiwa Halima Mdee anakisema hapa ni *valued. Politics* na *economics* za nchi hii zinakuwa *determined* na Dar es Salaam kwa sababu ya mambo ambayo yanafanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Tukisema tunakuja hapa kuzungumza habari za barabara kutengeneza Mji wa Dar es Salaam kupitia Bajeti tunayozungumza hapa tunaota ndoto na ndiyo maana

Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja hapa akasema tutahitaji kuwa na utaratibu maalum. Kwa hiyo halima anachosema pale wala siwezi kumpinga. Ukichukua Bajeti yetu na mapato yanayotoka Dar es Salaam, bandari, viwanda vikubwa viko Dar es Salaam kwa hiyo mapato yanayotoka pale ni makubwa.

Lakini nchi yetu kwa sababu inajali watu inatenga hela kufuatana na mahitaji katika nchi nzima bila kujali fedha imetoka, Kilimanjaro wanazalisha kahawa, Mtwara wanazalisha, Mwanza wanazalisha, ukisema unaangalia pale itakuwa ni matatizo. Lakini nikiri mbele yako kwamba iko haja kuliangalia suala hili na tulishasema kwamba kuna haja ya kuliangalia jambo hilo kwa sura hiyo anayozungumza pale.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya Mamlaka ambazo zinawajibika kuweza kuthaminisha gharama zilizotumika katika utengenezaji wa miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo barabara ameweza kutaja Kamati kwa mfano *LAAC* ambayo ni Kamati ya Bunge. *(Makofi)*

Pia Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri na wengineo ila Waheshimiwa Wabunge hatukutajwa ili hali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63 kazi Kubwa ya Bunge na Wabunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Nini kauli ya Serikali katika suala zima la Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yao kwenye suala zima la kuthaminisha gharama zilizotumika katika ujenzi au utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Serikali.

**SPIKA:** Haya, lakini kwa kweli hili ni swali jingine tena la mbali, Mheshimiwa Naibu Waziri jibu tu kama unaweza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri, Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango Mheshimiwa Moses Machali anaingia kama Mbunge, Kamati ile kazi yake kubwa ni kufanya ukaguzi mule ndani, la kwanza hilo. La pili, pale ndani kuna kitengo cha ukaguzi wa ndani ambacho kitengo kile kikiungana na Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na wale wengine kwa wale Kamati ndiyo wanakwenda kukagua ile miradi. Mheshimiwa Mbunge atumie nafasi yake kama Mbunge wa Kasulu anapoingia katika Halmashauri adai mapato yanayotokana na Halmashauri na mapato yanayoletwa na Serikali pale.

Kwa hiyo, Mkaguzi Mkuu wa mambo haya wewe unaanza kuzi-*track* kutoka hapa unazifahamu mpaka kwenye Halmashauri ile. Ninaomba Wabunge wote tuchukue nafasi zetu, Mwenyekiti wa pesa zile za Mfuko wa kuchochea maendeleo ni Mbunge. Sasa kama Mbunge naye atakuwa anauliza hizi hela zimetumikaje itakuwa ni *problem.* Namwomba Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba Kamati ile ya fedha na uchumi Wabunge wote wanaingia katika Kamati hiyo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Uzoefu unaonyesha kwamba *tender* zinazotoka kwenye zile Halmashauri kwa mfano za kujenga

barabara, barabara inaanza kujengwa inafika wakati haijakamilika fedha zinaisha mvua inakuja inanyesha moramu iliyokuwa imewekwa inaondoka, baadaye yule mkandarasi anakuja anaanza upya pesa zinavyokuja zinapatikana kwa *phases*, uzoefu unaonyesha inakuwa *expensive* tena maradufu kwenye Halmashauri kwa sababu kazi kama vile inaanza upya katika *tender* iliyotolewa na kazi ilikwishaanza na ni kwa sababu ya ukosefu wa pesa na ku-*delay* kwenye *payment*.

Je, Serikali inatoa tamko gani au Serikali inatoa msimamo gani kuhusu kazi kama hizi kwamba kuanzia sasa *tender* kwenye Halmashauri za ujenzi wa barabara zitolewe baada ya fedha zote kupatikana ili kazi zisirudiwe na hatimaye kuwa gharama kubwa kwa Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hebu tusikilizane vizuri jamani hapa. Tunachosema hapa hela zote zinazokwenda katika miradi mbalimbali zinakuwa managed na Baraza la Madiwani ambapo na Wabunge wanakuwepo mule ndani. Pale ndani kuna kitu kinaitwa Bodi ya Manunuzi na Bodi ile Mwenyekiti wake anakuwa ameteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji, Madiwani wanakwenda kwenye full council ndipo anapopitisha lile jambo pale. Barabara yoyote inayojengwa katika Halmashauri inatengewa na kiasi cha pesa inajulikana kwamba mradi huu pesa zilizotengwa na mradi huu ni kiasi hiki. Anazungumza barabara za Moramu, ni kweli kama itatengenezwa ikafika mahali haikwisha mvuo ikija ikisomba pale habari imekwisha. Tunatakiwa tutafute thamani halisi ya pesa iliyotumika kwa ajili ya kufanya kazi ile pale.

Hii ni pamoja na Mainjinia na wale wote waliokuwepo wasimamie pamoja na Mwenyekiti pamoja na Madiwani walioko pale. Analozungumza hapa tumeshaliona, na ndiyo maana sasa hivi kuna utafiti katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tukishirikiana na wenzetu ujenzi kuona jinsi ambavyo tunaweza tukaenda mbele zaidi badala ya kutumia moramu tutumie ile lami laini kidogo ili hiki anachokizungumza hapa kisije kikatokea.

Nataka kusema hapa kwamba ni kweli wakati mwingine pametokea uchakachuaji na vitu vingine vinavyozunguzwa hapa. Ndiyo maana mnaona sisi wote pamoja na Kamati ya LAAC imeamua sasa kutokuwaita watu hapa Dodoma imeamua kwenda moja kwa moja mpaka katika Halmashauri zinazohusika ili kwenda kujipatia thamani halisi ya pesa iliyotumika.

Mwaka huu unaomalizika hapa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Halmashauri zetu ni trilioni 2.5 *this is a lot of money* kwa nchi maskini kama Tanzania, tunawaomba Wabunge tusaidiane sisi wote kwa pamoja. Sisi TAMISEMI tumeshaelekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, *we shall never leave stone unturned* tutapita kule kufuatilia hii miradi kuhakikisha kwamba inajengwa kwa kiwango kilichokusudiwa.

Na. 269

**Upatikanaji wa Sheria Ndogo**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kuna ucheleweshaji mkubwa wa upatikanaji wa Sheria Ndogo katika Serikali za Mitaa:-

Je, ucheleweshaji huo unasababishwa na nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Serikali za Mitaa kutunga Sheria Ndogo umetokana na Mamlaka iliyokasimiwa na Bunge kufuatia Sheria za Serikaliza Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na Mamlaka za Miji Sura ya 288. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa uwezo huo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kama vile kukusanya mapato na udhibiti na usimamizi wa shughuli mbalimbali katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo na utaratibu wa kisheria wa kutunga, kuidhinisha na kuchapisha Sheria Ndogo, zipo sababu zinazosababisha ucheleweshaji wa Sheria Ndogo hizo kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri kuwasilisha Sheria Ndogo bila mihtasari ya maoni ya wananchi walioshiriki kutoa maoni katika mchakato wa kuandaa Sheria Ndogo kama inavyoelekezwa na Sheria za Serikali za Mitaa. Hali hii husababisha Sheria Ndogo hizo kutoidhinishwa na kurudishwa kwenye Halmashauri husika ili ziwasilishwe zikiwa na maoni ya wananchi kama Sheria inavyoelekeza.

(ii)Halmashauri kuwasilisha Sheria Ndogo zenye maudhui yanayopingana na Sheria Mama na Sera za Kitaifa hivyo kusababisha jukumu kubwa la kuzihariri.

(iii) Mchakato mrefu wa kupitisha Sheria Ndogo kuanzia Halmashauri yenyewe, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, Mhariri wa Gazeti la Serikali na hatimaye Mpiga Chapa Mkuu ambapo Gazeti la Serikali hutolewa mara moja tu kwa wiki yaani kila Ijumaa.

(iv)Halmashauri kuwasilisha nakala pungufu ya Sheria Ndogo badala ya nakala nne zinazotakiwa.

(v) Halmashauri kukosea uandishi wa jina la Mheshimiwa Waziri Mkuu.

(vi)Halmashauri kukosea Ada ya Magazeti ya Serikali na kusababisha Halmashauri kutopata taarifa ya Sheria Ndogo zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali. Halmashauri zote zinatakiwa kulipia shilingi 100,000/- kwa mwaka kwa ajili ya ada ya Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzikumbusha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sheria wakati wa kutunga Sheria Ndogo ili kuepusha ucheleweshaji na usumbufu usiokuwa wa lazima na kuhakikisha Ada ya Gazeti la Serikali ya shilingi 100,000/- kwa mwaka inalipwa ili kuziwezesha kupata magazeti hayo kila wiki.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri katika sababu moja anayosema Sheria hizi zinachelewa ni Mpigachapa Mkuu kuchapisha katika Gazeti la Serikali mara moja kwa wiki.

Je, kuondoa tatizo hilo Serikali iko tayari kuanzisha Mpigachapa Mkuu Maalum atakayeshughulikia suala la Serikali za Mitaa peke yake.

Katika kuchelewesha upatikanaji wa Sheria hizi kuna baadhi ya Halmashauri hutumia rasimu za Sheria hizi katika kutekeleza makujumu yao ambalo mimi nahisi ni kosa.

Je, Serikali inasema vipi katika kwa Halmashauri hizi ambazo hutumia rasimu hizi wakati sheria hazijapita kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, huyu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali anayezungumzwa hapa ukisema akae pale tu kwa ajili ya Serikali za Mitaa wakati mwingine utakuta hana kazi kwa sababu kwanza tumeeleza huu mlolongo ambao tunatakiwa tuupitie mpaka kuhakikisha kwamba tumefikisha.

Baadaye tunarudisha ile kwenye Halmashauri na kusema sasa hii ni Sheria ndogo ambayo imekubalika na inaweza ikatumika. Kwa sababu hapa kuna Tawala za Mikoa, hapa kuna Wizara nyingine zote pamoja na Mashirika mengine ya Serikali nayo yanapitia hapo hapo.

Tulichofanya sisi kuondoa hilo tatizo hapa ni kwamba TAMISEMI tumeona tuweke watu maalum ambao wanakaa pale kama kitengo ili watusaidie kupitia na kusoma hizi Sheria ndogo haraka haraka zinapotoka katika Halmashauri kwa sababu ya zile ambazo nimezieleza ili tusije tukawa tunachelewesha kwa kiasi hicho kilichopita.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sikumpata vizuri naomba arudie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif unaweza kuuliza tena?

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, ni kwamba utaratibu unaandaliwa rasimu ambayo inafuata Mheshimiwa Naibu Waziri kausema, lakini kabla ya Sheria haijarudi, basi wahusika wanaitumia rasimu ile hasa katika kukusanya mapato.

Kwa hiyo, je, Serikali inasema nini kuhusu kitendo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU**, **TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa. Sheria ndogo inapotungwa na leo tena haya maswali mjue na Walimu wangu walionifundisha wako kule juu wananisikiliza.

Ni sawasawa unavyofanya *curriculum development* lazima uende kwa wadau uwaulize kwamba mnasemaje kuhusu hii Sheria. Ile tulipoitengeneza rasimu ilitengenezwa kama *model* ili mtu anapokwenda kutengeneza Sheria ndogo ndogo asije akatoka nje ya ile *model*.

Haiwezekani na hairuhusiwi mtu akatumia rasimu hiyo na rasimu hiyo inakatisha nchi nzima. Unangoja mpaka uone mkono wa Mheshimiwa Waziri Mkuu umeanguka pale (imesainiwa na Waziri Mkuu) ndipo inakuwa *authentic*.

Ukienda kutoza ushuru kule watakukataliatilia na watakuambia hii ni nini na hakuna mtu atakayekubali, ukienda Mahakamani haitakubalika vile vile na itakuwa ni kosa kwa kukiuka utaratibu uliowekwa na sheria.

Kwa hiyo, kama kuna watu wanaofanya hivyo naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kusema kwamba waache mara moja jambo hilo wasifanye, wasifanye. Huwezi kutumia rasimu kwa jambo hilo.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu wa ushirikishaji wa wananchi katika mchakato mzima wa sheria ndogo haukidhi haja hasa kwa kupitia matangazo kwa kuwa wananchi wengi hawasomi matangazo.

Je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kubadilisha utaratibu wa ushirikishwaji wa wananchi katika kutunga sheria ndogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU**, **TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sasa hapa sijui tutafanyaje, kwa sababu ushirikishwaji ni ushirikishwaji. Wananchi wa Kasulu, wananchi wa Tunduma, wananchi walioko katika maeneo ya Halmashauri, *the bottom line* lazima waseme kwamba tunaafiki kwamba hizi sheria zitumike. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu

akigundua kwamba hukufuata huo utaratibu, atazirudisha moja kwa moja mpaka katika Halmashauri inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika ni kwamba mkishajua kwamba hii ndiyo tutatengeneza kama mapendekezo, kwanza mtapeleka kwenye Baraza la Madiwani ambapo pale kuna wawakilishi, itakuwa imepitia kwenye Kamati ya Maendeleo inaitwa *Ward DC (Ward Development Committee)*, watakuwa wanangalia mle ndani watamaliza. Mkimaliza mtai-*pin on the board*, mtaiweka kwenye ukuta pale wananchi wote wasome, waangalie kwamba hii sheria inayokuja sasa ndiyo inakuja hapa.

Kwa mfano, mtu anaweza akasema hivi: "tunataka kuzuia kengele na adhana zote asubuhi watu wanatusumbua" Tukisikia sisi inasemwa hivyo, tunasema *no no no!* Hii kwa wananchi itakuwa ni kitu kibaya, tunarudisha pale. Wananchi wakiona pale, waislam, wakristo wakiangalia kengele zile kwamba wanataka kuzuia zisipigwe pale, watakataa, watasema hapana, watasema *no no no*, hii sheria itakuja kutuumiza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachozungumza hapa ni kwamba hawezi mtu akaleta sheria ndogo hapa bila kuipeleka kwanza kwa wananchi kuwauliza kwa sababu wao ndiyo wenye hiyo sheria, ni ya kwao. *(Makofi)*

Na. 270

**Stahili za Walimu Katika Shule**

**MHE. MOHAMED G. DEWJI (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sana pamekuwepo na malalamiko yanayohusu stahili za walimu katika shule za Singida Mjini na kwingineko nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa wakati tofauti imekuwa ikichukua hatua mahsusi ili kuhakikisha kwamba inamaliza malalamiko ya Walimu juu ya stahili zao mbalimbali. Hatua ambazo Serikali imekuwa inachukua ni pamoja na mwaka 2009, kuhakiki na kulipa madeni ya walimu ambapo jumla ya shilingi bilioni 32.2 zilitolewa kulipia stahili za walimu wa shule zote za msingi na shilingi bilioni 12.5 zilitolewa kulipa madeni ya stahili mbalimbali za walimu wa shule za sekondari nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2009/2010, Serikali imeweka utaratibu ambao walimu wanaopangwa maeneo mapya wanalipwa mishahara na stahili zao mara wanaporipoti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Na ili kufanikisha azma hii Mwezi Februari, 2011, Serikali ilipeleka katika Halmashauri zote nchini jumla ya shilingi bilioni 15.3 kwa ajili ya malipo ya posho ya kujikimu, nauli, mizigo na wategemezi kwa walimu wote wapya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini kutozalisha madeni na kuzingatia maelekezo ya Serikali kwa kulipa stahili za likizo, uhamisho na matibabu. Maelekezo haya hayatahusu malimbikizo ambayo yatakuwepo kutokana na kupanda kwa madaraja kwa walimu. Ili kutekeleza azma hii kwa mwaka 2010/2011, Serikali imepeleka katika Halmashauri zote nchini jumla ya shilingi bilioni 15.5 kwa ajili ya likizo na uhamisho kwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Kati ya fedha hizi shilingi milioni 457.3 zilipelekwa katika Mkoa wa Singida ambapo shilingi milioni 388.8 ni kwa ajili ya likizo na shilingi milioni 68.5 kwa ajili ya uhamisho.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa walimu wa Mkoa wa Singida kama walivyo walimu wengine kote nchini stahili zao zinashughulikiwa na zitalipwa baada ya taratibu zote kukamilika. Serikali inatambua kuwepo kwa madeni ya malimbikizo kutokana na kupanda kwa madaraja kwa nyakati tofauti, na Serikali inashughulikia kwa pamoja na Idara ya Utumishi na Hazina.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza pamoja na Serikali kujitahidi kulipa madeni haya kwa walimu, lakini bado Halmashauri ya Mji wa Singida walimu wanadai milioni 96 madeni mapya, na kwa Mkoa mzima milioni 580, kwa nchi nzima bilioni 29. Je, kupitia Bajeti hii tunayoijadili, Serikali itakuwa tayari kumaliza madeni haya ili walimu sasa wapate amani katika kazi zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa kila wakati Wakurugenzi wanazalisha madeni mapya; hivi ninavyozungumza yako madeni mapya ambayo hata hayajahakikiwa.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuhakiki upya madeni mengine ya walimu ili waondokane kabisa na adha ya kugombana na walimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, suala la madeni mapya kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi, tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi kutozalisha madeni mapya. Na madeni haya mapya ambayo sisi tumeelekeza kwamba yasizalishwe ni kwenye maeneo ya uhamisho, likizo pamoja na matibabu. Na kama ambavyo nimesema, sehemu kubwa ya madeni ya walimu yaliyopo sasa ambayo yanazungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge. Jana wamechangia kwa kiasi kikubwa ni ya malimbikizo ya mishahara ambayo hayawezi kuzuilika na yataendelea

kuwepo kwa sababu ya kupanda kwa madaraja ya walimu kwa nyakati tofauti tofauti, jambo ambalo ni la msingi katika utumishi. Madeni hayo yatatolewa maelekezo mazuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu jioni hii atakapokuwa anawasilisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, suala la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, uzalishaji wa madeni mapya. TAMISEMI kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika mipango yake ya utumaji wa fedha kwenye Halmashauri, tunatuma fedha kwenye Halmashauri zetu kwenye matumizi ya kawaida ambayo wao wanatakiwa wayawekee utaratibu wa ulipaji wa madeni yale kwenye Halmashauri zao, kwenye maeneo ya likizo, lakini pia pamoja na matibabu na masomo.

Mheshimiwa Spika, eneo la likizo, tunatuma fedha ambazo Mkurugenzi anatakiwa kujua kwamba ametumiwa labda milioni 44, atatakiwa kuandaa utaratibu wa matumizi ya milioni 44 kwa kuandaa orodha ya walimu ambao wanatakiwa kwenda likizo kwa thamani ile ya fedha, badala ya kuzalisha madeni mapya.

Lakini pia kwenye eneo la uhamisho, tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote nchini, hatuna sababu ya Mkurugenzi kuhamisha watumishi huku akiwa hana fedha. Kwa hiyo, kama Mkurugenzi wa Singida amehamisha watumishi akiwa hana fedha ni kosa ambalo tutalifuatilia tuweze kujua kwa nini alifanya hivyo wakati sisi tukiwa tumeishatoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, suala la matibabu, hili hatuwezi kulizuia kwa sababu huwezi kuzuia walimu kuugua. Lakini, kutokana na vyanzo vya Halmashauri na fedha ambayo kidogo tunaitumia, tunawasihi Wakurugenzi kuendelea kuwahudumia walimu wetu ili wapate matibabu wakati wote. Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa anapotujibu amejikita kwenye suala zima la likizo, matibabu, masomo, kitu ambacho hata ukifuatilia madeni ya walimu unaona hakina matatizo, kinakwenda vizuri.

Lakini, eneo kubwa ambalo haliwezi kuepukika ni suala la uhamisho na mapunjo ya walimu wakati ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Njombe walimu hao wanadai jumla ya shilingi milioni 81, Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini wanadai jumla ya shilingi milioni 274.

Sasa, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kwa sababu suala la uhamisho haliepukiki. Kwa nini Serikali sasa isitenge fedha ya kutosha kusaidia kupunguza kero za walimu wanapohitaji kuhamishwa kwa sababu aambazo ni za kimsingi na si za makusudi za kuwalaumu Wakurugenzi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi, lakini pia kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

Ambacho naweza kusema ni kwamba kwa madeni hayo ambayo yameanza kuonekana wakati na sisi tumewasiliana na Chama cha Walimu Tanzania, wametupa orodha ya madeni yote nchini, lakini kwa kupata orodha ile hatuwezi, mpaka tufanye uhakiki kutoka Halmashauri na Halmashauri.

Kule kwenye Halmashauri sisi tumeunda Kamati inayoweza kupitia madeni yale ya awali, na Kamati ile tumemtaka Afisa Elimu, Mkurugenzi anapofanya lile lazima ahusishe Mkurugenzi mwenyewe kwa maana ya Afisa Utumishi, Afisa Elimu, Katibu wa Chama cha Walimu, Katibu *TSD* ili waweze kwenda pamoja ili kuzuia uzalishaji wa madeni kama haya ambayo sasa hata Chama cha Walimu wametuletea orodha yao.

Kwa hiyo, napenda kukiri kwamba uwepo wa madeni hayo ni lazima sasa twende kwenye Halmashauri zetu kuhakiki na ndipo sasa tutatoa jibu la msingi la Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Na. 271

**Mikopo ya Matrekta Madogo**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Pembejeo ni kuwasaidia wakulima kuwa na kilimo bora zaidi chenye tija kwa kuwapatia mikopo ya pembejeo za kilimo kama matrekta madogo ili kuondokana na kilimo cha jembe la mkono:-

(a) Je, ni lini wakulima 17 kutoka Wilaya ya Magu walioomba mikopo ya matrekta madogo na makubwa watapatiwa matrekta hayo?

(b) Je, ni lini mamlaka husika itaondoa urasimu na kuwafikishia wakulima matrekta hayo kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Busega. Kwanza kabla ya hapo, nitoe maelezo mafupi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ili kutoa fursa kwa walengwa katika sekta ya kilimo kuweza kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu ili kuongeza tija katika kilimo. Mfuko wa Pembejeo hutegemea kwa kiasi kikubwa Bajeti inayotengwa na Serikali kila mwaka ili kutoa mikopo kwa maombi yaliyopokelewa na kiasi cha riba kinachotozwa huongeza mtaji kwa kadri mikopo inavyorejeshwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Busega lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2010/2011, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa umetoa mikopo 21 ya matrekta mapya yenye thamani ya shilingi 689,160,000/= kwa wakulima wa Wilaya ya Magu. Aidha, mchakato wa maombi yaliyopelekwa katika msimu wa 2010/2011 uko katika hatua mbalimbali kwa ajili ya kupata mikopo katika Bajeti ya mwaka 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa una utaratibu wake ambao unalenga kujiridhisha kwamba waombaji wa mikopo ni wakulima halisi na si wajasiriamali ambao wanaweza kupata mikopo kutoka taasisi nyingine za kifedha. Ili kutimiza hili, waombaji huhakikiwa kama kweli ni wadau katika sekta ya kilimo.

Utaratibu huu huchukua muda, lakini nia na madhumuni ni kujiridhisha hatua kwa hatua ili kutoa mikopo inayolenga kutimiza maudhui ya Mfuko na kulinda fedha za umma kwa ujumla. Maombi ya mikopo yanayopokelewa kila mwaka yana thamani kubwa kuliko uwezo wa Mfuko kuyashughulikia mara moja. Kutokana na sababu hiyo ni dhahiri kwamba utoaji wa mikopo kwa wakati muafaka pia huathirika kwa kiasi kikubwa.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu yenye ukweli ya Naibu Waziri, lakini kwa kweli hayatii matumaini sana kwa watu wangu.

Kwanza, kwa kuwa utaratibu wa kupata mikopo hii kwa kutumia dhamana ya hati za nyumba au ardhi iliyopimwa ni mgumu sana kwa wananchi wa kawaida kule vijijini.

Sasa, Serikali haioni kwamba kuna haja itoe fursa ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta *(tractor hire service centre)* katika maeneo haya ya vijijini kwa kutumia vikundi vilivyosajiliwa au vyama vya kuweka na kukopa ili wananchi waweze kuwa wanakodisha matrekta badala ya kusubiri mkulima mmoja mmoja kukopeshwa trekta?

Mheshimiwa Spika, pili, kama hilo linawezekana au ataliona Naibu Waziri ni wazo zuri. Sasa atakuwa tayari au yeye mwenyewe au kutuma watalaam wake kuja Busega kutoa elimu kwa vikundi ili vikundi vyetu vizuri kama *Lamadi SACCOS, Tugeme SACCOS* na WAWAMA na vingine vingine vizuri viweze kupata elimu hiyo na viweze kukopeshwa matrekta kuanzisha vituo hivyo vya kukodisha matrekta? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba dhamana kwa maana ya Hati ya nyumba zisizohamishika ni ngumu vijijini.

Lakini tayari tunao utaratibu ndiyo maana tunawahamasisha wakulima kujiunga kwenye vyama vya Ushirika. Na kupitia kwenye vyama vyao vya ushirika hususan *SACCOS*, wanayo fursa ya kutumia Muungano wa vyama vya ushirika kama chama kile cha *SCULT* na Mfuko wa Pembejeo unakubali kabisa dhamana ambayo inawekwa na *SCULT* kwa kuwadhamini wanachama wake.

Kwa hiyo, alivyosema Mheshimiwa Kamani ni sahihi kabisa na ni utaratibu ambao tunautumia ili kuhakikisha kwamba wakulima wale ambao hawana dhamana, wanaweza wakapata dhamana kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, ziko njia nyingine, Halmashauri ya Wilaya pia inaweza nayo ikawadhamini wakulima wake. Utaratibu huu unawezekana, tulishakubaliana, tumejadili na Halmashauri za Wilaya, ziangalie jinsi zinavyoweza kuwadhamini wakulima aidha mmoja mmoja au pia kwenye vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishaji wa vituo au *tractor hire service centre*. Hili ndilo lengo hasa ambalo ni la Wizara yetu. Kwa hiyo, kwa pamoja na swali lake la pili, ningependa kusema nitatuma watalaam wa Mfuko wa Pembejeo ili waende katika Jimbo lile wakawaelimishe wananchi na wakulima wale namna ya kuanzisha vituo hivi na namna wanavyoweza kujiunga wakapata dhamana kupitia kwenye vyama vyao.

Na. 272

**Ulipaji wa Madeni ya Vyama vya Ushirika**

**MHE. STEPHEN J. MASELE** aliuliza:-

Katika juhudi za kufufua vyama vya ushirika, Serikali iliamua kulipa madeni yote ya vyama vya Ushirika nchini ikiwemo *SHIRECU:-*

Je, ni lini Serikali itakamilisha ulipaji wa mapunjo ya mishahara kwa mamia ya wafanyakazi wa *SHIRECU* Mkoani Shinyanga, waliopunguzwa kazi au kustaafu kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kulipa madeni ya vyama vya ushirika ni kuviwezesha kufanya mabadiliko ya utendaji na kuviimarisha vyama kibiashara. Azma ya Serikali ni kuviondolea baadhi ya madeni vyama hivyo kama sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Mageuzi na modenaizesheni ya vyama vya Ushirika nchini inayolenga

kuvifanya kuwa endelevu, vyenye nguvu ya kiuchumi na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma vyama vya ushirika vilishindwa kulipa madeni yake kutokana na sababu nyingi zikiwemo uendeshaji mbaya, mitaji midogo isiyoyawezesha kushindana katika soko huria, kutegemea mikopo ya benki za biashara ambayo vilishindwa kuirejesha na kushuka mara kwa mara kwa bei za mazao katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2010, Serikali imelipa madeni ya vyama vya Ushirika 38 kiasi cha shilingi 15,015,073,960/=.

Miongoni mwa madeni yaliyopo ni deni la watumishi wa *SHIRECU* waliopunguzwa kazi au kustaafishwa ambalo linafikia shilingi 3,271,226,640/= ambapo kati ya hizo tayari Serikali imekwishalipa shilingi 654,245,282/= sawa na asilimia 20. Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti zake za kila mwaka hadi deni lote litakapokwisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalipa madeni ya vyama vya Ushirika ili kuvifufua kwa sababu ndiyo njia rahisi ya kuwafikishia wananchi wengi misaada na huduma kuliko kuhudumia mtu mmoja mmoja. Hata hivyo, Serikali inaendelea kulipa madeni kwa masharti kwamba vyama vya Ushirika havitaruhusiwa kulimbikiza madeni tena. Aidha, Wizara yangu itavifanyia vyama vya Ushirika ukaguzi wa mara kwa mara ili kudhibiti wizi, ubadhirifu wa fedha na mali unaofanywa hususan wakati wa msimu wa ununuzi wa mazao.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Lakini, nilitaka kujua Serikali imetenga kiasi gani kulipa madeni hayo kwa wafanyakazi katika mwaka huu wa fedha kwa kuwa wafanyakazi hao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu sana na sasa wanaanza kukata tama?

Pili, Serikali itamaliza lini kulipa pesa ambazo iliahidi kuwalipa wanunuzi wa pamba katika fungu la *Stimulus Package?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mbunge avute subira kidogo tu jumatatu tutasoma hotuba hapa na tutataja ni kiasi gani tumetenga kwa kuendelea kulipa madeni haya.

Lakini kuhusu kulipa *Stimulus Package* naomba nikiri kwamba ni kweli wakati Rais alipotoa agizo kwamba tuongeze shilingi themanini kwa kila kilo kwa wakulima wa pamba, tulianza kufanya utaratibu huo na wakulima wengi kama siyo wote wameshalipwa.

Mheshimiwa Spika, kilichojitokeza ni kwamba wale *ginners* ambao walilipa fedha zao kwa wakulima hao ndiyo bado wanadai, nataka nikiri kwamba madeni hayo yamehakikiwa sasa sasa yamefikishwa Hazina na tunafuatilia ili kusudi yaweze kulipwa. Kwa hiyo, naomba awe na subira kidogo, kwa sababu deni hilo tayari limefikishwa Hazina kwa ajili ya malipo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, hali ya madeni ya ushirika yanaikumba pia ushirika wa Mbiku, Mbinga,

Je, ni lini Serikali itafanya uhakiki wa madeni hayo na kuwalipa hawa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Serikali imekwishafanya uhakiki wa madeni ninaamini kabisa hata Mbiku imeshafanyiwa uhakika, kinachofanyika hivi sasa ni kuendelea kulipa madeni yale ambayo bado hayajalipwa.

Mheshimiwa Spika, madeni ni mengi nikikuonesha orodha ya vyama vya ushirika na gharama ni kubwa. Tunachokifanya ni kwamba kila mwaka tunatenga fedha kidogo kwa jinsi fedha zinavyopatikana ili tuendelee kuyapunguza. Kwa hiyo madeni ya Mbiku yamekwishahakikiwa kilichobakia ni kuwalipa tu.

Na. 273

**Fedha Kidogo Inayotengwa kwa ajili ya Shule Maalum ya Walemavu**

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR** aliuliza:-

Pamoja na juhudi za Serikali kuwasaidia walemavu katika suala la elimu maalum, lakini fungu la Bajeti linalotolewa kwa ajili ya shule hizo maalum ni kidogo sana na shule zilizo nyingi zinaendeshwa na Mashirika ya Kujitolea:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kuongeza fungu la Bajeti yake ili iendeshe shule hizo kwa mwongozo mzuri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali Na. 31 la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, tarehe 13 Juni, 2011, nililieleza Bunge lako Tukufu mikakati ya Serikali ya kushughulikia matatizo ya shule maalum hususan uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, kimsingi fedha za kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kujisomea hutengwa katika Bajeti ya Wizara kila mwaka. Hata hivyo, fedha inayotolewa haikidhi mahitaji yote yanayotakiwa. Kwa kuzingatia ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- Kutoa ruzuku ya shilingi 20,000/= kwa kila mwanafunzi mwenye ulemavu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (MMEM II) kwa wanafunzi wa shule za msingi.

- Kutoa ruzuku ya shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi mwenye ulemavu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) kwa wanafunzi wote wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya fedha kwa ajili ya uendeshaji na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zenye wanafunzi wenye ulamavu ni mkubwa ikilinganishwa na shule za kawaida. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara yangu imekuwa ikitenga fedha kwa shule zenye wanafunzi wenye ulemavu kulingana na ukomo wa Bajeti ya Wizara na kwa kuzingatia mahitaji maalum yaliyopewa kipaumbele kila mwaka. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Wizara yangu ilitenga kiasi cha shilingi 631,400,000/= mwaka 2008/2009, shilingi 986,400,000/= mwaka 2009/2010 na shilingi 986,400,000/= mwaka 2010/2011. Kiasi cha fedha kilichotajwa hapo juu kilitolewa chote katika Bajeti kwa miaka iliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wadau wote wakiwemo washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Dini na asasi zisizo za Kiserikali wanaochangia na pia natoa wito kwa wadau wengine wa elimu kutoa michango ya fedha na vifaa ili kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kujisomea katika mazingira stahiki.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili mDOGO ya nyongeza.

(a) Tatizo la elimu maalum kila siku limekuwa na matatizo hakuna mabadiliko na hatuwezi kukwepa kusomesha watoto hawa ili kukidhi mahitaji ya fedha hizi kidogo. Serikali haioni sasa umefika wakati muafaka fedha hizi ziende moja kwa moja kwenye dawati la elimu badala ya kupitia Halmashauri ambako zinachukua muda mrefu kufikia walengwa?

(b)Naomba Waziri anipe mchanganuo wa fedha alizozitaja zimetumika vipi, ili nipate kuelewa ametumia pesa hizi ili kusaidia shule hizi za watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Nina wasiwasi na sehemu ya pili ya swali lakini Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba fedha za elimu maalum zikae kwenye dawati la elimu Wizarani ni kweli, lakini kama nilivyosema kwamba namna ya kugatua au kurahisisha

utendaji wa kazi, wale vijana wetu wapo kwenye shule za msingi kwenye Halmashauri zote nchini. Kwa hiyo, Wizara au Serikali iliona ni rahisi fedha hizi ziende kama fedha zingine zinavyokwenda za MMES au MMEM kwenye Halmashauri, ili zipate namna ya urahisi wa kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini sijaona kama kuna ugumu sana wa mpaka labda fedha hizi zipitie kwenye akaunti za shule, pale itakapoonekana kuna ugumu huo, naomba sisi kama Wizara tulichukue tulifanyie kazi tutaendelea kuona kama inawezekana kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili Mbunge anasema angalau apate mchanganuo wa namna fedha zinavyotumika, kwa sababu ni Mbunge ana haki ya kujua haya. Naomba nimwahidi kwamba tutakaa na watalaamu wetu na nitamwomba Mbunge hata baada ya wiki moja mimi nitaweza kumpa mchanganuo wa fedha hizo jinsi zinavyotumika, hakuna shida. *(Makofi)*

Na. 274

**Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) Kuchukua Eneo la Kijiji**

**MHE. SAID R. BWANAMDOGO** aliuliza:-

Mwaka 2009 Chuo cha Usimamizi *IFM* kilichukua eneo la kujenga chuo hicho katika vijiji cha Msata/Kihangaiko lakini hadi sasa ujenzi haujaanza:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hilo?

(b) Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia ya kuchukuliwa maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, Mbunge wa Chalinze, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali bado ina nia thabiti ya kujenga Chuo cha Usimamizi wa Fedha katika Kijiji cha Msata na Kihangaiko. Ujenzi wa Chuo hiki unategemwa kufanywa kwa utaratibu wa *PPP*. Kazi zinazoendelea sasa ni upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi ili kupata gharama za mradi na utafutaji wa wabia.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na kulijulisha Bunge kwamba, wananchi wanaomiliki maeneo hayo watalipwa fidia katika mwaka huu wa fedha hatua kwa hatua kadri ambavyo uhakiki wa kuwatambua wahusika na stahili zao utakapokamilika.

**MHE. SAID R. BWANAMDOGO:**Mheshimiwa Spika ahsante sana, pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kazi hiyo katika vijiji vilivyohusika, lakini hadi kufikia tarehe 31 Juni,2011 fedha hiyo haijalipwa. Kwa bahati mbaya sana Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2011/2012 mimi sijaona kiasi kilichotengwa kwenye Wizara husika.

(a) Sasa Naibu Waziri ananiambia kwamba atalipa fedha hizi. Naomba anieleze ni wapi ambapo imeonekana kwenye Bajeti yake.

(b) Kwa sababu suala hili, kama nilivyosema tangu Bajeti iliyopita ilikuwa imeshatengewa fungu, mradi huu una hamu kubwa kwa wananchi naomba Naibu Waziri aniambie kwamba ulipaji wa fedha hizi utaanza mwezi gani, japokuwa ameshasema kwamba ni mwaka huu wa fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba katika mwaka wa fedha 2010/2011 kulitengwa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya fidia hizi. Hata hivyo kwa sababu nyaraka za wahusika zilichelewa kufika Wizarani haikuweza kulipwa na naomba nimhakikishie tena Mbunge kwamba nyaraka hizo tayari zimefika na fedha zitakuwepo na zitalipwa kama nilivyoahidi kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nini kimetengwa kwa mwaka huu ni kwamba katika mwaka huu wa fedha kumetengwa shilingi milioni 200 ambazo zipo chini ya idara ya mipango ya Wizara ya Fedha chini ya Fungu 50.

Mheshimiwa Spika, swali la kwamba Serikali ulipaji utafanyika lini. Naomba nimhakikishie tu Mbunge kwamba ulipaji utaanza kulipwa mara tu baada ya kumaliza Bunge lako Tukufu.

Na. 275

**Fedha zilizotumika kunusuru Uchumi wa TANZANIA**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Taarifa ndani ya Bunge na kwenye vyombo mbalimbali vya habari inaonesha kuwa wakati mtikisiko wa uchumi wa dunia, Tanzania ilitumia shilingi 1.7 trilioni kama mpango wa kunusuru uchumi wa Tanzania *(Stimulus Package).*

(a) Je, ni makampuni mangapi kwa majina, na ni kiasi gani cha fedha zililipwa kwa ajili ya kunusuru uchumi wa Tanzania?

(b) Je, fedha hizo zilitoka wapi na kiasi gani kila kianzia *source* makampuni hayo yalipewa kama mkopo au msaada, na kama ni mkopo. Je, ni lini fedha hizi zitaanza kulipwa?

(c) Je, ni fedha kiasi gani zimetumika hadi tarehe 30 Disemba, 2010. Kwa kuwa hizi ni fedha za umma. Je, zinakaguliwa na *CAG,* na ukaguzi wake unafanyika vipi ikizingatiwa fedha hizo zilitolewa kwa makampuni binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye kipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa kunusuru uchumi wa Tanzania kufuatia msukosuko wa Fedha duniani, jumla ya makampuni 97 yalinufaika moja kwa moja. Makampuni haya yalisaidiwa kwa ajili ya kufidia hasara. Hata hivyo kutokana na kanuni za kibenki sitoweza kuyajata makampuni haya yaliyonufaika kama alivyotaka Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango huo ulikisiwa kugharimu shilingi trilioni 1.7 kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi. Vyanzo hivi ni pamoja na mikopo ya ndani shilingi bilioni 828 ili kufidia pengo la mapato; shilingi bilioni 436.2, zikiwa ni mkopo nafuu kutoka *IFM* uliopatikana kupitia utaratibu wa *Exogenous shock facility (ESF)* na shilingi 428.3 bilioni zilizotengwa ndani ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kulinda ajira, kipato kuwezesha utoaji mikopo na uwekezaji katika miundo mbinu. Urejeshwaji wa mikopo husika utafanywa kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kanuni za Kibenki, si sahihi kutoa taarifa za mteja mmoja mmoja kwa umma kama ambavyo swali la Mheshimiwa Mbunge lilivyotaka.

(c) Mheshemiwa Spika, hadi Desemba 2010, fedha zilizokuwa zimetumika chini ya mpango huo wa kunusuru uchumi zilifikia shilingi trilioni 1.4535, pengo likiwa ni shilingi bilioni 239. Pengo hili lilitokana na kukosekana kwa fedha toka kwa baadhi ya vyanzo, ikiwa ni pamoja na wafadhili mbalimbali.

Kwa kuwa fedha hizi ziliingizwa kwenye Bajeti ya Serikali zitafanyiwa ukaguzi na *CAG* kama ilivyo kwa fedha nyingine za Umma.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *CAG,* katika taarifa yake ya mwaka 2009/2010 alibaini kwamba bilioni 48 hazikuwa na

maelezo; na Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iliahidi kwamba watafanya tena uchunguzi kuhusu pesa hizi na taarifa hiyo italetwa hapa Bungeni.

(a) Je, ni lini taarifa hiyo italetwa hapa Bungeni?

(b) Katika majibu yake Naibu Spika amesema kwamba hawezi kutoa orodha ya makampuni yaliyonufaika na *stimulus package.* Je, haoni kwamba kukataa kutoa taarifa kwa Wabunge ni kukiuka zaidi utaratibu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, lakini umemsingizia Naibu Spika, hapa ni Naibu Waziri.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, Samahani. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu bilioni 48 ambazo zimekosa maelezo toshelezi, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Leticia Nyerere…

**SPIKA**: Kupongezana hamna, jibu swali. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Kwa kufuatilia kwa karibu masuala ya uwajibikaji na uadilifu. Ni kweli kwamba kuna bilioni 48 zilihojiwa na *CAG* na naomba nitoe taarifa kwamba maelezo kuhusu fedha hizi yameshapelekwa kwenye ofisi ya *CAG* kwa ajili ya hatua zinazofuata.

Maelezo zaidi yataletwa Bungeni wakati tunawasilisha majibu ya Serikali kwenye ripoti ya taarifa za Kamati za Bunge za *POAC, PAC, LAAC* mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la orodha hii, hili ni suala la kikanuni ambalo bado tutaendelea kuliangalia na hizi taarifa baada ya kuwasiliana na *BOT* tutaziwasilisha Bungeni kwa ajili ya kuangaliwa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, pesa zilizotumika kwenye *Stimulus Package* ni pesa nyingi sana na ni pesa za umma, Waziri anatuambia kuleta orodha ni kukiuka Kanuni ni Kanuni gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, chini ya sheria za Mabenki, suala la taarifa binafsi ya mteja na benki ni suala la siri, na chini ya taratibu hizo ndiyo maana nikasema siwezi kuzileta.

**SPIKA**:Mheshimiwa Waziri mkalifanyie kazi katika ofisi yenu, kwa sababu swali halijasema ulete hela za benki, linasema ni makampuni mangapi kwa majina, mkalifanyie kazi mtatujibu hapa. (*Makofi*)

Na. 276

**Utengenezaji wa Chumvi – Manyoni**

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Wananchi wa Ikasi na Chinangali wanajishughulisha na utengenezaji wa chumvi ambayo inauzwa ndani na nje ya nchi wanatumia teknolojia duni katika utengenezaji chumvi yao?

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza Wananchi hao kupata ujuzi wa kisasa na zana za kisasa za kutengeneza chumvi ili kuongeza ufanisi katika biashara yao?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa mkopo wa vifaa au fedha kupitia vikundi ambavyo wameviunda ili kuwasaidia kukuza na kuboresha biashara zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza Programu mbalimbali za kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa chumvi katika Wilaya ya Bahi, Chamwino, Manyoni, Singida na Iramba. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2009 hadi 2011, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania, ilitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa chumvi kuhusu uchanganyaji wa madini joto katika chumvi wanayozalisha ili kuiongezea ubora na mafunzo ya kuzalisha chumvi safi yenye ubora unaokidhi kwa matumizi ya binadamu na wanyama kulingana na viwango vya *TBS.* Mafunzo hayo yaliyotolewa katika vijiji vifuatavyo: Ilindi, Kigwe, Chimendeli, Chipanga na Chali katika Wilaya ya Bahi; Kikuyu, Majiri na Ikasi katika Wilaya ya Manyoni; na Nkongilangi na Shelui katika Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiweka mazingira wezeshi na kuhamasisha Wananchi kujiunga na vikundi ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo na vifaa kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa chumvi yenye viwango vya soko kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge. Hivyo, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza wachimbaji wadogo nchini, kwa lengo la kuwajengea wachimbaji wadogo uwezo wa kifedha na wa kitaaluma kwa ajili ya kununua au kukopeshwa vifaa vya kuendeleza uchimbaji wa madini ikiwemo chumvi.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa Manyoni wakiwemo wazalishaji wa chumvi, wanaweza kupata mikopo ya vifaa vya uchimbaji baada ya kutimiza masharti

yanayotakiwa. Hivyo, ombi langu kwa wachimbaji wadogo wa maeneo husika ni kuwa wawasiliane na Ofisi zetu za Idara za Madini Singida na Dodoma, kwa maelezo zaidi kuhusu utaratibu huu. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu, itaendelea kuboresha taratibu za mfuko huu ili uweze kuwasaidia wachimbaji wadogo wengi zaidi. Aidha, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, waendelee kuwahamasisha wachimbaji wadogo kwenye maeneo yao, wajiunge kwenye vikundi ili waweze kufikiwa na kunufaika na Mfuko huu.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Sheria inataka kila anayetengeneza chumvi lazima achanganye na madini joto *(iodine)* na usipofanya hivyo unavunja sheria. Sasa hivi watengenezaji wadogo wa chumvi wanahangaika wanatafuta madini joto hayapatikani, wamenituma mimi kama Mbunge, nimeshafika pale kwenye Idara ya Madini mara mbili sipati madini joto. Je, Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje madini joto yapatikane ili tusivunje sheria? (*Makofi*)

(b) Jibu la msingi linasema kwamba watengenezaji wa chumvi wadogo huwasiliana na Idara za Madini Singida na Manyoni sasa ili kuwapunguzia safari za kwenda huko na gharama; anaweza akatujulisha masharti ya msingi ili na sisi Wabunge tukawajulishe wachimbaji wadogo wa chumvi ili waweze kupata mikopo ya fedha na vifaa vya kutengenezea chumvi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hizo sheria si unawagawia tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapteni Chiligati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba; ni sharti la msingi kuchanganya *iodine* kwenye chumvi inayozalishwa ili iweze kutumika na binadamu. Kwa sababu kutokufanya hivyo, kunasababisha maradhi kama ya udumavu wa akili na kuvimba tezi na kadhalika.

Kwa hiyo, *UNESCO* imepitisha hili kwamba, lazima chumvi iwe na *iodine*. Tatizo hili tumelikuta tulipokwenda kwenye ziara Kilwa kwa Mheshimiwa Mtanda na Mtwara na pia tulipokwenda Manyoni na Bahi, kwa sababu haya ndiyo maeneo ya uzalishaji mkubwa wa chumvi kwa wachimbaji wadogo.

Tumekubaliana kwamba, Serikali ifanye mkakati kwa hivi sasa *iodine* ina gharama kubwa, kwa kipindi chake kile inakuwa kama shilingi 45,000, wameombwa wapewe kama nusu ya gharama iwe kama shilingi 22,000 na nyingine iwe ni ruzuku ya Serikali. Ninaomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge na wazalishaji wengine wa chumvi kwamba, jambo hili linafanyiwa kazi na tunakwenda kuangalia namna ya kulipatia ufadhili ili waweze kuboresha chumvi ili iweze kukidhi mahitaji ya *human consumption*.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, nilichosema ni kwamba, wakiwa kwenye vikundi wanaweza kufikiwa na Mfuko wa Wachimbaji wadogo. Sasa mahitaji pale Singida pana Kampuni ipo London, ambayo inawasilisha wachimbaji wadogo, lakini imejikita zaidi kwenye dhahabu, tunawaelekeza kwa kushirikiana na *GST* kwa sababu pia pana masuala ya teknolojia kwamba, waangalie vifaa vinavyohusu chumvi, ambavyo ni tofauti kidogo na vile vya uzalishaji wa dhahabu.

Tumeshawaelekeza kwamba, Mfuko huu ujielekeze kwa wachimbaji wadogo kwenye maeneo ya Manyoni na Bahi, lakini pia maeneo ya Lindi na Mtwara.

Na. 277

**Hitaji la Umeme – Mlalo**

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI** aliuliza:-

Je, ni lini Tarafa ya Mtae na Umba katika Jimbo la Mlalo zitafikishiwa umeme wa Gridi ya Taifa, kama ilivyokwishapangwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Jenerali Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kupeleka Umeme Tarafa ya Mtae, katika Vijiji vya Majengo, Makose, *Rangwi Mission*, Rangwi Mjini, Shagayu, Sunga, Mpanga, Kibaoni, Mponde, Marungu, Zaghati, Manolo na Mtae, utahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kV 33, yenye urefu wa kilometa 35, pamoja na mtandao wa njia ya umeme msongo wa kV 0.4, ambazo ni msongo wa usambazaji umbali wa kilometa 12. Vilevile Mradi huu utahusisha ufungaji wa transfoma kumi, ikiwa ni transfoma nane za KVA 50 na mbili za KVA 100 kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kupeleka umeme Tarafa ya Mtae ni shilingi bilioni moja katika tathmini iliyofanywa. Mradi huu umechelewa kutekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Hata hivyo, Serikali inaendelea na juhudi ya kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuupatia utekelezaji Mradi huu. Matarajio ya Serikali ni kuwa, utekelezaji wa Mradi huu wa umeme utaanza kwa kuwasiliana na *REA* kulingana na namna watakavyokuwa wanapokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Lunguza, Mng’aro na Mnazi, ambavyo vipo kwenye Tarafa ya Umba, bado haijafanyika. Hata hivyo, kwa kuwa ni dhamira ya Serikali kuhakikisha vijiji vyote nchini vinapatiwa umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, punde fedha kwa ajili ya tathmini ya upelekaji umeme katika Tarafa ya Umba zitakapopatikana, kazi hiyo ya tathmini itaanza mara moja.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi huu ulikuwa utekelezwe zaidi ya miaka kumi iliyopita na Wananchi katika maeneo yale wamekwishaweka *wiring* zao na vilevile mwaka jana wakati wa Uchaguzi, Mheshimiwa Kikwete, aliwaahidi Wananchi wa Tarafa ya Mtae kwamba sasa umeme utafika:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa ahadi gani kwa Wananchi wa Mtae badala ya kusema tu kwamba fedha zitakapopatikana?

(b) Katika Kijiji cha Rangwi kuna maporomoko ya Mto Umba, ambayo yana maji ya kutosha kabisa. Je, Waziri atakubaliana nami kutuma timu ambayo itakwenda kufanya utafiti jinsi gani tunaweza tukatumia maporomoko yale? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mradi wa Mtae umechelewa kama miaka kumi, lakini lazima niseme ukweli kwamba, kuna Miradi mingi ya namna hiyo, ambayo imechelewa katika kipindi hiki na ndiyo maana tukaanzisha *REA* ili kuipatia utekelezaji wa haraka. Kwa bahati mbaya, Mradi huu ulikuwa umekadiriwa uanze utekelezaji mwaka jana.

Kati ya shilingi bilioni 50 ambazo zilikuwa zimekadiriwa ziwafikie *REA*, walipata kama asilimia 25, kwa hiyo, Miradi mingi ambayo ilikuwa inaanza imechelewa. Vilevile kule Chanika Kibaoni, kwa Mheshimiwa Dkt. Kigoda, kuna Miradi mingine na Korogwe kwa Mheshimiwa Majimarefu na Kilindi pia kuna miradi mingine imechelewa.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba, kwa ujumla, kuna Miradi kadhaa kwa Wana-Tanga pale, ambayo imechelewa. Ninaomba nimuahidi kwamba, mwaka huu *REA* inaomba shilingi milioni 58, kwa kadiri fedha zitakavyoingia. Tumekubaliana pia ndani ya Serikali kwamba, tuanzishe vyanzo vingine vya kusaidia kama bilioni zingine 50, 60, ambazo zitasukuma Miradi hii ya haraka, kwa sababu pia pana mikakati na kama ulivyosema pana Ahadi ya Rais, lakini pia kuna mikakati ya kuongeza usambazaji kwa Watanzania ili kufikia lengo la Watanzania wengi zaidi ya wanaopata *access* ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hili la Kijiji la Rangwi, ninaomba nimthibitishie Mhesimiwa Mbunge kwamba, kama tulivyofanya kwa Vijiji vya Kasulu na Kibondo na Namtumbo, ambapo tumesema pana vyanzo vya maji, tutaomba *REA* waende wakaifanyie tathmini waangalie *economic viability* kama inawezekana kwamba, itazalisha umeme kwa gharama nafuu na ambao utawafikia watu wengi zaidi; hii inaweza ikawa ni bora zaidi hata kuliko kupeleka umeme wa gridi. Ninashukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Hili nililomwagiza Naibu Waziri wa Fedha, linatokana na Kanuni ya 45(3), ambayo inasema: “Iwapo ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika Kikao kingine cha Bunge.” Kwa hiyo, ni kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

Angalieni *Order Paper* yenu, kila mtu anayo, leo hii ninyi Waheshimiwa Wabunge, mmeuliza maswali mafupi katika *Order Paper* yenu. Hivi ndiyo inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni. Tunapoendelea na kipindi hiki, *TBC* wanatangaza *live*; wewe unapoleta swali lako lina *page* nzima hivi wale wanasomaje mpaka wakupate ili upatiwe majibu, majibu ya Waziri yakuwa *quoted live*, lakini inabidi wasome haraka sana swali lako.

Kwa hiyo, mkiangalia leo maswali yameulizwa kwa kifupi, hata swali la Mheshimiwa Leticia lingeweza kutosha *paragraph* moja tu; lakini amenyumbulisha wee mpaka linajaa *page* nzima isiyo rasmi. Someni vizuri, ulizeni maswali mafupi. Wenzenu wanapopitisha wanasoma, wakati Waziri anatoka hapa anakujibu ndiyo wanasoma swali lako. Sasa umemwandikia *page* nzima! Kwa hiyo, jifunzeni hilo pia tuweze kwenda na utaratibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo nina wageni wachache. Kwanza kabisa, ninayo furaha kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Uganda, ambao wako hapa. Nitawaita mmoja mmoja ili msimame, ninyi ni wageni maarufu kwetu sisi. Yuko Mheshimiwa Cecilia Ogwai, Kiongozi wa Msafara; Mheshimiwa Epetait Francis; Mheshimiwa Sassagah Isaiah; Mheshimiwa Mutumba Sebuliba; Mheshimiwa Jack Wamanga Wamai; Mheshimiwa Mpuuga Mathias; Mheshimiwa Ssemujju Ibrahim Nganda; Mheshimiwa Ebil Fred; Mheshimiwa Aol Betty Ocan; na Katibu wao, Ndugu Nabitaka Barbara. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Hawa Waheshimiwa Wabunge, kwanza, wamekuja kuliangalia Bunge letu na kuona mambo yetu; lakini zaidi wamekuja kujifunza jinsi Kambi ya Upinzani katika Bunge inavyofanya kazi. Kwa utaratibu huo huo, hata sisi tutawapeleka hawa wa kwetu wakaone Kambi za Upinzani, zinavyofanya kazi sehemu nyingine. Tutafanya na sisi hivyo hivyo, kwa sababu kama tulivyoeleza toka mwanzo, lengo la kuwa na Kambi ya Upinzani, kwa sababu hawa wanatarajiwa kuchukua Serikali na Kambi Tawala inatakiwa ibakie kung'ang'ania Serikali yao. Hakuna uadui wala chuki, wala vyovyote vile; ni sisi ni Wabunge wa pamoja. Kwa hiyo, hilo ningependa sana lijulikane, kwa sababu kuna wananchi wengine wanaanza kufikiria kwamba, ukishakuwa Kambi ya Upinzani watu wasiongee, wasifanye nini; hiyo siyo sahihi. Hapa tunabishana humu humu tu basi. Tukitoka tunashikana mikono, tunakunywa chai, tunaendelea na kazi kama kawaida. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninadhani mtajifunza mengi kwa wenzetu kama vile wao wamekuja kujifunza kwenu, lakini muwafundishe ya kweli kweli.

Tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kutoka Jimboni kwake. Wazee wote msimame mliko huko. Tunafurahi kuwaona hapa, Mheshimiwa Waziri, ametumia faida ya Jiografia, asingeweza kuwaleta wote hapa. Faida ya jiografia tu wewe ungewatoa Njombe wote hawa ingekuwa kazi. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi wanne ambao ni Viongozi wa *Higher Education Conference* Dodoma, wako huku nyuma; ahsante sana. Tunawatakia kazi njema. Tuna wanafunzi na walimu 50 wa Shule ya Sekondari ya Makole Dodoma. Hapo mlipo msimame na walimu. Ahsante, tunawatakieni masomo mema. Tuna wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Biashara *(CBE)* Dodoma; wako wapi watalaam hawa? Ahsante sana, tunawakaribisha ninyi jirani zetu hapa. Tuna wanafunzi 50 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Dodoma nao wasimame walipo. Ninadhani wamekosa nafasi wako *basement*.

Pia tuna wanafunzi 50 na walimu wao kutoka Shule ya Zanaki Dar es Salaam; karibuni sana. Someni vizuri, hiyo shule ina sifa zake, kwa hiyo, mui- *maintain* sifa ya shule hiyo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha St. John's, wataalam wengine wa St. John's majirani; ahsante sana. Mnazo sababu zote za kuja hapa. Karibuni sana.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba 227.

Nina tangazo la Mheshimiwa Idd Azzan, huyu ni Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anasema wanamichezo wote wa mpira wa miguu na *netball*, mnaombwa kuhudhuria mazoezi kwa wingi ili kujiandaa vyema kwa michezo ya Jumamosi tarehe 23 Julai. Michezo ya Jumamosi itahusisha michezo miwili dhidi ya *NMB* na *Tanzania Stars Veterans* na itachezwa kwa mtindo wa Bonanza. Tafadhali, tujitoe wote ili tuendeleze ushindi wetu wa kawaida. Maana mkishindwa hapa mimi sitatangaza, kwa hiyo, ni vizuri mkaendelea kushinda.

Nina tangazo lingine linatoka ofisini kwangu kwamba, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imeleta wataalam kwa ajili ya kupima afya za Wabunge, kuanzia leo tarehe 20, ambao wapo katika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge, tuna huduma ya kupima hapa, kwa hiyo, tumieni nafasi hiyo kwa sababu ni vizuri sana kufanya hiyo shughuli. Ninaomba muitumie nafasi hiyo.

Tangazo lingine kutoka Ofisini kwangu pia linasema, Waheshimiwa Wabunge wote, mnaalikwa kuhudhuria Maonesho ya Uzinduzi wa Meza ya Maabara inayohamishika ya kufundishia masomo ya sayansi kwa vitendo katika Shule za Sekondari. Uzinduzi huo utafanywa leo Jumatano tarehe 20, kuanzia saa saba na nusu mchana, katika Viwanja vya Maonesho vya Bunge. Mgeni Rasmi katika shughuli hiyo fupi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutembelea Maonesho hayo yatakayoendelea hadi tarehe 22. Kwa hiyo, uzinduzi unafanyika leo saa saba na nusu, lakini maonesho yataendelea hadi tarehe hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo; tunaendelea. Hii hotuba tunayoendelea hivi sasa, tutamalizia kuichangia saa saba ili tupate muda mrefu jioni.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, akishamaliza mimi sijaelewa na anayesema sijamwona. Haya Mtema maana hii miongozo siipendi sana.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninatumia Kanuni ya 68(7). Ninaomba mwongozo wako, kutokana na kipindi kilichoisha cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maswali yanayohusu watu wenye ulemavu huwa ni adimu sana Bungeni na kutokana na utafiti wangu huwa yanaulizwa mara moja kwa mwezi. Liliulizwa mwezi wa sita na sasa hivi limeulizwa moja. Ninaomba mwongozo wako, kwa kuwa alipouliza mara ya mwisho, Mheshimiwa Margareth Mkanga, hukuruhusu swali lolote la nyongeza kutoka kwa Wabunge wengine. Leo hii asubuhi imetokea tena Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, ameuliza swali la msingi hujaruhusu pia swali la nyongeza kutoka kwa Wabunge wengine. Ninatambua kwamba, unaongozwa na Kanuni na muda, lakini kuna swali lililofuata baadaye ulimruhusu Mheshimiwa Subira na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani aulize. Ninaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwongozo ni rahisi sana, mimi nina *manage* Ukumbi. Sasa aliposimama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Kanuni inasema akisimama tu inabidi wengine wote niwaache. Kwa hiyo, ndiyo ninafuata hivyo. Tunaendelea. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu ndani ya nyumba hii. Tunao wachangiaji kama ifuatavyo; Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii adimu hapa Bungeni ili niweze kuwa mshiriki wa kuchangia katika Hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka mzima hadi siku ya leo. Nina machache; la kwanza kabisa ninalotaka kuanza nalo ni kuipongeza Hotuba ya Waziri.

**SPIKA:** Wanaotoka nje ya Ukumbi, watoke kwa utulivu ili watu tuendelee na kazi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Katika hali halisi na jinsi alivyoiandaa Hotuba hii, niaamini itaungwa mkono mwisho wa safari yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuidodosa Hotuba hii, ninapenda nizungumze yafuatayo: La kwanza, ninataka kuongelea suala zima la shule zetu za msingi, jinsi gani zinavyoathirika na watoto kuendelea kukaa chini kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna misemo mbalimbali ambayo iko katika Wizara hii; wanasema elimu ni ufunguo wa maisha; elimu ni nuru; elimu haina mwisho; lakini je, kweli elimu haina mwisho wakati mtoto anapoendelea kukaa chini? Elimu ni mwanga, walimu wanaendelea kudai madai yao. Elimu ni ufunguo wa maisha, wakati shule zetu za sekondari hazina walimu wa kutosha. Misemo hii ina maana gani? Tuitafakari misemo hii na tuiweke katika utekelezaji. Ninashindwa kabisa kuelewa pamoja na kwamba, mimi siyo mwalimu, lakini ninaamini kabisa mtoto anapojifunza akiwa amekaa chini, anatofautisha maisha haya kwa namna gani kwamba sasa hivi niko shuleni au niko nyumbani?

Anapokuwa shuleni mazingira lazima yabadilike. Mtoto akizoea kukaa chini, tena anakalia jiwe, mwandiko wake ukoje? Shule ya Msingi ndiyo hapa anapoanza kuandika A, B, C, D, akiwa kwenye jiwe. Mimi kweli ninajisikia vibaya; ni Serikali yangu kwa maana ya chama changu, lakini katika hili bado hawajanitendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini mtoto anapokaa chini wakati anaandika au akisoma la kwanza mpaka la nne akiwa anakaa chini, sidhani kama tunamjengea uhalali wa kisaikolojia ya kweli katika elimu. Anaharibika hata kisaikolojia. Atajua kabisa kwamba, ilimradi nimeanza la kwanza ninakaa chini, labda na Chuo Kikuu nako wanakaa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuwajali watoto hawa tuwatoe chini. Mimi nilishashuhudia mtoto anakaa chini anaandika, tulipompelekea dawati alishindwa kulikalia na kuandika. Alinyanyua mguu wake akaweka sambamba na hapo alipokalia ile fomu, akaendelea kuandika juu ya paja kumbe ana dawati. Wanaathirika watoto hawa. Tufike mahali tufikirie sasa kuwatoa chini watoto hawa.

Tuna misitu yetu; mimi huwa ninajiuliza hii misitu yetu ni ya wafanyabiashara tu? Tuna misitu Kanda ya Ziwa huko inaitwa Buhindi; kuna misitu mingine Kusini na Miziro inatajwa; hivi hatuwezi kutoa *tender* kwa watu maalum kwa awamu wakatengeneza madawati na Serikali nayo ikatengeneza madawati na wahisani nao wakaendelea kutupatia madawati tukaendelea kuwatoa watoto chini jamani? Muda mrefu sasa, ninadhani watoto wetu wanatusikia, itafika mahali watatujibu, watatuambia tumechoka kukaa chini. Kweli mimi ninasema kwa uchungu, ninajua ni Serikali yangu, lakini hebu tufike mahali sasa tuwatoe watoto chini.

Bajeti ijayo kama tutakuja kukaa humu humu, Mungu akitujalia uzima, hebu tufike mahali tuzungumzie ufanisi wa kuwatoa watoto chini uko asilimia gani, tuendelea kuwatoa watoto chini. Tutumie misitu yetu. Ninarudia; tutumie uwezo wetu wa kifedha, Wizara hii iwaze kwa undani zaidi kuwatoa watoto kukalia chini, ikibidi tuwaite hata Wakurugenzi; hivi kweli ikitolewa amri kwamba kila Halmashauri itafute mbinu ya kuwatoa watoto chini utaona wataweka mashindano ya Wakurugenzi. Tutawapongeza wale watakaoweza kulifanikisha zoezi hili. Wakati mwingine ninadhani Serikali inanyamaza mno, tuwatoe watoto wetu chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kuhusu madai ya walimu. Ninashukuru leo kulikuwa na swali la Mheshimiwa Mbunge wa Singida; Waziri amejitahidi amelijibu vizuri. Hakutamka kwamba, madeni sasa tutayamaliza wakati fulani, tunaongelea madai yao sugu ya miaka mingi, walimu wametuvumilia. Mimi huwa ninalinganisha mtu anayedai na mdaiwa. Unajua huwa kipo kitu hamkijui, mtu mkishapeana kitu, kwa mfano, mtu anadai kitu chake, kwanza, huwa kuna hofu mnashindwa hata kuwa mnakutana kwa amani. Unaanza sasa kumwogopa mwenzio. Ukishamwona anakuja yule anayekudai, unainama uso huwezi kumwangalia ana kwa ana kwa kuhofu kwamba, labda atazungumzia deni lake.

Mtaendeleo hivyo, mbele ya safari kunaingia chuki, unastukia kunajengeka chuki kati ya mtu anayedai na mdaiwa, sasa hata salamu inakuwa nguvu.

La tatu, mwisho kunakuwa na kuadhibiana, kunakuwa na adhabu kabisa. Kwa hiyo, ninaomba tujenge urafiki na walimu hawa jamani, tuwalipe madeni yao, tutoe hofu, tutoe woga, tutoe chuki, tujenge urafiki na walimu hawa ni jeshi kubwa mno, kama tutajengeana chuki tuombe tuwe marafiki nao.

La nne, katika hili, hawa walimu wanaendelea kudai usafiri, ninaomba tuwape uhuru wa kukopa; wengine wako mbali wa vijijini tuwapatie pikipiki. Juzi Mbunge Mheshimiwa Vulu, Mkwere huyu akasema anaomba pikipiki zigawiwe kwa walimu au wakopeshwe basi; hebu tulifikirie hili suala la walimu kukopeshwa pikipiki; wote wa mjini na vijijini, kwani wote wana shida. *Capitation* zao sasa hivi haziendi, wanasema wao hamuwapi hiyo hela anayopewa kila mwanafunzi. Kuna nini; tutauliza kwenye mafungu? Kwa nini hamuipeleki hiyo hela sasa hivi, hamuwapi kabisa hao watoto hela yao, ambayo ni haki yao. Enzi za Makweta, walikuwa wanapata nusu ya mshahara na walimu hawa. Hizo *system* zimeishia wapi; mbona tunapoingia sasa hivi tunafuta; tunatoka kuzuri tunakuja kubaya?

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba jamani katika mlolongo mzima wa Vyuo Shirikishi vya Elimu ya Juu, ambavyo vinatokana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Butimba nayo ilikuwemo. Hivi Mwanza sisi kila kitu hakuna tu? Ninaomba hilo wazo lilirudi la kuanzisha Chuo Kikuu Shirikishi Butimba. Butimba ina kila kitu, pale ni pazuri kabisa kwa Mwanza. Ninawaomba, pale pana mabweni, pana nyumba za walimu, maabara za kutosha na *computer* nzuri. Kuna chuo kingine cha Miziki na Michezo,

ambacho ingawa ni cha Diploma; kwa nini sasa kisikamilike ikawa wanamalizika na *degree* hapo hapo? Ninawaomba hicho Chuo hebu kifufueni, tena Maprofesa walishafanya *survey* pale wakasema kinatosha na eneo linatosha. Butimba Mwanza jamani, kwa nini kila kitu Mwanza mwisho?

Kitakuwa Chuo cha Kanda, siyo Watu wa Mwanza tu na wa Kanda ya Magharibi, wanapaswa waingie pale. Ninaomba jamani hicho Chuo kifikiriwe na kiweze kuzungumzwa, kama si sasa basi kiwemo katika mawazo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye Bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu kwa kunipa afya njema.

Ninaunga mkono Bajeti ya Kambi ya Upinzani, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. Vilevile ninawapongeza Wanawake wa Tanzania, kwa kazi nzuri wanayoifanya, mara wanapopata watoto ndiyo wanakuwa walimu wa kwanza kuwafundisha mpaka wanajua kuongea, kutamka na baada ya hapo, Serikali inachukua majukumu yake ya kuwaelimisha kuanzia shule za awali mpaka Vyuo Vikuu na hatimaye Taifa linapata watu wenye kufanya kazi. Ninawapongeza Wanawake wa Tanzania, kwa sababu kazi yao ni nzuri. Inapofikia sasa kwa Serikali kuwajibika katika kuwapatia elimu hawa watoto, hapo ndiyo kunapokuwa na matatizo.

Katika ukurasa wa tano wa Hotuba, suala zima la majukumu ya Wizara yamebainisha wazi kwamba, ni pamoja na kuweka viwango bora vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, elimu ya sekondari, elimu ya watu wazima, elimu ya nje, elimu rasmi, elimu ya ufundi na mafunzo na Chuo Kikuu. Ukiangalia ni namna gani sasa wanatekeleza haya majukumu yao, ndiyo hapo mtihani unapokuja. Haiwezekani, Wizara hii pamoja na kujua majukumu yake, lakini majukumu haya inayaweka pembeni, wanafumba macho, hawatengenezi bajeti ambazo zinastahili mpaka kuondoa malalamiko kwa walimu na wanafunzi kila kukicha haya ni matatizo. Hii inadhihirisha kabisa, hii Wizara imeshindwa kutekeleza majukumu yake ingawa wameandika kwenye vitabu vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kipindi kirefu sasa kila anaposimama Mbunge awe wa CCM, awe wa Upinzani, anatoa malalamiko ya walimu. Katika vyombo vya habari, umesikiliza wiki hii hii wanaona kabisa hii Wizara inapitishwa Bajeti yake; na ninaomba Waheshimiwa Wabung, kwamba, hii Bajeti isipite kwa sababu Wizara hii haitekelezi kwa makini madai ya walimu na haitoi majibu kwa walimu kila kukicha. Inapokaribia wakati wa uchaguzi, ndiyo wanajifanya wapole kwa sababu wanawatumia walimu hawa katika kusimamia uchaguzi, wanaposhindwa uchaguzi shughuli inaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu mtindo haufai katika kutekeleza majukumu yenu. Iwapo mmepata madaraka, ni vyema sasa mkatumia madaraka yenu katika kutekeleza

majukumu yenu. Kila Wizara ina wajibu wake, lakini Wizara ya Elimu, kwa kipindi kirefu haitekelezi majukumu yake kwa vitendo; sana sana wanapoteza kodi za Watanzania kwa kuandika maandishi, kuchapisha vitabu na kuvigawa humu katika Bunge na maeneo mengine. Majukumu hayo yamekuwa ni nadharia siyo ya vitendo. Mmekuja kwa upole kwa sababu mnataka mpitishiwe bajeti yenu. Kwa kweli siungi mkono hii bajeti mpaka mtoe majibu ni lini bilioni 29.2 wanazodai walimu kama madeni; mtatuonesha mnazitoa lini na muwe na *deadline;* lini mwisho ndiyo muanze bajeti nyingine.

Haiwezekani ulete bajeti ya mwendelezo wa mwaka huu wakati mwaka wa nyuma hujalipa. Lipa deni upate kupewa bajeti yako mpya. Onesha kwenye bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuzungumzia suala zima la elimu ya awali. Hii elimu ya awali iko wapi; inapatikana vipi? Hawa watoto hii elimu ya awali wanaipata humu madarasani na utupe takwimu shughuli ngapi zipo Tanzania za msingi na shule ngapi zina elimu za awali, walimu hawa wanapata stahili gani, elimu ya watu wazima.

Unaiombea hiyo bajeti, watu wazima hawa ambao sasa hivi wanaongezeka kwa kutokujua kusoma na kuandika na wakati Wizara ipo, Serikali ipo, kodi mnakusanya; kwa nini ongezeko linaongezeka; miaka 50 ya Uhuru watu wasiojua kusoma na kuandika wanazidi kuongezeka? Hamwoni kwamba mmeshindwa? Vyema mkasema kwamba, mkubali yaishe, tumeshindwa wapishe watu wanaoweza ili waongoze. Haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya watu wazima inapangiwa mafungu, lakini ukienda huko inakotolewa hiyo elimu hewa hakuna kitu. Hizo hela zinafanya kazi gani? Kuna walimu ambao huwa wanajitolea kwenye shule zetu za msingi, wanaofundisha hiyo elimu ya watu wazima mishahara hawapewi wana madai kibao, wala hawahesabiki. Kwanza, hata hawa kuandamana hawaandamani, wanashindwa hata kudai kwa sababu ni wale vijana ambao wanajitolea, hawajui wadai haki zao wapi. Ukitangaza hapa wanaweza wakaandamana nchi nzima na kuona maandamano hayo ni haki yao ya msingi kudai haki zao.

Marekani, nchi ambayo inatupa msaada, mwezi Machi, 2011 waliandamana wakielekea Ikulu ya Marekani kudai kupinga mfumo wa afya katika Nchi ya Marekani. Iweje leo Watanzania wasiandamane; wakiandamana ooh amani inavunjika; amani bila haki, lete haki watu wataacha kuandamana. Hii ni haki ya msingi, wanapeleka ujumbe kwa watawala kwamba, hatutaki kunyanyaswa wala kubaguliwa. Kwa hiyo, ni vyema kama ni Serikali sikivu, isikie vilio vya Wananchi, isikie vilio vya Walimu na Wanafunzi. *(Makofi)*

Ninakwenda Chuo Kikuu Dodoma. Leo Chuo Kikuu cha Dodoma inavyotangazwa kwamba, wanafunzi wameshindwa kwenda *field*, hakuna mwanafunzi anayemaliza Chuo Kikuu Dodoma atakayepata ajira, kwa sababu waajiri wanahitaji

wanafunzi waliosoma darasani na waliokwenda *field*. Kwa hiyo, mnawatangazia hali ya hatari Wanafunzi wa Dodoma, wapeni stahiki zao wanazostahili.

*SAUT*, Tawi la Mtwara, wamekwenda *field* kuanzia mwezi wa saba mwanzoni, Serikali iliwaahidi itawapa hela, halafu kibaya zaidi zile *field* wale kule wamekuwa wapole kwa sababu wako pembezoni mwa nchi. Wamekuwa wapole, wamekwenda *field*, lakini mpaka leo ninavyozungumza, hawajapewa hizo hela. Hivi wale watoto waishi vipi? Kuna watoto wa kike, watoto wa kiume, mnataka wawe akina nani hao? Hamwoni kama mnawapeleka wakapate UKIMWI kwa sababu ya kujikimu? Mnadhalilisha usomi katika nchi hii. Enzi ya Mwalimu haikuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya elimu ndani ya nchi yetu ni Janga la Taifa.

**SPIKA:** Enzi ya Mwalimu, waliokuwa Chuo Kikuu walikuwa wachache. Endelea! *(Kicheko)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na Walimu kuwa Chuo Kikuu wachache na wanafunzi walikuwa wachache na hela ilikuwa chache. Sasa hivi mnachimba madini, mnasafirisha twiga nchi za nje, mnauza *uranium*, mnafanya kila ghasia ndani ya nchi hii. Mnakusanya hela nyingi, ni vyema hela mkazitumia kwa kuelimisha Watanzania. Uzeni mashangingi, toeni posho za ajabu, pelekeni hiyo hela kwenye elimu ili tuwanufaishe Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nchi hii tunadai uhuru, Wananchi walikuwa 9,000, madini yalikuwa hayachimbwi. Sasa hivi Wananchi karibuni milioni 40 madini yanachimbwa. Kwa hiyo, msifananishe na wakati wa Mwalimu, alifanya kazi yake. Sasa ni wajibu wenu, kama mnashindwa kaeni pembeni, muwapishe wale tunaoweza tuchukue nchi tuongoze nchi hii. Siyo kutumalizia madini, halafu na elimu haipo. Matatizo lukuki, haiwezekani.

**SPIKA:** Acha aendelee kuongea.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Hiyo ndiyo demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nichangie kwenye upande wa elimu hususan tabu wanazopata walimu wetu na udhalilishaji wanaofanyiwa. Kwa nini ninasema udhalilishaji? Enzi ya Mwalimu, walimu walikuwa wanaheshimiwa. Enzi ya sasa walimu hawaheshimiwi. Kwa sababu leo walimu wanaandaa migomo, waandaa maandamano, elimu inaporomoka. Hawafundishi vizuri, hali inakuwa mbaya. Nimeshuhudia mwenyewe nikiwa Mkoa wa Tanga kwenye Kamati ya *LAAC*, walimu walikuja waliacha madarasa siku ya kazi. Waliacha kazi za kufundisha walipoona Kamati ya *LAAC* walitufuata jamani sisi tangu tulipoajiriwa, wengine hawakutoka Vyuo Vikuu wadogo, wengine walikuwa na miji yao wametokea Kigoma, walienda kupata elimu lakini wamepangiwa Tanga.

Leo hela ya uhamisho imekuwa ni mgogoro, wakienda kudai hela ya familia, eti Mkurugenzi anawajibu ninyi ni watoto tu! Hivi walimu wote wanaoajiriwa nchini ni watoto? Hii nchi tunaipeleka wapi? Mnawadhalilisha walimu wetu, wanakuwa hawaheshimiki katika jamii. Hata wanafunzi wenyewe wengine wana pesa kuliko walimu. Elimu itaendelea vipi? Hamwoni kama mnadumaza elimu? Hivyo basi; ni vyema tukawapa heshima yao walimu wetu, wakaonekana katika jamii kama wale walimu wa zamani, walimu wa sasa wana matatizo makubwa na kama hii Serikali ni sikivu ni bora ikasikia ikajipanga upya.

Ikaangalia ni namna gani ya kuwahudumia walimu, siyo kuwabeza beza na kuwatumia wakati wa uchaguzi, unapomalizika uchaguzi mnawafanya kama makarai, mnawatumia wakati wa kuingia madarakani, mkishaingia madarakani mnatupa karai, linatumiwa wakati wa ujenzi. Ujenzi ukiishamalizika karai linatupwa mbali hata sebuleni halikai. *(Kicheko/Makofi)*

Tuwaenzi walimu wetu. Lazima tuone kwamba, walimu ndiyo kila kitu. Hakuna daktari, hakuna nani bila walimu. Bora tuboreshe majengo yetu na miundombinu. Leo katika hii hela wanayosema hapa kila mwanafunzi wa sekondari anapata 25,000, mwanafunzi wa shule ya msingi anapata dola kumi; ukienda katika hali halisi ya vitabu, utakuta kila mwanafunzi anapelekewa shilingi 3,000. Hii nini? *(Makofi)*

Hizo hela nyingine ziko wapi? Tuambieni hizo hela huwa mnazipeleka wapi? Utasikia vivunge, vivunge; vivunge vipi? Wizara ya Elimu imejipanga vipi katika kupeleka hii elimu ya TEHAMA huko katika vijiji vingine hakuna umeme, hakuna maji, hakuna chochote. Tuwape miaka mingapi ili mtekeleze hayo mnayoyasema katika vitabu?

Hali ya nchi ni mbaya, hali ya elimu ni mbaya. Kila kona ni kilio. Kwa hiyo, waruhusuni wanasiasa wenye uchungu na nchi hii, waandamane labda ndiyo mtasikia; lakini kututisha tisha oooh maandamano nini! Hamna, maandamano ni haki yetu. Hata Marekani waliotupa misaada Wananchi wanaandamana na sisi tutaendelea kuandamana ili msikie na hakuna njia yoyote ya kutusikiliza zaidi ya maandamano.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Ahsante.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Utaratibu gani huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kifungu cha 64. Nilikusikiliza sana Mheshimiwa Spika, unasema tuendelee.

**SPIKA:** Kifungu cha 64.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** 64(1)(f) na (g). Ninachotaka kusema kwa kifungu hiki Mheshimiwa Spika, kulingana na ushauri ulioutoa, nilitaka kuomba tu; jazba hizi, maneno makali, ya uongo na ya uchonganishi, tuyapunguze kidogo. Mimi ninafadhaika sana kwa kifungu cha (g), hawezi hapa Mheshimiwa Mbunge, kuwaita walimu makarai, haifai. Hawezi kusimama Mheshimiwa Mbunge akasema kwamba, Serikali inawatumia walimu halafu inawamwaga kama makarai. Hata mara moja, Serikali haijawahi kuwatumia walimu katika uchaguzi. Kama ni Tume ya Uchaguzi, inatumia tu watu wake, lakini kwa utaratibu unaotambulika kikanuni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninajua ni mpango mahususi, wanajipanga lakini umeshatoa tahadhari hapa kwamba, tunazungumza na *public* watuone watu tuliokomaa, tuzungumze lugha sahihi, tufikishe ujumbe sahihi bila kudhalilisha watu wengine. Kifungu hiki kimevunjwa sana na Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anachangia. Sisemi afute, lakini kama ulivyosema. tuendelee kuvumiliana. Tunamvumilia lakini jazba zipungue, tuseme maneno ya ukweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya huo ndiyo utaratibu ulioko kwa mujibu wa kanuni.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushuuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwa mchangiaji kwenye Hotuba hii ambayo ni muhimu sana, kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu na nitakayoanza nayo sikuyapanga kuanza nayo, lakini nadhani ipo haja …

**SPIKA:** Unaweza kuhama hiyo mashine, maana haisikiki. Sehemu ile kila wakati ina matatizo na iko sehemu nyingine hapa katikati ina matatizo, iangalieni wataalam.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninasema kwamba, ninataka nianze na mambo ambayo pengine sikuyapanga kuyafanya, kwa sababu nilidhani yanaeleweka. Tunatakiwa tuipongeze sana Serikali hii, kwa kazi kubwa iliyofanya kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ninataka niongee kwa takwimu, sasa kama kuna watu hawaoni waombe tuwasaidie. *(Makofi)*

Katika mahitaji ya madarasa Kitaifa kwenye Shule za Msingi yalitakiwa madarasa 985,000. *I mean* nyumba za walimu 985,000 zimeweza kujengwa. nyumba 3,874,000 kwenye Shule za Msingi. Katika madarasa, samahani kidogo hapa nirudie; madarasa yalitakiwa 198,607, Serikali imeweza kujenga madarasa 110,000 Kitaifa. Hayo siyo madogo ni mafanikio makubwa. Katika nyumba za walimu, zilitakiwa nyumba 197,519, zimejengwa nyumba 39,623. Haya siyo madogo. Kwenye Shule za Sekondari, yalitakiwa madarasa 70,102, Serikali imejenga madarasa 45,645. Nyumba za walimu zilitakiwa 61,904, zimejengwa 20,187. Haya ni mafanikio makubwa sana, ambayo tuna

sababu za kila aina kuishukuru Serikali. Imefanya hivyo pia kwenye suala la kuongeza idadi ya walimu na udahili wa wanafunzi wanaokwenda Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie, mtaalam mmoja aliwahi kusema kwamba, *if you want to plan for one year sow the seeds.* Kwamba, ukitaka ku-*plan* kupanga kwa mwaka mmoja panda mbegu. *If you want to plan for ten years, plant trees,* ukitaka kupanga kwa miaka kumi panda miti. *But if you want to plan for life time, develop a man.* Ukitaka kupanga kwa miaka mingi kwa maisha, mwendeleze binadamu. Hii ndiyo kazi inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Nne. Vilevile sishangai, kwa sababu wakati ninafanya *dissertation* yangu ya *Ph.D,* Profesa aliwahi kuniambia hivi; kazi ya kukosoa anaiweza kila mtu hata asiyekuwa na uwezo anaweza akakosoa, lakini kazi ya kufanya kazi siyo kila mtu anaweza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba Wananchi waelewe kwamba, kukosoa kila mtu anaweza, lakini siyo kufanya kazi. Haya mafanikio makubwa yaliyofanyika, tulitakiwa tuyaenzi na ndiyo Mwenyezi Mungu, katubariki ili tuweze kusonga mbele zaidi. Tukipuuza haya hatuwezi kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie sehemu ya pili. Nilikuwa ninaangalia Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nikaangalia takwimu za udahili wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati na Sekondari. Ukiangalia udahili wa Vyuo vya Elimu vya Kati, tumeusahau na tulikuja hapa tukakubali kwamba, tuondoe asilimia nne zilizokuwa kwenye *Vocational Training (VETA),* ziende kwenye kusaidia *higher learning institutions,* kwa maana ya mikopo. Serikali ikatuahidi kwamba, italeta mkakati wa namna ya kuongeza udahili wa wanafunzi Katika vyuo vya Kati ili kuona vijana wetu wanapata nafasi wanazohitaji.

Ninasema hivyo kwa sababu kwa sasa hivi udahili wa Vyuo Vikuu umefikia 118,000 mpaka hapa tulipo hivi sasa. Udahili wa Vyuo vya Kati na Vyuo vya hapa, nina maana Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya Elimu, kuna Vyuo vya Uganga kwenye Sekta ya Afya. Huduma za jamii kwenye mambo ya utalii, *tourism industry* na kilimo. Kwa hiyo, hili ni kundi kubwa sana ambalo ndiyo tunategemea hawa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne waingie kwenye lile kundi kwa kupata zile *skills* ili waweze kujiajiri au kuajiriwa.

Sasa hili kundi udahili wake mpaka hivi sasa ilikuwa ni 68,000. Sasa utajiuliza; tunajenga Taifa la aina gani kama udahili wa Vyuo Vikuu unakuwa mkubwa kuliko wa kundi la tatu ambalo ndilo linafanya kazi kubwa zaidi? Wenzetu Wajerumani, Wajapani na Wamarekani, wameendelea kwa sababu nguvu kubwa wameielekeza kwenye *labour force,* kuipa *skills* za kufanyia kazi na ndiyo maana wameweza kufanikiwa. Leo sisi katika idadi yetu ya milioni 44, nguvu kazi ya milioni 21 imewezeshwa kuwa na *skills* za kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa ninadhani hapa tukubaliane kwamba, Serikali ilete mkakati na iseme wazi kwamba, ina mpango gani wa kuona vyuo hivi nilivyovitaja, vinavyotoa stadi hizi, kwanza, vinaongezewa fedha katika vyuo vilivyopo sasa hivi na vilevile iwapo kuna upanuzi. Kwa mfano, Vyuo vya Ufundi, tumekuwa na Vyuo vya Arusha, Dar es

Salaam na Mbeya. Vyuo hivi sasa hivi vimeshaanza kutoa digrii, kwa hiyo, vinaacha *gap* ya *technicians,* ambayo ndiyo muhimu sana Kitaifa. Sasa je, Serkali ina mpango gani wa kufungua vyuo vingine vya ufundi ili ku-*cover gap* hili?

Ningeshauri kwamba, tuwawezeshe wenzetu wa *VETA* kwenye Vyuo vya Mikoa, uchaguliwe Mkoa mmoja kila Kanda kuwe na Chuo cha Ufundi, yaani *Technical College*, kwa ajili ya kuchukua hawa vijana. Hii ndiyo nguvu ya vijana walio wengi, ambao wanahitaji kuwezeshwa na hawa ndiyo wanaoweza kukuta baadaye malalamiko makubwa katika nchi yetu.

Niseme kwa wenzetu ambao wamezungumzia suala la maandamano kwamba, maandamano ambayo wanayafanya wao siyo maandamano yanayoitwa na Wananchi, yanatoka juu kwenda chini, lakini tukipeleka *skills,* vijana hawa ninaowasema wote zikapatikana, tutakuwa tumefanya jambo la maana sana. Tusipopeleka hawa, ndiyo watakuja kuanzisha maandamano ya kweli, siyo haya yanayosemwa na mwenzetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, hivi sasa vyuo vingi vimeanzishwa na kila chuo kinafanya tathmini ya mitaala yake kwa utaratibu wake. Hatujui sasa hivi Serikali inataka madaktari wangapi? Wahandisi wangapi? *Technicians* wangapi? Kwa hiyo, vitu vinakwenda shaghalabaghala. Kwa hiyo, ninashauri ifanywe tathmini kama ilivyokuwa zamani, kulikuwa na *manpower* ambayo ilikuwa inandaa tathmini kuna wataalam wangapi kila sekta. La sivyo, tunaweza tukaanza kutoa wataalam wa aina moja kwenye kila chuo. Tukifanya tathmini, itatupa nafasi ya Serikali kutekeleza Mpango wetu wa Miaka Mitano, ambayo imeonesha kipaumbele kwamba, itaekeleza kwenye kuandaa wataalam na teknolojia. Kwa maana hii, tunaweza tukavielekeza vyuo vyetu vi-*train* watu ambao wanaweza wakasimamia *resources* tulizonazo, ambazo leo tunalalamika kwamba, zinaibiwa kwa sababu hatuna wataalam. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilione hilo, ifanye tathmini kuwe na mtazamo wa pamoja wa takwimu unaoonesha mahitaji ya Taifa ya fani mbalimbali na zile ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, itabidi tuchague vijana *bright* wapelekwe nje zionekane kwenye takwimu hizo ambazo zitakuwa zimeandaliwa Kitaifa. *(Makofi)*

La nne, kuna suala la mfumo wa tuzo, *national qualification framework*; hili limeongelewa muda mrefu. Tuliliongelea humu mwaka 2007, tarehe 14 tumechangia humu na Serikali ikatuahidi kwamba, italeta mfumo huo mapema sana. Huu ni mwaka wa nne, mfumo huo bado tunaambiwa ndiyo unakamilishwa na tunaambiwa toleo la kwanza. Inashangaza, ninadhani siyo vizuri katika utendaji mahiri, *national qualifications framework,* ambayo hatugundui mpya, tuna-*cut* na ku-*pest* na kuangalia mahitaji ya nchi yetu isingechukua muda mrefu kama huo.

La tano, niiombe Serikali, tumekuwa tukisema kwamba, tuna upungufu wa wanasayansi, tunasema vijana wengi wanakwenda sekondari hawajui Kiingereza au

hawajui yale masomo ya sayansi. Ninadhani tumeacha kuwekeza zaidi kwenye Shule za Msingi.

Tuweke masomo ya sayansi zaidi katika Shule zetu za Msingi kuanzia la kwanza mpaka la saba. Watoto wasome zaidi masomo ya sayansi na wawezeshwe kwa vitendo, kufikiria baadaye kugundua; siyo mtindo uliopo sasa hivi ambao umeelekezwa kwenye mitihani zaidi na hauwezi kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo shule Tanzania ambazo zinatumia mtindo huo mzuri sana, unakuta mtoto wa darasa la tano, ana uwezo wa kupambanua mambo kwa sababu anajifunza kuwa mwanasayansi baadaye. *(Makofi)*

La mwisho, kwa kuzingatia mazingira magumu ya Wilaya yangu ya Makete, ipo pembezoni, kwanza, ninaishukuru Serikali kwa kutupa nyumba kumi za walimu ambazo sisi tulijenga *two in one* na baadaye tukawa-*accommodate* walimu 18. Serikali itusaidie fedha kwa ajili ya nyumba za Walimu wa Sekondari na itusaidie kuongeza mgao wa walimu na mabweni kwa ajili ya watoto wa kike ambao wanapata mimba, kwa sababu wanapanga mitaani. Ninadhani tukiyafanya haya, tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaiunga mkono hoja hii na ninaipongeza Serikali yangu sana; imefanya kazi kubwa. Wananchi waelewe tu kwamba, kila mtu anaweza kukosoa, hata asiyejua kusoma, anaweza kuyaona makosa; lakini kufanya mazuri, siyo wote wanaweza. Kwa hiyo, tuiunge mkono Serikali ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi hii. Ninaomba niseme kwamba, wakale wamesema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba niipongeze Serikali kwa kujenga Sekondari za Kata. Ninaipongeza pia …

**SPIKA:** Mheshimiwa Vullu, ninadhani unavunja Kanuni. Mheshimiwa Machangu, endelea.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, pia ipeleke wanafunzi wengi Vyuo vya Ualimu kwa ajili ya kufundisha shule hizi. Vilevile ninaipongeza kwa kurudisha michezo mashuleni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze na suala la ukaguzi. Ukaguzi kitaaluma mashuleni ni Idara ambayo inaonekana imetelekezwa. Ukaguzi unakagua ufundishaji wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Wapo walimu ambao wanakwepa ufundishaji hata zaidi ya asilimia 30 ya vipindi vyao. Wapo walimu ambao hawaandai hata vipindi; ukaguzi utasaidia kudhibiti utoro na ufundishaji hafifu mashuleni. Kwa mfano,

ukichukulia Shule za Msingi, Halmashauri za Wilaya zina vijiji vingi na kijiji kimoja inawezekana kina shule mbili au tatu za msingi; huyu Mkaguzi anakwendaje kukagua shule hizi zote bila gari wala pikipiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali sasa iiangalie kwa umakini Idara ya Ukaguzi. Hatuwezi kujivunia kwamba, tunataka wanafunzi wafaulu wakati hatufanyi *monitoring and evaluation* na ukaguzi ni aina mojawapo ya *monitoring and evaluation* kuona ni kitu gani kinafanyika mashuleni. Ninaomba turekebishe sheria, Idara hii ikae chini ya Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, *after all* wanafunzi wanapokuwa wamefanya mitihani vibaya, Mkurugenzi wa Halmashauri ndiyo anawajibika. Kwa vyovyote vile, hana sababu ya kutokuwaadabisha walimu ambao wanakwepa vipindi mara atakapokuwa amepata taarifa ya Mkaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo pia ukaguzi mashuleni, walimu inaelekea wamesahau majukumu yao; inatakiwa wanafunzi wanapokwenda asubuhi wapangiwe majukumu na mwalimu wa zamu. Yapo majukumu ya kusafisha madarasa, yapo majukumu ya kufagia *path ways* zilizopo shuleni, yapo majukumu ya kuokota makatasi kule shuleni, lakini pia kusafisha vyoo vinavyotumiwa na wanafunzi na walimu. Siku hizi walimu wamesahau majukumu yao, kuwaambia wanafunzi wafanye siyo kuwapa adhabu ni kuwafundisha. Mtoto huyu milele hatakaa asahau kwamba, kile choo chetu nyumbani inabidi niende nikakifagie. Kwa hiyo, ninaomba walimu wakumbuke majukumu yao na wayatekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo pia majukumu ya walimu kulea watoto mashuleni, kuangalia usafi wa miili yao wanapokuwa kwenye *parade* na kuangalia usafi wa mavazi yao. Yupo mwanafunzi anaweza kukaa mwezi mzima hajaoga na wewe ukimwangalia utamjua. Wapo wanafunzi ambao wanavaa mashati hata wiki mbili, tatu, bila kufuliwa! Hii ni kazi ya walimu, tunaomba Serikali iwakumbushe walimu watekeleze majukumu yao; namna hii pia tutakuwa tunawafundisha hao watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo pia malezi ambayo yanatakiwa yafanwe na wazazi. Mimi ninaamini kabisa kwamba, kulea mtoto ni kazi ya mzazi. Ninaamini kabisa kukaa na mtoto wa kike kumweleza kuhusu kutokujamiiana kabla hajamaliza masomo, kuhusu Janga la UKIMWI, ni kazi ya mzazi. Serikali itaangalia usalama wa mtoto, amani ya mtoto na haki za motto, lakini kazi ya kulea watoto ni ya wazazi. Ninaomba wazazi wachukue majukumu yao. Ikiwezekana tukawakumbusha wazazi hao kupitia kwa Maaskofu na Masheikh ili kwenye nyumba zao za ibada, wakumbushwe majukumu yao wazazi hawa; ni muhimu sana wazazi wawalee watoto wao na ni muhimu sana wawalinde. Mtoto anapokuwa anatoka shule saa kumi, lakini anarudi nyumbani saa mbili, kuna haja kubwa kabisa mzazi aweze kumwadabisha mtoto huyu na ajue anapochelewa anatoka wapi na hivyo ndiyo kumlea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niende kwenye suala la Shule za Walemavu. Zipo shule za walemavu, kwa mfano, Mkoa wa Kilimanjaro eneo la Njiapanda Himo katika Wilaya ya Moshi Vijijini, ipo Shule ya Watoto wenye mtindio wa ubongo na watoto walipelekwa pale wakiwa wadogo. Sasa hivi wale watoto wamekuwa wakubwa. Kuna

tatizo la chakula, hakuna walimu wenye vipaji *(Special Education),* kwa ajili ya kuwafundisha na kwa kuwa walipelekwa wakiwa wadogo, sasa wamekuwa wakubwa, lakini pamoja na ulemavu wao, wanahitaji kuwa na bweni lingine la kutengenisha wavulana na wasichana. Ninaomba Serikali iliangalie hili na ni vyema hizi shule zikawa zinatunzwa na Serikali kuwe na uhakika wa walimu na uhakika wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu *NGOs* ambazo zinasaidia kusomesha watoto yatima. Kama tunavyojua, kutokana na Janga la UKIMWI, watoto yatima wamekuwa wengi; zipo *NGO* nyingi zinafanya hivyo na ninaomba niwashukuru sana. Kwa mfano, kuna *NGO* moja Mkoani Kilimanjaro ya *Tanzania Wemen Research Foundation,* ambao wanasema kwamba, hata baada ya kusomesha hawa watoto, shule za *primary* za *private* na sekondari, wanapokuwa wanataka sasa hawa watoto kwenda Chuo Kikuu, inakuwa matatizo kupata mikopo. Kwa kuwa *NGOs* hizi zina *complement effort* ya Serikali, ninaomba sana niishauri Serikali, waziangalie vizuri na ikiwezekana wajue idadi ya wanafunzi ambao wanao ili watoto hawa waweze kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna shule ambazo Serikali ilizitenga wakasema ni Shule za Sayansi za Watoto wa Kike na kama nilivyosema, mojawapo ya hizo shule, ipo Mkoani Kilimanjaro. Shule ya Ashira, Shule ya Weruweru na Shule ya Machame, ambazo ninajua Viongozi wetu wengi wamesoma pale. Sasa ninaloliomba, shule hizi hazina walimu wa sayansi, hakuna walimu wa fizikia, hakuna walimu wa kemia wala hakuna walimu wa mahesabu! Kama kweli tunahitaji madaktari wanawake, kama kweli tunahitaji mainjinia wanawake na sisi Serikali yetu imeshapanga tunakwenda kwenye mpango wa 50/50, ninaiomba sana Serikali, iliangalie hili na ipeleke walimu wa sayansi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongeza nguvukazi katika Shule za Msingi na Sekondari; inawezekana kabisa tukaongeza walimu, hasa tukichukua wale waliostaafu tukawaajiri upya, wakapewa *contract* hata kama ni kwa ujira ambao ni mdogo, lakini wakasaidia kuongeza nguvukazi katika Shule za Kata kule kwenye mikoa. Mkoani Kilimanjaro, kwa miaka mitatu mfululizo, hakuna walimu wapya waliopelekwa. Vibali vya walimu wa kujitolea navyo vinachukua muda mrefu sana na walimu zaidi ya asilimia kumi wa Shule za Msingi, wapo wamestaafu mwaka jana na mwaka huu; ninaomba Serikali iliangalie hili ipeleke walimu.

Jambo lingine, ninaomba pia Vyuo Vikuu vyetu, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi na Chuo Kikuu cha Sokoine, wana mambo mazuri ambayo wanaweza kupeleka kwa wakulima wa mikoa waliyopo au mikoa inayowazunguka. Kwa mfano, Sokoine, wana miche mizuri ya miembe ya miaka mitatu, ambayo kila Mkurugenzi anabeba lori anakuja kuichukua. Ninaomba sasa wataalamu hawa watoke kidogo kwenye Mkoa waliopo au kweye vyuo, waende wakawaelekeze Viongozi wa Idara ya Kilimo walioko kwenye Wilaya, kwa ajili ya kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za walimu na *hostel* za watoto wa kike; ninaomba kwamba, mwaka jana Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya *Public Private Partnership;* inawezekana kabisa Wakurugenzi wa Wilaya wakagawa maeneo ya kujenga nyumba katika Shule zetu za Sekondari, wakawagawia Wafanyabiashara na Wananchi

wanaopenda kufanya hivyo, wajenge nyumba nafuu, ikiwezekana nyumba moja iwe na vyumba viwili, vikodishwe kwa shilingi 15,000. Inawezekana kabisa walimu wakapata nyumba kwa mtindo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba nilipongeze Baraza la Mitihani, kwa kuweza kudhibiti wizi wa mitihani. Ninalipongeza pia kwa kudhibiti matumizi ya *slips* na *result slip fake* katika maofisi. Sasa ninaomba urasimu wa kuchukua *slips* usiwepo kwa ajili ya kuwapunguzia wanafunzi hawa gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ninaomba Kidato cha II, mtihani wake ule ni wa kujaribu wanafunzi. Kumbeba mwanafunzi kutoka Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne; mwisho wa siku tutazalisha watu ambao hawawezi kutusaidia katika Taifa hili. Ninaomba Mtihani wa Kidato cha II urudishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Kwanza, ninawapongeza sana Wizara ya Elimu, kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa hotuba nzuri ambayo tunaamini sote kwamba, italeta maendeleo katika Wizara hii ya Elimu. Ninaomba nitoe wasiwasi wangu kwamba, nimekuwa Mbunge kwa miaka mitano iliyopita na huu ni wa sita; tunapokaa hapa Bungeni tunakuwa tukipitisha Bajeti ambazo Wizara inakuwa imejiwekea malengo kwenye vitengo mbalimbali na taasisi zake. Ninasikitika sana kwamba, mara nyingi wamekuwa wakishindwa kutekeleza yale ambayo wamekuwa wamejipangia kwa sababu Hazina wanakuwa hawatoi fedha kwa wakati, lakini bado hata fedha hizo wanakuwa hawatoi zote. Sasa ninashindwa kuelewa, labda tupatiwe msaada ili watendaji hawa wakae wakijua kwamba, fedha zao halisi zitakazokuja ni zipi na kwa wakati upi ili waweze kuji-*tune* kwa fedha hizo ambazo zitakuwa zinatoka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitoe wasiwasi wangu na dukuduku langu kwamba, ninashindwa kuelewa utekelezaji wa Wizara hii. Kwa maana ya kwamba, tunapochangia hapa wengi wamekuwa wakizungumza matatizo mengi ambayo yapo kwenye Idara ya Sekondari pamoja na Elimu ya Msingi; lakini sielewi tunamwambia Waziri yupi kwa sababu mambo mengi hasa katika suala la ugatuaji yamepelekwa TAMISEMI*;* sasa tunamweleza Waziri wa TAMISEMI ama tunamweleza Waziri wa Elimu? Ni yepi ambayo Waziri wa Elimu atayachukua hapa? Kwa sababu, mengi yanaelekezwa katika matatizo ya Shule za Sekondari; tukisema nyumba za walimu, tukisema walimu wachache, matatizo ya walimu, mishahara na marupurupu yote yako TAMISEMI! Sasa sielewi kwa nini Serikali isiache suala hili libaki kwenye Wizara ya elimu tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tumewapongeza watoto waliofaulu mitihani yao ya Kidato cha Sita. Matokeo yake, Waziri wa TAMISEMI ndiye aliyekwenda kutoa vyeti!

Sikumwona hata Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Baraza la Mitihani! Kwa kweli mimi nilishindwa kuelewa ni nani hasa sasa anapaswa kusimamia; na je, Waziri anapofika labda Mikoani; Afisa Elimu wa Mkoa au wa Wilaya wanahusika kwa nani? Watawajibika kwa nani? Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana suala hili liwekwe vizuri ili Watanzania wote tuweze kuelewa ni nani hasa tunayem-*face* katika matatizo hasa ya Elimu ya Msingi pamoja na Sekondari. Kuna matatizo pia, kwa Maafisa Elimu; kuna malalamiko makubwa ambayo yanatokea kwamba, Afisa Elimu siyo Mkuu wa Idara, kwa hiyo, hata mshahara wake na marupurupu yake ni madogo kuliko hata wa Wilaya. Sasa ninaomba hili suala, Wizara iliweke wazi; nani ni nani na kipi ni kipi?

Nilikuwa ninaomba pia nizungumzie suala la mimba za wanafunzi mashuleni. Kuna Tume ambayo ilikuwa ikishughulikia, imepita nchi nzima ikisaidiana na *UNICEF* kuangalia ni namna gani na ni ufumbuzi upi utakaoletwa hapa ili tuweze kujua kwamba, mtoto huyu anapopata mimba shuleni je, aendelee na masomo ama asiendelee na masomo? Tumeona wenzetu Zanzibar kule kwao wamefanikiwa, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba nipate majibu kama Tume hii imefikia wapi na tunachukua lipi na wameshauri nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kwa kuzungumzia suala hili la siasa vyuoni. Ninasikitika sana hasa kwa kuona Chuo Kikuu cha Dodoma, mimi nilikuwepo wakati tunaanza mchakato wa kukijenga, nilikuwa kwenye Kamati. Tulianza kwa shida, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu yeye peke yake ndiye aliyejifunga mkanda kuhakikisha kwamba, Chuo kile kinajengwa maana alikuwa anajua mahitaji ya Watanzania. Chuo kile kwa kusimamiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kimeweza kusimama na kuchukua wanafunzi wengi. Ninasikitika, labda nitoe pole tu kwa Profesa Kikula na wenzake wote, kwa sababu wamekuwa wakifundisha kwa migogoro mingi sana. Ninaamini hata taaluma ile ambayo wanakuwa wamepanga kuitoa, hawaitoi ipasavyo. Wakati mwingine huenda hawalali kutokana na vurugu za kisiasa zinazojitokeza chuoni pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu, ninakumbuka tulikwenda Chuo cha Mkwawa, Iringa; wakati tukiwa kule tukasikia kwamba, wanafunzi wa *UDOM* wamegoma. Wanafunzi wa Mkwawa wakasema jamani, angalieni majengo yetu haya, sisi tunatamani twende hata kule kwenye vumbi tukakae kule, wenzetu mmewapendelea halafu bado wanagoma! Tupelekeni sisi. Chuo ambacho kimependwa, lakini kimekuwa ni tatizo kubwa katika Taifa, hawapendeki! Sasa tatizo hili linatoka wapi? Mimi ninaiomba Serikali isimamie, labda nimwombe Msajili wa Vyama Vya Siasa, atumie Kanuni na Sheria, inayokataza Vyama vya Siasa visiingize siasa ndani ya Vyuo vyetu Vikuu. Tuwaache wanafunzi wetu wasome; hapa tunalalamika sijui mikopo midogo, tunaongeza pesa na nini! Sasa mwanafunzi akisoma nusu, ameshagoma; hizo pesa zitarudije kama watashindwa kumaliza masomo na kupata ajira; pesa walizozipata watazirudisha vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali iingilie kati na hii inaleta matabaka vyuoni; kama harakati za kisiasa, somo la siasa libaki kama somo la siasa! Kwa sababu siasa vyuoni, mpaka Wahadhiri wetu wanajiingiza kwenye masuala ya kisiasa; kunakuwa

hakuna usawa! Utaingia darasani kwa sababu wewe tu ni mshabiki wa chama fulani, basi mwalimu ambaye ni mshabiki wa chama fulani anaweza hata akakukwamisha kwenye masomo yako. Ninaomba suala hili likemewe likome kabisa kwenye vyuo ili wanafunzi wetu waweze kusoma na wahadhiri wetu wafanye kazi zao za kufundisha; mbona kwenye majeshi na taasisi nyingine tumeweza? Kama mtu anataka siasa asubiri, miaka mitatu si mingi, miaka minne si mingi; akae pembeni, akifika pale yeye ni mwanafunzi, akitoka pembeni yeye ni mwanachama wa chama chochote kule alipo! Pale asipeleke siasa. Mimi kwa kweli suala hili linanitia huzuni sana, kuona kwamba, rasilimali zetu zinakwenda kuingizwa katika masuala ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi wanasema Bodi ya Mikopo kumekuwa na matatizo, lakini juzi tulipokwenda kutembelea, ninawapongeza kwa sababu, wameweka mwakilishi wao kila chuo kwa ajili ya kutatua matatizo. Nami ninaamini kabisa kuwa, Hazina wanapochelewesha pesa, wanaiponza Bodi ya Mikopo. Bado ninaamini kwamba, suala hili la Bodi ya Mikopo na mikopo kwa wanafunzi, lilikuwa linaingizwa kisiasa. Fedha zinakuwa zimefika pale, kwa sababu hakuna dawati; sasa hujui nani ni nani; mtu anaamua kukwamisha kabisa kwa makusudi ili kuiadhibu Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naipongeza Bodi ya Mikopo kwamba wameweka dawati pale na wao wasimamie kwa umakini zaidi kuona kwamba fedha zile ambazo mwanafunzi amekusudiwa alipwe kwa wakati, hiyo itaondoa maltatizo. Nawapongeze kwa fedha ambazo wameongeza Sh. 7,500/= kwa ajili ya chakula. Naamini ni hatua nzuri na wanafunzi wetu tunaomba walipokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado niseme kwamba kuna matatizo makubwa sana katika kujaza zile fomu. Wanafunzi waelimishwe namna ya kujaza zile fomu, wengi wanasikiliza kutoka kwa wenzao, anajaza kwamba kwetu kuna bati, kwetu kuna hivi, kwetu kuna hivikumbe unapojaza vile vitu unavyo ndivyo unajipunguzia ile thamani ya kupewa mkopo wako. Eleza shida na dhiki uliyoanyo ili uweze kupata msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanafunzi pia tunawaomba wawataje wale wenzao wanaopata mikopo wakati kwao kuna uwezo, kwa sababu wamekuwa wakilalamika chini chini, wengine wanadanganya wanapata mikopo, wanawazuia wale wengine ambao hawana uwezo wanakosa nafasi ya kupata mikopo. Mkopo huu ulikuwa unalenga watoto maskini ili waweze kusaidiwa, siyo wote. Serikali haiwezi kumfikia kila mtu, ni kwa ajili ya watu wachache, watoto wa maskini, ambao hawawezi, wana akili zao maskini wamefaulu vizuri wapatiwe mikopo. Kwa hiyo, ninaomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kwa kusema kwamba Mkoa wetu wa Singida una vyuo viwili vya elimu;, Kinapanda pamoja na Chuo cha Elimu pale Singida. Lakini Chuo cha Kinapanda kina uchakavu sana wa majengo. Nilikuwa naomba Wizara ikitupie macho kuona kwamba ni namna gani watakikarabati. Nasikitika kwamba Chuo hiki kinatoa walimu lakini bado Mkoa wetu wa Singida unakuwa na upungufu wa walimu. Tunaomba basi mtuangalie kwa sababu Chuo hicho kipo pale angalau na sisi tuweze kupata walimu wa kutosha. Lakini tuviwezeshe pia tuviangalie vizuri vyuo vya watu

binafsi na taasisi mbalimbali ambazo zimeanzisha Vyuo vya Ualimu ili kuweza kupunguza tatizo hili la ualimu. Naomba sana Vyuo vinavyofundisha walimu wetu kama *DUSE* viangaliwe na kuongezewa fedha ili kuweza kutoa walimu watakaokidhi mahitaji ya Watanzania ili Taifa letu liweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishie hapa kwa kusema kwamba nawaomba sana ndugu zangu wanasiasa tuipende nchi yetu, tumwombe na kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, ametukirimia amani, hiki kidogo alichotupa naomba tusisimangane, wala tusivurugane, kwa sababu watoto wetu wakishindwa kupata elimu dhamira yetu hakika Mungu atasimama na sisi kudai haki ya watoto wetu ambayo tumeivuruga kwa madhumuni tu eti ya siasa. Kama ni siasa, kama ni uongozi, kama ni kitu chochote, wote tunaingia kwenye nyumba za ibada, tukamwombe Mungu wetu kule, Mungu atatusikia, wakati wako ukifika utafika, kuliko kutaka kukwamisha maendeleo ya mtu mwingine eti kwa sababu tu wewe unataka kupata uongozi. Hakika na Mungu wako hatakubarikia katika uongozi huo kwa sababu umeupata katika njia za kudhulumu watu wengine. Naomba sana Mungu atubariki, Mungu abariki nchi yetu na ninasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante mchungaji.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante mchungaji. Namwita Mheshimiwa Bwanamdogo, atafuatia na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. SAID R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika bajeti iliyo mbele yetu. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya wataalamu kutoka kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, ambayo kwa hakika bajeti ambayo imeletwa mbele yetu hapa tulichangia kiasi cha kutosha kwenye vikao vyetu. Lakini tu basi nimeona kuna mawili matatu angalau niweze kuchangia kwa sababu ya muda ambao nimepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watu wanaleta hisia kwamba Shule za Kata ni za kisiasa na hivyo hazina maana yoyote. Mimi binafsi siungani na wazo kwa sababu sote ni mashahidi kwamba Shule za Kata hizi zimeleta ukombozi mkubwa kwa vijana wetu. Mimi nakumbuka kazi kubwa sana ya ujenzi wa shule hizi ilikuwa mwaka 2006 ambapo kwa kweli nguvu kubwa ya Serikali iliwekwa kwenye ujenzi wa Sekondari za Kata. Nami nasema, anayezipuuza shule hizi, basi huyo ana agenda yake ya siri, hawatakii heri Watanzania. *(Makofi)*

Hawa vijana ambao leo wanamaliza Kidato cha Nne, ni jeshi kubwa bila Sekondari za Kata, tungewaweka wapi? Nichukue fursa hii kutoa rai kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze kwamba tuendelee na ujenzi wetu wa Shule zetu za Kata kama vile ambavyo tumepanga. Kwa namna ya pekee, nawashukuru kwa dhati kabisa Madiwani watatu na wananchi wa maeneo hayo kwamba mara baada ya kupata Udiwani kwenye Kata zao mwaka jana baada ya uchaguzi mkuu, tayari wameshakamilisha ujenzi wa Sekondari za Kata. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza kipekee Mheshimiwa Hussein Hadi Ng'oka - Diwani wa Kata ya Kimange, amefanya kazi kubwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Mohamed Mzimba wa Kata ya Busoga amefanya kazi kubwa, lakini pia nampongeza kwa dhati kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Nassir Ahmed wa Kata ya Bwilingu, amefanya kazi kubwa, kwani shule yake tayari imeshaanza kufanya kazi. Nina hakika hata Mwenyekiti wetu wa Halmashauri ambaye ametokea Kata mpya ya Pera naye atafanya juhudi hizi kuhakikisha kwamba sekondari inapatikana kwenye Kata yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna matatizo mawili matatu kwenye shule hizi, lakini hatukuwa na jinsi kwa sababu tuliwajibika lazima tuchukue *approach* mojawapo, ama tuanze na ubora, twende uwingi au tuanze uwingi twende na ubora. Lakini viongozi wetu wakuu wakaona ni vizuri tuanze na uwingi, baadaye twende na ubora. Ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto za walimu wachache, madarasa machache na nyinginezo hizi zote tutaweza kuzikabili kadri ya muda unavyokwenda ili hatimaye tuwe na sekondari bora katika maeneo yetu. Lakini jambo moja ambalo nimeona nilisemee hapa ni kwenye Shule hizi za Kata juu ya Wajumbe wa Bodi. Tufanye utaratibu mpya, badala ya kumwachia Mkuu wa Shule peke yake ateue Wajumbe wa Bodi, sasa uandaliwe utaratibu mwingine muafaka. Sisi wote ni mashahidi, maeneo yetu mbalimbali Wajumbe wa Bodi wanakaa nje ya shule ilipo. Hili ni tatizo. Kwa hiyo, ufanyike utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba Wajumbe wa Bodi wanapatikana kwenye maeneo yanayozunguka shule husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nampongeza kwa namna ya pekee Waziri wetu, ameweza kueleza mlolongo mzima, namna gani Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba inajenga Vyuo vya *VETA* angalau kila Wilaya. Mimi nashukuru kwa sababu naamini kwamba vyuo hivi vya *VETA* na vyuo vingine vya ufundi vitaweza kuwachukua vijana wetu wengi ambao wanamaliza Kidato cha Nne kwenye Shule zetu na hatimaye kuweza michango yao kwenye maendeleo. Lakini katika suala hili, nina takwimu hapa kidogo ambayo tunaonyesha kuporomoka kidogo kwa vijana ambao wanajiunga na Vyuo vya *VETA*.

Kwa mfano, mwaka 2008, walioandikishwa ni karibu 66,000 na waliomalizi ni 56,000. Hii maana yake ni asilimia 85. Lakini ukiangalia mwaka 2009, walioandikishwa ni 73,000, waliomaliza ni 54,000 ni asilimia 74. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anaweka utaratibu ambao hawa vijana wanaojiunga na *VETA,* basi

wengi wao waweze kumaliza ili hatimaye asilimia hii isishuke kama ilivyo kwa miaka hii miwili, kwamba 2008 ilikuwa asilimia 85 lakini 2009 ni asilimia 74 hili ni poromoko kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo wenzangu pia wamegusia ni kuimarisha Idara ya Ukaguzi. Ukaguzi ndiyo chombo pekee ambacho kinaweza kikaharakisha ukuaji wa elimu yetu. Kwa mujibu wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa tunashukuru sana kwamba kwenye Shule za Sekondari angalau ukaguzi umekuwa kwa asilimia 72.4, kwamba shule nyingi zimekuwa zimepitiwa na Wakaguzi wetu. Lakini lazima tukubali kwamba vitengo vingine ambavyo vimeachwa hivi, kwa mfano, shule na vitengo maalum ni asilimia 29.9 Shule za Msingi ni asilimia 37.8 lakini Vyuo vya Ualimu ni asilimia 43.0.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu kuimarisha idara hii ili hatimaye iweze kufanya kazi yake iliyokusudiwa. Maeneo mengi ya nchi yetu, idara inashindwa kufanya kazi yake kwa sababu haina vitendea kazi, magari hamna, kwa hiyo, ni matatizo makubwa kabisa kwenye Idara ya Ukaguzi. Naiomba Serikali ifanye kila ifanyavyo iweze kuimarisha Idara hii ya Ukaguzi kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ualimu unakwenda zaidi ya kisaikolojia. Mwalimu mzuri lazima uwe kisaikolojia uko sawasawa. Lakini kwa haya madai mbalimbali ya walimu, malipo ya kuanza kazi yenyewe yanakuwa kazi kuyapata, motisha ni shida; uhamisho, shida; likizo vurugu tupu. Sasa katika hali ya kawaida, huyu mwalimu wa aina hii, hawezi kuingia darasani na akafundisha kama vile ambavyo amepanga. Ni lazima Serikali ione jinsi ya kuweza kurekebisha madai mbalimbali ya walimu ili kuwajengea saikolojia nzuri kwa ajili ya kazi yao ambayo wanaifanya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna madai mengi ya walimu, kwa mkoa wa Pwani pekee, walimu wanadai Sh. 1,333,934,962/=, huu ni mzigo mkubwa lazima walimu hawa walipwe. Lakini ukiangalia hivyo, Wilaya ya Bagamoyo, kati ya hizo Wilaya, Bagamoyo ni Sh. 337,737,808/= ambazo ni kwa ajili ya uhamisho, likizo, matibabu, masomo na mapunjo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti sana nikagundua kwamba zaidi ya asilimia 70 ya fedha hizi kwa Wilaya ya Bagamoyo zinatoka Wilaya ya Chalinze. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha bajeti yake, basi angalau alione, kwamba bajeti yake ina changamoto kubwa, maana katika fedha ilizopangwa asilimia 49 zinakwenda Bodi ya Mikopo, asilimia 51 ndiyo ihudumiye mambo yote ikiwemo mishahara na maendeleo mbalimbali. Ni mzigo mkubwa, lakini hatuna jinsi, lazima tuone jinsi gani ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu ili waweze kufanya mambo yao kama walivyopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zinatengwa kama *capitation* kwa ajili ya vijana waliopo mashuleni ili hatimaye walimu wazitumie kuwasaidia kuendeleza hao vijana, bado nazo ni tatizo kufika kwenye shule zetu. Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wamechangia sana katika hili, lakini nami nikaona kwa sababu ni jambo nzito na ni

jambo nyeti mno, nami nitoe mchango wangu ili hatimaye basi, ione namna gani inaweza ikasaidia ili fedha hizi ambazo ni kidogo, siyo nyingi sana, ziweze kufika ili ziwasaidie vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kuna kila sababu ya kuamini na ipo hivyo kwamba Shule za Mijini zina fursa nzuri za ufaulu kuliko Shule za Vijijini, ni kwa sababu ya miundombinu. Jana Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema hapa, nami nakubaliana naye kabisa kwamba unapoleta mtihani ule ule kwa mwanafunzi anayesoma Tambaza, halafu ukauleta mtihani ule ule kwa mwanafunzi anayesoma Matimbwili kule kwangu ndani kabisa, kwa kweli inakuwa hutendi haki kabisa. Ninajua kwamba kitaalamu hilo sijui utaliwekaje, lakini nataka kusema hapa kwamba jambo moja la msingi hapa ni Serikali ihakikishe kwamba inapata walimu wa kutosha kwa ajili ya sekondari hizi, kwa ajili ya Shule za Msingi na kwa ajili ya vyuo mbalimbali ambavyo tunakusudia kuvianzisha kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna lingine linaonekana na ni desturi ya Wakurugenzi walio wengi kwenye Wilaya huko, fedha nyingi ambazo zinatengwa kwenye Halmashauri zetu, baadhi yao huzichukua fedha hizo kuzipeleka kwenye miradi mingine na kuiacha Sekta ya Elimu kama yatima. Hili ni tatizo kubwa, baadhi ya Wakurugenzi wanazichukua kwa maana kwamba wafanyie miradi fulani ili hatimaye wazirudishe lakini inafika…

*(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SAID R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia katika Idara hii ya elimu ambayo ni Idara muhimu sana. Kabla ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu pamoja na Watendaji wa Wizara hii ya Elimu kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuandaa hii bajeti ambayo tunaipitisha leo hapa. Katika bajeti hii au katika kitabu hiki cha bajeti, nilikuwa nakisoma kwa makini sana, nikaona kwamba bahati nzuri wameweza kuainisha changamoto ambazo zinaikabili sana Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba, nikianza kwa Elimu ya Shule ya Msingi, suala lolote ukitaka kufanikiwa ni lazima uhakikishe kwamba, unapoanza msingi unauweka katika hali nzuri. Sasa sisi katika elimu tumesema kwamba kiwango cha elimu kinashuka, lakini suala la kujiuliza ni kwamba kwa nini kiwango cha elimu kinashuka? Nami nilikuwa nategemea kwamba kiwango cha elimu kufuatana na utandawazi wa sasa hivi lazima kipande. Sasa kinashuka!

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwa makini nikawa najiuliza mwenyewe, kwanini kiwango cha elimu sasa hivi kinashuka badala ya kupanda? Sasa ukiangalia katika shule

zetu za msingi, kwanza kabisa kuna madarasa ya awali, madarasa mengi sana hayana walimu. Utakuta mtu anafundisha Darasa la Awali, ni mtu wa kujitolea. Naiomba Wizara hii iweze kutengeneza mkakati sahihi wa kupata walimu wa kufundisha madarasa yale ya awali, halafu nimeona vijijini kwa mfano kule kwenye Jimbo langu, nimekuta shule nyingi sana, mwalimu anayefundisha, yule anayejitolea, wanasema kwamba wanachangia tu wananchi. Sasa kwanini Serikali isimwekee mshahara, alipwe mishahara kama wengine? Atachangiwa na wananchi mpaka lini? Hii inaonyesha kabisa hata mtaala ule unaofundishwa pale haukaguliwi vizuri, kwa sababu ni mtu anayejitolea, na kama mtu anajitolea kufundisha, maana yake huwezi kumkagua hata akikosea huwezi kumdhibiti. Naiomba Wizara ifikirie hilo suala. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo nimeliona ambalo linachangia kushuka kwa kiwango cha elimu na katika changamoto hapa nimesema, nimeona kwamba wameshaainisha tayari. Vifaa havitoshi mashuleni, kwa mfano, ukiangalia shule zetu hazina vitabu, ambalo ni suala la kushangaza. Unaweza kukuta katika darasa kuna watoto 80, lakini kuna vitabu vinne tu. Bahati nzuri katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi wamesema kwamba tutanunua vitabu vya kutosha kwa Shule za Msingi. Naomba suala hili litiliwe mkazo na tulifanyie haraka ili watoto wetu wasiendelee kufeli mitihani.

Suala lingine la muhimu ni kuhusu mishahara ya Walimu. Mishahara ya Walimu bado ni tatizo, nikianza kunukuu katika hotuba ya Rais ambayo aliitoa mwanzoni mwa Kikao cha Kwanza cha Bunge. Alisema, atahakikisha kwamba mishahara ya watumishi wa Serikali inaongezwa. Sasa naiomba Serikali katika Wizara ya Elimu hususan Walimu, waongezewe mishahara ili waridhike na wafanye kazi vizuri. Tusipowaongezea mishahara, tatizo la kufeli wanafunzi litaendelea kuwepo. Kwa mfano, Walimu wa Shule za Msingi tunajua kabisa mishahara yao ni midogo, ndiyo maana watoto hawafundishiki. Mtoto anafundishika kuanzisha Shule za Msingi, sasa asipofundishika maana yake usitegemee kwamba utakuja kuvuna tunda zuri baadaye akiwa Sekondari. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba inawajengea mazingira mazuri Walimu wa Shule za Msingi.

Tukija kwenye vifaa na mazingira wanayoishi Walimu siyo mazuri sana. Utakuta Mwalimu badala ya kukaa shuleni, anakaa Kijijini na amepanga nyumba. Sasa tuna tatizo kubwa la upungufu wa nyumba za Walimu, shule nyingi sana hazina nyumba za Walimu. Sasa wewe unategemea Mwalimu atoke Kijijini amepanga nyumba, na nyumba yenyewe labda inavuja, haijatengenezwa vizuri, aende akafundishe halafu utegemee watoto watafaulu. Mwalimu akifundisha *under stress* usitegemee kwamba anaweza kufundisha vizuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe inajenga majengo ya nyumba za Walimu.

Suala lingine ambalo naliona ni tatizo kubwa sana, kwa mfano kwenye Jimbo langu Walimu wanasafiri kilomita kuanzia 80 mpaka 100 kwenda kuchukua mshahara Wilayani halafu wanalala kule kule. Ni lazima tuzingatie muda wa kufundisha. Naiomba Serikali ipeleka Benki katika Jimbo la Mufindi Kusini. Katika Jimbo langu hakuna Benki. Kama kungekuwa na Benki, Walimu wangeweza kuchukua mishahara yao pale pale Jimboni, lakini wanatembea kilomita nyingi sana kutafuta mishahara yao. Sasa naiomba Serikali iliangalie hilo kwamba Benki ni kitendea kazi kizuri kwa Walimu ili

kuweza kupata mishahara yao kwa muda unaotakiwa. Naiomba Serikali pia ihakikishe kwamba Jimbo la Mufindi Kusini linapata Benki na Walimu, walipwe mishahara kwa muda unaotakiwa badala ya kupoteza muda mrefu kwenda kuchukua mshahara Wilayani. Hili ni tatizo kubwa sana.

Suala lingine ambalo naliona katika Wizara ya Elimu ni kama inakuwa na matawi mengi sana. Tunasema Wizara ya Elimu wanapangiwa na Utumishi. Watu wa Utumishi wanashughulikia mambo ya Elimu. Ukiangalia tena TAMISEMI imeshikilia Wizara ya Elimu. Sasa hata bajeti wakipanga ni lazima ikaguliwe, sijui na iende Utumishi, mara iende Wizara ya Fedha na kadhalika. Kwa nini kunakuwa na mlolongo mrefu katika Wizara hii muhimu? Mimi naomba Wizara ijitegemee ipange bajeti, ilete hapa Bungeni ili sisi tuipitishe kutokana na mahitaji yao.

Pia kuna masuala ya malimbikizo ya mishahara ya Walimu. Naishukuru sana Serikali imetoe ripoti kwamba wamelipa asilimia kubwa sana. Lakini bado kuna Walimu wa kuanzia mwaka 2008 wengine bado wanadai malimbikizo yao. Ninaomba Serikali ihakikishe kwamba Walimu wote wanalipwa malimbikizo yao.

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye upandaji wa madaraja. Tumesikia kwamba kila mwaka ni lazima Walimu wapande madaraja, lakini utakuta kuna Walimu wengine wanakaa miaka miwili au mitatu hawajapandishwa madaraja. Kuna matatizo gani? Huyu mtu ameajiriwa, kwa hiyo, ni haki yake apande daraja. Analipwa mshahara mdogo, lakini kupandishwa daraja nayo ni shida. Kwa nini inaleta shida? Tunaiomba Wizara pamoja na Katibu wa Wizara hii ahakikishe kwamba hakuna masharti magumu ya kupandisha Walimu madaraja, kwani ni haki ya kila Mwalimu kupanda daraja kwa wakati. Hiyo ni haki yake.

Kwa mfano, mwaka huu hajapanda daraja, mwakani unampandisha, anakaa miaka miwili, maana yake hayo madaraja yataji-*double*. Ina maana utampandisha mara tatu? Kwa hiyo, hesabu hiyo ni lazima ifanyike na iangaliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye masuala ya Walimu wa Sayansi. Katika Jimbo langu, kuna tatizo kubwa sana la Walimu wa Sayansi. Naiomba Serikali kwamba kwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne, wanaokwenda Kidato cha Tano na Sita, Serikali iangalie na kutoa motisha kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi. Hata kwa kusoma bure *Form Five* na *Six* ili waweze kusoma masomo ya Sayansi, kisha tupate Walimu wa kutosha. Tusipofanya hivyo, tutashindwa kupata Walimu. Kwenye Jimbo langu Walimu wa Sayansi ni tatizo kubwa. Kila siku hapa tunaimba kwamba hatuna Madaktari, hatuna Ma-*engineer*, hatuna watu waliosoma masuala ya *Chemisty*. Watasoma kutoka wapi kama hatuwajengei msingi kuanzia Shule za Awali? Sasa mimi naishauri Serikali kwamba wanaoingia *Form Five* na *Six* kwa kuwapa motisha kwa masomo ya Sayansi kwamba wasome bure, hii tutakuwa tunatibu ugonjwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni michango. Michango katika Shule za Sekondari za Kata, tunajua kabisa wazazi wengi hawajiwezi kuilipa. Sasa tunasema

kiwango cha ada ni Sh. 20,000/=, hiyo inaeleweka na ninaishukuru Serikali kwa kuweka kiwango kidogo cha ada. Lakini ukipiga hesabu sahihi, siyo Sh. 20,000/= kwa sababu kuna michango mingi sana. Kuna *form* moja nilikuwa naisoma unakuta kuna michango mingi sana imeandikwa. Sasa kwa nini tunaweka michango mingi sana na tunajua kabisa wananchi wetu hawawezi kulipa ile michango? Utakuta mwanafunzi anatolewa darasani, anaambiwa afuate michango. Sasa hivi wanakwepesha, wanasema asifuate ada, bali afuate michango. Sasa huyu mwanafunzi unapomtoa darasani, hujui kwamba anapoteza muda wake wa kusoma?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwamba ile michango ambayo imewekwa ipunguzwe, kwani kuna michango mingine ambayo tunasema ni ya madawati, sasa unaangalia kila mwaka ni madawati, kila mwaka madawati lakini ukienda shuleni hayo madawati hayapo. Sasa kama ni lugha imetumika, hebu naomba turekebishe na tuwe *uniform.* Kama tunasema ada ni Sh. 20,000/=, basi iwe hivyo na kama ni majukumu mengine, ijulikane kwamba Serikali inachukua majukumu ya kujenga madarasa na majukumu ya kununua vifaa tusiwatwishe mzigo wazazi. Naiomba sana Serikali kwa hilo iangalie tena ile michango ya shuleni ambayo ipo ili kuweza kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba nichangie kuhusu shule za watu binafsi. Tukianza na Shule za Msingi, siku hizi tunasema ni *Medium School* na wengine wanasema ni *International School*. Zile shule ni nzuri sana na watoto wanaosoma kule wanafaulu na tunakubali kwamba wanafaulu vizuri. Lakini kile kiwango cha ada kilichowekwa ni kikubwa sana. Mimi sijawahi kuona Shule ya Msingi ada yake inashinda ada ya Chuo Kikuu.

Kwa mfano, Shule ya Msingi mtoto mmoja analipiwa ada shilingi milioni mbili, shule binafsi mzazi analipa ada shilingi milioni tano; ina maana kwamba watoto watakaokwenda kusoma pale ni watoto wa mabepari, lakini watoto wa kawaida hawawezi kusoma pale na Serikali tunayo, inaangalia tu viwango vya ada vinapanda kila siku. Shule ya Msingi mtu analipa ada ya mtoto shilingi milioni tatu! Naomba Serikali ifanye utafiti kuhusu hilo, tunapenda watoto wetu kila mzazi amsomeshe shule bora na nzuri, lakini sasa kwa nini ada kila siku inapanda kwa shule za *private*?

Kitu kingine ninachokiona ni kwamba eti kwa sababu wanafundisha Kiingereza. Ah, jamani hilo suala jamani hebu tuliangalie, kwani Kiingereza ni nini? Kiingereza ni lugha kama lugha nyingine, sisi tunataka watoto wetu wafundishwe na wapate elimu bora. Wao wana uwezo ndiyo maana sasa hivi hata kwenye *East Africa,* mimi bado naweka *question mark*, kwamba labda uwiano wa kuajiri kwenye *East Africa* utakuwa tofauti kwa sababu ya *perception* kwamba wenzetu labda wa Kenya na Uganda wanajua Kiingereza, sisi hatujui. *Perception* hii naomba ifutike haraka sana, sisi tunataka ubora wa elimu na wengine wanasema sisi Watanzania hatuna ubora, kwa nini tunajishusha wenyewe? Sisi tuna ubora wa kutosha kabisa, huwezi kumpima mtu kwa Kiingereza kwamba anajua kuzungumza Kiingereza ndiyo unampima ubora. Hii *perception* naomba tuifute haraka sana.

Kwenye *East Africa* tukiangalia ajira, lazima tutoe uwiano kama wa ajira ukiwa tofauti na sisi Watanzania, mimi hilo sikubaliani nalo hata siku moja, kwani kila mtu ana uwezo wake katika *angle* zake. Kwa mfano, mtu ni Daktari unasema awe Mwanasheria, ni lazima uwezo utakuwa tofauti. Lakini tufuate viwango vilivyowekwa kama ni Ma-*engineer* wa kujenga barabara hapa Tanzania, basi waajiriwe ili wafanye kazi na tunao Ma-*engineer* wanafanya kazi vizuri sana, lakini hatuwezi kusema *Engineer* wa Tanzania hana uwezo, lakini wa Kenya ana uwezo. Hii mimi sikubaliani nayo hata siku moja. Tuna imani kabisa na ndiyo maana tumesoma Vyuo Vikuu, watoto wetu tunawasomesha Vyuo Vikuu, na ni lazima tujiamini na tuna uwezo wa kufanya kazi na ukitaka kumpima mtu kama anaweza kufanya kazi, mpe cheo au mpe kazi. Sasa kwa nini hatutoi kazi? Tuna matatizo gani?

Ninaomba Wizara zote zinazohusika, Watanzania wapewe kazi na wapimwe kwa kufanya kazi, usiwapime kwa mdomo. Sisi tuna tabia ya kupima watu kwa mdomo, kwa nini tunawapima watu kwa mdomo? Naomba hili lieleweke Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hatuwezi kuendelea kama tunapima watu kwa mdomo. Tunataka tuone *Ma-engineer* wetu wanaajiriwa katika barabara, ujenzi, katika fani za maji na Madaktari lazima wafanye kazi na Watanzania ni lazima waajiriwe. Sasa unaweza ukaona Madaktari wanakuwa chini ya *foreigner,* anaanza kunyanyaswa pale na utakuta anakimbiakimbia kwenye *corridor* anasema anawahi kupeleka *report*. Hili mimi siwezi kukubaliana nalo hata siku moja. Tunajiamini kabisa, kwani sisi tumesoma, ni lazima tupewe kazi na tufanye kazi.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwenye *East Africa* tulisema kwamba labda tutaongeza upana kwenye Sekta ya Afya na Elimu, kwa nini tusiwape sekta nyeti hizi? Sisi tuna utaratibu wetu, tukishindwa utasikia, mbona wenzetu Kenya wanafanya hivi?

*(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mheshimiwa Clara D. Mwantuka.

**MHE. CLARA D. MWANTUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu ambayo nilikuwa naililia siku zote siipati lakini leo nakushukuru sana, nimeipata.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye alinipa nafasi hii kuwepo hapa leo ambapo kwa akili zangu na kwa jinsi ninavyoumwaumwa nilifikiri nitashindwa kuja. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mungu. Pia nampongeza Waziri wa Wizara ya Elimu na timu yake ambao wametuletea hotuba nzuri na mimi nikiwa ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati hii. Napenda nimpongeze pia

Mwenyekiti wangu, Mama Sitta ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kupigania Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa Wizara kwamba sehemu kubwa inaonekana kwamba inachangia kuzorotesha elimu. Kwanza, nikichukua mpango wa mitaala, mitaala inayotumika inaonekana kila mwaka inabadilika na kila Waziri anayechaguliwa anakuja na mtaala wake. Hii inawachanganya hata Watendaji ambao ni Walimu kuyumbayumba. Nikichukulia mfano, kuna mpango huu wa *RUAZA* ambao kuna baadhi ya Walimu hawaufahamu. Kuna mambo ya *TEHAMA* ndiyo kabisa inapokuja kule vijijini ambapo hakuna umeme, wanafanyaje? Kwa hiyo, Walimu wengine hawajui *TEHAMA* ni nini?

Isitoshe, watoto wenyewe jinsi tunavyowachukua, tunawaanzia na masomo pengine hata ya Darasa la Tatu ambapo zamani walikuwa wanaanza na alfabeti, inakwenda silabi, neno na kuendelea kwenye sentensi. Lakini sasa hivi wakaanza alfabeti kidogo halafu ukurasa wa pili wanakwenda na sentensi. Sasa watoto kwa kweli unawapa kazi ngumu sana kuelewa haraka. Kwa watoto wa mijini sawa, lakini kwa wale wa pembezoni ambapo kidogo hata lugha zenyewe inakuwa tatizo, wanapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisije nikasahau, nianze na Vyuo Vikuu. Kusini nawashukuru Wamisionari Mtwara Parish kwa kukubali kuweka chuo, lakini naiomba Serikali na yenyewe itafute sehemu, ijenge chuo na ijulikane kwamba chuo kile kimejengwa na Serikali. Hii itasaidia kanda nzima ya Kusini. Hilo ni ombi la kwanza nalitoa.

Vilevile, katika Shule za Msingi, uandaaji wa masomo kwa Walimu kulingana na utaalam uliopo sasa, unakuwa na vipengele vingi kiasi kwamba Mwalimu anaandaa somo, siyo kwa ajili ya kumnufaisha mwanafunzi, bali ni kwa ajili ya Mwalimu Mkuu na Wakaguzi kwamba watakapokuja kukagua wakute wana mpango wa kazi na maandalio ya somo. Sasa hili halina maana kwani nia yetu ni kumfundisha mwanafunzi ili afanye inavyotakiwa. Kwa mfano, wanafunzi wa Darasa la Kwanza wanaotoka pembezoni mwa nchi, wanapoondoka asubuhi nyumbani hawajatia kitu tumboni na sehemu nyingine shule nyingi utakuta hawana chakula cha mchana, kwa hiyo, hawa watoto hawafundishiki. Unapowapa masomo mazito yanawapita kimo, wanashindwa kuwa na mtiririko mzuri. Hivyo naomba Wizara iangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia vitabu vya Kiada havipo shuleni na kama vipo, basi ni vichache na watunzi wa vitabu wanatunga kwa ajili ya biashara, wanafanya mawasiliano labda na Wizara kisha vinaingia shuleni. Sasa ukienda shule nyingine utakuta vitabu vya Kiada vinavyotumika kwa masomo fulani ni tofauti, wakati zamani ilikuwa kila shule ukienda vitabu vya Kiada ni vilevile. Sasa hilo nalo liangaliwe na somo la Jiografia na Historia vitabu vilikuwa hakuna, Makao Makuu Mkoani vimeletwa hivi karibuni, yaani mwezi uliopita au mwezi huu. Sasa pembezoni watapata lini na huu ni mwezi wa Saba? Ina maana kwamba Jiografia haijafundishwa shuleni kwa sababu hapakuwa na vitabu. Hivyo, naomba Wizara iliangalie hilo.

Kitu kingine ni kwamba, Elimu bila Walimu hakuna Elimu ingawaje na bila watoto Elimu haipo, lakini Walimu ndiyo wahunzi wakuu wa kutufua sisi wote tuliopo humu ndani kuanzia Rais huko aliko, Mawaziri wote, Wabunge na Viongozi wengine wote. Wahunzi ni Walimu, kwa hiyo, Walimu ilibidi wawe watu wa kwanza, yaani ingekuwa mshahara wao unafikiriwa kwa sababu hawana muda wa kazi. Walimu wanafanya kazi mchana na usiku, hawana Jumamosi wala Jumapili kwa sababu siku nyingine saa za kazi zikiisha ndiyo wanakwenda kuandaa masomo juu ya nini wakafundishe kesho.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba zamani kulikuwa na *teaching allowance* sijui zimepotelea wapi? Kwani zile zilikuwa zinawasaidia Walimu kupunguza makali ya kazi zao, hivyo huo mpango naomba urudiwe ili Walimu wanufaike pia. Vilevile Mwalimu ukimpa mshahara mzuri na maslahi mazuri, kwa mfano makazi na posho kama *teaching allowance* akipata, nafikiri ndiyo kazi yake ataipenda na italeta manufaa kwa watoto.

Jamani, zamani Mwalimu alikuwa mtu wa heshima enzi zetu za ukoloni. Mwalimu alikuwa wa kujihimu. Mnaelewa maana ya kujihimu? Ilikuwa hakosi mwanamke wa kumwoa hata kwa kumwomba hivi, ilikuwa rahisi kulingana na heshima yake. Akina sisi, ah! Mwalimu amenitaka, eeh! Sasa alikuwa anaheshimika kulingana na hadhi aliyokuwa nayo katika mazingira yake. Lakini Walimu wa leo wengine wanasikitisha, utamkuta Mwalimu utafikiri anatoka kilabuni. Anaweza akashindana na mtu ambaye hana mwelekeo, ni ombaomba mtaani pale ikaonekana ni afadhali ombaomba kuliko Mwalimu. Mwalimu mwingine anaweza kwenda kufundisha darasani amevaa kandambili, Bara na Pwani, sasa hali kama hii inamfanya Mwalimu asiipende kazi yake. Hivyo, naomba watazamwe sana hawa Walimu na wanapodai maslahi yao, wapewe.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kwamba Mwalimu atapendwa wakati anapokuwa kazini tu, lakini akifa, kama hana jamaa yake katika familia wa kufuatilia mafao yake, basi yamekwenda na maji. Kuna baadhi ya Walimu Masasi, wengine walikuwa wanalalamika tangu enzi ya Mheshimiwa Mrope, wanapeleka malalamiko kwamba yaletwe huku, sasa sijui huku yalikuwa yanasikilizwa? Nami pia napewa malalamiko hayo, nafikiri hata mwenzangu wa Jimbo analalamikiwa na kwamba hali ni ngumu, mafao ya watoto wetu vipi? Maana familia zao walizoziacha zinahangaika na zinaendelea kuhangaika kwa kukosa msaada. Sasa hali kama hii inasemekana kwamba kama hakuna kumbukumbu eti azitoe mzazi, inawezekana? *(Makofi)*

Mwalimu mwingine amefariki akiwa na utu uzima, kumbukumbu zake zote alizitunza mwenyewe. Akifa haitakuwa rahisi kwa familia au mtu mwingine kwenda kuzipata. Lakini kwa sababu kumbukumbu za watumishi wote zinakuwepo ofisini, basi zitumike kuwatafutia hawa mafao yao. Kutowapatia kumbukumbu hizo ni kwamba tunaziibia familia haki zao. Hivyo, naiomba Wizara iliangalie hili, kwani wapo wengine wamenipa barua zao, nimekuja nazo hapa ambazo itabidi niziwasilishe kwenu wahusika mwone ni jinsi gani mfanye ili mzipatie familia hizo mafao. Nafikiri hilo limeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshukuru kwa zile zawadi walizopewa wale wanafunzi saba ambao wamefaulu mtihani wa Kidato cha Sita, lakini wakitokea Shule za Kata ambazo walisoma mpaka Kidato cha Nne. Mimi nilidhani kwamba pongezi ile wangepewa wale wanaofaulu ile *Form Four* kwamba wamefanya vizuri pale. Sasa hawa waliopewa ni kwamba walitoka kule wakaenda kwenye shule nyingine, ambako walifuliwa kwa namna nyingine. Ingekuwa vyema hawa wa Kidato cha Nne kama wanapata *Division One, Two* na kuendelea, lakini sasa kwa kuwa haikufanyika hivyo, ningeomba basi ili kuwapongeza hawa na kuzipa moyo zile Shule za Sekondari za Kata, basi hata waliopata alama 29 wapatiwe nafasi, walau wawaze hivi ili waone kwamba kweli shule za Kata zina manufaa. Lakini sasa kulingana na kwamba hapakuwa na Walimu wa kutosha wamejitahidi wakafikia kupata alama hizo, basi hawa wana vichwa vizuri, tungewapongeza kwa jinsi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika shule hizi za Sekondari za Kata, wazazi wanalalamika juu ya suala la madawati, kwamba mtoto wa kwanza amekwenda pale amepeleka dawati, akimaliza muda wake inawezekana ndugu yake toka nitoke anakwenda shule ile ile, lakini na yeye anaambiwa apeleke dawati. Sasa wazazi wanajiuliza, haya madawati yanaliwa na mchwa au yanafanyaje hadi mpaka yasiwepo ambayo ndugu yake ataweza kurithi? Hili nalo naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani na Taifa. Mimi nashindwa kuelewa kwa sababu haiwezekani shule nzima Darasa la Saba itokee kwamba wote wanafaulu, nini kinafanyika hapa? Baraza la Mitihani la Taifa, lilifanyie kazi hili. Mimi kijijini kwangu ninapotoka kuna baadhi ya Wazazi wamekataa kuwapeleka watoto wao kwenda kuanza Shule ya Sekondari kwa sababu anamjua mwanawe kwamba hata jina lake hawezi kuandika. Leo huyu amefaulu vipi kwenda Sekondari? Kwa hiyo, mzazi anaona kwamba atapoteza fedha zake bure, hivyo ni afadhali ampeleke mwanawe akajifunze cherehani, pengine hata kaboka lake likichanika atamwekea kiraka. Hivyo, hilo nalo liangaliwe kwamba nini kinafanyika hapa cha kuweza kuwapeleka watoto hata wasio na uwezo kwa sababu wanawatia hasara wazazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hali ya madeni ya Walimu hawa bado ni mbaya kiasi kwamba wengine wamekufa nayo. Walimu wamekufa wangali wanadai. Sasa ndiyo ile niliyosema siku fulani kwamba wakifa na kila kitu kimekwenda, mrithi anapofuatilia inaonekana kwamba hakuna kitu. Mwingine aliandika barua zake mpaka zikapita kwa Afisa Elimu akiomba ashughulikiwe. Ikitokea akafa kabla, basi palepale hakuna kitu. Nawaomba Wizara kulingana na kumbukumbu zinazokuwepo kwenye ofisi zenu, angalieni haki za watu hawa, familia zao zipate ili ziwasaidie kwani kwa kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme juu ya maendeleo ya elimu ya Watu Wazima. Mimi nafikiri wakati ule Elimu ya Watu Wazima ilikuwa inasaidia kwa sababu wengine hawakujua kusoma, kuhesabu na kuandika. Ile ilikuwa inawasaidia wengine hata kama kuuza karanga barazani kwake au amelima bustani ya nyanya, akipata zile akiuza

kulingana na elimu ndogo aliyopata inaweza ikamsaidia. Naomba hili lirudishwe maana sijui limeishia wapi, hivyo naomba hilo nalo litazamwe ili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kuna shule nyingine ambazo mpaka leo watoto wanakaa chini, kama alivyotangulia kusema ndugu yangu Mheshimiwa Maria Hewa, bado kuna shule moja ambayo nimetembelea pale Masasi Mjini, ipo mjini, kuna shule ndogo ya Kambarage ambayo ina wanafunzi wanaoishia Darasa la Nne, wakitoka hapo wanakwenda Shule ya Msingi Nyasa, wanakaa chini mpaka leo. Vyoo vilikuwa viwili, kimoja kimekwishaharibika kabisa, wanatumia choo kimoja. Hiyo ni shule. Kweli tunataka watoto hawa waende pale waishi vizuri?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Halmashauri zetu kutokuwa na pesa, ningeomba kwamba hili kule zinakotoka wahamasishwe, Wizara pengine kwa kutumia ninyi kuwahamasisha Wakurugenzi walitilie mkazo. Nafikiri hilo litatuliwe. Hapa nimeona kwenye takwimu kwamba fedha zinatengwa kwa ajili ya madawati, hivyo hilo litazamwe kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa kwamba mtoto kukaa chini na anaandikia kwenye goti, hati yake haiwi nzuri na unamjengea mwanzo mbaya. Hivyo nalo hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema juu ya mpango wa wanafunzi kula chakula shuleni. Zile pesa ambazo tulisema kwamba zinatolewa kwa kila mwanafunzi, sijui mwaka gani ilikuwa shilingi elfu tisa na kitu, ule mpango urudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unamaliza na nukta, kengele inakonga hapo hapo! Haya ahsante nashukuru. *(Kicheko/Makofi)*

Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Philipa Mturano, lakini badala yake wamebadilishana na Mheshimiwa Christina L. Mughwai, halafu atafuatia Mheshimiwa Anastazia J. Wambura.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mambo mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini mimi nitachangia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, eneo langu la kwanza ningependa kuzungumzia juu ya namna ambavyo shule za *private* hasa za Sekondari zinaendeshwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, kwa sababu amenisaidia kuondoa mambo ambayo nilikuwa napenda kuyazungumzia lakini nami nitaongezea.

Mheshimiwa Spika, shule za *private* zinaonekana kama vile hazina msimamizi. Shule hizi zinajipangia mambo, zinatoza ada kubwa, zinatoza michango mikubwa kana kwamba haziko chini ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza kabisa,

nikianza na fomu za udahili kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na shule za *private*, tuchukulie mfano, kidato cha Kwanza au cha Tano, fomu hizi zinauzwa kwa bei kubwa sana. Nashindwa kuelewa ni kwa vipi fomu yenye kurasa mbili tu na tena ni *photocopy* iuzwe kati ya Sh.15,000/=, Sh. 20,000/= na nyingine hata Sh. 30,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili nikitambua kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani ni wamiliki wa shule hizi. Kwa hiyo, katika ngazi ya udahili kununua fomu ni mzigo mkubwa kwa wazazi. Japokuwa natambua mchango wa shule za *private* katika elimu ya hapa nchini, fomu wanaziuza kwa bei ghali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo shule hizi zina kiwango cha wanafunzi wanaochukuliwa. Kwa mfano, kidato cha Kwanza wanachukua watoto 100 tu, lakini unakuta shule inauza fomu 5,000 hadi 10,000 kulingana na jinsi ambavyo shule hiyo inapendwa na wazazi wengi. Sasa nashindwa kuelewa ni kwanini shule iuze fomu nyingi, 5,000, 8,000 hadi 10,000 ilihali wakijua kwamba watachukua wanafunzi 100 tu.

Mheshimiwa Spika, hizi shule zimekuwa zikifanya biashara kubwa kupitia hizi fomu za *interview* kwa wanafunzi wanaojiunga, na sidhani kama mapato haya makubwa kwa sababu yanakwenda mpaka Sh. 200,000,000/= kwa idadi ya wanafunzi walionunua fomu, yanalipiwa kodi Serikalini au vipi? Naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iliangalie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, shule hizi za *private* zinatoza michango mikubwa. Mimi naelewa kabisa shule inapaswa itimize vigezo, sasa nashindwa kuelewa inakuwaje wazazi wanatakiwa kuchangia majengo ya shule za *private*?

Shule hizi ni shule za *private,* siyo za Serikali, inakuwaje zijengwe na hela za wazazi? Nikichukulia mfano wa shule moja ambayo iko katika Jimbo la Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mwaka jana kila mwanafunzi aliyejiunga na shule hiyo alitakiwa alipe Sh. 300,000/= kama mchango wa majengo ya shule na mimi ni mzazi mwenye mwanafunzi katika shule hiyo. Mwaka huu kila mzazi alitakiwa alipe Sh. 400,000/=.

Mheshimiwa Spika, Sh. 400,000/= ni ada kubwa tu hata ya mwaka mzima, inakuwaje ichangwe kwa ajili ya majengo ambayo ni ya *private*? Naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nakuomba Mheshimiwa Waziri, hii shule iko katika Jimbo lako, unione nitakutajia jina la shule hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nani sasa amwone mwenzake? Nani akamwone mwingine?

**MJUMBE FULANI:** Mwambie wewe ndiye ukamwone.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mimi nitakuona Mheshimiwa Waziri, nitakuletea jina.

**SPIKA:** Haya ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nitamwona Mheshimiwa Waziri kwa sababu hii shule iko katika Jimbo lake, hivyo nitamweleza na nimesema mimi ni mzazi katika shule hiyo. Tunaumizwa, wazazi wanabeba mzigo, ada zenyewe ni kubwa, ada kwa mwaka ni karibu Sh. 2,000,000/= na bado uchangie mchango wa majengo. Hiyo ni shule ya *private*, kwanini haikuwa na majengo? Kwa nini wazazi wachangie majengo ya shule? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara, siyo kwamba wazazi wanaokwenda kwenye shule za *private* wana uwezo, siyo wote wenye uwezo, ila ni kutokana na mapungufu yaliyoko katika shule zetu za umma na vilevile mchango unaotolewa na shule zetu za *private* ndiyo maana wazazi wanapeleka watoto katika shule hizo. Kwa hiyo, wasibebeshwe mzigo. Nawaomba wamiliki wa shule hizi za *private* wapunguze maumivu kwa wazazi kwa kupunguza mzigo wanaowabebesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka katika shule hizi za *private*, naomba nami niongelee suala la mishahara ya Walimu. Katika hili, mengi yameshasemwa, lakini hoja ninayotaka kuizungumzia hapa ni kwamba Walimu katika Waraka wa Serikali wa mwaka 2009, mwezi Desemba, unataka Walimu wote wanaomaliza *degree* ya kwanza, waanze na mshahara wa ngazi ya *TGTS – D*. Lakini cha kushangaza ni kwamba hata wale Walimu ambao wanakuwa wameshavuka lile daraja D, lakini wakaenda kujiendeleza wakapata ile *degree* ya kwanza, wanaporudi makazini wanalazimishwa kuja kuanza tena na mshahara wa *Class* D. Sasa hapa nashindwa kuelewa, kama Mwalimu kutokana na uzoefu wake na miaka mingi ambayo ameitumikia nchi hii katika Wizara ya Elimu alishavuka lile daraja D, akaenda labda F, akaenda shule kujiendeleza, leo hii anaporudi ana *degree* yake mkononi, Mwajiri wake anamwambia unarudia katika mshahara wa *Class D*.

Waziri katika hotuba yake hajalizungumzia hilo na wala Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, naye hakulisema hilo. Naitaka Serikali ilete ufafanuzi na majibu ya kuridhisha ili kama wana nia ya kuwakatisha tamaa Walimu wasiende kujiendeleza, basi waseme kwa sababu haina maana mtu aende shule kujiendeleza halafu akirudi apunguziwe mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea suala la mishahara ya Walimu, kuna tatizo lingine la ada ya mitihani ya kidato cha Nne na kidato cha Sita. Serikali ilikuwa inatoza ada za mitihani ya kitaifa kwa Kidato cha Nne na Sita lakini ada hizi zilifutwa kwa madai kwamba Serikali itakuwa inazilipia. Lakini cha kushangaza ni kwamba ada za mitihani ya kitaifa katika Kidato cha IV na VI zilifutwa tu katika Shule za Sekondari za Serikali, lakini zinaendelea kutozwa katika Shule za Sekondari za Umma.

Mheshimiwa Spika, mimi naona hili siyo sawasawa kwa sababu Wazazi na walimiki wa shule hizi wanalalamikia tatizo hili. Nchi yetu ni moja, watoto wetu ni hao hao, iwe wanasoma shule za *private* au za Serikali lakini lengo ni moja la kupata watoto walioelimika. Kwa hiyo, kama suala lilikuwa ni kupunguza ada za mitihani kwa wazazi, basi ni vyema Wazazi wote watendewe haki wa shule za *private* kama ilivyo kwa Shule za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile sielewi sasa hii *issue* iko Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* au ni Wizara yenyewe inatakiwa isimamie? Nahitaji jibu katika hilo. Lakini pia kumekuwa na malalamiko ya usahihishaji wa mitihani katika Baraza la Mitihani. Muda unaotumika kusahihisha mitihani ni mdogo, siku hizi watoto wanaosoma shule zetu za Sekondari ni wengi, lakini muda wa kusahihisha mitihani ni mwezi mmoja tu. Tunaelewa unyeti na umuhimu wa suala la mitihani. Sasa kama Walimu watapewa muda wa mwezi mmoja tu, kwa kweli hawa Walimu wanakuwa wanafanyakazi kubwa usiku na mchana ili waweze ku-*meet* ile *dead line* ya mwezi mmoja.

Ni vizuri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Baraza la Mitihani la Taifa, wakaangalia upya namna ufanisi utakavyoweza kupatikana katika usahihishaji wa mitihani, ikiwa ni pamoja na kuangalia upya posho za Walimu wanaofanya kazi ya kusahihisha mitihani. Kwa kweli wamekuwa wakilalamika kwamba hela wanayopewa ni ndogo, ukizingatia kwamba wanafanya kazi usiku na mchana, Jumamosi na Jumatatu, siku zote za wiki, ili waweze ku-*meet* hiyo *dead line*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la Walimu kutokueleweka vizuri wanawajibika katika Wizara ipi. Je, Walimu wako utumishi, TAMISEMI, au wako Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi? Utata huu unafanya kumbukumbu za Walimu kupotea na inakuwa vigumu wanapokuwa wakifuatilia haki zao. Tunaliomba hili nalo liwekwe wazi ili kumbukumbu za Walimu ziwe sahihi, ijulikane wanawajibika kwa mwajiri mmoja na iwe rahisi wanapokuwa wakifuatilia mambo yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la uhaba wa Walimu. Tunajua kwamba kuna suala la uhaba wa Walimu, lakini labda nitoe wazo kidogo, pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Maafisa wengi ni Walimu na sidhani kama wote wana kazi ya kutosheleza kukaa ofisini. Tunapokuwa na *crisis* ya uhaba wa Walimu, kwanini Maofisa walioko Wizarani ambao nao ni Walimu wasipangiwe vipindi katika mashule mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wazo hili kwa sababu tumekuwa tukiwashuhudia hao maofisa wa Wizarani baada ya kazi wakiendesha *tuitions* mbalimbali katika shule, kumbe wanaweza kufundisha. Kwa hiyo, naomba hilo nalo hasa katika shule zilizo karibu wanaweza kupangiwa vipindi ili kuokoa suala la upungufu wa Walimu walau kwa kiwango kidogo.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi ya kusema, nashukuru kwa muda huu na naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika sekta hii muhimu. Sekta ya elimu, sekta ambayo iliwasaidia wenzetu wa nchi ya China na India kujikwamua kiuchumi baada ya kuwa wamepata matatizo magumu sana ya kiuchumi miaka ile ya 1960 na

wakaamua sasa kuitumia kikamilifu sekta ya elimu ambapo waliwaelimisha watoto wao na baadaye kuwatoa katika soko la ajira na ndiyo maana sasa hivi tunawaona wako juu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia, kuna simu ambazo nimezipata asubuhi kutoka kwa wananchi mbalimbali wakimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya na wengi wao ni wale ambao wamekuwa wakifuatilia masuala yao kuhusu haki zao katika mamlaka mbalimbali kwa miaka kama mitatu hivi wakawa hawakupatiwa ufumbuzi. Wakati mwingine wanapigwa danadana, barua zao hazijibiwi lakini walipoamua kuandika barua katika Ofisi ya Waziri Mkuu hawakwenda *physical* walijibiwa haraka ndani ya wiki mbili na matatizo yao yakatatuliwa ndani ya mwezi mmoja. Wanamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanamwombea maisha marefu na afya njema siku zote ili aendelee vizuri na majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue tena nafasi hii kuishukuru Wizara ile iliyokuwa ya Miundombinu kipindi kile ikisimamiwa na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa pamoja na mamlaka zote za Serikali ambazo zilihusika katika kutatua mgogoro wa ardhi baina ya *TBA* na Kata ya Reli kule Mtwara. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ndiyo iliyoniagiza, ikanipa maelezo kuhusu tatizo hili, nikalileta Serikalini, kwa kweli wanashukuru sana. Tatizo hili limetatuliwa vizuri na sasa hivi Kata ya Reli inaendelea na ujenzi wa shule hii ya Sekondari ya Reli na ndani ya muda mfupi inawezekana ikawa ni *High School.* Nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Mtwara, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo limenifanya kusimama, limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana, ni lile la uhaba wa Walimu katika nchi yetu pamoja na *un-equal distribution,* mtawanyiko wa Walimu ambao hauko sawa. Naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jitihada kubwa sana ambazo imefanya kudahili wanafunzi wengi katika Vyuo vyetu Vikuu ili kusomea Fani ya Ualimu. Kwa mfano, *University of* Dodoma peke yake tulikuwa na wanafunzi, kabla ya hawa wa mwaka wa tatu hawajamaliza, tulikuwa nao 9,000, tunao wengine katika vyuo vingine jambo ambalo linatupa matumaini kwamba ndani ya muda mfupi tunaweza tukatatua tatizo hili la Walimu.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kukataa kwamba bado tuna uhaba wa Walimu katika shule zetu za msingi na za sekondari na kubwa zaidi, changamoto tuliyonayo, ni Walimu wa Sayansi. Walimu wa Sayansi hawatoshi, ni wachache sana. Inawezekana katika nchi yetu pengine upungufu wa hawa Walimu wa Sayansi, ni zaidi ya robo tatu. Nadhani tunaafikiana sote kwa pamoja kwamba bila ya wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, tutaendelea kuwa na upungufu wa Madaktari, tutaendelea kuwa na upungufu wa wataalamu wa afya na hasa tukizingatia kwamba sasa hivi tuna mkakati wa kuweka vituo vya afya karibu kila Kata katika nchi yetu. Tutakuwa na shida ya Wahandisi, Walimu wa Sayansi katika ngazi zote, shule za msingi, sekondari na hata Vyuo Vikuu, tutakuwa hatuna wataalamu wengi wa kompyuta na hasa kwa mfano katika vyuo vyetu vikuu, Walimu wa Sayansi ni wachache na utakuta kwa mfano Chuo Kikuu cha Dodoma, Walimu wa Sayansi pale wengine wanatoka nje. Walimu wa Sayansi, Hesabu wanatoka India pamoja na nchi zingine. Kwa hiyo, tunahitaji sisi wenyewe tuwe na msingi mzuri

katika masomo ya sayansi ili kusudi tuweze kukidhi hii haja ya upungufu wa Walimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu wa jinsi gani tatizo la uhaba wa Walimu hili lilivyokuwa kubwa katika nchi yetu. Mkoa wa Mtwara, tuna vitabu vingi tu vya kutosha, vitabu vya aina zote tunavyo, lakini tuna tatizo kubwa, tuna shule 128 za Serikali, mahitaji ya Walimu wote ni 3,101, Walimu waliopo ni 1,187 na tuna upungufu wa Walimu 1,914, kwa asilimia ina maana kwamba tuna Walimu asilimia 38 tu ya mahitaji lakini kwa upande wa Sayansi upungufu ni mkubwa zaidi. Kwa sababu tuna mahitaji ya Walimu wa Sayansi 1,170, Walimu tulionao ni 231, upungufu ni 939. Kwa asilimia ni kwamba tuna Walimu asilimia 19 tu ya mahitaji, hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwa uchambuzi zaidi, Walimu wa *Biology* tunaowahitaji kwa Mkoa wa Mtwara, ni 265, Walimu ambao tunao 71. *Chemistry*, Walimu tunaohitaji ni 269, tulionao ni 48 na *Physics*, Walimu 259 ndio tunaowahitaji tulionao 32. Ukienda kwenye Hesabu, tunahitaji Walimu 377, lakini tunao Walimu 80 tu. Kwa hiyo, matatizo ni makubwa lakini hata hivyo Mkoa ule unajitahidi kuhamasisha ili kusudi waweze kusaidiana. Shule zile ambazo ni za karibu utakuta Mwalimu wa *Biology* anaweza akafundisha shule zaidi ya mbili au tatu wakisaidiana, wa *Chemistry* hivyohivyo, lakini bado utakuta kuna shule ambazo mtoto anaanza Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne hajafundishwa masomo haya niliyoyataja hata siku moja. Kibaya zaidi na cha kusikitisha ni kwamba wakati wa mitihani bado wanapelekewa mitihani ya masomo haya. Sasa sijui tunatarajia nini na hili suala limeturudisha sana nyuma, ufaulu wetu umekuwa mdogo kutokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mapendekezo tu, kwa baadhi ya wananchi ambao tulikuwa tukiongea nao, walikuwa wanapendekeza kwamba wanafunzi hawa ambao hawakusoma hata siku moja masomo haya wafanye hii mitihani kwa ridhaa yao, wakubali wao wenyewe, kwa sababu wako wengine ambao wanajisomea pengine wanafundishwa nyumbani, wanajitahidi kusoma, wanaweza wakafaulu. Kwa hiyo, labda wajaze fomu ili kusudi kama wataweza kufanya hii mitihani wa-*indicate* kwamba watafanya lakini kama hawana chanzo chochote kile cha kuelimishwa, ni vizuri basi wasifanye mitihani hii ambayo hawakufundishwa hata siku moja inachangia sana kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine kuhusiana na hili ni kwamba Serikali kwa ujumla kama wenzangu walivyokuwa wamependekeza, iweke vivutio kwa ajili ya Walimu ili kusudi wengi waipende fani ya Ualimu. Kwa upande wa Walimu wa Sayansi, Serikali iweke sasa vivutio vya pekee. Kama nilivyosema kwamba kuna shule nyingine ambazo ziko mbali sana, sio rahisi kusema kwamba utamtoa Mwalimu mahali fulani aende kule akafundishe, sio rahisi sana lakini kama atakuwa amepewa usafiri, akapewa gari ambayo inatumia mafuta kidogo, anaweza akaenda shule nyingi zaidi angalau akawapa mwanga ili kusudi waweze kutumia vizuri vile vitabu ambavyo wanakuwa wamepewa, inaweza ikasaidia sana. Hivi sasa tumesikia kwamba baadaye ule mkongo wa mawasiliano unaweza ukatumika ili kusudi waweze kuwa wanafundisha *distance*

*learning,* inaweza ikasaidia zaidi lakini kwa kuanzia basi tuwawezeshe kwa kuwapa usafiri.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni kwamba labda wataalamu wa Wizarani waanze sasa kufanya ziara katika shule zile za Kidato cha Tano na Sita ili kusudi kuweza kuwahamasisha watoto wale wanaosoma masomo ya Sayansi na kuangalia vipaji vyao ili waweze kwenda kusomea fani ya Walimu watakapokuwa wamemaliza masomo yao ya Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kwa kweli napenda kusema kwamba labda Wizara inachangia sana katika suala la kuwafukuza Walimu katika fani hii kutokana na kuchelewesha kuwapandisha madaraja na kuchelewesha pia kubadilisha vile viwango vya madaraja waliyonayo. Walimu wengi wapo ambao unakuta ni Walimu lakini wanabadilisha fani anaenda kusoma tena *B.COM*, anakwenda kufanya kazi Benki na wengine wanaenda kuwa wafanyabiashara. Kwa kweli tunawafukuza wenyewe, hili jambo la kuwa-*retain* Walimu wetu linawezekana sana, wala sio siri kwamba Walimu wanahama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mtawanyiko ambao sio sawa, *un-equal distribution,* wengi wanapenda kukaa Mijini, kwenye Manispaa, maeneo ambayo yana huduma za maji, umeme, huduma za kifedha, ndipo ambapo wengi wanapenda kukaa pale, wakipangiwa vijijini wanaondoka. Sasa utakuta watu wamesoma pamoja mwingine utamkuta yuko Manispaa pale Mtwara, mwingine amepelekwa Mihambwe kule Tandahimba, hakuna umeme, maji ni shida tupu. Nilichokuwa nataka kupendekeza ni kwamba Walimu hawa wanaopelekwa mbali wapewe Posho ya Mazingira Magumu ili angalau na yeye aweze kununua walau *solar* hata ndogo a-*charge* simu yake, apate ule mwanga ambao anauhitaji kwa ajili ya maandalizi ya masomo, anaweza akanunua hata vifaa vya kuhifadhia maji na vitu vingine, lakini hata hivyo anaweza akapata pia nauli ya kufuatilia huduma za kibenki katika Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tu kwa kifupi, labda pendekezo tu kuhusu hii Bodi ya Mikopo. Kumekuwa na matatizo pengine ucheleweshaji mkubwa kuhusu utoaji wa mikopo, lakini nina wasiwasi kuhusu ufuatiliaji wa hii mikopo. Napendekeza kwamba Bodi ya Mikopo iwe na dirisha katika Mabenki yetu Wilayani. Nadhani hii inaweza ikasaidia sana na hasa kutakapokuwa na vitambulisho vile vya kitaifa, itasaidia sana katika uharakishaji wa utoaji mikopo na nina uhakika kwamba watakuwa wana-*link* Benki na Makao Makuu. Watakapo-*link* basi tatizo lile la ugomaji kutokana na ucheleweshaji wa mikopo linaweza kwisha. Hata hivyo, ule urejeshaji wa mikopo pia utakuwa rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie tu kwa kuomba lile suala la kutoa elimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Serikali inatoa tamko gani kwa sababu ilituma Tume ikazunguka nchi nzima ili kusudi kuweza kuona ni jinsi gani wanaweza wakawasaidia wale wanafunzi ambao wanabeba mimba mashuleni. Kwa hiyo, napenda kupata tamko kwa Serikali kwa ujumla imeona nini baada ya matokeo ya hii Tume.

Mheshimiwa Spika, nisingependa nigongewe kengele ya pili, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia tatizo la Walimu. Katika Jimbo la Mbozi Magharibi lenye Shule za Sekondari 11, lina uhaba mkubwa wa walimu. Kwa wastani, kila Sekondari ina walimu watatu, lakini katika maeneo ya vijijini, Sekondari nyingi zina walimu chini ya watatu. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri katika mwaka huu wa fedha, atupangie walimu wa kutosha ili waweze kukidhi uhaba huo na kufanya ubora wa elimu uongezeke kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Kata waweze kupata elimu bora badala ya bora elimu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mbozi Magharibi hakuna Sekondari hata moja ambayo haina maabara kwa masomo yote ya Sayansi. Hivyo basi, tunaomba Wizara itutengee fedha angalau kwa mwaka huu wa fedha, tusherehekee miaka 50 ya Uhuru angalau kwa shule chache kuwa na Maabara.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lina uhaba mkubwa wa vitabu vya kiada na ziada vinavyoendana na mitaala ya elimu katika Taifa, hivyo kufanya wananchi wa Mbozi Magharibi kukosa elimu bora. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ituangalie.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mbozi Magharibi hakuna Sekondari hata moja yenye umeme wa jua *(Solar Power System)* zitakazowasaidia wanafunzi kusoma, maana katika Jimbo letu ni Kata moja moja tu yenye umeme wa *Grid* ya Taifa. Hivyo basi, ili kuendana na sera ya ubora na usawa katika elimu, tunaomba sasa Wizara ya Elimu ipange mkakati wa kusambaza umeme wa jua katika shule zote za Sekondari Jimboni Mbozi Magharibi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi kushikiri kwa asilimia 100 katika ujenzi wa nyumba za walimu, lakini Serikali haipo tayari kuongeza nguvu hususan katika kumalizia *(Finishing)* za nyumba hizo. Hivyo basi, tunaomba mwaka huu wa fedha itenge fedha za kutosha ili tumalizie ujenzi katika Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa huduma za maji mashuleni, unahatarisha hofu ya kuzuka magonjwa ya milipuko kama Kipindupindu mashuleni, kwani Jimbo la Mbozi Magharibi shule zote hazina maji kwa ajili ya wanafunzi kutumia kama vile wanapokwenda kujisaidia shuleni. Hivyo, tunaomba Wizara ichimbe visima katika shule hizo ili tuokoe afya za wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na udogo wa malipo ya walimu, bado walimu wa Jimbo la Mbozi Magharibi hawajalipwa madeni na malimbikizo yao ya mishahara hususan pia kwa walimu wapya ambao hawajalipwa mishahara ya mwezi Februari na

Machi, 2011. Je, Serikali itueleze ni lini watalipwa mishahara yao, kwani huku ni kurudisha nyuma morali wa kufundisha kwa walimu hao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nguvukazi ya wananchi ikiwemo kuchangia fedha katika ujenzi wa madarasa, bado Serikali inachelea kupanga fedha za kutosha katika kumaliziai madarasa hayo. Hivyo basi, tunaomba Serikali kwa mwaka huu wa fedha ipange fedha za kutosha ili tuweze kumalizia ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa Chuo cha Ufundi/*VETA*: Jimbo la Mbozi Magharibi ambalo ndiyo Wilaya mpya ya Mombas halina kabisa Chuo chochote cha Ufundi, hivyo basi, kuonekana kwamba tumetengwa na Serikali. Hivyo, tunaomba Serikali itutengee fedha ili nasi tupate chuo kimoja cha ufundi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, imani yetu sote ni kwamba elimu ni ufunguo wa maisha. Ukweli huu uko ndani ya falsafa kuwa taaluma zote zilizopo zinategemea Wizara ya Elimu. Hakuna Waganga, Wahandisi, Maafisa Kilimo, Waganga wa mifugo, Mafundi wa kila aina, Waandishi wa Habari, Wanazuoni wa taaluma mbalimbali wanatokana na sekta hii muhimu ya elimu. Kwa Jimbo letu na Wilaya yetu mpya ya Mbogwe tunayo mahitjaji ya msingi ya kupta Shule za Kidato cha tano na sita na Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Spika, Jimbo letu kimsingi tunahitaji japo Shule za *'A' Level* zipatazo mbili. Napendekeza shule za Mbogwa na Masumbwe Sekondari zianzishwe kidato cha tano na sita. Hatua hii itaboresha kiwango cha elimu jimboni kwa kuwa jimbo letu na Wilaya yetu imo ndani ya Mkoa wa Shinyanga ambao mara nyingi umekuwa haufanyi vizuri katika matokeo ya mitihani ya Kitaifa katika ngazi mbalimbali. Ni kwa kuboresha sekta ya elimu ndipo tutakapopata ukombozi wa kweli dhidi ya maadui watatu wakuu katika nchi yetu ambao ni ujinga, umasikini na maradhi.

Mheshimiwa Spika, katika karne hii ya 21 ambayo ni ya Sayansi na Teknolojia ambamo elimu ndicho chombo kinachotamalaki katika kuleta mapinduzi katika Jimbo la Mbogwe, Taifa na katika ngazi ya kimataifa, Jimbo letu linahitaji uwekezaji wa kutosha katika Sekta ya Elimu ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi katika Sekta ya Afya, Kilimo na kiuchumi hakika.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga umekuwa ukikabiliwa na matatizo mbalimbali ya kijamii kama vile ukiukwaji wa haki za binadamu kwa baadhi ya watu kujihusisha katika vitendo vya kijinai vya kuua wanawake pamoja na walemavu wa ngozi, yaani *albino*. Upigaji ramli chonganishi umekuwa chanzo cha mauaji ya kinyama na kuwa na athari katika maendeleo na kudidimiza haki za makundi haya ya wananchi ambapo kwao suala la amani na utulivu linakuwa ni kitendawili kwa kuwa wanakuwa hawana uhakika juu ya nini kitatokea katika muda unaofuata. Ukombozi na mapinduzi ya

kifikra miongoni mwa wananchi utatokana na uwekezaji katika Sekta ya Elimu jimboni Mbogwe na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja lakini naiomba Serikali itusaidie kupata Chuo cha VETA jimboni na Wilayani Mbogwe ili kuwapatia stadi mbalimbali za maisha ili hatimaye waweze kujiajiri na kuboresha maisha yao na kupigana na adui umasikini.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uanzishaji wa vidato vya tano na sita katika Shule za Sekondari Mbogwe na Masumbwe, ni matarajio yangu kuwa elimu ndiyo nyenzo pekee itakayoleta mwamko mpya wa kifikra miongoni mwa wananchi wa Jimbo la Mbogwe na nchi nzima kwa ujumla.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, suala la migomo katika Vyuo vyetu imeshakuwa ni tabia ya wanafunzi kugoma ovyo kwa lengo la kudai maslahi yao. Lakini kumbe siyo kweli. Hili ni tatizo lao wenyewe wanafunzi kwa kuendekeza Siasa vyuoni, kwani suala la maslahi au mikopo, lipo tokea zamani na huwa yanatolewa maslahi kwa utaratibu uliowekwa. Hivyo, nashauri kwa upande wa Serikali itimize wajibu wake kikamilifu kwa kuwapatia maslahi wanafunzi kwa wakati. Vilevile Serikali iweke mikataba maalum baina ya Serikali na mwanafunzi kwa lengo la kudhibiti suala hilo lisiendelee kuwa kero katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo ya shule, kuna baadhi ya majengo ya Shule yameshakuwa mabovu na yanahitaji kufanyiwa ukarabati wa haraka sana. Hivyo, naishauri Serikali kuweka mpango mkakati wa kuyafanyia matengenezo kwa majengo yote ya shule ambayo yameshachakaa.

Mheshimiwa Spika, naamini kila mtanzania anajua kazi kubwa ya kazi ya ualimu, na sisi sote tusingefika hapa kama hatukusomeshwa vizuri na walimu hao. Aidha, kila miaka ikienda mbele maslahi ya walimu yanazidi kupungua kutokana na kuzidi kwa hali ngumu ya maisha. Hivyo, naishauri Wizara na Serikali kuanzisha posho maalum kwa ajili ya kulinda maisha ya walimu ili posho hiyo iweze kumsaidia, kwani nahisi sekta hii itakosa walimu wa kufundisha Shule zetu za *Primary* na Sekondari hasa zile za vijijini na tunaweza kukosa Taifa lililosoma hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu shule nyingi hazina au hawapelekewi vifaa vya kutosha kwa kuwafundishia vijana wetu. Hivyo, naishauri Serikali kuzipatia Shule zote vifaa vya shule pamoja na kuimarisha maabara, kwani dunia tunayokwenda nayo ni ya Sayansi na Teknolojia, hivyo tunahitaji mafunzo ya Sayansi kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuanzisha shule za *VETA* kwa upande wa Zanzibar.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu hatma ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wamefukuzwa kutokana na mgomo na utaratibu gani ambao unatumika kuwarudisha wanafunzi hao ili uonevu usiwepo.

Mheshimiwa Spika, je, ili kuondoa migogoro inapotokea, Serikali haioni kwamba huu ni muda muafaka wa Serikali kuhakikisha wanatenga fedha ili wanafunzi hao waende *field*?

Mheshimiwa Spika, tumesikia kuna mikakati ya kujenga *VETA* kila Wilaya. Je, Serikali haioni haja ya kukarabati Vyuo vya Ufundi vilivyo Mikoani, hasa vilivyotelekezwa kikiwemo kile Chuo cha Kyaramo cha Musoma vijijini ili vijana waweze kupata ujuzi na kujikwamua na ajira kwa kujiajiri wenyewe?

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, napendekeza kwanza wanafunzi wa Vyuo Vikuu mikopo yao ambayo huwa inasumbua watengewe pesa kwa ajili ya mwanzo wa mwaka ili kuepuka usumbufu wanaoupata kwa ajili vijana wengi wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Wizara wengi wanafanya kazi kwa mazoea. Mara nyingi huwa hawathamini watu wanapokwenda kuwaona. Kwa mfano, wakati nilipofika Baraza la Mitihani niliongeza na mtu kwa simu bila kumwona mhusika. Huu ni utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu nina shule ya Msingi *VETA* iko Mnyuzi, hadi leo Serikali haijaendelezwa. Je, Serikali ina mpango gani na hiki Chuo cha *VETA* Mnyuzi? Katika Jimbo langu, nina Sekondari zaidi ya 25, lakini hakuna *Form V* na *VI*: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *high level* katika Jimbo langu? Pili, ni lini walimu watasambazwa vijijini ambako kuna walimu wengi wanaowekwa mjini tu? Lini walimu watasambazwa vijijini?

Mheshimiwa Spika, kama kuna vitabu vya kusomea, basi Sekondari zangu hazina. Katika Wizara ya Elimu napenda kusema ya kuwa Katibu Mkuu awe makini kwani tunapokwenda kwenye shida, apokee wageni, asipende tu watu wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, swalil la msingi hapa inawezekana vipi Idara za Elimu ya Msingi na Sekondari ambazo ni mihimili ya Idara zote za Wizara ya Elimu tena zenye majukumu makubwa yakiwemo ya kusimamia ubora wa elimu katika ngazi hizo zilinganishwa na vitengo vya manunuzi na Ugavi?

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo kwa walimu wapya kupata fedha zao za kujikimu baada ya kuripoti katika maeneo yao ya kazi. Mfano tarehe 24 Januari, 2011 walimu hawa walipewa barua za kuripoti kwa Wakuu wa Vyuo ambapo wangezikuta barua zao za ajira pamoja na fedha za kujikimu. Lakini walimu hawa waliotokea vyuoni na hii ndiyo ajira yao ya kwanza kwa Wakuu hao wa Vyuo hawakupata barua wala fedha za kujikimu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa hawa walimu ndiyo ajira yao ya kwanza na huko wanakopangiwa hakuna ndugu wala rafiki, hivyo kunawasababishia kuishi katika mazingira magumu sana hasa kwa walimu wa kike.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Vyuo walipofuatilia kwa Katibu Mkuu walijibiwa kuwa Walimu wa Vyuo vya Ualimu walisahaulika. Hivi kweli inaingia akilini kweli jambo hili likatokea na kupewa majibu mepesi kiasi hicho? Tunaomba Wizara iwe makini sana katika masuala yake.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji walimu katika vyuo vyetu, katika Sekondari na Shule zetu za msingi, hivyo tuhakikishe walimu wetu wanapata fedha zao kwa wakati ili waweze kufanya kazi zao kwa furaha kwa sababu tusipofanya hivyo tutaliingiza Taifa letu katika mgogoro mkubwa sana hasa wa kielimu. Ili tupate elimu bora ni lazima watoa elimu ambao ni walimu wawe na maisha mazuri, walipwe vizuri na kwa wakati ili wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo lingine kubwa ambalo linawafanya walimu washindwe kukaa au kuripoti kwenye maeneo waliyopangiwa nalo ni tatizo la nyumba. Nyumba ni kitu muhimu sana katika maisha ya kila binadamu. Katika maeneo ya vijijini kuna tatizo kubwa sana kwa sababu hakuna hata nyumba za kupanga na hata ukibahatika kupata inakuwa na hali mbaya na haina hadhi ya kukaa mwalimu ambaye ametoka maeneo tofauti na vijijini na hivyo kufanya walimu hawa kugoma kwenda kwenye maeneo hayo. Hivyo, tunaiomba Serikali kuhakikisha tatizo hili linakwisha ili watoto wetu waweze kupata elimu bora ambayo itawasaidia katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi kwenye Taarifa ya Habari imeonyeshwa shule moja ilivyo na hali mbaya ya matundu ya vyoo hali ya shule hiyo ni mbaya kwanza ni chakavu, machafu na pia hayatoshi kwa idadi ya wanafunzi waliopo. Hii ni hatari kwa aya ya watoto wetu na inaweza kuhatarisha maisha kwa watoto. Hivyo basi, tunaiomba Serikali itenge pesa za kutosha katika eneo hili la matundu ya vyoo.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa michango yao kwa Taifa letu. Aidha, napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara/Serikali iwaangalie walimu wa Shule za Msingi za mazoezi kwani kuna tabia ya walimu wa kada hiyo kuanzia kazi hadi kustaafu katika kituo hicho hicho. Hii inadumaza sana ufanisi wa kazi. Ikiwezekana, basi wabadilishwe kutoka Ligula (Mtwara) hadi Nambambo (Nachingwea), Manumbu (Korogwe) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wako walimu waliojiendeleza hadi kupata Shahada ya Kwanza na Shahada za Uzamili wakiwa kwenye shule hizi za mazoezi, lakini

hawapangiwi nafasi zinazofanana na Shahada walizonazo na hawa ni wengi. Hivi ni kwanini baada ya kupata au kufuzu Shahada hawahamishiwi kwenye maeneo yanayofanana na elimu zao? Mwalimu wa Shahada anafundishaje Shule za Msingi huku Sekondari zikiwa hazina Walimu? Ninayo orodha ndefu ya walimu wa aina hiyo pale Chang'ombe na Ligula.

Mheshimiwa Spika, ilani ya uchaguzi ya CCM 2005 - 2010 iliahidi Chuo cha Ualimu Mtwara kupandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu Kiambata, lakini hadi leo hakuna hatua iliyochukuliwa kukidhi ahadi hii. Napenda kupata maelezo ya kina, kwanini hadi leo ahadi hii haijakamilishwa?

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopo ni kuwa walimu wa somo la TEHAMA hupangiwa kufundisha somo hilo bila *skills* na *knowledge* za kutosha kwa somo hilo. Ni vyema basi walimu wanaopangiwa somo hili wapewe kozi za Kompyuta za mara kwa mara ili waendane na wakati. Wengi wao wanafundisha somo hilo bila wenyewe kuwa na uelewa wa kutosha na pia bila vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, dunia hii ya sasa, masomo huria ni mchango mkubwa wa maendeleo duniani. Aidha, Serikali hupunguza sana gharama za uendeshaji. Ni vyema basi Chuo chetu kikuu huria cha Tanzania kikaongezewa bajeti ili kuokoa Watanzania wengi ambao watakosa nafasi kwenye *Conversional University*.

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa wanafunzi wetu wa Shule za Msingi na Sekondari utegemea sana mchango wa mwanafunzi mwenyewe mzazi/mlezi na mchango wa mwalimu kwa mwanafunzi/wanafunzi. Matokeo ya Kidato cha Nne mwaka 2010 yalishuka sana kukiwa na sababu mbalimbali. Lakini pamoja na sababu nyingi, baadhi ni Serikali kutoondoa yale yaliyovunja ari kwa walimu. Aidha, wanasiasa walichangia sana kuwasogeza vijana wetu kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu na kuacha majukumu yao ya kutafuta elimu na sasa sisi wanasiasa tunailazimu Serikali baada ya matokeo yale mabovu. Hata ushiriki wa wazazi/walezi kwa elimu ya vijana wetu siyo nzuri.

Natoa ushauri kwamba wadau wote wa elimu ya vijana wetu tuache yale yaliyo vikwazo kwa maendeleo ya elimu ya vijana wetu ili Taifa letu lipate wataalam wenye uwezo na kusukuma mbele Taifa hili. Kila mmoja wetu asaidie elimu yetu kutukuka na kuachana na yanayoturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwa maandishi hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kuchangia mambo matatu. Mambo hayo ni Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Walimu.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Elimu ya Awali, kwanza kabisa kama tunataka elimu yetu iwe bora, ni lazima mtoto aandaliwe kwa Elimu ya Awali na hivyo basi, mtoto asomeshwe kwa vitendo ili atakapoingia katika Elimu ya Msingi asiwe mgeni na masomo atakayoyakuta huko. Maana katika Elimu ya Awali, mtoto anakuwa au shule nyingi za

awali, watoto huwa wanasomeshwa masomo kwa Kiingereza hasa zile za kulipia. Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba hata hizo za Serikali ambazo ziko kwenye Halmashauri, basi nazo ziboreshwe angalau mwanafunzi akitoka hapo akiingia Shule ya Msingi, anaendelea na siyo kuanza Alifu.

Mheshimiwa Spika, kwanini tusiboreshe mitaala yetu ya Elimu ya Msingi ili mtoto anapotoka katika Elimu ya Awali asiyaone masomo mageni? Kwani Elimu ya Awali huwa wanasoma Kiingereza zaidi. Baadhi ya shule cha kusikitisha anapoingia elimu ya msingi ni Kiswahili kitupu, kwa hiyo, hapo unamrudisha nyumba na ndiyo maana elimu yetu inakuwa bora elimu tu na siyo elimu bora.

Mheshimiwa Spika, nikija katika elimu ya msingi, wakati sasa umefika kurejesha elimu hii ya msingi ya kusoma kwa vitendo. Nakumbuka niliposoma mimi kipindi cha Sayansi huwa tunapelekwa *laboratory* kusoma kwa vitendo, tunafundishwa jinsi ya kuchuguza kitu kwa *Microscope*, tunajifunza kwa makundi. Hali kadhalika katika siku za *project* tunapelekwa shamba kulima, kupanda na kuvuna. Pia wakati wa mavuno au kazi za mikono hapo inakuwa tunafundishwa ubunifu wa kutengeneza vitu kwa mikono.

Mheshimiwa Spika, naomba haya yote yarejeshwe, kwani mtoto akitoka hapo siyo lazima apate ajira Serikalini, yeye atakuwa na uwezo wa kujiajiri mwenyewe kwa sababu hiyo *VETA* siyo wananchi wengi wanaoweza kulipia watoto wao kwenda pale kusoma, jamani lazima tuwafikirie walio wengi siyo matajiri, ni masikini hasa.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kwa walimu ni watu waliosahaulika kabisa hata mishahara yao basi haikidhi haja. Kwa wanavyolitumikia Taifa hili karibia toka Rais hadi Mwenyekiti wa Kata anatokana na Mwalimu. Imefika wakati sasa tuwape motisha walimu wetu ili bado waendelee kusomesha kwa bidii ili Taifa lipate wataalam. Tunakoendea, tuwatunze walimu wetu. Katika bajeti hii shilingi bilioni 525.941 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwanini pesa hizi zisitiwe kwenye kwenye mishahara ya walimu ili basi wapate kufanya kazi kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, katika pesa za maendeleo, shilingi bilioni 139.632 ni pesa kidogo sana. Kwa kipindi hiki cha sayansi na teknolojia, maendeleo gani utayafanya? Naomba hapa nifahamishwe.

Mheshimiwa Spika, kwanini hatubuni njia mbadala ya haya yote ili tuwe na elimu bora ili nayo iweze kutoa walimu bora pia tupate wanafunzi bora tuondokane na bora elimu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa nia njema na nzuri ya kuhakikisha kuwa elimu inakuwa haki ya kila mtoto wa Kitanzania kwa kujenga Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina changamoto nyingi sana, naomba niziguse chache zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosisitiza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Idara ya Ukaguzi inatakiwa iimarishwe, ipewe fedha za kutosha, vitendea kazi kama magari na ofisi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Kwa sasa Idara hii haifanyi kazi yake, haikagui Shule za Msingi kama inavyotakiwa na kwa sekondari haifanyi kabisa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za *TSD* zilifunguliwa kwa nia njema ya Serikali ili kuwezesha mambo muhimu ya uajiri ikiwemo upandishwaji wa vyeo na nidhamu kwa ujumla. Kwa sasa *TSD – Teachers Service Department* haifanyi kazi, wanategemea wapewe uwezesho na Wakurugenzi wao na katika Halmashauri ambazo mapato ni hafifu, basi hawafanyi kabisa vikao wanavyopaswa kufanya. *TSD* imekuwa kijiwe cha walimu. Kama Serikali inaona haiwezi ku-*allocate* fedha na vitendea kazi, ni vyema isianzishe Idara ambazo hazitakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya walimu siyo mikubwa, wote tunakubaliana, na zilizo benki wanazopaswa kuchukua mishahara, Mwalimu anaweza akasafiri umbali wa kilometa 97 hadi kilometa 100 kwenda kufuata mshahara tena kwa usafiri wa pikipiki na malori. Naomba Serikali iwaangalie walimu hawa kwa jicho la huruma ili wapewe posho maalum kwa mazingira magumu, itawasaidia walimu na itawatia moyo na kuwafanya wapende kufanya kazi hata vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ilivyo Tanzania wanaokwenda kusomea ualimu wanaonekana kama wameshindwa kupata kazi/kozi nyingine yoyote, kwa hiyo *last option* ni ualimu, hata jamii inaona hivyo. Mtoto anayemaliza *Form IV* anaambiwa hee, hata ualimu umekosa? Ina maana ni kitu cha mwisho, hata *pass* kwa wanaotakiwa kwenda vyuoni *Division III* na *IV points 28*, kwanini wasipelekwe wa *Division I* na *II*? Zamani hata waliopata *Division I* na *II* kwa Vyuo vya Diploma, kwa mfano Mkwawa, Korogwe, Shycom tulikwenda tuliopata *Division I* na *II* na sio waliofeli.

Mheshimiwa Spika, elimu ni haki ya kila mtoto ikijumuishwa na wale waliopata mimba. Watoto wa kike wanaopata mimba wanahitaji elimu zaidi kuliko watoto wengine kwa mahitiaji yake na mtoto atakayezaliwa. Tanzania sasa ina mimba za utotoni kwa kiwango kikubwa. Asilimia 25 ya wanawake chini ya miaka 18 tayari ni wazazi. Kwanini Serikali isitilie mkazo suala la watoto wa kike wanaofukuzwa kwa mimba shuleni warudi kusoma? Kwanini watoto wanaozaliwa waadhibiwe kwa kuzaliwa kwao? Ni watoto *Innocent,* wasinyimwe haki ya kutunzwa vizuri. Ikumbukwe kwamba mimba nyingine ni za kubakwa na *'force sex',* inakuwaje wanaadhibiwa? Serikali ichukue hatua na siyo kutafakari.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wanalalamika kuwa walimu wanaopangiwa kwenye Halmashauri zao hawaendi kuripoti katika vituo vyao ambapo fedha zao zinakuwa zimepangwa na wakati mwingine wanapewa wanakwenda kuripoti tu na kuondoka: Je, fedha hizo huwa zinakwenda wapi? Nashauri wale

wanaoripoti na kuondoka wakiwa wamechukua pesa za kujikimu, watafutwe, wadaiwe, warudishe hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko ya mitaala linaathiri sana mtiririko wa elimu yetu. Kama mabadiliko hayo ni muhimu, sawa. Tatizo, walimu hawapewi mafunzo ya mabadiliko hayo na vitabu vinakuwa havijafika kwenye shule. Mabadiliko ya mitaala haviendi sambamba na nyanja zake husika. Lingine, wakati walimu wanaanza kuzoea mitaala wanayotumia, mabadiliko yanatokea, hilo haliwapi nafasi nzuri ya kufundisha kwa uzoefu wao.

Mheshimiwa Spika, bado sikubaliani na Mtindo wa mtihani wa *Multiple choice* hata kama *Marking Scheme* inaonyesha kwa sasa kutakuwa na sehemu ya kuonyesha njia, kwa somo la hesabu, sawa. Je, kwa masomo ya Sayansi na lugha? Historia na mengine hakutakuwa na eneo la onesha njia ya kufikia jibu? Je, hapo mtoto atapimwa stadi gani, kama sio atafaulu kwa bahati nasibu tu?

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaipongeza Wizara kwa kupasisha watoto wa kike, kufaulu masomo ya sayansi. Vilevile natoa shukrani za ziada kwa kipindi kile mlivyoweza kuzuia uchakachuaji wa mitihani, kwani tayari wazazi na walimu pamoja na wanafunzi walikuwa hawakazani katika masomo, anajua kwamba mwisho wa mwaka Mzee yupo, atasaidia kununua mtihani. Lakini Serikali ilipofanya udhibiti katika elimu kuzuia kuchakachuliwa, hapo tuliona walimu na wanafunzi kushindwa kuchakachua. Iliyobakia Serikali kuzidisha bidii ya kusomesha walimu na pia kuwajali walimu kimaslahi ili kuwazidishia nguvu za kuzidi kuipenda kazi yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kutoa msukumo wa kukiendeleza Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwani hata wale waliokata tamaa ya kusoma, wanaweza kujiunga na kujiendeleza ikiwa na sifa ya kujiunga. Lakini naiomba Wizara kutilia mkazo kwa Zanzibar (Unguja) ukiangalia kielimu baina ya Pemba na Unguja, vijana kutoka Unguja wapo nyuma kielimu. Hivyo, zidisheni nguvu kwa Unguja ili wazee wa vijana wetu wajiunge kwa wingi katika Chuo hicho. Katika ukurasa wa 45 kifungu cha 78(d) kinaelezea kufanikisha kupatikana kwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vituo na ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za vituo katika Mikoa ndani yake ipo Pemba (ekari nne). Sasa nimeshitushwa, mbona Unguja haikuwekwa au kuna mpango mwingine wa mafanikio? Naomba kupata jibu kwa suala hilo.

Elimu ya watu wazima: Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuamua kuanzisha Elimu ya Watu Wazima ili kila mtu aweze kufuta ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu, kisomo hicho sasa kimeshuka kwa ajili ya Serikali kutowajali walimu waliokuwa wanajitolea kusomesha wazee wetu.

Elimu ya watu wazima ni kwa Tanzania nzima, lakini ukurasa wa 58 unazungumzia kwa baadhi ya mikoa na kanda. Inaonesha kwamba Serikali bado inashindwa kutilia nguvu kwa kusomesha Tanzania nzima. Tatizo ni hakuna walengwa/wodini au ndio Wizara kushindwa kutekeleza ilani ya CCM inayotaka elimu

kwa wote. Hiyo tathmini ya mwaka 2000 - 2010 itaanza lini na tutapata taarifa yake mwezi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, inaonekana kuwa ruzuku iliyotengwa kwa ajili ya wanafunzi haziwafikii ipasavyo, pia kuna uelewa mdogo kwa Walimu Wakuu kuhusu ruzuku ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kuwa walimu wakuu wengi hawaelewi ni kiasi gani cha ruzuku wanatakiwa kukipata kwa mwaka kutokana na idadi ya wanafunzi na badala yake kujulikana zaidi Wilayani ambapo fedha hizo au ruzuku haifiki yote shuleni na walimu kuridhia kwa kuwa hawaelewi kiwango maalum wanachotakiwa kukipata. Hivyo kupelekea kutopata pesa wanazostahili kuzipata. Mfano, Shule ya Msingi kupata Sh. 5,000/= badala ya Sh.10,000/= na Shule ya Sekondari kupata Sh. 7,500/= badala ya Sh. 25,000/= *(URT, PETS 2009, MMES)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza/nashauri Walimu wote Wakuu wapatiwe nakala au kitabu cha *MMEM II*. Ili kuwa na uelewa, ni kiasi gani wapate na kila mwanafunzi anastahiki kiasi gani ili kuzuia ufisadi katika hili? Pia ningependa Waziri atueleze pesa nyingine huwa zinakwenda wapi na zinafanyiwa nini wakati hazifiki mashuleni kwa walengwa ipasavyo? Mfano, mwaka 2009/2010 kulikuwa na mapungufu ya shilingi bilioni 2.5 sasa na asilimia 57 tunataka kujua pesa hizo ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, watoto wengi wa kike huachishwa masomo yao na kukosa elimu kwa sababu ya mimba za utotoni na kupelekea kukatizwa masomo yao na kutopata elimu. Tutambue kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika jamii na pia kuleta maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Tanzania haitoweza kuendelea iwapo wasichana hawa hawatendewi haki kwa kuendelea kuwanyima haki na fursa ya kupata elimu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa wasichana siyo msaada, hongo, fursa, upendeleo wala uhisani, bali ni haki yao ya msingi. Hivyo wasichana nao wanastahiki kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Baraza la Mitihani Zanzibar umekuwa ni hadithi ambazo hazina utekelezaji wala uwajibikaji. Naomba Waziri atueleze ni lini ujenzi wa kituo hicho utaanza Zanzibar? Ni kiasi gani kilichotengwa katika bajeti kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho?

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba kama Serikali imeshindwa kuboresha Shule za Kata na nyinginezo ni muhimu kuzifunga kama inavyofanya kwenye Zahanati na Vituo vya Afya visivyo bora; pili, maudhui ya mitaala yabadilike haraka na yaendane na mahitaji ya jamii ili wahitimu watumie maarifa wanayopata shuleni kuzalisha; Mitaala ikazie elimu ya ufundi, stadi za kazi, kukuza vipaji mbalimbali kwa wanafunzi; tatu, uundaji wa mitaala sahihi ihusishe wadau wote hasa walimu na wazazi. Pia mabadiliko ya mitaala yaendane na mafunzo ya walimu kazini; nne, mazingira bora ya kufundishia

yatawamotisha walimu kufanya na kuipenda kazi yao; na tano,ni wakati muafaka Serikali ikaacha uonevu, watoto wapimwe kadri walivyosoma. Walimu wengi kwenye Shule za Kata hawamalizi *syllabus* na baadhi ya masomo hawasomi kabisa hivyo kupelekea wanafunzi wa shule hizo kufeli sana.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mapendekezo ya kuboresha elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali inaendelea na utaratibu wa kupeleka vijana ambao hawakufanya vizuri kwenye mitihani ya *Form IV* kusomea Ualimu? Elimu haiwezi kuboreshwa kama vijana wanaosomea Ualimu ni wale ambao wamepata *Divisio IV*. Tubadili utaratibu. *Incentives* ziwekwe ili vijana wanaofanya vizuri zaidi ndio wasomee Ualimu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi iondolewe kwenye utaratibu wa kuripoti kwa utawala wa Wizara. Iwe kurugenzi huru na iimarishwe. Vilevile, kila mwaka Kurugenzi hii itoe taarifa ya hali ya ubora wa elimu nchini. Taarifa hii ionyeshe ukaguzi wa *competence* za wanafunzi kulingana na madarasa waliyomo. Taarifa hii iletwe Bungeni na ijadiliwe na wadau. Taarifa ionyeshe ubora wa elimu kwa kila shule na kila mwanafunzi nchini.

Mheshimiwa Spika, ubora wa elimu kati ya maeneo ya mijini na vijijini una tofauti kubwa. Hali hii haisaidii kujenga Taifa lenye maendeleo yenye uwiano ulio sawa. Kwa msingi huo, Serikali iweke mpango maalum wa kuboresha elimu maeneo ya vijijini. Walimu wanaopangwa maeneo ya vijijini wapewe motisha wa kwenda na kubaki huko. Kuwepo posho maalum ya mazingira magumu. Halmashauri zigawanywe katika makundi matatu, Mazingira ya kawaida, Mazingira ya kati na Mazingira magumu. Posho na malipo mengine yaendane na tofauti hii kwa sababu ukweli ni kwamba mazingira katika nchi yetu hayalingani.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya mshahara, malipo maalum (posho) yatolewe kulingana na matokeo ya ufundishaji na mahudhurio ya Walimu. Haiwezekani Walimu walipwe sawa hata kama wengine hawahudhuirii darasani na wala hawafundishi ipasavyo. Utaratibu utengenezwe ambapo wanafunzi wakifanya vizuri kutokana na jitihada za Walimu, basi Walimu hao wazawadiwe kutokana na juhudi hizo. Hii itasaidia Walimu kuhakikisha wanajielekeza zaidi kwenye matunda ya ufundishaji wao.

Mheshimiwa Spika, ni uonevu wa hali ya juu kuwatahini wanafunzi katika masomo ambayo hawakufundishwa. Kama shule haina Mwalimu wa Hesabu, inakuwaje wanafunzi wanalazimika kufanya mtihani wa hesabu na anakosa fursa ya kuendelea katika maisha kutokana na jambo lililo nje ya uwezo wake?

Mheshimiwa Spika, kwenye mpango wa *MMES II, Capitation grant* imepangwa kuwa Sh. 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa Shule ya Sekondari. Lakini kwenye mpango wa bajeti, kila mwanafunzi amepangiwa Sh. 20,000/= kwa nini?

Mheshimiwa Spika, vitabu vingi vya kiada vina makosa mengi ya kimaudhui. Vingine vimeandikwa bila kufuata maelekezo ya mitaala na hivyo vimekuwa vinapotosha wanafunzi. Pia vingi vina makosa ya lugha. Kamati ya Uidhinishaji wa Vitabu vya Kiada *(EMAC)* ivunjwe na kuundwa upya kwani inaelekea imeshindwa kazi yake ya kuhakikisha ubora wa vitabu. Vilevile, utaratibu wa matumizi ya vitabu vya aina moja urudishwe.

Mheshimiwa Spika, walimu wanapata adha kubwa kupata malipo yao. Inaweza kuchukua siku tatu kwa mwalimu kufuatilia mshahara. Serikali iruhusu walimu waamue mishahara yao ipitie wapi? Msingi uwe ni *Convenience* ya Mwalimu, siyo ya Serikali. Kama sisi Wabunge tunaulizwa mshahara upitie wapi, kwanini Walimu nao wasiulizwe? Kwani ni lazima pesa yao ipitie *NMB* wakati Benki hii imeonyesha kutokuwa na ufanisi kutokana na ukiritimba na uhakika wa kupata biashara? Benki ya *CRDB* na nyingine ziruhusiwe kutoa fedha za mishahara ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, wastani wa wanafunzi 450,000 kila mwaka hawakufaulu mtihani wa Darasa la Saba. Vilevile, hawakupata nafasi yoyote ya elimu zaidi ya Darasa la Saba. Hawa ni vijana wengi wanaoachwa kila mwaka. Serikali iseme wanakwenda wapi? Wanafanya nini ?

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI:** Mheshimiwa Spika, nitaanza na suala la matatizo ya walimu ambayo imekuwa ni kikwazo kikubwa kwao. Walimu wanafanya kazi kwa mazingira magumu, hawana makazi, magari, wanaishi mbali na shule jambo ambalo linazorotesha kuanza masomo kwa wakati unaofaa. Hivyo naiomba Serikali kulichukulia hatua suala hili na kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, walimu wamekuwa wakilalamikia suala la kucheleweshewa ulipwaji wa fedha zao za mishahara jambo ambalo linawafanya kuwa na hali mbaya kimaisha, jambo ambalo linawafanya kuwa hali duni kimaisha. Hivyo, naiomba Wizara na Serikali kulichukulia hatua suala hili ilikuweza kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Elimu pamoja na Serikali kuwapa kipaumbele wanafunzi wa Sekondari kupewa mafunzo mazuri ili waweze kufanya vizuri shuleni na kukemewa kuepuka kufanya mambo ambayo hawapaswi kuyashiriki kikamilifu katika masomo yao. Kwani atakapofaulu, hapo ndipo anaweza kufikia hiyo elimu ya juu inayotakikana.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu ya juu, hivi sasa mikopo imekuwa ikiwakwamisha wanafunzi wa Vyuo Vikuu walioko Vyuoni. Tatizo la upatikanaji wa mikopo imekuwa ni kikwazo kwa wanafunzi hao kwani Bodi ya Mikopo imekuwa ikiwakwamisha wanafunzi hao kwani hawaipati kwa muda muafaka, hivyo naiomba Wizara ya Elimu pamoja na Bodi ya Mikopo kulichukulia hatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Vyuo Vikuu imekuwa kukitokea migomo ambayo inasababishwa na suala la mikopo kwa wanafunzi hao, jambo ambalo

linapelekea wanafunzi hao kufukuzwa Vyuoni. Hivyo naiomba Wizara, Serikali na Bodi ya Mikopo kuliangalia suala hili kwa wanafunzi hao ili matatizo kama hayo yasitokee.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira za Walimu limekuwa ni tatizo sugu kwa pande zote mbili Bara na Visiwani. Walimu wameshasoma, lakini mpaka hii leo bado hawajaajiriwa jambo ambalo linawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, mashuleni imekuwa kuna wanafunzi wengi na walimu hawatoshi, hivyo namwomba Waziri suala hili la kuuwaajiri Walimu ambao wameshasomea fani hii lipatiwe ufumbuzi ili na wao waweze kufaidika na taaluma hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kumekuwa na tatizo kubwa kuhusu mitaala katika Baraza la mitihani, kubadilisha *syllabus* jambo ambalo linawafanya wanafunzi kufanya vibaya mashuleni, ukiangalia hasa vitabu vya shule kama Nyambari Nyangwine. Hivyo namwomba Waziri wa Elimu kuliangalia suala hili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwapatia Walimu mashuleni mafunzo ili kuweza kukabiliana na mfumo huo wa ubadilishwaji wa *syllabus*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yako kulipiga vita kwa nguvu zote suala la wanafunzi wa vyuoni na mashuleni kushirikishwa na mambo ya siasa, wanafunzi wasikubali, kwani yanaweza kupelekea maafa kwa wanafunzi hao pamoja na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba yangu hii niliyoichangia kwa maandishi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kutawatendea haki Walimu tarajali wanaosoma katika vyuo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo lenyewe ni kwamba Serikali imekuwa ikiwapatia Sh. 900/= tu wanapokwenda kufanya mafunzo ya Ualimu kwa vitendo, yaani *Block Teaching Practice Abbreviated as BTP*. Kimsingi Sh. 900/= ni pesa kidogo sana kwa matumizi ya siku nzima. Kamati ya Bunge imeshauri kwamba mwangalie namna ya kuboresha kiwango hicho. Nami naungana na Kamati kwa kuitaka Serikali iongeze kiwango hicho angalau kutoka Sh. 900/= hadi Sh. 5,000/= kama inavyofanya kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu kutoka Sh.5,000/= hadi Sh. 7,500/= kwa mwaka 2011/2012.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nilitembelea shule kadhaa za msingi katika Jimbo langu la Ngorongoro na kuzungumza na Walimu. Matatizo yao ya msingi ni haya yafuatayo:-

- Kutopata mishahara yao kwa wakati;

- Walimu wapya kulipwa mshahara sawa na wale waliofundisha miaka mitatu mpaka minne;

- Walimu kutopandishwa madaraja kwa muda mrefu;

- Barua mbalimbali za maulizo za Walimu hazijibiwi na wahusika/Maafisa Elimu;

- Walimu kutothibitishwa kazini na haki zao kupotea;

- Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu kutopata motisha hiyo na kukata tamaa;

- Kutopata huduma za afya na mahitaji mengine;

- Usafiri wa shida/matatizo; na

- Hawapati Semina za mara kwa mara.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii na pia kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri inayoleta matumaini katika kuboresha elimu nchini kwetu. Hata hivyo, ningependa kuchangia na kutoa mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya kiashiria *(Indicator)* ya lengo la tatu la Milenia *(MDG 3)* ni kuondoa tofauti ya kijinsia katika Elimu ya Msingi, Sekondari na ngazi zote za elimu ifikapo mwaka 2015. Wakati takwimu zinaonyesha kuwa kuna usawa katika uandikishaji wa wavulana na wasichana katika Elimu ya Msingi, bado idadi ya wavulana inazidi wasichana katika Elimu ya Sekondari na Vyuo vya elimu ya juu hasa kwa wasichana walio vijijini.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa watoto wa kike ni kichochea cha kuondoa umasikini katika familia, jamii na nchi kwa ujumla. Kuna ushahidi unaoendelea kuonyesha kuwa elimu kwa wasichana inaweza kusaidia nchi kupata mafanikio katika utekelezaji wa malengo mengine ya Milenia hasa lengo lihusulo kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi *(MDG 5)* na kupunguza vifo vya watoto wadogo *(MDG 4).*

Mheshimiwa Spika, vikwazo vya kuwaandikisha wasichana shule na hivyo kuweza kumalizia masomo yao ni pamoja na vitendo vya ukatili wanaokumbana nao mashuleni na wakiwa njiani kuelekea shule, mila na desturi zetu zinazompa majukumu makubwa ya kuhudumia familia na hali duni ya wazazi/walezi na familia.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, ili Tanzania iweze pia kuwa na usawa wa kijinsia katika Elimu ya Sekondari, ni lazima kuwepo hatua za makusudi za kuhakikisha wasichana wanabaki shuleni/wanasoma. Ujenzi wa Mabweni ya wanafunzi wasichana ni lazima upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, katika karne hii ya 21 tofauti za kiuchumi kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinatokana na viwango tofauti katika taaluma za kisayansi, teknolojia na uvumbuzi. Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi inayodhamiria kujenga uchumi imara na wa ushindani, haina njia mbadala ya kukuza viwango vya taaluma katika fani za sayansi kwa kila ngazi ya elimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchache wa wataalam wa jinsia zote katika nchi yetu, idadi ya wanasayansi, wahandisi na wavumbuzi wa kike ni ndogo zaidi ikilinganishwa na wa kiume. Hali hii inajitokeza katika ngazi za Sekondari, Vyuo na Taasisi nyingine. Ninaipongeza wizara kwa kuweka mikakati maalum ya kuwezesha ushiriki wa wasichana katika masomo ya Sayansi kwa wasichana, programu za TUSEME na Tunzo/zawadi mbalimbali kwa wasichana wanaofaulu vizuri katika masomo ya Sayansi na Hesabu ngazi ya Sekondari na vyuo kila mwaka. Aidha, nafarijika na jitihada zilizofanywa za kuongeza idadi ya wasichana kusoma masomo ya Sayansi kwa kuweka mikakati kwa *pre-entry training* kwa wanafunzi wa kike ili wafikie sifa stahiki za kujiunga na vyuo kusoma Sayansi na Uhandisi. Mikakati kama hii pia imepongezwa na Jumuiya ya Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye Ripoti ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Mkutano wa 55 wa Hali ya wanawake Duniani uliofanyika mwezi Februari, 2011. Kauli mbiu ya Mkutano huu ambayo pia ilikuwa ndiyo kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani ni "Fursa sawa katika Elimu, Mafunzo, Sayansi na Teknolojia: Njia ya wanawake kupata ajira bora."

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iendelee kutekeleza mipango na mikakati ya kumotisha wasichana waweze kupenda kusoma masomo ya sayansi kwa kuchukua hatua za makusudi na kutenga raslimali watu na fedha za kutosha ili kuongeza idadi ya wasichana kuchukua masomo ya Sayansi ambayo yatawawezesha kuongeza namba ya wanawake wanaofanya kazi katika sekta zinazoaminika kuwa ni za wanaume na hivyo kupunguza ubaguzi wa kijinsia.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufundisha na kujifunza bado yapo chini. Maboresho ni lazima yafanyike.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa elimu maalum bado haukidhi. Walimu wa Elimu Maalumu ni wachache, hawatoshi kabisa. Sidhani kama Wizara inalifanyia kazi suala hili, kwa kuwa limekuwa likipigiwa kelele kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, vifaa ni tatizo kubwa kwa wanafunzi wenye ulemavu, wanasoma kwenye mazingira magumu sana, vifaa ni vichache, havitoshi kiasi kwamba wanashuka kielimu.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa elimu jumuishi, viziwi bado wana matatizo makubwa sana. Viziwi hawatakiwi kuchanganyika na wanafunzi wa kawaida. Hawana Shule ya Sekondari hata moja. Changamoto yao ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, miundombinu siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu, kwa upande wa ngazi, vyoo, Wizara iliangilie hilo.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vipo saba tu na ni viwili tu vinavyofanya kazi. Athari ya kufungwa kwa vyuo hivi ni kuzagaa Mitaani, kunyimwa fursa ya kupata Mafunzo ya Ufundi Stadi ambayo ndiyo mkombozi kwa vile watu wenye ulemavu hawajaingizwa kikamilifu katika mfumo rasmi wa elimu na pia ni kuwadidimiza kwenye umasikini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kutoa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya anaonipa kila siku hasa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua nia ya Serikali katika kutoa elimu kwa wananchi wake, lakini bado bidii na jitihada zaidi zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, elimu hasa ya msingi na sekondari imeshuka kwa kiwango cha juu sana, hali ya shule za Serikali zinazotoa elimu na ambazo zilikuwa tegemeo la wananchi wetu sasa zinatisha kimiundombinu na huduma ya elimu itolewayo.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi zinazojengwa na zilizojengwa na wananchi (Shule za Kata) nyingi zimeanza kutoa huduma ya elimu wakati hazijatimiza vigezo vya kuanza kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi zimekamilika kimajengo na huku hazina Walimu, vifaa vya kufundishia, maabara na maktaba zenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, inatia uchungu kuona sasa wazazi wenye uwezo hawana imani na Shule ya Serikali yao na hii inathibitika pale ambapo mzazi anapoamua kumlipia mwanaye akapate elimu katika shule ya binafsi kuliko katika shule za Serikali. Hiki ni kipimo kidogo cha imani ya wananchi juu ya Serikali yao waliyoiweka madarakani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na sakata la kufunga Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Hivi vimefungwa kutokana na kutokidhi vigezo vya kutoa huduma kwa Watanzania. Ningependa basi utaratibu huu wa kufunga maeneo yasiyokidhi vigezo, basi tuufanye katika mashule ambayo hayakidhi vigezo vya kuwa Sekondari.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuna baadhi ya shule zina Walimu watatu wanaofundisha shule zetu za Kata. Utakuta shule ina Walimu wa Michezo, Kiswahili na *Civics*, lakini inasikitisha pia kuona wakati wa mitihani watoto wanatakiwa kujibu

mitihani zaidi ya tisa ambayo hawakuweza kabisa kufundishwa darasani, na matokeo yake ni mtoto kupewa daraja la sifuri ama daraja la nne na kuonekana ameshindwa katika mitihani yake ya mwisho na inapelekea mtoto huyu kujiona duni na asiye na uwezo (akili) na imepelekea wanafunzi wengi sana kukata tamaa na wengine hata kujiua kutokana na matokeo mabaya ambayo ni kosa la Serikali na sio kosa la mzazi/mlezi au mtoto mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, huko ni kukiuka haki za binadamu kwa kumfanyisha mtoto mtihani ambapo hakulisoma somo husika. Ipo haja sasa ya kumruhusu mtoto kutofanya mtihani kwa masomo ambayo hajaweza wala kuwahi kufundishwa darasani.

Mheshimiwa Spika, pia kubadilika kwa mitaala mara kwa mara bila kuwaandaa Walimu husika kumechangia elimu yetu kuteremka sana na kukosa msimamo. Pia inatia aibu kwa nchi kuona sasa Walimu ambao ndio wanaozalisha wataalamu hapa nchini, hali zao ni mbaya sana. Ipo haja ya kuboresha maslahi ya walimu. Elimu bora inatoka kwa Mwalimu bora. Hebu sasa tufike mahali Serikali ihakikishe kuwa kila Mwalimu anakuwa bora kwa kila shule.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mwalimu anaona anaweza kwenda kuongeza elimu ambayo ataitumia kuwapa watoto wa kitanzania, basi Serikali imsaidie Mwalimu huyu awe bora.

Mheshimiwa Spika, kujenga nyumba katika maeneo ya shule siyo suluhisho la kuwafanya tu Walimu wapte ari ya kufundisha, bali ni kuwapa viwanja maeneo ya karibu na shule na kuwapa mikopo nafuu ya kujenga nyumba watakazomiliki wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, bado tunaanzisha mitaala mipya bila maandalizi ya kutosha kwa watakao somo husika. Kwa mfano, *TEHAMA*. Walimu tuliowapa jukumu la kufundisha *TEHAMA* tumewaandaa vipi? Hapa tunatania, elimu bado, hata uwezo wa Mwalimu kuwa na kompyuta hana, hajawahi hata kuitumia, lakini tunampa jukumu la kufundisha.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa Serikali ihakikishe inawaandaa watoa taaluma kabla ya kutoa elimu, halafu ndiyo mitaala ibadilikie na baada ya Serikali kuwa imefanya tafiti za kutosha kuona sasa maandalizi ya kubadilisha mtaala yapo na uwezo upo, ndiyo kazi ya kubadili mtaala ufanyike ili kulifanya somo husika kufika kwa kina kwa wanafunzi.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanikisha kuleta hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili nasi Wabunge tupate kuboresha bajeti ya Wizara hii. Napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa wa Watanzania kukaa pamoja na kujadili kwa kina kuhusu Sera ya Elimu kwa sababu kumekuwepo na mabadiliko ya kila siku katika Wizara hii. Kila Waziri anayeingia katika Wizara hii na Katibu wake

wanaandaa mambo mapya ambayo kwa kiasi kikubwa wanachanganya Walimu na wanafunzi, hivyo basi, ipo haja ya kuandaa Sera ya Elimu ambayo ni endelevu na kila kiongozii anayeingia madarakani ataendelea kuitumia na siyo kuandaa mambo mapya kila siku kama vile kubadilisha mitaala bila ya kupeleka Walimu mafunzo, hivyo kuendelea kushuka kwa kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia kuhusu matatizo katika Shule za Msingi ama Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza Elimu ya Msingi, lakini bado kuna changamoto kwenye baadhi ya Shule za Msingi kama vile msongamano kwenye madarasa, njaa kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni na uhaba mkubwa wa Walimu na vifaa vya kufundishia, hivyo matatizo haya na mengine yanasababisha uwezo wa wanafunzi darasani kumudu masomo kuendelea kushuka.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niishauri Serikali kwamba izingatie suala la kupatikana kwa chakula mashuleni, hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka ili tuweze kunusuru watoto wetu waache kusinzia madarasani kwa ajili ya njaa na waweze kusikiliza vizuri masomo na kuyazingatia, kwani kuna usemi unaosema kuwa mtoto mwenye njaa ni vigumu kufundishika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kushirikiana na Watanzania kwa kujenga Shule za Sekondari za Kata kwa wingi lakini bado kuna changamoto nyingi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wiki chache zilizopita tulileteWa wanafunzi hapa Bungeni waliofanya vizuri katika masomo yao ya Kidato cha Sita na baadhi yao walimaliza masomo yao ya Kidato cha Nne katika Sekondari za Kata. Swali la kujiuliza: Je, ni kweli za Kata zinafanya vizuri kama tulivyoambiwa na wanavyoambiwa Watanzania wakati kiwango cha ufaulu kimezidi kushuka? Kwa mfano, katika Mkoa wa Pwani asilimia 60 ya watoto wamepata *(Division Zero)* daraja sifuri kwa maana kuwa hawapati cheti. Je, watoto hawa tunawapeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, kuna shule Mkoani Lindi, Wilaya ya Kilwa mwaka 2009/2010 ilikuwa na wanafunzi 60 na wote walipata *Division Zero,* hii inaitwa Shule ya Sekondari Nanjirinji. Je, haya ndiyo mafanikio ya Shule za Sekondari za Kata tunazozipigia debe kwamba zinafanya vizuri?

Mheshimiwa Spika, nami napenda nishauri machache katika Wizara hii ili tuweze kuwakomboa wanafunzi wetu wanaomaliza Kidato cha Nne. Kwanza, kupunguza idadi kubwa ya masomo ya lazima ambayo kwa kiasi fulani yanachangia mwelekeo uliopo hivi sasa na wanafunzi kusoma kwa ajili ya kufaulu mitihani badala ya kuwajengea uwezo wa kukuza uelewa. Pili, kuingiza elimu zaidi ya vitendo kuliko nadharia.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mawasilisho mazuri ya bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali, kwa uwiano ulio sawa, ni ukweli usiopingika kwamba maendeleo baina ya Mikoa hailingani na hivyo hata mazingira ya ufanyaji kazi kuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa iliyo pembezoni maendeleo yake ni duni ukilinganisha na Mikoa mingine. Mikoa hii inakabiliwa na upungufui mkubwa wa Walimu. Nashauri Serikali ichukue uamuzi wa makusudi kuhakikisha kwamba linatengwa fungu maalum kwa walimu ambao wako tayari kufanya kazi katika mazingira magumu, hususan katika Jimbo la Kalambo Mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara itazame upya kuhusu sera na baadhi ya kanuni zinazotumika. Fursa anayopewa mtoto anayemaliza (hitimu) Elimu ya Shule ya Msingi na kushindwa kuchaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari akiwa na nia ya kukariri ili apewe fursa ya kusoma kwa sheria ya sasa kwa Shule za Msingi, nafasi hiyo hapewi wakati kwa mwanafunzi ambaye anahitimu Elimu ya Sekondari na kwa bahati mbaya asipofanya vizuri anapewa nafasi ya kurudia ili kusafisha cheti, fursa ambayo inapaswa kupewa nafasi kama nia ya kujifunza ipo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na sheria kama siyo kanuni ambayo imekuwa ikitumika pale ambapo mwanafunzi anapopata mimba kwa kuwashitaki wazazi wa binti pamoja na wazazi wa mvulana aliyesababisha ujauzito kwa msichana. Kuwashitaki wazazi kwa vijana kupeana mimba siyo busara hata kidogo, kwani hakuna mzazi hata mmoja mwenye busara ya kawaida kwa mila za kibantu anayeweza kumtuma mtoto wake akajihusishe na masuala ya ngono. Hivyo kumshitaki mzazi ni sawa na kumtukana mzazi huyu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijikite katika kurudisha hadhi ya Walimu kama ilivyokuwa siku za nyuma wakati kazi ya Walimu ilikuwa ni kazi yenye heshima kubwa kwa jamii. Kazi ya ualimu iwe ni kazi ya kupendwa na kuthaminiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kupongeza hotuba ya Waziri ambayo imeeleza mipango vizuri sana. Pamoja na mipango mizuri, lakini vifaa vya kisasa ambavyo vinahitajika vingi havipo mashuleni na hata hivyo vilivyokuwepo ni vidogo mno. Utakuta shule nzima yenye madarasa ya kuanzia Darasa la Kwanza mpaka *Form four* ina *Computer* tatu tu na isitoshe inayo *laboratory*, lakini hazina vifaa na kwa vile Waziri amesema atafanikisha haya naomba afanikishe kwa vitendo na siyo kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, elimu itolewe kwa wazazi ili waone umuhimu wa mtoto kuanza masomo kuanzia miaka minne ili huyu mtoto ajengeke vizuri. Mtoto anayesoma *Nursery* na baadaye akiingia Elimu ya Msingi anakuwa anafahamu vizuri masomo yake kuliko yule anayeanza Shule ya Msingi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, mfumo ambao tulikuwa nao zamani ambao mtoto ananza kuanzia Darasa la Kwanza hadi Darasa la Nane urudishwe na akifika Darasa la Nane afanye mtihani wa kuingia sekondari. Hii itawawezesha wale ambao wamefeli kufikia miaka 15 ambapo mtoto huyu atakuwa na uwezo wa kufanya kazi na kuweza kujiendesha maisha yake.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kupima afya watoto mashuleni uwe unafanyika angalau mara nne kwa mwaka kuliko ile hali ya sasa hivi. Kuna shule nyingine hazipimi afya za watoto na hao wanaopima hawapimi kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia, ni mikopo ya Vyuo Vikuu. Hakuna utaratibu mzuri. Naiomba Wizara husika ifuatilie vya kutosha ili ijue kwanini huu utaratibu mzuri wa Serikali uliopangwa haufuatwi? Watoto kwenye darasa moja huwa hizi posho hawapati kwa wakati mmoja. Hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuongeza posho kutoka Sh. 5,000/= mpaka Sh. 7,000/=.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuna vijana wengi ambao wako Vyuo Vikuu waathirika wa ugonjwa wa Ukimwi. Naiomba Serikali ichukue juhudi ya kuwapima wanafunzi wa Vyuo Vikuu na wale ambao wana virusi vya Ukimwi waweze kutengwa na wenziwe na waweze kupewa dawa.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake na upendo wake Mkuu kwa kuniwezesha nami leo hii kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri na yenye kukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha ya kila mwanadamu, bila elimu huwezi kufanya kitu. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mpango wake mzuri wa kujenga Shule za Sekondari kila Kata. Shule hizi zimeleta mabadiliko makubwa sana katika kumkomboa mtoto na hasa katika sehemu za vijijini. Napongeza sana mpango huo. Aidha, naombe sasa Serikali kama ilivyoleta huo mpango wa kujenga Sekondari kila Kata, ilete tena mpango wa kujenga bweni katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea tatizo hili katika Mkoa wangu wa Geita. Katika Mkoa wa Geita katika Wilaya ya Nyang'hwale tatizo hili ni kubwa sana. Watoto wanateseka sana. Mtoto wa *Form I* au *II* anakuwa na umri wa miaka 12 au 13 tu, ni mtoto mdogo mno kuanza kuishi peke yake bila ulinzi wa mzazi au Matroni. Mtoto huyu

analazimika kuanza kuishi maisha ya kubahatisha ukizingatia na umri wake huo. Matokeo yake mtoto huyu kwanza hawezi kupata muda mwingi wa kujisomea, maana itabidi atafute muda wa kuandaa chakula na kujiingiza kwenye vitendo vya uhuni maana anakuwa huru sana. Pia maeneo ambayo wanaishi ni ya kutisha sana, unaweza kuwakuta wanalala chini kabisa, pia nyumba zenyewe hazina ulinzi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi iliangalie suala hili kwa jicho la huruma. Watoto hawa wanateseka sana, wengine hulazimika kuwa wazazi bila kupenda kutokana na mazingira wanayoishi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ipeleke walimu wenye sifa katika maeneo haya ya Mkoa wa Geita. Hatuna kabisa Walimu wa masomo ya Sayansi, matokeo yake watoto wengi sana wanapata ‘F’ somo la Hesabu ambalo ndiyo kiungo kikubwa sana katika masomo yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenye kipengele cha sita au cha nane.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupata ufafanuzi wa kina kwamba kwanini *TCM* wameamua kuondoa *mature age entry?* Haioni kuwa kufanya hivyo tutakuwa tunawanyima fursa Watanzania wengi ambao elimu yao haitokani moja kwa moja na *Form Six* au daraja ambalo ni sawa na hili, kwamba wale wote ambao hawakupata muda wa kwenda Vyuo Vikuu moja kwa moja *(Direct entry)* ndio wamenyimwa fursa ya kujiendeleza?

Mheshimiwa Spika, napenda Wizara na vyombo vingine husika kuliangalia hili.

Mheshimiwa Spika, sehemu yangu ya pili ni juu ya miundombinu kwenye Vyuo vyetu Vikuu hasa vile vilivyojengwa zamani. Kuna ufinyu wa *theatre* au *teaching lab/classes* kutokana na ukweli kwamba majengo haya licha ya kutokuwa na *capacity* ya ku-*accomodate* idadi kubwa ya wanafunzi, lakini pia ni machakavu na hayana *morden teaching instrument*. Mathalan udahili wa wanafunzi kwa miaka ya hivi karibuni ni mara zaidi ya 10 ya udahili uliokuwa ukifanyika miaka ya themanini na sabini.

Mheshimiwa Spika, vilevile changamoto nyingine kubwa na hili nalisema kwa sababu nami ni mwathirika, wakati nikifundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vifaa vya kufundishia bado ni duni haviendani na wakati wa sasa, ambao unasisitiza *TEHAMA*. Kwani hadi sasa tunafundishia kwa kutumia chaki, na baadhi ya *theatres*/madarasa hayana kundio *(Visual teaching aid)*, kama *Microphone* na *Installed speakers*. Vilevile wanafunzi hulazimika kukaa nje ya *theatre* na usikilizaji unakuwa *impaired*, kitu ambacho kinapelekea uhafifu na uelewa kwa wanafunzi, kitu ambacho ni hatari kwa maendeleo ya Taifa letu na inapelekea hata vyuo husika kuonekana kama

hawatoi *the right product* na katika ushindani wa sasa ambapo Vyuo Vikuu Binafsi ni vingi sana.

Vilevile vifaa kama *Computer* kwenye maabara hakuna kabisa, au ni vya zamani sana. Vilevile *laboratory* ni chache sana na kuna *course* nyingine zinahitaji *Software* kwenye kufundishia baadhi ya mitaala, lakini hakuna kabisa. Hii ni changamoto kubwa ambayo inahitaji majibu na suluhisho la kuchukua.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika miundombinu ya Vyuo Vikuu, Wizara pia haina budi kuhalalisha uwepo Ofisi za Wahadhiri, kwani ofisi zilizopo hazitoshelezi mahitaji ya wahadhiri, kwani sasa kuna idadi kubwa ya wahadhiri. Vilevile nyumba za wahadhiri nazo ni changamoto kubwa kwani wahadhiri, mimi mwenyewe nikiwa mhanga, tunalazimika kukaa mbali na Vyuo kama Boko, Bunju au Mbezi na foleni za Dar es Salaam na tunajilipia wenyewe, licha ya kwamba nyumba ni moja ya *package* kwa Wahadhiri, lakini inakuwa ni nadharia tu, kwani hamna majengo ya ku-*accomodate* Wahadhiri. Hii pia lazima iangaliwe kwa makini, kwani inapunguza ufanisi katika Sekta ya Elimu, kwani Wahadhiri hupoteza muda mwingi kutoka au kwenda majumbani na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu nitauelekeza katika *discipline* za walimu wetu hasa wa Sekondari na Msingi ambapo kumezuka tabia ya baadhi ya Walimu hasa wa kiume *either* kwa kujihusisha kimapenzi na wanafunzi kwa kuwarubuni ya kuwapa maksi au kwa kuwabaka bila ya ridhaa yao. Hii ni tabia mbaya sana ambayo haiendani na *ethics* za kazi ya Ualimu. Hivyo, wanastahili adhabu kali na siyo kuhamishwa kituo tu, basi.

Mheshimiwa Spika, mchango wa nne ni juu ya udhaifu wa majengo yanayojengwa chini ya mpango wa *MMEM* na ni hatari na inatia fedheha sana kuona majengo ndani ya mwaka tu nyufa nyingi, mavumbi sakafuni na unakuta pesa nyingi zimetumika. Hii inabidi ichukuliwe kwa udhamira mkubwa kwa kushirikiana na Wizara ya Tamisemi ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni muhimu kuwepo na uharaka wa kujenga maabara katika shule zetu za Sekondari kama kipaumbele cha upekee. Ukosefu wa maabara unachangia kwa kiwango kikubwa na ufundishaji kwa vitendo, na wahanga wakubwa kwa hili ni Shule za Kata. Vilevile inatia aibu kuona Shule ya Kata ina Walimu watatu au wanne, hamna vitabu, na mwisho wa siku wanapimwa kwa mitihani sawa. Hii siyo haki kabisa, na inaua elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kuhusu vifaa kwa wanafunzi walemavu, hawapewi kipaumbele kabisa. Ruzuku ya Sh. 20,000/= alizosema Naibu Waziri ni ndogo sana. Inabidi majengo yawe ni ya ku-*accommodate* walemavu. Vilevile ni aibu kweli kuona wanafunzi katika Shule za Msingi tena hasa za Jijini kama Dar es Salaam wanakaa chini. Ni aibu sana. Hapa tunakuwa tunadumaza elimu na siyo afya ya elimu na uelewa unakuwa hafifu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho walimu wanatakiwa wapewe *motivation* kama ilivyopendekezwa hapa ili kuwapa morali ya kufundisha vijijini.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itoe agizo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, wanafunzi wote wa Shule za Msingi wavae viatu vyeusi na soksi. Ni muda muafaka tubadilike. Baada ya miaka 50 ya Uhuru, naamini kila mzazi ana uwezo wa kununua *pair* moja ya viatu kwa mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana, linahitaji utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha elimu inatolewa kwa kiwango kinachostahili na pia juhudi zinazofanyika katika utatuzi wa migogoro mbalimbali inayotokea kwenye vyuo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niipongeze Serikali kwa kuongeza posho za wanafunzi wa vyuo vikuu. Bila shaka angalizo hili litaleta tija na mafanikio kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa umakini wa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote, naomba Serikali iongeze juhudi za kujenga maabara kwenye Shule za Sekondari. Kuwepo kwa maabara kwenye shule zetu kutasaidia sana kuibua vipaji vya wanafunzi na ukizingatia kwamba taaluma ya sayansi inahitajika sana nchini kwa muda huu. Naomba Serikali inieleze, imejipanga vipi katika ujenzi wa maabara mashuleni?

Mheshimiwa Spika, wakati nilipouliza swali la nyongeza kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, niliwahi kuuliza: Je, Serikali imejipanga vipi kuweza kutoa mikopo ya pikipiki au gari kwa walimu ili kuweza kupunguza adha ya usafiri? Je, mpaka sasa Serikali imepanga mkakati gani wa kuwasiliana na vyombo husika?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe kipaumbele zaidi kwa baadhi ya Shule za Mkoa wa Pwani kwa kutupatia walimu na vitabu zaidi kwa shule zetu ili tuweze kuongeza idadi ya ufaulu kwa wanafunzi wetu. Naomba kupata jibu la mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa msukumo kwa elimu nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibaha Mjini, tunayo mapungufu makubwa yanayokwamisha elimu bora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunao upungufu wa madawati 2,309, meza za walimu 511, viti 576 na matundu ya vyoo 425. Tunao msongamano mashuleni na tunahitaji shule sita za msingi kuanzishwa na zinakosa madarasa, ofisi na vyoo.

Mheshimiwa Spika, tuna ukosefu wa fedha za kuendeshea vitengo vinne vya watoto wenye ulemavu wapatao 51. Mfuko wa Elimu hauna fedha. Fedha za likizo za walimu zinakuja pungufu na kusababisha madeni.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna upungufu mkubwa kwenye miundombinu ya Shule za Sekondari, nyumba za walimu za kuishi, maji na umeme na kufanya walimu kukimbia shule hizi. Kuna ukosefu wa majengo muhimu kama maabara, maktaba, majengo ya utawala, chumba cha Sayansikimu, Chumba cha Kompyuta na Jiografia ili kutekeleza elimu za vitendo. Vile vile kuna ukosefu wa Hosteli kwa ajili ya kuanzisha Vidato vya Tano na Sita kwa kila Tarafa. Hata usafiri kwa maana ya gari ya ukaguzi wa shule hamna.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie kwa makini upungufu huu na iyapatie ufumbuzi ili kuboresha elimu katika Jimbo la Kibaha Mjini na nchi wa ujumla.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya elimu iongezwe kukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maslahi ya walimu yaangaliwe. Walimu walipwe mishahara na stahiki nyingine kama malipo ya uhamisho, matibabu na likizo. Nasema hivyo kwa sababu kipato ndicho kinaamua utulivu wa mtu kufanya kazi. Huwezi kufikiria kujenga nyumba kama kigezo cha mwalimu kufundisha. Mwalimu anaweza kuwa anaishi shuleni na akakosa morali ya kufundisha kama hana mahitaji yake. Mwalimu akilipwa vizuri anaweza kutafuta yeye mwenyewe mahali pazuri pa kuishi kwa uwezo wake, akapata akatulia akafundisha. Kupitia mshahara mwalimu anaweza kununua au kukopa gari au pikipiki akawa na uwezo wa kufika shuleni hata kama anaishi umbali mrefu kutoka shuleni.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa walimu kiuweledi. Katika jamii yetu utasikia hata wazazi wanauliza watoto wao, umekosa kazi hata ya ualimu, taaluma hii inadharauliwa wakati ni taaluma muhimu. Inadharauliwa kwa sababu mara nyingi vyuo hudahili wanafunzi ambao hawakufaulu vizuri. Hutegemei kupata walimu wenye uwezo katika msingi huo. Wizara sasa ifikiriwe kuweka *standard* ya kiwango cha elimu inayotakiwa kujiunga na Vyuo vya Ualimu, division II na III tu.

Mheshimiwa Spika, umbali wa shule za Kata na mimba kwa wasichana. Shule za Kata, shule za Kata zimejengwa mbali kwa baadhi ya vijiji na hivyo kulazimisha

wanafunzi kutembea umbali wa kilomita kumi na zaidi kuweza kufika shuleni. Watoto wa kike wanakutana na vishawishi vingi njiani kwa kupewa *lift* na vijana hasa waendesha pikipiki. Matokeo wasichana hujiingiza katika mahusiano na kupata mimba. Takwimu zina onyesha mimba za watoo wakike na hasa kwenye shule za kata zimeongezeka. Sekta binafsi kujenga hostels za bei nafuu kwa matumizi ya watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitabu vya kiada (*text books*). Serikali kupitia wanataaluma wa elimu itunge vitabu vyenye mtaala unaofanana nchi nzima. Kitabu cha somo moja kiwe kimoja nchi nzima hasa katika shule za msingi na sekondari kwani vitabu vinavyotumika sasa hivi vingine havina viwango na kupitishwa kwa upendeleo au kwa kujuana. Vitabu hivi vimekuwa vingi Serikali iweke uthibiti ili vitabu vilenge kuinua kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu matabaka ya elimu nchini. Nchi yetu imejenga matabaka ya viwango vya elimu kati ya walionacho na wasiokuwa nacho. Shule za *English Medium* zimeleta matabaka, zina kila *facility*, vitabu, maabara, walimu, mazingira na hivyo kutoa elimu bora kwa watoto wa watu wenye uwezo. Matabaka hayo yatakwenda hadi katika ajira, watoto wa vigogo wenye uwezo ndio watakaoajiriwa na si watoto wa wakulima katika shule za kata. Zamani ilikuwa ni fahari kushinda kwenda shule ya Serikali sasa imekuwa mkosi. Serikali iangalie mpango wa ushindani kati ya shule zake na shule binafsi ili kupunguza matabaka yanayojitokeza.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, kiwango cha elimu katika Mikoa ya ya Kusini hususan Lindi kimeshuka sana na sababu ambazo zimepelekea kushuka huko ni walimu wanaopangiwa kuja huko wanaripoti na kurudi katika maeneo walikotoka. Lindi ni sehemu ya kuchukulia ajira kwa walimu, madaktari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikadhibiti vyeti kwa kipindi maalum kwa mkataba tutakaokubaliana baina ya Serikali na walimu. Shule nyingi za Kata kunakosekana maadili kwani wanafunzi wanakuwa huru kwani, wanapangishiwa sehemu za kulala na wazazi wao, matokeo yake ni mimba kwa wasichana na vijana kufanya mambo nje na taratibu za wanafunzi wanavyopaswa kuwa, mkakati kabla ya kujengwa vema tukajengewa mabweni ya kulala wanafunzi hao kwanza ili tuimarishe elimu ya kidato cha nne uwanja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, yapo matatizo mengi kwenye Idara ya Elimu ya Msingi. Shule nyingi hazina walimu wa kutosha, nyumba za walimu ni chache, kiasi kwamba walimu wanakatishwa tamaa na kwa sababu jukumu la ujenzi sehemu kubwa wameachiwa wananchi wachange michango wajenge nyumba za walimu, matokeo yake nyumba zinazojengwa zinakuwa hazina viwango na hivyo kutofanana na hadhi ya kuishi mwalimu. Naomba Wizara iweke Bajeti maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu vijijini.

Mheshimiwa Spika, pawepo na posho maalum ya mazingira magumu kama ilivyokuwa kipindi fulani, miaka ya nyuma kwa shule zote zilizopo vijijini hasa vijiji ambavyo vipo ndani sana. Hali ya walimu wa shule za msingi nashauri iboreshwe ili

kuleta matumaini kwa walimu. Imefikia hali hata wanafunzi wa shule za msingi ukiwauliza swali kuwa nani kati yenu angependa awe mwalimu baadaye, unaweza usimpate sababu kubwa ni maisha ambayo wanayaona kwa walimu wao. Naomba Wizara ya Elimu iangalie upungufu wa walimu katika Wilaya ya Mbarali ili kuziba pengo la upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie elimu ya sekondari. Wilaya ya Mbarali ina shule za sekondari za Serikali kumi na tatu. Katika shule hizi 11 hazina umeme hata na *solar*. Jitihada kubwa zinafanyika kujenga maabara, lakini maabara zinahitaji kuwepo umeme. Je, Serikali itakuwa tayari kuunga mkono jitihada za wananchi na Halmashauri katika kuweka umeme wa *solar* katika shule hizi kumi na moja? Shule hizi zina upungufu mkubwa wa walimu. Naomba Wizara inileteе walimu ili taaluma inayotolewa iwe ya kiwango kinachofaa. Upo uhaba wa nyumba za walimu. Je, Wizara ipo tayari sasa kuleta walimu ili kutowakatisha tamaa wazazi kwa matokeo mabaya ya mitihani na kutowakatisha tamaa wazazi wanaoshirikiana na Serikali kwa kuchangia michango ya hali na mali kwa watoto wao kutofaulu vizuri mitihani yao ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule za kidato cha tano na sita. Wilaya ya Mbarali ina shule moja tu ya *High School*. Hata hivyo, tunayo shule tarajiwa (*Rujewa High School*) madarasa yapo, bweni lipo bado umeme ambao upo jirani na chanzo, pia tunakosa vitanda kwa ajili ya *hostel* lakini hata hivyo tunakosa *hostel* ya wavulana. Je, Serikali kupitia Wizara ya elimu ipo tayari kusaidia ukamilishaji wa mapungufu haya? Pia Madibira sekondari bado ina mapungufu. Naomba ushirikishwaji katika ujenzi wa *Igurusi High School* ambayo wananchi wameanza maandalizi.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, kila nikiwa Jimboni Hanang na kupitia simu zao walimu wanalalamika kuwa maslahi bado duni huku Halmashauri haziwalipi madeni yao yanayotokana na posho mbalimbali ili waweze kuongezea mishahara yao kwa lengo la kuboresha maisha. Hata wakidai inachukua muda hata karibu mwaka mzima wakati mwingine, naomba maelezo kamili.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang wakazi wake wengi ni wafugaji wasiopenda shule. Hivyo, naomba Serikali ione umuhimu wa kujenga hosteli ili watoto wasitoke shule. Huko watoto wanaishia kuwa na mimba kwa ajili ya kuishi katika mageto.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang haina *VETA*, naomba Wizara ione umuhimu wa kujenga *VETA* moja ili vijana wanapohitimu darasa la saba au shule za sekondari awe na mahali pa kujifunza stadi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, shule nyingi za sekondari za Kata zinazofundisha masomo ya sayansi, hazina maabara, nyenzo ambayo ni lazima kwa wanafunzi hao kuyaelewa masomo hayo. Pamoja na nia na juhudi za dhati za Serikali

kujenga maabara hizo katika kila shule fedha zitakazohitajika ni nyingi zaidi ya uwezo wa Serikali kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuiomba Serikali ifikirie kujenga maabara chache za kuhudumia shule nyingi kama kianzio ili kila maabara moja ihudumie angalau shule tano na shule zipangiwe zamu za kutumia maabara hizo. Mpango huu utafanikiwa zaidi kwenye Kata zilizo karibu kama zile za Miji kama jiji la Tanga ambalo linaweza kupewa kipaumbele kama Jimbo la kuanzia. Hatua ya pili, itakuwa ni kujenga maabara kwa shule zinazopata maabara zao wenyewe nje ya mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wengi, hasa wale wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari wanajikuta hawana nafasi za ajira katika kampuni, mashirika na taasisi zilizopo. Vijana hawa wanahitaji kutayarishwa vema kuweza kujiajiri wenyewe kama wajasiriamali. Pendekezo langu ni kurejesha hasa katika shule za msingi utaratibu uliokuwepo zamani wa kufundisha useremala, uashi, ufundi cherehani na kadhalika kwenye shule za msingi. Kwa kuwa gharama za kujenga karakana katika kila shule ni kubwa, vyuo vya *VETA* vingetumika kwa kutoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mtindo wa kutumia TEHAMA kwa masomo katika ngazi zote za elimu umeenea sana duniani sasa hivi na unaleta manufaa makubwa. Nasi pia ingekuwa vema tukautumia katika shule za sekondari sio tu kwa kupitia mtandao bali pia kutumia CD zinazosambazwa kama kule Uingereza kwa kujifundishia wanafunzi wenyewe. Vile vile vijana hawa wapewe chachu za ubunifu na utundu wa kubuni kwa kushindanishwa kutumia TEHAMA kutengeneza *robots* za mambo mbalimbali kama njia ya kukimu hamu yao ya teknolojia badala ya kucheza tu michezo ya komputa bila ya kujua michezo hiyo imebuniwa vipi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu wake na watendaji wote Serikalini kwa kazi nzuri na hasa Hotuba nzuri yenye kuonesha matumaini mapya kwenye Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri shule nyingi za ngazi za msingi na sekondari ambazo zimekuwa zikijengwa katika ngazi za Kata zimekuwa zikifadhiliwa na watu mbalimbali ingawa na Serikali pia imekuwa ikisaidia. Wasiwasi wangu ni tabia ya baadhi ya watu kutoa msaada na kutaka shule hizo ziitwe kwa majina yao.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kuwaenzi si tatizo, lakini, je, majina hayo ya kuwaenzi watu hao mashuhuri Serikali ina imani gani na nyendo zao baada ya miaka kadhaa mbele? Mtu unaweza kuwa mwema hivi sasa lakini baada ya miaka kadhaa akawa hana sifa ya uadilifu au heshima katika jamii je, shule hiyo itabadili jina?

Mheshimiwa Spika, ni vyema kuwaenzi viongozi au watu mashuhuri ambao wameshafariki hivyo kuwa na uhakika na uamuzi huo. Ni vema Serikali ikatoa maelezo kwenye Halmashauri kuhusu suala hili ili hali hii isiendelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Jimbo la Mbinga Magharibi liko mpakani mwa Tanzania na Malawi. Mara nyingi walimu wanaopangwa huko huwa hawaendi, hii ni kutokana na miundombinu mibovu na huduma za mambo muhimu kama umeme, simu, barabara na usafiri wa reli kukosekana.

Mheshimiwa Spika, hali ya shule zetu hasa za sekondari ni mbaya hakuna maabara katika shule yoyote kwenye Jimbo. Hakuna mabweni ya wanafunzi na kadhalika. Kwa kukosekana umeme wanafunzi wanakosa mafunzo ya ziada kama *preparation* na masomo ya sayansi ambayo yanahitaji elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, idara ya ukaguzi haifanyi kazi ya kukagua elimu kwa madai kuwa hawana usafiri. Nashauri kwa kuwa walimu wengi hawataki kufundisha Jimboni kwangu, ufanyike mpango maalum ili wanafunzi wanaotoka eneo hilo wapatiwe mafunzo ya ualimu ili warudi kufundisha kwao. Naomba shule ya sekondari ya Lundo igeuzwe kwa muda kuwa chuo cha ualimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu siasa mashuleni. Waziri aje na maelezo yanayotosheleza kuhusu *neutrality* ya siasa mashuleni *as we know: "Man by nature is a political animal" by Plato*. Kwa nini Serikali inazuia wananafunzi wasijihusishe na siasa wakati hiyo ni fani kama fani zingine? Mbona chama tawala (CCM) wao wakiwa na ziara mikoani, viongozi wa chama na Serikali wanawamuru walimu na wanafunzi waende kuwapokea viongozi hao, lakini wakifanya hivyo watu wa vyama vingine wanachukuliwa hatua. Waziri atueleze unyanyapaa huu wa vyama vingine ambavyo vimeanzishwa kisheria kwa nini Serikali ina wanyima hali wao wakifanya hizo siasa, Waziri alitolee tamko.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee maabara. Hakuna maabara kabisa kwenye shule za Kata za Mikoani, shule za mijini zisiwadanganye 80% ya Watanzania wanasoma shule za Kata, Waziri atuambie kwa nini hakuna mpango mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kujenga maabara katika shule za Kata? Tunajenga Taifa gani lisilojifunza sayansi?

Mheshimiwa Spika, chakula mashuleni ni haki ya kila mwanafunzi hasa wa shule za msingi na sekondari. Waziri atuambie tofauti na mikoa hiyo miwili. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka chakula kwenye shule hizo? Naishauri Wizara au Serikali kuhimiza Halmashauri kupanga mikakati ya chakula katika shule zote za sekondari na msingi, ili wanafunzi hao watulie na kusoma?

Mheshimiwa Spika, migomo ya Vyuo Vikuu inaweza kumalizwa endapo Serikali itapeleka mahitaji ya mikopo kwa wakati katika Vyuo Vikuu. Pia Serikali iboresha

mabweni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hasa sehemu ya Mlimani mahali ambapo bado pana eneo kubwa ambalo linafaa kujenga mabweni, hii itasaidia wananafunzi kupata maeneo mazuri ya kulala na kupumzika ili waweze kusoma vizuri. Serikali isitulize migomo ya Vyuo Vikuu kwa kutumia Polisi kwani kufanya hivyo wamekuwa wakizalisha walemavu wengi na kuwaathiri kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo ni Wizara nyeti ambayo inahitaji utlivu na umakini wa hali ya juu ambayo utajenga Taifa letu la baadaye.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kusimamia vizuri Sekta ya Elimu, nawatia shime, tunazo changamoto nyingi sana kama zilivyoainishwa. Tulipotoka ni mbali, tumepiga hatua kubwa katika suala zima la elimu kuanzia chekecheka (shule za awali) shule za msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu pamoja na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, tukibeza mafanikio yaliyopo sasa hivi ni kujibeza wenyewe. Katika Sekta ya Elimu ni mengi mno yamefanyika nawapongeza wananchi wote hususan wananchi wa Wilaya ya Kwimba kwa ushirikiano na ushauri wao katika kuendeleza Sekta ya Elimu, tumejenga vyumba vya madarasa kwa shule za msingi, sekondari, nyumba za walimu, vifaa vya kufundishia pamoja na walimu waliopo. Hivyo, ni vizuri kuishukuru Serikali na tutoe ushauri, si kulaumu Serikali muda wote.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa aisaidie Wilaya ya Kwimba mambo yafuatayo:-

(i) Walimu wa msingi na sekondari;

(ii) Serikali isaidie ujenzi wa maabara na hosteli katika kila Tarafa angalau kwa kuanzia;

(iii) Serikali iharakishe ujenzi wa Chuo cha *VETA* kwani eneo lipo, *VETA* Makao Makuu wameshafika;

(iv) Si vibaya Wizara iwe na utaratibu mzuri wa kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge fedha za *capitation*, fedha hizi hazina usimamizi mzuri; na

(v) Serikali itoe miongozo kwa waratibu elimu Kata, majukumu yao wengi wa hao ma-MEK hawajui majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu tumeanzisha shule ya sekondari kwa vijana hasa wa kike kwa wale waliokatishwa masomo kwa kupewa mimba wakiwa sekondari au waliacha sekondari kutokana na mazingira magumu kwa wakati huo. Shule hiyo ya sekondari ipo Kata ya Nyambiti (Ibingo *Mission*) hadi sasa tunao vijana zaidi ya 80, kwa kidato cha kwanza na cha pili, tumejenga madarasa na hivi sasa tunajenga mabweni ya ziada.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali mambo mawili. Kwanza, isaidie nguvu tulizoanzisha kwa kuwasaidia vijana wetu hao ambao kwa sasa wamehamasika sana kusoma baada ya kukaa nje ya shule kutokana na mazingira yaliyozunguka kwa wakati huo. Pili, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu akiondoa wanafunzi wa MEMKWA zilizoko nchi nzima, shule tuliyoanzisha inawezekana ikawa ni shule pekee ya aina hiyo, Waziri afike aje ajionee, aongee na vijana hao atashangaa, atahamasika na atajifunza mengi. Namwomba sana Waziri wakati anajibu hoja, hili alisemee ili vijana wetu ambao waliishia kidato cha kwanza na pili na kukatishwa masomo waweze kujiendeleza kwa njia hiyo, shule hiyo itasajiliwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kujua ni sifa gani inayotakiwa kuwa nayo ili iweze kuwa chuo kikuu kishirikishi cha ualimu, Dar es Salaam. Chuo cha Ualimu, Butimba kina mabweni ya kutosha, kina miundombinu na panafikika kwa urahisi, kina maabara ya sayansi je, chuo cha Butimba kina tofauti gani na Chuo cha Mkwawa (Kusini *MUCE*), Chuo cha Chang'ombe (Kaskazini Mashariki *DUCE*). Je, Chuo cha Butimba ambacho kiko Kanda ya Ziwa na Magharibi hakina sifa za kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ni lini Chuo cha Butimba kitaingizwa katika utaratibu huo kama vilivyo vyuo vingine vya Chang'ombe na Mkwawa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa za ujenzi wa sekondari kwani Mkoa wa Singida ulipoanzishwa 1963 haukuwa na sekondari hata moja na 1965 ndio tukaanza na sekondari ya Mwenge. Hivi sasa Halmashauri yangu ina sekondari zaidi ya 56. Kuna kila sababu ya kujipongeza kwa mafanikio hayo. Kama siyo ujenzi wa sekondari hizi wanafunzi wanaosoma katika shule wangekuwa wapi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo bado zipo changamoto zinazotukabili ambazo ni:-

Kwanza, upungufu wa walimu. Sekondari nyingi Jimboni kwangu zina upungufu mkubwa wa walimu. Halmashauri yangu ya Singida ina upungufu wa walimu 300, idadi ambayo ni kubwa sana na ina athari kubwa kwa mustakabali wa ufanisi wa sekondari zetu. Noamba tuongezewe walimu.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa walimu unatokana na mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na upangaji usioridhisha na uwiano usio mzuri wa shule za mjini na za vijijini. Walimu wanajazwa zaidi mijini wakati vijijini kuna upungufu mkubwa. Pia kuna haja ya kuwapa walimu wa vijijini motisha kwa kuwapa posho ya mazingira magumu. Hili lazima tulifanye ili kuwahamisha walimu waende vijijini.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni kweli walimu wanawake wanastahili kuwafuata waume zao, lakini fursa hii inatumika vibaya na kuna uongo mwingi na baadhi ya ndoa ni

*fake*. Mbona hakuna walimu wanawake wanaodai kuwafuata waume zao waliopo vijijini? Hii inachangia kuleta upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri pawe na utaratibu wa kuwa na mikataba kati ya walimu na Serikali au Halmashauri za Wilaya. Mwalimu anapoajiriwa na katika mikataba hiyo lazima suala la kukaa katika vituo kwa muda usiopungua miaka mitatu hata kama mwalimu ataolewa, alazimike kubaki kituoni kwake.

Mheshimiwa Spika, pili, ni uhaba wa maabara. Maabara ni muhimu kwa wanafunzi wetu hasa wale wanaochukua masomo ya sayansi. Je, mpango wa kujenga maabara kila sekondari umefikia wapi kwa msaada wa mkopo wa benki ya Afrika (*ADB*)? Maabara inaendana na upatikanaji wa umeme mashuleni. Je, ni nani anawajibika kuweka umeme katika sekondari? Ni Serikali kuu au Halmashauri za Wilaya, naomba ufafanuzi. Naomba sekondari ya Puma ipatiwe umeme na zile za Ihanja ambapo umeme upo.

Mheshimiwa Spika, *Teachers Service Department* ya mkoani Singida ina upungufu mkubwa wa watumishi hasa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Singida ambayo ina mtumishi mmoja tu. Naomba nyongeza ya watumishi ili walimu waweze kuhudumiwa kero zao tofauti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kutoa mawazo yangu katika mpango mzima wa elimu, pamoja na Bajeti iliyotengwa. Kwanza kabisa, naiomba Serikali pale ambapo inatuletea Bajeti kuipitisha, ihakikishe Bajeti tunayopitishwa inakamilika na iwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011, tulipitisha Bajeti ya shilingi bilioni 665.573 kati ya hizo billioni 525.941 matumizi ya kawaida na bilioni 139.632 zilikuwa za maendeleo. Lakini matumizi ya kawaida zilikuwa 503.379 na matumizi ya maendeleo bilioni 76.821. Katika pesa hizo upungufu mkubwa ni pesa ambazo hazikufika. Pamoja na Bajeti kuwa ndogo, lakini pamoja na hii ndogo haikukamilika. Huu ni udhaifu wa Serikali kutoa Bajeti na upelekaji wa pesa kutofikia kiwango. Ni bora kuleta Bajeti hata kama ni ndogo lakini inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni lini hasa Serikali itamaliza madeni ya walimu. Malalamiko imekuwa kila kukicha, ni vema wakalipwa ili tumalize malalamiko hasa ukizingatia mshahara wao haukidhi siku 30. Hasa walimu wa shule za mshingi mishahara yao ni duni, walimu hawana hata nyumba za kuishi, na hii inapelekea wakae maeneo ya mbali na shule. Hii pia inaondoa ufanisi wa kazi zao shuleni. Ahadi ya Serikali iliyoko madarakani ni kujenga nyumba za walimu 22,000 ifikapo 2010, lakini mpaka sasa hazizidi nyumba 400. Pia Serikali iliahidi kutoa Sh. 25,000/= katika Mpango wake wa Elimu ya Sekondari lakini ilitoa Sh. 7,000/=, ni kidogo tu. Je, napenda kujua ni kwa nini Serikali haikufikia hata nusu ya lengo?

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa Halmashauri nao wamekuwa tatizo. Mwalimu anapotaka kwenda kusoma, hata kama atakuwa ametimiza masharti lakini akifika kwa Mkurugenzi anakwama. Hii si kwa walimu wote, anayemtaka hata kama hajakidhi vigezo atakwenda na huenda akalipiwa na Halmashauri. Hasa mambo kama haya yametokea Kanda ya Ziwa. Kwa kuwa yananihusu kwa karibu, nimejifunza. Ni bora basi walimu wanaotaka kuongeza elimu wakawa na dawati lao hata kama ni Wizarani. Kuliko huko, wanakopitia kwani inaonekana baadhi yao wanaogopa kupoteza nafasi zao kama wengine wakiongeza elimu.

Mheshimiwa Spika, imefika sasa wakati sisi kama Watanzania tuamue kwa pamoja na kwa maandishi kuhusu sera yetu ya elimu. Maana yaweza kuja haribiwa na wanasiasa ambao wanaweza kuja kuongoza nchi hapo baadaye. Kama Watanzania ni vema tukawa na Sera ya Elimu ya Taifa. Watanzania kwa wingi wao waliokosa elimu hata wakidanganywa, ng’ombe anauzwa Sh. 2,000/= wanakubali na kutoa kura zao ili waweze nunua Sh. 2,000/=, hawawezi kupima. Wanaweza kutuletea Rais wa ajabu, akatusumbua.

Mheshimiwa Spika, ili tufanikiwe, ni vizuri kuboresha mishahara pamoja na makazi, vitendea kazi, ili walimu waweze kutulia. Tazama sasa walimu wa shule za msingi, wengine pia ni Watendaji wa Mitaa. Saa ngapi afundishe na saa ngapi aende kufanya kazi za mtaa? Ndipo shule inakuwa inahudumia kazi za mtaa na kukuta watu wako shuleni wanasubiri huduma za mtaa. Huu ni ukosefu wa nidhamu ya ualimu. Utendaji una vihela vidogo, darasani mpaka asubiri mwisho wa mwezi, basi huamua kufanya kazi zote mbili kwa wakati mmoja.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu wa nyumba za walimu ni kubwa na la Kitaifa, naomba Serikali kwa mwaka wa fedha ujao itenge fedha za kutosha ili kuondoa tatizo hili. Hii imekuwa kama kitendawili na kusababisha walimu wengi kuondoka. Vile vile walimu wanaokuja kufundisha vijijini wapewe mafao, posho na mishahara mzuri ili waweze kukaa vijijini na kufundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, mabweni ni tatizo. Ili wasichana kuepukana na mimba mashuleni ujenzi wa mabweni ni muhimu. Naamini Serikali imejipanga vizuri, naomba kupata maelezo ya namna gani tatizo hili litashughulikiwa?

Mheshimiwa Spika, suala la malipo ya walimu. Kumekuwa na kero ya malipo ya walimu pale ambapo wanapata uhamisho au kupandishwa cheo wamekuwa hawalipwi haraka, ni muhimu Serikali ikawa inalipa malipo haraka. Kuna walimu ambao wanadai malipo yao lakini mpaka sasa hawajalipwa. Hivyo, naomba wafanyiwe haraka kulipwa, ni walimu kutoka wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kero ambayo baadhi ya wanafunzi kufukuzwa shule au kutofanya mtihani kwa sababu ya kutolipa ada ya shule. Mimi binafsi nimejaribu kuifanyia kazi, lakini naomba Serikali nayo ieleze msimamo wa Wizara kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu vifaa vya kufundishia shuleni. Vitabu ni vichache na baadhi ya vifaa vingine bado ni vichache sana, naomba *capitation* iweze kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanaoifanya pamoja na upungufu mkubwa wa fedha za kuweza kufikia malengo. *Inshallah* tutafika!

Mheshimiwa Spika, kazi ya ualimu sasa kukimbiliwa na wale ambao wamekosa kazi za kufanya kwa sababu hakuna vivutio. Naomba tuitoe kazi ya ualimu hapo ilipo sasa ili tuipende kazi hiyo pamoja na kwamba ni kazi ya wito. Shule zetu hazina maabara yaliyotimia na nyingine hazina kabisa. Hatuwezi kuzalisha wanasayansi mahiri bila ya mafunzo ya sayansi kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naomba tujitahidi kujenga shule za bweni ili watoto wetu waepukane na hizi *Tution Classes* kwani zinachangia mambo mengi mabaya hasa kwa watoto wetu wa kike.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa walimu ni tatizo na hii nayo inachangiwa na kutotoa motisha kwa walimu wanaopelekwa Mikoa ya pembezoni na kupatikana upungufu mkubwa wa walimu huko vijijini. Kama hiyo haitoshi, walimu wengi wamerundikana mjini tu. Mabadiliko ya mitaala mara kwa mara bila ya kuwapa mafunzo walimu wetu ni jambo ambalo linachangia kupungua kwa ufaulu wa wanafunzi. Naomba sana vituo vya walimu viboreshwe ili viendelee kuwapa mafunzo walimu wetu kama vile malengo yaliyokusudiwa. Ili tupate elimu bora lazima tuwe na walimu walio bora na wenye kukidhi mahitaji kulingana na mabadiliko yanayojitokeza siku hadi ziku.

Mheshimiwa Spika, shule ya msingi Kipumbwi, Pwani iliyojengwa kwa kupitia mradi wa *TASAF*, ambayo ni vyumba viwili tu, naomba ipatiwe usajili ili iweze kuingizwa kwenye mpango wa MMEM. Pia ipatiwe walimu kwani kuna walimu wawili tu ambao wanafundisha elimu ya awali, darasa la kwanza, la pili na la tatu. Shule hiyo iko Kipumbwi, wilaya ya Pangani, Tanga. Wanawezaje walimu wawili kufundisha madarasa manne na matunda yakapatikana.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, wapo walimu wamepandishwa madaraja miaka miwili iliyopita hawajalipwa malimbikizo yao na hata wale waliobahatika kulipwa hawalipwi fedha yote kwa mfano, kama alikuwa anadai Sh. 1,000,000/=, hulipwa nusu na kuambiwa kwamba zimekatwa, hivi kutomlipa kwa wakati mwalimu huyu malimbikizo yake iweje apate adhabu ya kukatwa kiwango kikubwa eti kwamba ni gharama za kutunziwa, hivi yeye ndiye aliyeomba atunziwe? Huu ni uonevu mkubwa na dhuluma ya wazi. Naishauri Serikali malimbikizo ya walimu hao walipwe bila makato ili kuwajengea morali ya kazi.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma walimu walikuwa wanalipwa posho ya ufundishaji, utaratibu huu uliondolewa kwa sababu zipi? Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua lengo la mwalimu *House* la Chama cha Walimu, 2007 lilitolewa ombi kwa Mheshimiwa Rais kwamba warejeshewe posho ya ufundishaji ili walimu hawa waendelee kuwa na moyo wa kuipenda kazi yao. Vile vile nashauri fedha hiyo ya motisha itolewe kwa walimu wanaofundisha darasani na sio maafisa walioko maofisini.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la vitendea kazi kama vitabu vya somo la TEHAMA linatakiwa lifundishwe kwa vitendo lakini linafundishwa kwa nadharia, hivyo, naishauri Serikali ipeleke vitendea kazi ili watoto wetu wasome kwa vitendo na nadharia.

Mheshimiwa Spika, walimu wana madeni mengine ambayo Wakurugenzi au Maafisa Elimu wanafanya kwa makusudi kabisa, walimu wanapokwenda kwenye kusahihisha mitihani ya *Mock* hawalipwi hukopwa kwa kuambiwa waende watakujalipwa, kitendo hiki si kizuri hata kidogo, ni vema walimu wakawa wanalipwa kama maafisa wengine wa Serikali wanaokwenda ziara za aina mbalimbali ambapo huwa hawakopwi.

Mheshimiwa Spika, watoto wa kike wanaopewa mimba na wanafunzi wenzao, naomba ili kuendeleza lengo la mtoto wa kike kusoma, ni vema Serikali iweke utaratibu wa kuwarudisha shuleni mara baada ya kujifungua, badala ya kuwaacha kwani kwa kufanya hivyo adhabu anayoipata ya kufukuzwa shuleni yule wa kiume naye afanyiwe hivyo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fungu lililotengwa kwa ajili ya wanafunzi walemavu na kwa mahitaji ya jamii hii ni makubwa, bado Wizara inaendelea na kigugumizi cha kutokuwajali walemavu. Wakati umefika kwa Wizara sasa kuiangalia upya Bajeti yake ya mwaka huu na kwa kushirikiana na wadau wengine pamoja na wafadhili wa ndani na nje ili iweze kuisaidia jamii hii ambayo wengi wake ni Watanzania walio na kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la walimu. Kutokana na matatizo ambayo yamedumu kwa muda mrefu na kwa kuwa Wabunge wengi wametoa vilio vyao katika Bunge hili kwa nyakati tofauti. Walimu wanadai stahili zao, makazi, posho na hata kupandiswa vyeo na mambo mengi yanayomstahili kama mfanyakazi mwingine. Hali za walimu wetu zinazidi kudidimia na hii inapelekea kushuka kwa mori na ari ya walimu kufundisha na kupelekea wanafunzi wetu kutokufanya vizuri katika mitihani yao na kushuka kwa kiwango cha elimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya MMEM na MMES ni nzuri lakini utayari wake kibajeti bado haukuweza kupunguza au kutatua matatizo yanayowakabili walimu wetu. Ili kuhakikisha utayari wa ufaulu wa wanafunzi wetu, ni wakati muafaka wa kuangalia na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na fedha hizo hizo kuelekezwa katika maeneo ambayo mahitaji yake ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Wizara inaonekana ni finyu. Lakini halisia Bajeti ya Wizara ni nzuri na inatosheleza, bali mpangilio wa matumizi ndio tatizo. Kwa kuwa Wizara imepanga kutumia Sh. 6,235,785,394/= katika matumizi ya kawaida ya Wizara kwa ajili ya usafiri wa ndani *Hospitality and Service* na *Other Operating Service*. Matumizi ambayo hayana ulazima mkubwa na ambayo hata yakipunguzwa hayawezi kupunguza ufanisi wa Wizara. Namwomba Mheshimiwa Waziri fungu hili alipunguze angalau kwa asilimia 50% ili fedha hizo ziweze kuelekezwa kwa kuwalipa walimu madeni yao. Vile vile kuweza kuwasaidia walimu ili Bajeti yao nayo iweze kuwasaidia. Namwomba Waziri aangalie vizuri mpangilio mzima ambao watendaji wake wameufanya katika upangaji mzima wa matumizi.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia Afya njema ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana katika ukombozi wa nchi yoyote ile ambayo imedhamiria kuiweka jamii yale katika ramani ya nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza muhimu ni lazima jamii itambue ni wapi ambapo tulijikwaa na kuanza kurudi nyuma badala ya kwenda mbele. Tatizo kubwa linaloikabili nchi yetu ni kupendelea kusema sana kuliko vitendo. Pia tatizo hilo linatupelekea kutojifunza kutokana na historia na pia kushindwa kuondoka na utamaduni wa uvivu, robo tatu ya maisha ya Watanzania ni kupenda kutegemea ndugu bila kuwa na mawazo ya kujitegemea kwa kuwa na uvivu wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenye rasilimali kibao, lakini Watanzania tunaishi katika lindi la umaskini, ushauri wangu kila mara ni kutatua matatizo kuanzia misingi badala ya kukata matawi. Suala la rasilimali ya kuendesha shule, vyuo na kuwapatia stahili zao walimu ni kuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika. Ili kupata hivi vyanzo ni Serikali kuamua kwa makusudi kumwekea kila mtoto wa Tanzania fungu lake linalotokana na rasilimali ya madini, misitu, maji, na kadhalika. Kila mtoto akiwekewa fungu la fedha hadi umri wa miaka 18 akiwa mtu mzima, tutakuwa tumepata vyanzo.

Mheshimiwa Spika, madhara ya walimu wa *UPE* (*Universal Primary Education*), hatukujifunza kabisa leo tunarudia mchezo huo mchafu wa siasa wa kuanzisha shule za Kata. Hatujifunzi tunapenda sana wingi wa maonesho tu na wala hatujali ubora. Ushauri ni kusitisha kuendelea kupanua shule za Kata bali tuziboreshe kwanza kwa kutatua matatizo ya *facilities* za kufundishia kama vile vitabu vinavyohitajika kwa kujisomea, maabara na kadhalika. Hivi vitapatikana tu iwapo kila mtoto wa Tanzania atawekewa fedha yake na Serikali toka akiwa tumboni mwa mama yake.

Mheshimiwa Spika, inakuwaje shule za binafsi huwa zinafanya vizuri sana kuliko shule za Serikali wakati walimu ni wale wale waliosoma katika vyuo vile vile? Wizara ijipeleleze na itaweza kufanya vizuri iwapo itaweka masuala ya Itikadi pembeni.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla kwa juhudi za kuendeleza elimu. Mafanikio ya kuwezesha kila Kata kuwa na sekondari moja hadi mbili

katika kila Kata na kupanua fursa kwa Watanzania walio wengi hasa wa vijijini. Napongeza pia mpango wa kuweka *High School* kwa kila Tarafa ili vijana wanaotoka shule za Kata wapate fursa. Mambo muhimu ya kuzingatia, ni kuwezesha miundo ya shule ili kuwezesha shule ziwe na walimu wa kutosha, wasihame punde wanapopangiwa. Maji yapatikane mashuleni, barabara na umeme ili kutoa fursa ya kuandaa vizuri mada ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, pia ni vema Lugha ya kufundishia iangaliwe na ndio iwe Lugha inayotumika kwenye usahili wa kazi ili kuepusha kupima watu kwa kigezo cha Lugha ambayo haikutumika katika msingi wa mafunzo. Vile vile mikopo ya vyuo vikuu iwalenge maskini sana walioko vijijini kwani kwa kupewa wahusika itatoa fursa wanayostahili. Kadhalika Wizara iangalie uwezekano wa kuwafundisha walimu na kuwarudisha katika maeneo walikotokea ambako wamezoea mazingira.

Mheshimiwa Spika, upangaji wa walimu nao uzingatie uwiano wa idadi ya wanafunzi waliopo. Vyuo vya Ufundi (*VETA*) vianzishwe na vitoe mafunzo yatakayowezesha wahitimu kujiajiri punde wanapomaliza masomo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi. Awali ya yote naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na timu yake kwa Hotuba nzuri inayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya msingi. Nashauri kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ya msingi kwani hizi sasa idadi kubwa ya wahitimu wa darasa la saba hawawezi hata kuandika barua ya maombi ya kazi na ukilinganisha uwezo huo walikuwa nao wahitimu wa darasa hili hilo miaka ya 70.

Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya shule hizi yamechakaa sana na mengine hayajawahi kukarabatiwa toka yajengwe. Ieleweke kimojawapo cha kuvutia zaidi ya miaka 30 ili watoto wapende kwenda shule ni pamoja na ubora wa majengo na madawati yaliyopo kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Spika, bado shule nyingi zina walimu waliomaliza darasa la saba (*UPE*) na hawa huwa wanajihusisha na miradi yao binafsi kama kilimo, ulevi na hawana mtu wa kuwasimamia. Utategemea atafundisha saa ngapi na ndiyo maana hizo shule hazijawahi kutoa mwanafunzi anayechaguliwa kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu elimu ya sekondari. Bado nasisitiza suala la mitaala ya elimu ya sekondari ifanyiwe mapitio ili mwanafunzi anayehitimu elimu ya sekondari Tanzania afanane na ile ya Kimataifa na hasa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mpango wa MMES II ifanywe ni lazima kila shule ya sekondari ambapo hakuna umeme wa *Grid*, wapatiwe umeme wa *solar* ili wanafunzi hawa waweze kusoma hata usiku ili kuinua kiwango cha elimu yao.

Mheshimiwa Spika, niende katika idara ya ualimu. Utaratibu wa kufundisha walimu kwenye vyuo vya walimu kwa *Specialization* yaani walimu wachukue mafunzo ya walimu wa masomo machache yasiyozidi matatu au manne badala ya kufundishwa masomo mengi kama mwalimu wa hesabu, fizikia na kemia awe amefaulu (*credit*) kwenye masomo hayo badala ya kutaka division *IV* ya *point* 28 hata kama masomo husika hakufaulu anachaguliwa kujiunga na kozi ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu elimu ya juu. Nashauri mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi, wabuni mfumo unaopunguza sana kiwango wanachopewa *cash* kwani maeneo mengi wanafunzi hawa hulewa na fedha hizo kila wanapopewa. Wengine hufanyia shughuli zingine kila wanapoingiziwa fedha hizo kwenye akaunti zao. Kama ni fedha za vitabu wapewe *coupons*, fedha za chakula pale vyuo vina *canteens* wapewe *coupons*, wabaki na fedha kidogo ya *pocket money* na kadhalika. Fedha hizi zinawafanya wasahau kuwa ni fedha za mikopo na kwa vile wengine wanajihusisha na vitendo vya ulevi na uhuni ndiyo chanzo kikubwa cha wao kujiingiza kwenye siasa na kuanza kuipinga Serikali yao ambayo imewafadhili, fedha ya walipa kodi wa nchi hii na kujihusisha kwenye migomo na maandamano. Mbona vyuo vya St. Augustine chini ya *RC* hawajawahi kuwa na migomo? Hebu Serikali ipate mfano huo na namna wanavyoingia mikataba na wanavyuo wanaojiunga na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo na utaratibu wa nani apate mikopo hii, ufanyiwe marekebisho yaani uboreshwe ilin kuondoa kasoro zilizopo.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, pamoja na Naibu Waziri kwa Hotuba yao. Naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, madai ya walimu pamoja na ufinyu wa Bajeti naomba sana walimu walipwe malimbikizo ya madai yao.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikatengeneza mkakati mzuri wa kujenga nyumba za walimu ili kuwasaidia walimu hasa wapya wawe na uhakika kuwa wanakwenda kufundisha kwenye maeneo ambayo hawatapata shida.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la wanafunzi kukaa chini, namwomba sana Waziri aliangalie sana suala hili la wanafunzi kukaa chini, linatengeneza tabaka kati ya wanafunzi wanaosoma katika mazingira mazuri na wanaosoma katika mazingira mabaya. Naomba sana Serikali isiache mzigo wa madawati uwe wa wazazi peke yake. Serikali iboreshe mazingira ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aboreshe shule za sekondari hasa katika maeneo ya kuboresha na kujenga maabara. Ni muhimu sana ili tuweze kupata wataalam, tupo katika zama za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ningependa kuchangia katika eneo la vitabu. Hatuwezi kuboresha elimu kama tuna upungufu wa vitabu. Serikali ihakikishe kila mwanafunzi atapata kitabu cha kusoma cha kila somo husika.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa maamuzi ya kutaka kujenga Chuo cha *VETA* katika kila Wilaya. Mkakati huu usiishie kwenye mpango tu bali uende kwenye Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI SELEMANI KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara iongeze na kuangalia upya mishahara ya walimu. Kazi ya ualimu ni kazi kubwa sana na ngumu. Hivyo, Serikali naomba sana katika eneo hili la mshahara litazamwe kwa nguvu kubwa sana kwani tukitaka elimu ikue nchini lazima mishahara ipandishwe na angalau ifikie kiasi cha Sh. 500,000/= kwa walimu wanaoanza kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, lazima Wizara iache kuweka malimbikizo ya muda mrefu ya madeni mengi yanayodaiwa na walimu wengi katika Jimbo la Mpanda Vijijini na chini kwa ujumla. Yapo madeni mengi yanayodaiwa ya uhamisho, likizo, mapunjo ya mishahara yao, pamoja na posho stahili mbalimbali ambazo wanafanya kazi bila kulipwa. Ili watumishi walimu waweze kufanya kazi lazima eneo hili lipewe umuhimu wa kipekee ili tuweze kuwapa motisha wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linatakiwa kuangaliwa kwa kina sana ni upungufu wa walimu katika shule mbalimbali hasa katika Jimbo langu la Mpanda vijijini ambako kuna upungufu mkubwa sana wa walimu katika shule za sekondari zilizopo katika Jimbo langu, inatisha sana. Kuna shule za sekondari za Ikola, Kabungu, Umoja, Katuma, Mishamo, Mwese na Karema hazina walimu wa kutosha na nyingine zina walimu watatu tu ambao hawatoshelezi kupeleka elimu inayostahili. Sambamba na shule za msingi nako kuna matatizo makubwa sana kwani kuna baadhi ya shule zina walimu wachache sana. Naiomba Wizara iangalie sana wananchi wa Wilaya ya Mpanda kupewa mgao wa walimu wa kutosha ili waweze kukidhi mahitaji ya walimu wanaohitajika katika shule mbalimbali ambao wakipatikana watainua kiwango cha elimu ambacho kiko chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambazo zinahitajika kuboresha ni kuandaa mazingira ya kufanyia kazi. Maeneo wanayofanyia kazi walimu yanatisha sana kwani kuna maeneo mengine wanayofanyia kazi walimu ni kama wametoswa kabisa, hakuna nyumba za walimu na mbaya zaidi hata shule zenyewe ambazo wanafanyia kazi mbaya sana na zinaonekana kama magofu. Mfano, ni shule ya msingi ya Mwese No. 3, shule ya msingi Kabungu, shule ya msingi Milala, shule ya msingi Ikola na shule zote zilizojengwa kipindi cha uhuru zina hali mbaya sana. Naiomba sana Wizara iangalie

maeneo haya ili yaweze kufanyiwa ukarabati ili kujenga sura na taswira ya kuonekana na kuwashawishi walimu wanaofanya kazi katika maeneo ambayo yana hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Wizara ilikazie na kuliangalia sana ni kuboresha Kitengo cha Ukaguzi. Kitengo hiki ni muhimu sana kukiboresha kwani bila kuwa na ukaguzi walimu wanajisahau sana, hufanya kazi wanavyotaka wao. Lakini kama Wizara itaboresha watakuwa wamesaidia sana kuwafanya walimu waweze kuwajibikia vema ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, endapo haya niliyoyaeleza yatajibiwa vizuri, nitaunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ningependa niseme kwamba, elimu ndio msingi wa mwanzo wa maisha ya mwanadamu, ni ufunguo na ukombozi wa maisha na maendeleo ya mwanadamu ndio mfumo bora wa kumwongoza mwanadamu na hata kutoa uwezo wa kuwaongoza wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa ambalo halina elimu halitokuwa na ukombozi wa kimawazo, kifikra, ni Taifa ambalo litavia, litadumaa na kamwe halitofikia katika mustakabali wa maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunazo shule nyingi tokea za *nursery*, za msingi, za sekondari pamoja na vyuo vikuu, hata hivyo nikubali kwamba bado tuna matatizo yafuatayo katika shule zetu, tatizo la walimu na tatizo la maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la walimu limekuwa ni tatizo sugu katika maeneo mbalimbali ya Wilaya na Kata za Tanzania Bara. Suala hili limechangiwa na mambo haya. Kwanza, uhaba wa walimu na wale ambao wapo wanakosa hamasa ya kufundisha kutokana na kwamba kile wanacholipwa kama mshahara hakitoshi hata kwa nauli ya kufikia eneo ambalo anakwenda kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina wajibu wa kuwaangalia walimu juu ya maslahi yao na napenda niseme kwamba Serikali isidharau juu ya taaluma, bila ya taaluma ya elimu Taifa hili halitoweza kufika popote. Ni ukweli usiopingika kwamba sisi kama Wabunge hapa Bungeni tumetokana na taaluma hiyo hiyo ya elimu na ndiyo kila mmoja anakuwa mahiri wa kusema kwa sababu ya uwezo wake wa kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mzima wa elimu unaendana na kuwepo maabara katika shule. Suala la kukosekana maabara katika shule zetu kunashusha kiwango katika msingi mzima wa elimu katika Taifa letu. Kuna masomo ambayo yanamlazimu mtu kusoma katika vitabu lakini kuna masomo mtu anatakiwa asome kwa matendo na ndiyo lazima kwamba suala la maabara na vifaa vya maabara ni lazima kuwepo katika mashule yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba kitengo cha Bodi ya Mikopo ni kitengo muhimu sana na kinahitaji uadilifu, kitengo hiki hakihitaji kuwa na ubaguzi wa kuwabagua Watanzania kwa sababu ya dini zao, uzawa wao na maeneo yao wanayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ili iwahamasishe walimu katika kuwapatia elimu ya kweli watoto wetu na hatimaye waondokane na elimu ya *tution* ni kuwapatia walimu mishahara ambayo itakidhi hali halisi ya maisha, lakini vile vile watapatiwa nyumba za kuishi katika maeneo ya shule wao na familia zao. Vile vile ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba inawalipa walimu mishahara kwa wakati pamoja na posho nyingine ambazo wanastahili kupewa.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu na wanafunzi wa masomo ya sayansi. Wanafunzi wengi sasa wanapendelea kujifunza masomo ya *arts*. Nchi haiwezi kuendelea kwa maeneo hayo peke yake bali maeneo ya sayansi ikiwemo hisabati.

Mheshimiwa Spika, ili masomo ya sayansi na hisabati wanafunzi na hata walimu wayapende ipo haja ya kutafuta motisha ya ziada, vinginevyo huu ulimwengu wa sayansi na teknolojia kwetu sisi utakuwa ndoto na badala yake ajira zinazohusiana na maeneo ya sayansi na hisabati itabidi zije zitawaliwe na walimu na wafanyakazi kutoka nje ya nchi yetu. Pia ipo haja zijengwe maabara na vifaa katika maabara hizo vipatikane.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inazungukwa na shule za sekondari za Kata ambazo uanzishwaji wake ni jambo zuri lakini shule hizi zinakabiliwa na matatizo mengi sana. Shule hizo hazina walimu wa kutosha, ziko baadhi ya shule zina walimu wawili. Je, katika hali hiyo tutegemee kupata tija gani kwa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, shule hizo hazina nyumba za kuishi, kwa hivyo, walimu wanaopelekwa katika mazingira kama hayo si rahisi kukaa. Kwa hivyo, nionavyo, kama Serikali itajenga nyumba nyingi za kuishi walimu, basi hilo pekee litahamasisha walimu waweze kuishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa huna uingiaji mkubwa wa wanafunzi katika kidato cha kwanza. Matokeo yake ya idadi kubwa ya wanafunzi hao itasababisha ongezeko kubwa la wanafunzi watakaoingia kidato cha tano. Je, Serikali inajiandaa vipi katika kulikabili hilo ili wanafunzi wote watakaokuwa na sifa ya kuingia au kujiunga na kidato cha tano wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, ipo haja Wizara ifanye utafiti wa kina, kwa nini wahitimu katika kada zote za elimu wa sasa hawalingani na wahitimu waliomaliza katika miaka 70 na 80. Mhitimu wa shahada ya Chuo Kikuu wa leo uwezo wake haulingani na hao wa nyuma. Hali hiyo ni ya kijumla na sio mmoja mmoja yaani wengi wao wa sasa wanaonekana kana kwamba huwa hawamalizi chuo kikuu.

Mheshimiwa Spika, hali ya usafiri wa wanafunzi katika Jiji la Dar es Salaam inakatisha tamaa. Je, ule utaratibu wa wanafunzi kusoma katika maeneo ya karibu na makazi yao umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, ahsante

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze kwa dhati kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kujenga shule za sekondari za Kata. Shule hizo zimekuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi, watoto wanaomaliza darasa la saba wameweza kupata shule za kusoma, tofauti na zamani ambapo shule hizo zilikuwa hazipo na wanafunzi walikuwa wanakosa kusoma kwa ukosefu wa shule.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatika bado lipo tatizo kubwa la ukosefu wa walimu wa kutosha, vifaa vya kufundishia, maabara na majengo ya maabara lakini pia tatizo la hosteli za wasichana ni kubwa sana, naomba Serikali isaidie. Hosteli zijengwe ili wasichana waweze kuepukana na vishawishi wanavyokumbana navyo mitaani wanakopangisha.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi bado kuna tatizo kubwa sana, Wakaguzi hawana uwezo wa kuwapeleka kufanya ukaguzi mashuleni kwa sababu hawana fedha ya kuwawezesha kwenda kufanya *field*, wanashinda maofisini wamekaa kama vile hawana shughuli za kufanya sababu ya ukosefu wa pesa.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi wamekuwa wakisaidiana na Maafisa Elimu, lakini Maafisa Elimu sasa hivi hawatoi msaada wa pesa kwa Wakaguzi na Katibu Mkuu wa Wizara amekataa wasipewe *OC* yao, nataka kujua Wakaguzi hao wanapata pesa wapi ile ili waweze kwenda kufanya *field*.

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo la Wakaguzi limeikuta Kibondo, Wakaguzi hawana uwezo wa pesa wa kwenda kufanya *field*. Naomba Waziri atakapokuwa anajibu anipatie majibu ili niweze kuelewa hatma ya kilio cha Wakaguzi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. SALEH PAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natanguliza kwamba naunga mkono hoja. Nawapongeza Waziri, naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara wa Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazofanya. Katika kipindi cha miaka 59 iliyopita tumepata mafanikio makubwa sana katika sekta hii. Tumefanikiwa kiidadi ya wahitimu na kuingiza wanafunzi wengi katika elimu ya msingi (*enrolment*) na hivyo kuelekea katika kufanikisha *MDGs*.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliopo sasa katika Sekta ya Elimu uchukuliwe kama ni changamoto au *challenge* ambazo zisiwakatishe tamaa. Kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba Wizara inajipanga vizuri katika kupambana na changamoto hizo. Kuwe na mkakati maalum unaopimika kila mwaka katika kutatua changamoto hizo. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

Kwanza, ni upungufu wa walimu. Serikali ijitahidi kuongeza idadi ya walimu katika miaka mitano ijayo. Tujipange kutoa walimu wa kutosha ili tuwe na *ratio* nzuri ya walimu na wanafunzi. Hata katika vyuo vikuu, tuongeze walimu katika ngazi zote.

Pili, uhaba wa madawati. Kila mwaka tuongeze idadi ya madawati, ni aibu kwa watoto wetu kukaa chini madarasani. Hili tatizo lifike mwisho ifikapo 2015.

Tatu, uhaba wa maabara. Kwa zile shule zilizo karibu katika kila Kata zipatiwe angalau *fully fledged*, maabara katika shule moja ya karibu kwa mafunzo ya vitendo hasa kwa masomo ya safari.

Nne, ni nyumba za walimu. Serikali itenge Bajeti ya kutosha kwa ujenzi wa nyumba za walimu ngazi zote. Tuweke mpango unaopimika wa kujenga nyumba na kulimaliza tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Tano, ni *Schools Rehabilitation Programme*. Miaka ya nyuma kulikuwa na mpango huu. Hali ya shule za sekondari madawati, majengo, mabweni na mabwalo. Wizara iwe na mpango *comprehensive* wa ukarabati na fedha zitengwe kila mwaka. Zile shule za zamani za Serikali ziko kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia kila la heri katika utekelezaji. Kama mnavyofahamu Bajeti hii ni mwanzo wa Bajeti nyingine. Katika Bajeti ijayo tunaomba hayo yafanyiwe kazi.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza mtoa mada kwa uwasilishaji wake mzuri. Pia napenda kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma unakabiliwa na uhaba mkubwa wa *Library* ya Mkoa na *Library* ya Kata ya Mwanga na Businde ndio imepandishwa hadhi ya kuwa *Library* ya Mkoa. *Library* hiyo ni ndogo na ni finyu sana kiasi kwamba bado kuna vitabu vingi vipo kwenye mabox havina hata pa kukaa. Je, Bajeti hii italizingatia hilo la sivyo nakamata mshahara wa Waziri, naomba Waziri aweze kuzingatia ili nasi tuweze kupata *Library* ya Mkoa na eneo lipo kubwa tu na la kutosha.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mkopo imekuwa Bodi ya kifisadi inatoa mikopo kwa kusuasua na pia kwa kuchelewa. Watendaji wakiajiriwa mara tu wanaanza kutembelea magari makubwa na ya thamani, lakini kubwa zaidi watu hawa hawajali wateja ambao ni wanafunzi, kumwona mtendaji tu utazungushwa mpaka basi. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe wito kupitia Bunge hili kwamba watumishi wa Bodi hiyo waache kujiona

Miungu watu kwani pesa hizo ni kodi za wananchi. Kwa hiyo, basi lazima wawahudumie wanafunzi kwa unyenyekevu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampa pole Mheshimiwa Waziri kwa kazi ngumu aliyoifanya katika mazingira magumu ya kukosa pesa za kutosha kukidhi malipo ya walimu kwa madai mbalimbali na vifaa vya kufundishia. Nimeona nichangie kwa maandishi pamoja na kupewa fursa ya kuchangia kwa kuzungumza jana, kuhusu migomo ya wanachuo na siasa vyuoni.

Mheshimiwa Spika, suala hili nimeona kwa kiasi kikubwa Serikali na chama tawala mmekuwa mkionyesha kuchukizwa sana na chama changu cha CHADEMA ndiyo kimekuwa kikitupiwa lawama nyingi kitu ambacho nimeona nijaribu kutolea maelezo mafupi. Hakuna chama chochote ambacho kingependa vurugu vyuoni na pia Chama cha Mapinduzi kisijiweke mbali na kutetea masilahi ya wanachuo. CHADEMA tunalaumiwa kwa sababu tumejiweka wazi kutetea maslahi ya wanachuo bila kificho. Katika utetezi wetu tumekwenda sambamba na kutoa lawama zetu za wazi kwa Serikali kutokana na malalamiko ambayo wanavyuo wamelalamika muda mrefu bila kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hali ya maisha inazidi kuwa ngumu, gharama za maisha zinapanda kila siku lakini posho za kujikimu zipo pale pale. Ucheleweshaji wa kupata pesa hizo ni tatizo kubwa na madai chungu nzima. Hii sheria ya kukataza siasa vyuoni nalo ni tatizo kwa dunia ya leo sio ile ya zamani. Siasa ni maisha, ni vigumu sana kudhibiti jambo hili na pia wanasiasa wasomi wanatakiwa ili waweze kuongoza kitaalam na kisasa zaidi ili twende na wakati, je, wataanzia wapi zaidi ya vyuoni?

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, C*apitation Fund* kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu ambazo Serikali hutenga kila mwaka ambapo mwanafunzi mwenye ulemavu wa shule ya msingi hupata dola 20 kila mwezi na wa sekondari hupata dola 25 kila mwezi. Lakini kiukweli pesa hizi haziwafikii walengwa. Naomba *commitment* ya Serikali katika utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ubora wa elimu kimeshuka sana. Wizara inapaswa kuliangalia upya suala hili kwa kuangalia ubora wa walimu, upatikanaji wa vifaa, maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hadhi ya walimu imefifishwa sana siku za hivi karibuni. Walimu siku hizi wamekuwa wakidharaulika tofauti na miaka ya zamani. Naomba *commitment* ya Serikali kurudisha hadhi na heshima ya walimu nchini. Utu wa mtu ni kazi yenye hadhi, miaka ya nyuma mwalimu alikuwa anaheshimika sana, ni lazima Serikali iandae makakati maalum wa kurudisha hadhi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata *commitment* ya Serikali katika kulipa deni la walimu la Sh. 29.2 billioni. Walimu wengi wanalalamika kuwa hawapandishi madaraja kwa wakati. Ningependa kujua Wilaya ya Kilombero, imetengewa walimu na madawati

mangapi yanatarajiwa kupelekwa? Ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kumaliza madarasa ambayo hayajamalizika.

Mheshimiwa Spika, chuo cha *SAUT,* Tawi la Mtwara wamepelekewa fedha zao za *field* mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua michango ya uji ni shilingi ngapi kwa kila mwanafunzi. Walimu maalum wapewe *incentives* za ziada kwa kuwa wanafanya kazi nzito ya kufundisha wanafunzi wenye ulemavu. Natambua kabisa kwamba hilo linawezekana kwa kuwa Serikali ina uwezo lakini pia walimu hawa ni wachache. Serikali itoe ruzuku kwa asasi zisizo za kiraia zinazosaidia elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule nyingi za Kata ziko katika mazingira yasiyo na huduma muhimu kama maji ya bomba na salama, barabara za uhakika, umeme, hospitali au huduma za afya na kadhalika na upungufu huu unafanya watumishi hawa kama vile walimu washindwe kuhimili maisha ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoshauriwa na Wabunge wengi, walimu wanaofanya kazi katika maeneo yatakayoainishwa kuwa ni magumu wapewe malipo ya ziada kwa ajili ya kuwashawishi ili wakae huko. Yapo malalamiko mengi kutoka kwa Maafisa Elimu wa Mikoa kuwa, wanaonekana kuwa na majukumu mengi ya kusimamia maendeleo ya elimu katika mikoa, lakini kipato cha watu hawa ni kidogo ukilinganisha na Maafisa Elimu wa Wilaya. Nashauri Maafisa Elimu wa Mikoa nafasi yao iangaliwe sambamba na marupurupu yao.

Mheshimiwa Spika, watoto wa kike wanasoma katika shule zetu za Kata wanaacha masomo kwa sababu ya mazingira magumu ikiwa ni pamoja na kupata ujauzito. Nashauri mkakati uwekwe, Serikali ijenge mabweni au *hostels* kwa kila shule ya sekondari ya Kata ili kunusuru maisha ya watoto wetu.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizara kwa kuendelea kuboresha utoaji wa elimu katika sekta nzima ya elimu na hususan katika sekondari za Kata. Aidha, naipongeza Wizara kwa kuendelea kulipa madeni ya walimu na wazabuni. Pamoja na yote hayo Wizara hii bado inazo changamoto nyingi zinazokwamisha juhudi za Wizara katika harakati zake za uboreshaji wa Sekta ya Elimu. Nitataja baadhi tu ya changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni tatizo la walimu katika Jimbo la Mwibara linalotokana na mgao mbovu wa walimu waliopo. Utakuta shule nyingi ndani ya Wilaya hiyo wamepangiwa Jimbo la Bunda na wengine wako mjini kwa visingizio vya kuwafuata waume wao wakati wengi wao au baadhi yao si kweli.

Mheshimiwa Spika, pili, zipo shule za msingi Kisorya na Namalebe ambazo ziliezuliwa na upepo mkali mwezi Machi 2011 na kusababisha watoto wakose mahali pa kusomea hadi sasa. Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imeshindwa kukarabati majengo

hayo ya madarasa na nyumba za walimu ambapo ni madarasa manne na nyumba mbili za walimu. Naomba Wizara itoe tamko ni lini shule hizi zitakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, tatu kuna kero ya ulipaji wa ada ya Sh. 20,000/= kwa shule zetu za Kata. Zamani wazazi walikuwa wakilipa ada hiyo shuleni lakini tangu mwaka jana Wizara imepiga marufuku na kuagiza ada hiyo ilipwe kupitia Benki. Katika Jimbo la Mwibara hakuna Benki na hivyo wazazi hulazimika kutumia zaidi ya Sh. 10,000/= kama nauli, chakula na malazi kupeleka Benki ada ya muhula mmoja ya Sh. 10,000/= kitendo hiki kinasababisha adha kubwa kwani fedha ambazo zinatumika kupelekea ada Benki zingetosha mzazi kulipa ada ya mwaka mzima Sh. 20,000/=. Naiomba Wizara irudi kwenye utaratibu wa zamani wa wazazi kulipia shuleni vinginevyo Wizara itoe maelezo na ufafanuzi wa kina juu ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la walimu wengi kufanya shughuli zao binafsi zikiwemo biashara wakati wa vipindi na wengine kwenda zaidi hata ya kunywa pombe wakati wa vipindi. Zinatolewa sababu nyingi juu ya tabia hii zikiwemo ukataji wa tamaa kimazingira za kimaisha, kukaa eneo moja muda mrefu, kutokuwepo ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara na udhaifu wa Walimu Wakuu kwani wengine hunufaika na walimu wafanyabiashara. Naomba tatizo hili lishughulikiwe mapema kwa vile haliko Jimbo la Mwibara tu. Naiomba Wizara ichukue hatua dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, changamoto ziko nyingi sana lakini kwa leo kutokana na muda naishia hapa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu na watendaji wa Wizara kwa uandaaji na uwasilishaji. Nawapongeza kwa kuendesha na kusimamia maendeleo ya elimu ambayo inakua haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu wastaafu (*primary* na *secondary*). Napendekeza katika miaka mitano ijayo walimu hawa waongezewe miaka ya kustaafu mpaka 65. Kweli hawa watasaidia kuliko vijana tunaowatumia wa *Ex-form VI*. Baada ya miaka mitano huu utaratibu uachwe. Inawezekana kila Halimashauri ikiwa inaombea walimu fulani kuendelea ili kuondoa aibu ya kukuta baadhi ya shule zina mwalimu mmoja, wawili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nichangie katika suala la malipo ya mitihani (*Examination fees*). Napendekeza pia wanafunzi watahiniwa wa shule binafsi wasamehewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji katika elimu. Napendekeza na kushauri kwamba wale wanaowekeza katika miradi ya elimu, faida wanayoipata na ikatumika kuwekeza katika upanuzi wa kujenga maabara, mabweni na kadhalika, mapato hayo yasamehewe kodi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati, kuna kila sababu ya kurudi nyuma na kuangalia mfumo mzima wa elimu na kufanya tathmini kama kweli elimu yetu inaweza kumudu ushindani katika soko la ajira kwa kulinganisha viwango vya elimu na nchi zingine zinazotuzunguka kama Kenya na Uganda. Kwa mfano, leo mfumo wa elimu tulionao ni ule ambao mwanafunzi anapohitimu masomo yake hawezi kutumia ujuzi alionao kwenye jamii hata katika mazingira ya kazi kikamilifu, hali inayoifanya elimu yetu kubaki kwenye makaratasi na siyo vitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vema Waziri akaliona hili na kujadiliana na wataalam pamoja na wadau wote wa elimu ili hatimaye tupate mfumo utakaowawezesha wahitimu kujitegemea na kumudu ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya kidato cha nne na yale ya darasa la saba. Mimi binafsi naona ni kama janga kubwa sana kwa Taifa letu. Kuna mikoa iliyofanya vibaya sana ikiwemo Mkoa wa Kigoma lakini katika Hotuba ya Waziri sijaona juhudi na mikakati yoyote iliyowekwa kuinua kiwango cha ufaulu katika mikoa hii. Sababu za kufeli zimeshatajwa na Wabunge na Wizara inajua. Hivyo basi, hakuna haja ya kurudia, lakini namuomba Waziri atoe ufafanuzi kuwa ni mikakati gani ya makusudi kabisa kuhusu kuinua kiwango cha ufaulu kwa mikoa hiyo ikiwemo Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la Wakaguzi. Inasikitisha sana kwa Wilaya kama Kasulu yenye takriban shule zaidi ya 225 lakini Wakaguzi ni nane tu tena wakitumia gari moja bovu sana. Kwa hiyo, namwomba Waziri anieleze ni mikakati gani ya uhakika imewekwa ili kunusuru idara ya ukaguzi kwa kuongezewa Wakaguzi, kuthaminiwa pamoja na kupewa vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuna Shule ya Walemavu Kabanga Wilayani Kasulu, lakini sasa hivi kuna walemavu wa ngozi watoto na wazazi ambao wamejengewa kituo cha kuishi wazazi hao. Afisa Elimu alishaandika barua kwa Serikali kuomba msaada ikiwa ni pamoja na kuwatenganisha watu wazima hawa kwa kuwajengea kituo chao maalum sehemu nyingine ili kupunguza kuelemewa kwa shule hiyo ya walemavu. Lakini pia shule hii inakabiliwa na changamoto zingine kama ukosefu wa walimu na vifaa vingine vya ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, nawatakia utekelezaji mwema. Ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA**: Mheshimiwa Spika, Elimu ndiyo uti wa mgongo. Yangu ni machache tu, walimu wanaojiendeleza hawapewi kipaumbele kabisa na mishahara yao haipandi wala madaraja; ni kwa nini? Faida ya kujiendeleza kusoma iko wapi? Serikali itoe maelezo ya kina juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, mikopo katika elimu ya juu haikidhi haja ya watoto wa Kitanzania wa kipato cha chini. Utaratibu mzuri ufanyike kwa sababu watoto wanaotokana na familia nzuri zaidi ndiyo wananufaika na mikopo hiyo, kiasi cha kwamba, wao wenyewe wanaanza kuwasaidia kuwapatia pesa wasio nacho. Mantiki

yake ikoje hapo? Wasio nacho wanazidi kuumia. Hali hii inachangia pia migomo isiyo na tija *(demoralization),* katika wanafunzi, *hence,* kutofanya vizuri katika masomo. Lugha itumikayo katika mikopo iwe ni moja.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaomaliza darasa la saba ambao hawachaguliwi kwenda sekondari ni wengi mno, wanarandaranda tu, hali inayopelekea kuwa na tabia mbaya katika jamii kama vile kuwa vibaka, machangudoa, kupata mimba zisizotarajiwa na kuongezeka kwa Gonjwa la UKIMWI. Hii ni hatari kwa Taifa. Mikakati mahususi ifanyike. Serikali inatoa tamko gani juu ya kuwawezesha vijana hawa katika kuwapatia mikopo yenye riba/masharti nafuu; maana wanazidi tu kudorora vijana hawa na maadili kutokomea?

Mheshimiwa Spika, Shule za Binafsi zidhibitiwe juu ya suala la ada ya wanafunzi; kwa nini wanapandisha ada kiholela? Inakuwaje wafanyabiashara ya mafuta wanadhibitiwa bei vituoni, sembuse kwenye Sekta ya Elimu ambayo ndiyo nyeti na ya jamii isidhibitiwe ada? Watoto wengi hususan wale wa kipato cha chini, ambao ndiyo wengi na wangependa wapate *better facilities* kwenye mashule hayo ya binafsi, utaratibu mzuri ufanyike angalau hata kama ni kwa levels.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA**: Mheshimiwa Spika, ninachukua hatua au nafasi ya kuchangia katika Wizara hii, nikianzia na watoa huduma ya elimu (Wizara). Wizara inachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha elimu nchini. Sababu kubwa ni mitaala (silabasi), hubadilika kila kukicha, vitabu ni haba, pamoja na uhaba huo vile vya kiada navyo huwa tofauti shule hadi shule. Kwa vile inakuwa watunzi hutunga vitabu vyao na hufanyika biashara kati yao na Wizara, kinachoendelea pale ni kutokuwepo kwa utaratibu maalum. Vilevile walimu hupata shida katika utekelezaji wa kufundisha. Katika mpango wa kazi, vipengele ni vingi na katika maandalio ya masomo pia. Kwa utaratibu huu, mwalimu huandaa kazi zao si kwa manufaa, bali ni kwa ajili ya Mwalimu Mkuu na Wakaguzi ili kutimiza wajibu tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa hii kwa walimu ambao ndiyo wahunzi wa kuwafua Marais, Mawaziri, Wabunge na kadhalika, maana bila ya walimu hakuna wataalam, kwani wote hupita shuleni. Hata hivyo, pamoja na kazi hizo nzito, walimu kwanza ni wavumilivu na wanahuruma mno; hukubali kufanya kazi katika mazingira magumu. Hutumia muda wao mwingi, kuandaa masomo hata baada ya saa za kazi, lakini hawapewi posho kwa muda huo wa ziada. Hivyo; ni vyema kabisa watu hawa wafikiriwe ipasavyo ili waipende kazi yao.

Siyo hayo tu, pale mwalimu apotezapo maisha, Wizara ione umuhimu endapo hakuna wa kufuatilia mafao yake katika familia, kwa vile kumbukumbu zinakuwepo maofisini, watafutwe watu wa familia yake kama vile watoto wake, wasaidiwe katika matatizo hususan ya elimu kwa wale wanaoachwa wakiwa wadogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mikoa ya Kusini hakuna Chuo Kikuu cha Serikali, kipo chuo kimoja cha *SAUT Mtwara Parish*, ambacho ni cha Misheni. Hivyo, kulingana na yote haya, ni vyema Serikali na Wizara ikae chini na kutafakari juu ya hili. Pia katika Bajeti, iongezewe fedha ili kukidhi haja ya uendeshaji wa elimu.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT**: Mheshimiwa Spika, mafunzo kazini ni muhimu sana kwa walimu ili waende na wakati katika mabadiliko ya mitaala. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuliwezesha hili kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari?

Mheshimiwa Spika, suala la Lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kufundishia pia kuendelezwa, lichukuliwe umuhimu sana, kwa sababu vijana wengi wanafeli kutokana na uhafifu wa kujua Lugha ya Kiingereza. Wenzetu nchi nyingi wanafundisha kwa kutumia lugha zao na wakatoa wasomi wengi sana bila kujua hata Kiingereza kama China, Korea na kadhalika. Ninaomba Lugha ya Kiingereza ifundishwe sana na ipewe kipaumbele kwa ajili ya kuielewa, lakini Kiswahili pia kifundishwe sana ili wanafunzi wakifahamu.

Mheshimiwa Spika, walimu wapya wanapoajiriwa watengenezewe haki zao mapema (mishahara) ili wanapofikisha mwezi wapewe waweze kujikimu na maisha. Pia pasiwe na kero ya ufuatiliaji wa hapa na pale, waweze kuweka akili yao yote pahala pamoja, yaani kufundisha watoto wetu. Walimu wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kuwa imara wakati wote. Elimu itolewe kwa walimu wa kada zote wa msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, walemavu wa ina zote washughulikiwe kwenye elimu, maana wanakuwa na wakati mgumu pale wanapokosa elimu kwa ajili ya kukosa walimu na visaidizi vya kupata elimu. Wasioona wapatiwe mashine za kufundishia, wasiosikia wapatatiwe visikivu na wasioweza kutembea wapatiwe baiskeli ili wafike kwa urahisi shuleni na pia wapatiwe vifaa kwa ajili ya ulemavu uliopo. Hii itasaidia binadamu wote kupata mambo muhimu pia kutofikiria dhana ya kuwatenga walemavu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA**: Mheshimiwa Spika, Shule zetu za Sekondari, hasa zile za Kata, zina upungufu mkubwa wa walimu hasa wa masomo ya sayansi. Hi ni hatari kwani Tanzania ijayo itakuwa na upungufu mkubwa wa wanasayansi. Mbaya zaidi ni kuwa, vijana wengi wanaomaliza shahada za ualimu katika masomo ya sanyansi, hawaendi mashuleni wanakipangiwa, wanatafuta ajira zingine. Ipo haja kubwa ya kutoa motisha kwa walimu wa sayansi kama vile nyongeza za mishahara au posho. Katika miaka ya sabini na themanini, walimu wa masomo ya sayansi walikuwa na mishahara mikubwa zaidi kuliko fani zingine.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iweke mkazo sana katika kuhakikisha Shule za Sekondari za Kata zinakuwa na maabara na vitabu vya kutosha. Hii itaongeza ufaulu katika shule zetu hizi na pia kuchangia kusomesha wanasayansi wengi kwa Tanzania ijayo.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Shule za Sekondari za Kata kwenye Mawilaya yenye eneo pana sana kama Chunya, wanapata tabu sana mwisho wa mwezi kufuata mishahara benki. Kwa mfano, walimu wanafundisha shule zilizo kwenye Kata kama Kapapala au Matwiga, inabidi wasafiri umbali wa kilomita zaidi ya 100 kufuata mshahara benki. Hii inafanya sehemu kubwa ya mishahara yao kwenda kwenye nauli na malazi kwenye nyumba za wageni. Halmashauri zifanye mpango wa kuwasaidia walimu hawa. Hii itakuwa motisha kwa walimu hawa kufundisha kwenye Kata za pembezoni.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na maandamano katika vyuo vingi nchini Tanzania. Serikali lazima ichukue hatua thabiti ili kuepuka maandamano haya. Pawe na mikataba kati ya wanafunzi na Serikali, itakayopunguza maandamano haya au kuyaondoa kabisa. Pili, malipo kwa wanafunzi yafanywe kwa wakati ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wengi wanafeli Mtihai wa Kidato cha Nne. Kuna ukosefu mkubwa wa walimu, maabara na vitabu, lazima hatua za haraka zichukuliwe ili matatizo haya yaondoke. Vilevile *syllabus* ni kubwa mno. Mfano Somo la Hisabati, *syllabus* inaongezwa mwaka hadi mwaka. Hivi karibuni *topics* nyingi zimeongezwa kama somo la biashara wakati hakuna kulichopunguzwa. Serikali ama ipunguze idadi ya masomo mwanafunzi anayetakiwa ayafanyie mtihani au *syllabus* zipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, fedha walizokopeshwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ambazo ziko tayari kukusanywa ni shilingi bilioni 21, fedha zilizokusanywa hadi hivi sasa ni shilingi bilioni 7.9; hii ni idadi ndogo sana, lazima bidii iongozwe ili fedha zote zikusanywe. Azma ya Serikali ni kuwa fedha za mikopo ziweze kuzunguka, yaani zile zinazolipwa ziweze kutumika kukopesha wanafunzi wapya. Hii itaipunguzia Serikali mzigo wa kutafuta fedha za mikopo ya wanafunzi kila mwaka.

**MHE. GREGORY G. TEU**: Mheshimiwa Spika, Chuo kikongwe cha Ualimu Mpwapwa *(Mpwapwa Teacher's College)*, kipandishwe hadhi na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha *University of Dodoma (UDOM).* Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati wa Uchaguzi Mkuu (2010). Je, utekelezaji wa ahadi hii umefikia hatua gani hivi sasa? Jukumu linatekelezwa na nani; na kwa utaratibu upi? Ni busara na hekima kubwa kuwa na Chuo Kikuu Kishiriki *(Affiliated University)* pale ambapo tunacho Chuo Kikuu kama tulivyo na Chuo chetu Kikuu Mkoani Dodoma.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED**: Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, bila ya elimu nchi haiwezi kupata maendeleo. Nchi yoyote iliyoendelea basi elimu inakuwa imepewa kipaumbele; hivyo basi ninashauri Serikali waipe kipaumbele elimu. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuamua kuanzisha Vyuo vya Ufundi kila Wilaya. Vijana wetu wanamaliza shule hawana shughuli ya kufanya, wanakaa vijiweni,

wanajiingiza katika mambo ambayo hayastahili; watakapokuwa na vyuo hivi watapa ujuzi wa kujiendeleza kimaisha.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuishauir Serikali iboreshe maisha ya walimu, kwani wana kazi nzito; bila ya kuwa na utulivu wa maisha hawatoweza kufundisha vizuri kwa kuwa watakuwa wanawaza watakula nini, watakaa wapi pengine nyumba wamekupanga, ada ya watoto wao hawana na wala kodi hawana. Hivyo basi, ninashauri walimu waangaliwe sana matatizo yao. Walimu wengine wanakaa mbali na shule wanazofundisha, ni vyema wakopeshwe pikipiki au baiskeli kwa ajili ya kuwarahisishia usafiri kule vijijini walikopangiwa kazi. Walimu wengi wanaacha kufundisha wanajishughulisha na shughuli nyingine, kwa sababu ya maisha magumu wanayokabiliana nayo wanapokuwa kazini.

**MHE. DKT. WILLIAM AUGUSTAO MGIMWA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kukupongeza wewe na Naibu Waziri, kwa kazi yenu nzuri mnayofanya kuiongoza Wizara ya Elimu. Pamoja pongezi hizi, sasa nichukue nafasi hii kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uimara wa elimu ndiyo nguzo kuu katika maendeleo yote ya Taifa. Tathmini iliyopo inaonesha kwamba, pamoja na upanuzi wa elimu ya sekondari *(quantitatively)*, bado ubora wa elimu *(qualitatively)* ni duni sana. Sababu kubwa ni ukosefu wa mambo yafuatayo: Uhaba wa walimu; ukosefu wa nyumba za walimu; ukosefu wa maabara ya sayansi; ukosefu wa vitabu; ukosefu wa madawati; na ukosefu wa mabweni.

Mheshimiwa Spika, niafahamu kwamba, katika kipindi cha 2011 – 2015, Serikali inatarajia kupata fedha za US$ 150 milioni kutoka *World Bank* na *ADB* kwa ajili ya kugharimia uboreshaji wa Elimu ya Sekondari, ikiwa ni pamoja na kufundisha walimu zaidi, *laboratories,* nyumba za walimu 1,200 na ukarabati wa sekondari 500.

Mheshimiwa Spika, msaada huu ni mdogo sana ukilinganisha ni ukubwa wa tatizo. Ninapendekeza Wizara ileze Programu ya Kitaifa kumaliza matatizo ya elimu Kitaifa na siyo kutegemea misaada.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa shule unaonesha hali ya kusikitisha. Hakuna taasisi zilizokaguliwa kwa zaidi ya asilimia 45.4 na kwa kusema kweli kuna shule Jimboni kwangu ambazo hazijawahi kukaguliwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano. Hali hii inachangia kudhoofisha taaluma ya elimu nchini. Je, Wizara ina mpango gani kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyopo inaonesha Wizara inadawa zaidi ya shilingi 29.2 bilioni, ambazo ni madai ya uhamisho, likizo, matibabu, masomo na mapunjo. Je, Wizara ina mkakati gani kulipa deni hilo?

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA**: Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge la Aprili, 2011, nilimpatia Mheshimiwa Waziri, nakala za madai ya Walimu

wa Shule za Msingi na Sekondari kama zilizowasilishwa na Mkurugenzi wa Wilaya ya Uyui, Tabora. Mpaka sasa sijapata majibu. Halmashauri inanikumbushia sina majibu; ninaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, ninazo Kata kumi Jimboni Igalula. Kata tano zina Shule za Sekondari. Nia ni kuzipandisha shule mbili za Goweko na Igalula ziwe na Vidato vya V na VI, masomo ya sayansi na Wananchi watachangia ujenzi wa madarasa. Tunaomba kujengewa mabweni na maabara kwa ajili ya hizo sekondari mbili za Vidato vya V na VI. Hivi sasa tupo kwenye utekelezaji wa ujenzi wa sekondari tano kwenye Kata tano mpya.

Mheshimiwa Spika, katika Sekondari za Kata tano Jimboni Igalula, tuna upungufu mkubwa wa walimu wa hisabati (20), fizikia (20), kemia (20), baiolojia (20) na masomo mengine matano pia yana upungufu wa ailimia 80 ya walimu.

Mheshimiwa Spika upungufu wa vitabu vya kiada pia ni mkubwa kwa masomo ya sayansi, hisabati na mengineyo kwa Vidato vya I – IV. Madarasa yana kitabu kimoja tu cha mwalimu. Tunaomba vitabu vya kiada na ziada ili wanafunzi waandaliwe vizuri sekondari ili waweze kufaulu vizuri waende Vidato vya V – VI na hatimaye Vyuo Vikuu na kupata wataalamu wa fani zote.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula na hata Wilaya ya Uyui, hawana chuo hata kimoja cha ufundi. Hivyo, vijana wanaomaliza Vidato vya IV na VI hawaajiriki. Hali ni mbaya zaidi kwa wanaomaliza darasa la saba. Tunaomba Chuo cha Ufundi.

Mheshimiwa Spika, asilimia 80 ya Wananchi wa nchi hii ni wakulima. Ninashauri masomo ya kilimo yafundishwe Shule za Msingi ili Sera ya Kilimo Kwanza ifanikiwe haraka. Miaka ya 60 masomo haya yalikuwa yanafundishwa Shule za Msingi na sasa baadhi ya shule hizi. Vijana wakielimika katika fani hii, ajira/kipato kitaongezeka, uchumi utakua, weledi katika kilimo utaongezeka. Tutajitosheleza kwa chakula nchini kwani wakulima watakuwa na elimu ambayo nyongeza itatolewa na maafisa ugani vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

**MHE. ISMAIL A. RAGE**: Mheshimiwa Spika, Tabora Manispaa, ina umaarufu sana tangu wakati wa mkoloni mpaka sasa, kwa ajili ya Shule za Sekondari. Kwa ajili ya Shule za Sekondari. Kwa hivi sasa tuna Shule 29 za Sekondari na Chuo kimoja cha Ualimu.

Mheshimiwa Spika, *Tabora Boy's Secondary School* ina historia ya pekee hasa kwa kuwa Viongozi wengi waliopita katika Uongozi wa nchi kama vile Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere, wamesoma pale, lakini hali ya shule inasikitisha sana, majengo ya zamani hata ukarabati ni wa tabu sana.

Mheshimiwa Spika, katika nchi za wenzetu, shule walisozoma Viongozi huwa zinaangaliwa kwa hali na mali. Ninaomba Wizara yako itoe tamko juu ya kuisimamia vizuri Shule hii.

Mheshimiwa Spika, hali Chuo cha Ualimu Tabora kwa sasa ni mbaya. Ninaomba Wizara iangalie uwezekano wa kukikarabati ili wanafunzi wawe na mapenzi na Serikali yao ya CCM. Moja na sababu ya kupoteza umaafuru wa Serikali yetu ni kutojali kuangalia vyuo vyetu hasa vya ualimu, kwani wana uchungu mkubwa sana na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Wizara kufanya utafiti wa kukibadili Chuo cha Tumbi kiwe Chuo Kikuu cha Kilimo hasa ukizingatia ya kuwa, Kanda ya Magharibi ina mchango mkubwa sana katika Sekta hii ya Kilimo. Kwa mfano, hivi sasa Zao la Tumbaku ndiyo linaloingiza fedha nyingi za kigeni kuliko zao lolote.

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie Hotuba ya Elimu. Mfumo wa elimu nchini bado haukidhi Viwango vya Kimataifa. Wanafunzi wetu wanawekewa mkazo zaidi kushinda mitihani, badala ya uelewa wa kutumia elimu makazini. Endapo nchi yetu itaendeleza mfumo wake wa elimu, usiozingatia kumwandaa mwanafunzi katika utayari wa kufanya kazi, hakika watoto wetu wanaosoma nchini wataendelea kudhalilika hasa wanapoomba nafasi za kazi katika Taasisi za Kimataifa zikiwemo Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Lugha ya Kiingereza siyo jambo la kupuuza katika mfumo wetu wa elimu, kwani ni Lugha ya Dunia. Pia ni ukweli usiopingika kwamba, kujifunza kiingereza kama somo katika Shule za Msingi, haitoshi; wakati umefika sasa tuamue kama tunaandaa wanafunzi wa kukidhi mahitaji machache tu ya ajira. Ninasema hivyo kwa sababu hata makampuni ya ndani ya nchi yanaajiriwa watu wenye uwezo wa kuongea Lugha za Kimataifa ikiwemo kiingereza. Serikali izingatie ubora wa elimu na uwezo wa kuwasiliana Kitaifa. Nchi yetu ni lazima ikubali kwenda na dunia ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN ALLY**: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana ya walimu wapya wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kukosa mishahara yao kwa wakati, hivyo husababisha usumbufu mkubwa sana. Je, Serikali itawasaidia vipi au itaweka mikakati gani ili kusaidia walimu hao kupata haki yao haraka wanapoajiriwa? Ninaiomba Wizara ilifikirie sana suala hili ili kuepusha migogoro na pia kuwarahisishia na kuwapunguzia ukali wa maisha walimu wapya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanafunzi muda mrefu wanakuwa shuleni kuliko muda wanaokuwa nyumbani, ninaiomba Wizara ipange Mpango Maalum wa kuwafundisha watoto wetu elimu ya nadharia kama hatari za madawa ya kulevya, mimba za utotoni na madhara yake. Pia wapwewe elimu ya afya ya jamii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID**: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri na Watendaji wote, kwa Hotuba nzuri sana na kwa jinsi wanavyojitahidi kufanya kazi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Waziri anaweza kuwaleza Wananchi kwa nini ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi ya Bahari ulisitishwa kule Buyu Zanzibar wakati ulianza tangu mwaka 2006 na kusitishwa hadi mwaka huu wa 2011/2012 ndiyo zimetengwa tena fedha za ujenzi na kubadilisha utaratibu mpya wa ujenzi huo? Kilitokea nini kwenye ujenzi wa kwanza na kufikia eneo hilo kukaa kama magofu yasiyo na mwenyewe na kukatisha tamaa ya ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri inaeleza kuwa, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Chuo uliendelea. Je, hiki ni Chuo gani mbona hakikutajwa? Mabweni ya Chuo cha Zanzibar ni mabovu sana hayakaliki na hupata tabu sana kutafuta makazi ya wanafunzi; je, ni lini Serikali itafanya ukarabati au kuyavunja na kuyajenga upya mabweni haya ili wanafunzi wasihangaike kutafuta makazi?

Mheshimiwa Spika, vijana wanaomaliza Ufundi Stadi *VETA* huwa wanapata elimu nzuri sana ya ufundi stadi kwa maisha yao na kwa Taifa letu; hivi Serikali haioni kuwa sasa ni wakati mwafaka kwa Serikali kujipanga kuwaandalia mipango mizuri ya kuwapatia mikopo ya vifaa vya kutendea kazi ili tuwe na uhakika kuwa elimu tuliyoitoa inafanyiwa kazi ipasavyo kwani wanafunzi wengi wanaopata mafunzo hayo huwa hawana mtaji wa kuwaendeleza mbele?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia hoja iliyo mbele yetu hususan eneo la Ukaguzi wa Shule na upungufu wa walimu katika Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya ukaguzi, mashule mengi hayajakaguliwa kwa muda mrefu wa walimu wengi hawatimizi wajibu wao, huku wakiendelea kulipwa kama kawaida. Kuna haja ya kukifanya Kitengo cha Ukaguzi kijitegemee kama ilivyo Ofisi ya Mkaguzi wa Mahesabu kama hatuwezi kukipatia mafungu ya kutosha. Ninaishauri Wizara ikipe kipaumbele Kitengo hiki ili kitekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya inahitaji jumla ya walimu 475, lakini waliopo ni 210, sawa na asilimia 44 tu ya walimu wanaohitajika kwa Shule za Sekondari. Kuna baadhi ya shule zina walimu wawili tu.

Mheshimiwa Spika, tulishaongea na Mheshimiwa Waziri, juu ya suala hili na kuahidi kutupatia angalu walimu 135 kuanzia Julai mwaka huu, walimu watakapohitimu; ni matarajio yangu kuwa, ombi langu litafikiriwa kama nilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JEROME DISMAS BWANAUSI**: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, kilio cha walimu lazima kififikie mwisho kwa kuwapatia posho maalum *(teaching allowance)* ili ziwasaidie kuhimili hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Spika, hali ya makazi ya walimu ni ngumu sana hasa maeneo ya vijijini. Ninaishukuru Serikali kwa kuendelea na juhudi zake za kuwaondolea adha walimu katika suala la makazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali katika kufanya malipo, lakini bado matatizo yapo; ni vyema Wizara ikafuatilia ili isitokee tena kuwepo na malimbikizo ya fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la baadhi ya walimu wanaopangiwa vituo vyao vya kazi kutofika au kufika na kuchukua posho za kujikimu na kutoweka. Wizara itueleze hatua inazozichukua na ni walimu wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni sugu na hasa katika baadhi ya maeneo hususan Mikoa ya Kusini na hasa katika Jimbo langu la Lulindi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nilipokuwa ninapitia taarifa mbalimbali kuhusu elimu, nimefuatilia majedwali mbalimbali yaliyoambatanishwa katika Hotuba ya Waziri Mkuu, alipokluwa anawasilisha makadirio ya Wizara yake kwa mwaka 2011/12, maeneo yafuatayo yanahitaji maelezo ya ziada:-

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mahitaji ya madarasa, nyumba za walimu, vyoo na madawati katika Mkoa wa Rukwa; mahitaji ya madarasa ni 6,654, yaliyopo 3,350 na pungufu 3,304. Kwa upungufu huu unatarajia mwujiza gani kama si kudorora kwa elimu?

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya nyumba za walimu ni 6,701, zilizopo ni 2,012, pungufu 4,689; madawati mahitaji 107.940, yaliyopo 58.991 na pungufu 48949. Katika hali hii, upatikanaji wa elimu bora itakuwa ni ngojera za kisiasa na tutaendelea katika hali hii mpaka lini? Ninaomba nipewe ufafanuzi wa matatizo haya; Serikali ina mpango gani wa kuyaondoa kabisa katika elimu ya msingi?

Mheshimiwa Spika, hali ni hiyo hiyo katika Elimu ya Sekondari; Mkoa wa Pwani kama kigezo, mahitaji ya madarasa 3,577, yaliyopo 2,486 na pungufu 1,091; nyumba za walimu pungufu 1,765, vyoo pungufu 1,567; na maabara mahitaji 355, yaliyopo ni 54 tu, pungufu 301. Tuitafakari kwa pamoja hali hii, kama hakuna jitihada za makusudi na

mikakati madhubuti kunusuru hali hii, huku bado kila kukicha tunahimiza kujenga shule mpya wakati zilizopo zipo hoi bin taaban. Hivi ni nini matokeo ya hali hii bila kuwepo na mazingira bora ya kufundishia, hakuna elimu bora itakayopatikana.

Mheshimiwa Spika, kama hatuwezi kuondosha na kuboresha maeneo haya, bado elimu itaendelea kuwa ni tatizo. Aidha, madeni ya malimbikizo ya walimu bado hayajapata ufumbuzi; ni lini Serikali itaondokana na kero hii inayojirudia mara kwa mara mwaka hadi mwaka? Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari leo, zimeandika kwamba, CWT kimetangaza mgogoro na Serikali juu ya maslahi yao; ni kwa nini Serikali inashindwa kulimaliza tatizo hilo kama hatuwezi kuboresha na kuondosha kero kwa walimu?

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali imeshindwa kulisimamia vyema ni Idara ya Ukaguzi kwa kupewa fedha kidogo na hakuna nyenzo. Bila ukaguzi wa mara kwa mara, hatutaondoa dosari na kasoro mbalimbali katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda ni Shule ya Kitaifa; tena ya wasichana; haina uzio kwa muda wote tangu imejengwa na haina gari la shule la kuwasaidia katika ufanisi wa kazi zao. Nitapenda kupata maelezo dosari hizi zote nilizozielezea kuna mkakati gani wa kuziondosha na upatikanaji wa elimu bora?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, mwenye ukarimu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa maandishi, ninaomba nichangie sehemu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, walimu hawapati haki zao kama vile kupandishwa daraja, kulipwa malimbikizo na hawapati semina elekezi, pamoja na *inservice training.* Matokeo yake ni kushuka kwa kiwango cha elimu nchini petu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii ninaomba niishauri Serikali isitafute mchawi wa suala zima la kushuka na kutopatikana ufanisi katika mfumo mzima wa uendeshaji katika Wizara ya elimu; ni kutoangalia, Serikali inatoa bajeti finyu, ambayo haikidhi, yaani haiendani na mahitaji ya kuendeleza shughuli nzima ya utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ni midogo kulingana na shughuli nzito ya kazi ya ualimu, mazingira magumu wanayofanyia kazi, hawana nyumba za kukaa, mishahara duni na ambayo hawaipati kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, walimu waandaliwe upya mishahara yao na walipwe malimbikizo yao yote kabla ya kuanza mchakato wa utendaji wa kazi wa mwaka huu wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako hili Tukufu, ninaomba nijikite katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishauri Serikali kuhusu mikopo inayotolewa kwa kigezo cha viwango, kwa sababu inabainika kwamba, wale wote wanaokuwa katika viwango vya mwanzo ni watoto wa wazazi wenye uwezo; kwa hiyo, mikopo itolewe sawa sawa kwa wote wanaostahili kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, mikopo hiyo itolewe mapema, kusiwe na urasimu, iendane na wakati yanapoanza masomo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, ninaomba nitoe methali ifuatayo kwa kumalizia: "Mti hawendi bila nyenzo."

Mheshimiwa Spika, tuelekeze bajeti nzuri kwenye Wizara Mama ya Elimu, usimamizi bora, mafao ya walimu, tuboreshe Mikataba yetu, tuwe na walimu bora; wenye ujuzi na utalaam katika kutoa elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Ahsante.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Wizara imejitahidi kutekeleza majukumu yake, lakini kuna upungufu mkubwa ambao hatuna budi kuushughulikia.

La kwanza ni utaratibu tulionao sasa wa kuweka mambo ya elimu katika Wizara mbili tofauti. Kuna mkanganyiko, kule Wilayani wameshindwa kusimamia majukumu yao vizuri; hawajui suala gani walipeleke Wizara ya Elimu au TAMISEMI! Tuache elimu ishughulikiwe na Wizara ya Elimu.

Pili, ni maslahi ya walimu. Walimu wana maslahi duni. Matokeo yake hawafundishi ipasavyo. Wapewe maslahi mazuri kama mishahara, nyumba za kuishi, mkopo na kadhalika ili wafundishe vizuri.

Tatu, tuache mtindo wa kuwapatia Daraja la III Wanafunzi wa Sekondari waliofeli somo la hesabu; tunawaonea. Mtoto anafaulu masomo mengine vizuri kiasi cha kupata Daraja la I, akifeli hesabu anapewa Daraja la III, kwani hesabu ndiyo kipimo pekee cha akili? Mtindo huu umekuwepo miaka mingi sana na haujasaidia kuboresha ufaulu wa somo la Hesabu. Tulipofuta utaratibu huu kwa masomo ya Kiswahili na Siasa *(Civics)*, bado kufuta huku hakukusababisha watoto waanze kufeli masomo haya. Daraja la III hawapewi mikopo ya elimu ya juu. Tunawaonea tuache.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Tanzania hivi sasa ina jumla ya wanafunzi milioni kumi na moja (Taarifa ya Hali ya Uchumi); maana yake Wizara ya Elimu kwa ujumla inasimamia asilimia 26 ya Watanzania. Hiki ni kiwango kikubwa sana na changamoto ni nyingi sana. Tunawaandaa vipi watoto hawa kuwa raia wema, wenye ujuzi na wenye kuweza kushindana?

Mwaka jana takriban asilimia 50 ya wanafunzi waliomaliza Kidato cha IV walifeli. Yalikuwa matokeo mabaya zaidi kuweza kutokea nchini. Huko Kenya walikuwa na matokeo mazuri zaidi toka nchi yao ipate Uhuru. Vyema kuona kuwa Watanzania hawa watakapokutana na wenzao wa Kenya kwenye Soko la Afrika Mashariki, watashindwa. Kuna haja kubwa sana ya kuangalia upya watoto wetu wanasoma nini. Pia ni vyema sasa tutumie mafanikio tuliyopata katika *access* kujielekeza kwenye *reality.* Vilevile ni vyema tutazame upya falsafa yetu ya elimu. Tunataka tujue tunatengeneza Taifa la namna gani. Hebu tubonge bongo zetu sawasawa.

Mheshimishwa Spika, umuhimu wa elimu ya ufundi, hauwezi kuelezwa zaidi sasa baada ya zaidi ya asilimia 80 ya watoto kufeli Kidato cha IV na zaidi ya asilimia 70 ya watoto kutakuwa na sifa ya kuendelea na masomo ya juu. Hivyo, suluhisho hapa ni Mpango wa *VETA* kila Wilaya. Tume-*mention VETA*, kwanza, gharama yake ni *6 billion TSh*. Hivyo, tunahitaji zaidi ya TSh. 700 bilioni kujenga *VETA* Wilaya zote (Halmashauri za Wilaya/Miji na Manispaa). Ninashauri kuwa, Serikali iingie Mkataba na Mifuko ya Pensheni wajenge hizi *VETA* na Serikali itenge kwenye bajeti yake shilingi bilioni 140 kila mwaka kwa miaka mitano kulipa Mifuko pesa zao pamoja na riba kidogo.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuhakikishe kuwa, watoto wanapata mafunzo ya ufundi ili kuendana na ukuaji wa uchumi. Uchumi unapokua unahitaji *skills.* Huko vijijini tunahitaji waashi, maseremala, makanika na kadhalika. Lazima tuwe na *policy* kwamba, watoto wote wanaoshindwa kwenda *"A" - Levels* wapate mafunzo ya ufundi. Huko vijijini mafundi hawa wanapotea kabisa. Uchumi unaokua unahitaji mafundi mchundo. Wizara ifikirie mpango huu wa ujenzi wa *VETA* za Wilaya. Msaada wangu ukihitajika nitawapa.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, ninaomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba nzuri, ambayo ameitoa hapa Bungeni. Ninaomba pia nimpongeze Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Phillipo Mulugo, kwa msaada wa hali ya juu, anaoutoa kwa Mheshimiwa Waziri na kwa hiyo, kwa pamoja kuleta ufanisi wa hali ya juu katika eneo hili muhimu la Elimu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Siha imeitikia wito wa kujenga Shule za Sekondari katika kila Kata *("O" – Level)* na sasa tumeanza kujenga *"A" - Level* katika kila tarafa. Tumeteua shule mbili za sekondari, yaani *Kishisha Secondary School* na *Sekirari Secondary School* ili kwa kushirikiana na Serikali, tuweze kuzifikisha shule hizi katika Kiwango cha Kimataifa. Shule zetu hazina nyumba za walimu, maabara, madarasa, nyumba za utawala na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ahadi ya Serikali ya kuzisaidia shule hizi kwa karibu ili tuweze kuwapa wanafunzi wetu huduma nzuri. Pia tumeteua *Sanya Day Secondary* na *Magadini Secondary* ili tujenge *"A" - Level*.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MH. IGNAS A. MALOCHA**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna zoezi la ujenzi/kupandisha baadhi ya Shule za Sekondari kuanza Kidato cha Tano na Sita ili kupokea wanafunzi wanaofaulu Kidato cha Nne. Mfano mzuri ni Jimbo langu la Kwela; kuna shule 18 za Kata lakini hakuna Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita. Shule zifuatazo zinaombewa kupandishwa Kidato cha Tano na Sita; Tarafa ya Mtowisa – *Vuma Secondary School*; Tarafa ya Laela – *Uchile Secondary school*; Tarafa ya Kipeta – *Kipeta Secondary School*; na Tarafa ya Mpui – *Mpui Secondary School*.

Mheshimiwa Spika, hakuna Chuo chochote cha Ufundi/VETA cha Serikali, zaidi ya vyuo vidogo vilivyopo. Chuo cha Kilimo/Mifugo kinachoendeshwa na Dhehebu la *ARC* kilichopo Laela, kinachotoa mafunzo ya wakulima wadogo wadogo na Chuo cha Ufundi Seremala kinachoendeshwa na Dhehebu la Morovian kilichopo Kijiji cha Kapenta; hivyo, tunaomba Serikali ianzishe Chuo cha Ufundi/*VETA* katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini au kupanua vyuo vidogo vidogo vinavyoendeshwa na Madhehebu ya Dini kwa kuvipatia ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe fedha za kutosha ili kusaidia vijana wanaofaulu mitihani na kukosa watu wa kuwasaidia, kuwalipia ada na mahitaji mbalimbali ya shule.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migomo vyuoni sasa imekuwa kama kitu cha kawaida. Hali hii sito tu kwamba inafanya wanavyuo hao kuharibu ratiba za kimasomo, bali pia husababisha vurugu ambazo wakati mwingine husababisha wanafunzi na hata raia wasio na hatia kuumia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa ushauri ufuatao: Kwa kuwa inaelekea migomo vyuoni kwa sehemu kubwa inachangiwa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, ninashauri ziara zote za Viongozi wa Kisiasa vyuoni zijulikane kwa Uongozi wa Vyuo na madhumuni ya ziara hizo pia yajulikane. Ziara zote zenye mwelekeo wa kisiasa, zipigwe marufuku. Aidha, wanafunzi na walimu watakaobainika kujihusisha na migomo, wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria, ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi na masomo wanafunzi sawia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, ninashauri ihakikishe matatizo ya wanafunzi yanatatuliwa mara moja pale yanapojitokeza. Mikopo itolewe mapema na huduma muhimu kama umeme na maji viwepo vyuoni wakati wote.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuvipongeza sana Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Sokoine, vyote vya Morogoro, kwa kutoshiriki kwenye migomo

ambayo sasa imekuwa kama fasheni katika Vyuo vya Elimu ya Juu.  Ninajua navyo vina matatizo ya hapa na pale, lakini njia mwafaka siyo kugoma bali kuzungumza. Ninavipongeza sana Vyuo hivyo, Uongozi pamoja na Wanafunzi.  Ninapenda pia nitumie fursa hii, kulaani kwa nguvu zangu zote, migomo ambayo imekuwa inafanyika katika vyuo mbalimbali, kinara kikiwa Chuo Kikuu cha Dodoma; ni aibu kubwa kwa Chuo, Uongozi na Wanafunzi wa Chuo hicho!

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani ni Chombo muhimu sana kwa mustakabali wa elimu nchini.  Hata hivyo, kumekuwa na udhaifu mkubwa sana katika suala zima la kusimamia mitihani kuanzia Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na kadhalika.  Mitihani mingi huvuja mapema au huwafikia watahiniwa mapema! Kumekuwa pia na malalamiko kwamba, kuna njama chafu katika usahihishaji na upangaji madaraja kwa watahiniwa.  Ninashauri Baraza kama Chombo kinachosimamia mitihani, lihakikishe kwamba, zoezi la kutunga, kusambaza, kusimamia na kusahihisha mitihani, linafanywa kwa uaminifu mkubwa.  Wale wote watakaobainika kuhusika kwa namna moja au nyingine, kuhujumu zoezi la kutunga, kusambaza, kusimamia na kusahihisha mitihani, basi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, dunia imepita katika hatua kadhaa za maendeleo, kuanzia *Stone Ages, Agricultural Revolution, Industrial Revolution* na sasa Mawasiliano na Teknolojia. Huu ni wakati muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kadhalika.  Hivyo, upo umuhimu mkubwa kuhakikisha kwamba, tunazalisha walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi.  Shule zetu nyingi hasa za Kata zinakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa walimu wa masomo ya sayansi.  Ninashauri zifanyike jitihada za kutosha za kufundisha walimu wengi wa masomo ya dayansi na kuwasambaza kwenye dekondari zetu.  Aidha, ninashauri kuwepo na motisha kwa vijana (wanafunzi) ili wapende masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, jiografia ya nchi yetu ni kubwa sana, Shule nyingi za Msingi na Sekondari zipo vijijini.  Miundombinu ya barabara ni mibovu, umeme hakuna, maji hakuna, maisha huko vijijini kwa ujumla ni magumu, yanakatisha tamaa! Ninashauri ili huyu mwalimu aweze kufanya kazi katika mazingira ya namna hiyo, apewe posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, umeme ni muhimu sana katika Sekondari za Kata. Tunajenga Maabara, tunataka vijana wetu wasome kompyuta.  Mambo haya yanataka kuwepo kwa nishati ya umeme.  Ninaomba Serikali kupitia Wizara hii, iwe na mpango mkakati wa kupeleka umeme katika shule na vyuo ili vijana wetu wasome vizuri.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kwamba, Serikali inadaiwa na walimu jumla ya shilingi 29,237,007,865.64.  Hizi ni takwimu za hadi Juni, 2011.  Hivi hii ni kweli?  Ninaomba kupata ukweli.  Kama ni kweli kuna mpango gani wa kumaliza tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA**: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuleta Hotuba nzuri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kuchangia maeneo mawili ya mafunzo ya Uhandisi wa Umwagiliaji na Mfuko wa Elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali imepanga kuendeleza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 345,000 za sasa mpaka hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2015. Lengo hili ni kubwa, linahitaji rasilimali nyingi zikiwemo maji, fedha na wataalamu. Ili kufikia malengo yetu, tunahitaji Wahandisi wa umwagiliaji 350, lakini waliopo ni 140 tu. Pamoja na kutafuta Wahandisi kutoka nje ya nchi, njia nzuri na endelevu ni kuwafundisha Wahandisi wetu humu nchini kwa kutumia Vyuo na Vyuo Vikuu vyetu. Ushauri wangu ni kwa Vyuo vyetu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SUA*, *Arusha Technical College*, Chuo cha Maji na vingine, kuandaa mitaala kwa pamoja na wadau (Wizara ya Kilimo, Taasisi zake na Makampuni Binafsi kama *TPC*, *Kagera Sugar Kilombero Sugar* na *Mtibwa Sugar* ili Vyuo vyetu vifundishe wanafunzi kulingana na mahitaji ya wale wanaowatumia. Ikibidi, kwa kipindi maalum tuwe na *Tailor-made Course* inayolenga kupunguza uhaba wa wataalamu.

Mheshimiwa Spika, pili, nina lengo la kuanzisha Mfuko wa Elimu katika Jimbo la Buyungu ili kusaidia kupunguza matatizo yanayowapata wanafunzi wengi wasio na uwezo wa kujiendeleza kimasomo. Ninaomba Wizara itusaidie wataalam wa kuanzisha, kuendesha na kusimamia Mifuko kama hiyo ili iwe endelevu. Ninajua kwamba, huko nyuma, Wilaya ya Kibondo ilianzisha Mfuko ulioitwa *Kibondo District Education Trust Fund (KIBODET)*, ambao ulikufa kimyakimya; tunahitaji kufanya jambo hili jema kwa utaalamu na umakini, ninaomba msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na timu yake, kwa kutekeleza majukumu yao pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kurejea tena hoja yangu niliyoitoa wakati wa Bajeti ya Waziri Mkuu, kuhusu posho za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Serikali. Niliomba nijibiwe ili nijiridhishe na hivyo kuondoa hoja yangu ambayo nilishakusudia kuitoa, baada ya kuwasilisha kusudio langu kwa Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kwa heshima niliyopewa kupitia Bajeti hii, kwa kufanyia kazi hoja yangu kama nilivyowaona ofisini kwao na mchango wangu kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huu ndiyo ushirikiano, kwani wote tunajenga nyumba moja. Hata hivyo, ninaomba kufahamu ni lini pesa hizo zitakuwa zimeshalipwa? Je, lini wanafunzi wategemee kupata posho mpya ya shilingi 7,500 kama ulivyoeleza?

Mheshimiwa Spika, eneo la pili la malalamiko ni kuwa imegundulika kwamba, baada ya kutenga bajeti kwa ajili ya vyuo, pesa hutolewa Hazina na kupelekwa Wizara ya Elimu na Ufundi, lakini pesa hizo hazifikishwi zote kwenye maeneo husika na pengine huhamishwa kwa matumizi mengine. Ninadhani huo siyo utaratibu mzuri; ni vyema pesa zifikishwe kwa wakati sehemu zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pesa ya utafiti; kwanza, tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutenga asilimia maalumu kwa ajili ya utafiti kupitia *COSTECH*, lakini utoaji wa pesa hizo inabidi lazima iandikwe *paper*, itathminiwe, ndipo ikubalike au la. Hali hiyo inachukua muda mrefu na pengine kuwa kama wanavyofanya wale wafadhili wengine wa nje *(Donors);* ni vyema sehemu ya fedha hiyo itumwe moja kwa moja katika maeneo husika kama Vyuo Vikuu na Taasisi za Kuendeleza Utafiti na hasa katika kuendeleza matumizi ya tafiti ambazo zimeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huo hasa uhusike kuwezesha *knowledge transfer* ili watu wengi zaidi waweze kuona matumizi ya tafiti za Kitanzania. Pesa hizo zisitumike katika Vyuo Vikuu tu, zitumike hata katika ngazi za Elimu ya Msingi kwa watu wa chini kwenye jamii, waliogundua teknolojia rahisi kutokana na mazingira yao.

Mheshimiwa Spika, tunazipongeza sana juhudi zilizofanywa na Serikali kupitia *VETA,* lakini kwa kuwa vyuo hivyo ni vichache na watu waliomaliza *Form IV* na hawajaweza kuendelea na masomo ni wengi; je, siyo vyema sasa baadhi ya madarasa katika Shule za Kata zikatumika katika kutoa *Extension Services* za *VETA* katika ngazi ya Kata? Kwamba, angalau kwa wiki moja, anaweza kutumwa mtaalam na kwenda kutoa *training* ya jambo fulani hata kama ni ku-*create awareness.*

Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari zipate ukumbi bora wa kusomea na ziwekewe umeme ili kuwezesha matumizi ya TEKNOHAMA.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa kutimiza miaka 50 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ninawapongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kuwa kinara wa Elimu na kielelezo cha mafanikio ya Elimu ya Chuo Kikuu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Mheshimiwa Waziri aungane na Wajumbe wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kuhakikisha Wabunge wanakuwa sehemu ya mafanikio ya ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi kwa kuwaomba wachangie angalau shilingi 200,000.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W.),* kwa Rehema zake kubwa kwangu; *Alhamdulillah.*

Mheshimiwa Spika, elimu ni kitu muhimu sana kwa binadamu yeyote katika maisha ya hapa duniani na hata akhera (baada ya kufa). Mwenyezi Mungu *(S.W.)* ameonesha umuhimu wa elimu katika Qurani Tukufu kwa kumwamrisha Mtume

Muhammad *(S.A.W.),* asome katika aya ya mwanzo ya kitabu hicho. Pia akaonesha tena umuhimu wa elimu pale aliposema katika Qurani Tukufu kwa mtindo wa kuuliza swali; Je wako sawa wale wenye elimu na wasiokuwa nayo? Bila ya shaka jawabu la swali hili alilouliza Muumba wa Mbingu na Ardhi ni hawawi sawa! Pia Kiongozi wa Umma huu; Mtume Muhammad *(S.A.W.),* amesema katika kutilia mkazo umuhimu wa elimu kuwa, anayeitaka dunia na asome; anayeitaka akhera na asome; na anayezitaka zote na asome!

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa nukuu hizo kutoka katika Kitabu Kitakatifu za kuonesha umuhimu wa elimu; Serikali pamoja na kuzifahamu nukuu hizo nilizozitoa, bado haijatilia maanani umuhimu wa elimu!

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na vijana waliojengeka kielimu ni lazima Serikali iweke mkazo wa kutoa elimu bora katika ngazi zote na hasa elimu ya msingi. Shule za Msingi ziwe na madarasa mazuri (majengo), walimu wazuri (waliomaliza kusomea ualimu), vifaa vya kufundishia pamoja na madawati ya kukalia wanafunzi. Pia walimu waboreshewe mishahara yao; walipwe stahili zao kwa wakati na wapandishwe vyeo kulingana na taaluma na jitihada zao kazini. Vilevile walimu wajengewe nyumba bora na za kutosha ili kuinua morali yao ya kazi na kuinua hadhi na heshima ya walimu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi kama jina lilivyo, ndiyo maana ya elimu hiyo ilivyo! Ndio msingi wa kubeba elimu nyingine yote atakayosoma mwanafunzi. Lazima Elimu ya Msingi iboreshwe sana katika nyanja zake zote.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa Elimu ya Msingi uwe ni pamoja na kuboresha ufundishaji wa Lugha ya Kiingereza. Kiingereza ndiyo lugha ya kufundishia sekondari. Mwanafunzi anayemaliza Elimu ya Msingi ni lazima awe pia na msingi mzuri wa Lugha ya Kiingereza ili aweze kumudu masomo ya sekondari vizuri.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Ufundi ni jambo la pili muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani, ikiwemo Nchi yetu ya Tanzania. Vijana wengi sana wanaomaliza Shule za Msingi na kukosa nafasi ya kuendelea na sekondari ni muhimu sana kupatiwa Elimu ya Ufundi ili waweze kujiajiri na kumudu kuendesha maisha yao na kuweza kuchangia katika kukuza Pato la Taifa na kupunguza umaskini. Pia vijana wanaomaliza sekondari na kukosa nafasi za kuendelea na elimu ya juu ni lazima na kwa umuhimu wa pekee, wapate Elimu ya Vyuo vya Ufundi ili kujenga kada ya wafanyakazi wa ngazi ya kati.

Mheshimiwa Spika, Shule za Binafsi *(Private Schools),* pamoja na mchango wao katika Taifa wa kuunga mkono juhudi za Serikali za kutoa elimu, bado kuna tatizo la kutoza ada kubwa! Ninaheshimu na ninathamini jitihada zao lakini ni muhimu sana Serikali kupitia Wizara ya Elimu, waliangalie tatizo la ada kubwa, kwani inaonekana baadhi ya shule hizo zina mwelekeo wa biashara zaidi. Tunafahamu gharama za uendeshaji wa shule ili ziwe shule bora.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba na kuishauri Serikali isaidie kutoa ruzuku kwa Shule Binafsi ili Watoto wa Watanzania maskini, waweze kusoma katika Shule za Binafsi ili kusiwe na tabaka la shule za walionacho na wasionacho.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mwenyezi Mungu, akupe wewe binafsi na Serikali yetu ufahamu, hekima na busara ili uliongoze Bunge hili na Serikali kwa busara na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii na mimi kuchangia katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maandamano Vyuo Vikuu; wale wanaoandamana siyo kwamba hawana akili, wana akili timamu ndiyo maana wanaandamana wanajua nini wanachokifanya. Wangekuwa wanapewa haki zao za msingi, wasingefanya maandamano yasiyokuwa na tija. Ushauri wangu kwa Serikali, inabidi Bodi ya Mikopo ichunguzwe, Hazina, pamoja na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu nao wachunguzwe na mikopo hii itolewe kwa muda mwafaka ili kuondosha migogoro hii baina ya Serikali na wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la siasa katika Vyuo vya Elimu ya Juu; ni suala ambalo haliepukiki kwa sasa, kwani tunawajengea vijana wetu ujasiri wa kuweza kujua siasa yetu ilivyo. Tuzungumzie kwa upande wa CHADEMA tu; kwa mfano, Mwenyekiti Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Ndugu Nape Nnauye, anatembelea Vyuo vya Elimu ya Juu kwenda kufanya nini kama siyo kueneza siasa? Vyama vya Upinzani vinapokwenda inaonekana kama wao ndiyo waanzilishi wa siasa hii. Siasa hii haikuanzia leo katika Vyuo vya elimu ya Juu, ilianza tangu Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ufundishaji kuanzia elimu ya chini mpaka elimu ya juu ni suala ambalo linatakiwa kuangaliwa kwa uangalifu sana. Msongamano wa wanafunzi darasani, unakuta darasa moja lina wanafunzi 200 mwalimu mmoja. Kwa hiyo, Wizara na Serikali iangalie hili tatizo linalotokana na nini la walimu kuwa wachache mashuleni na wanafunzi wengi darasani hasa vijijini. Kwa mfumo huu wa ufundishaji, hatutapata wataalamu bora hasa suala la watoto wa kike kwa upande wa sayansi. Wanafunzi wengi wa kike wanakuwa hawalipendi somo la sayansi kutokana na uhaba wa walimu wa sayansi mashuleni na vitendea kazi kwa kama vitabu, maabara na kadhalika. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali na Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iangalie suala hili la walimu hasa wa sayansi, wamekuwa ni wachache sana katika mashule yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuboresha mishahara ya walimu na makazi; walimu hawa wamekuwa wakipata shida sana. Walimu wanatoka umbali mkubwa sana kufuata mishahara yao; hivyo, mishahara yao inaishia kwenye madeni na mshahara wenyewe ni kidogo. Ninaishauri Serikali na Wizara iwapelekee walimu hawa mishahara yao karibu na sehemu zao za kazi. Hii ni kuwapunguzia umbali mrefu na madeni

wanayokopa kufuatilia mishahara yao. W wanaofuata mishahara yao umbali mrefu makazi yao ni duni; unategemea waje watoe wataalamu bora katika Taifa hili? Hiki ni kitu ambacho hakiwezekani. Mimi ninaishauri Serikali ijaribu kuboresha makazi ya walimu na mishahara na ikiwezekana wapewe posho kwa kazi ngumu wanazozifanya ili kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wanafunzi walemavu; kila aliyekuwia mzima wa viungo ni mlemavu mtarajiwa. Kabla hujafa hujaumbika. Kwa hiyo, hawa walemavu watengenezewe mazingira mazuri wawapo shuleni. Shule lazima zikidhi haja ya kila mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, suala la jinsia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, linatakiwa liangaliwe kwa makini kwa sababu watendaji wengi wa ngazi za juu katika Wizara hii ni wanaume. Kwa hiyo, suala hili lizingatiwe katika Wizara hii. Tumeona wanawake wengi wanaopewa nyadhifa mbalimbali katika Mawizara wamekuwa waadilifu. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri anapokuja kutoa majumuisho ya Bajeti hii, anifahamishe wapo wanawake wangapi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii endapo niliyoyachangia kwa maandishi yatajibiwa.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia hoja katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ninapenda kuongelea suala la Elimu ya Kujitegemea. Elimu ya Kujitegemea ni muhimu na ni vyema irudishwe mashuleni, kwani imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza uwezo wa wanafunzi kimatendo na pia kudumisha umoja na ushirikiano kwa kufanya kazi kwa pamoja, kwani inasaidia kujenga upendo na pia kuwafanya wanafunzi kupenda kufanya kazi kwa pamoja na pia kuwaongezea uwezo wa kufikiri na kuweza kutatua matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uhaba wa walimu. Ninaiomba Serikali ifikirie namna ya kuona ni kwa kiasi gani inaweza kuwatumia wanafunzi waliomaliza *Form IV* au *Form VI* kwa kushirikiana na Kurugenzi husika ili tatizo hili liweze kupatiwa ufumbuzi japo kwa kiasi fulani. Katika hili pia Wzara na Serikali kwa ujumla, iangalie namna ya kushirikiana na nchi marafiki, namna ya kutafuta walimu wa kuweza kuja kutusaidia *(Volunteers)*, kutoka nchi nyingine kama Japani, China na kwingineko. Hili linaweza kutusaidia kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninapenda kuongelea suala la motisha kwa walimu wanaofanya vizuri, yaani wanaofundisha na kuweza kufaulisha vizuri ni vyema utaratibu huu urejeshwe ili uweze kujenga ari ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, nne; ni kuhusu posho, yaani *teaching allowance* na *housing allowance*, zioneshwe kwenye mishahara yao na isijumuishwe kwenye mishahara yao, yaani zioneshwe na walimu wajue. Katika hili pia, kuthibitishwa na kupandishwa vyeo

walimu kuendane sambamba na malipo yao na siyo kupandishwa cheo halafu malimbikizo baadae; hii siyo haki hata kidogo. Serikali irekebishe hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu CWT, yaani mchango wa mwalimu wa asilimia mbili; je, pesa hizi zinamnufaisha vipi mchangiaji (mwalimu); na je, mwalimu ananufaika vipi baada ya kustaafu?

Mheshimiwa Spika, ninaomba hili lifanyiwe kazi. Ahsante, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA**: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, yapo matatizo yaliyoko katika Jimbo la Vunjo, ambayo yanahitaji Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iyatatue:-

Kwanza, wapo walimu wapya huko Vunjo ambao waliajiriwa tangu Januari, 2011 lakini kufikia Juni 30, 2011, hawajalipwa madeni ya maslahi yao. Wapo walimu 130 katika Halmashauri ya Moshi, ambao wanadai nauli, gharama za mizigo kiasi cha shilingi 390,000,000; nitashukuru kama Waziri atanihakikishia kama fedha hizo zimekwishalipwa na kama bado zitalipwa lini?

Pili, katika Halmashauri ya Moshi walimu wanadai shilingi 67,000,000 tangu mwaka 2008, zikiwa ni madai yanayohusiana na mishahara, matibabu na uhamisho. Nitashukuru sana kama Waziri atanifahamisha kama deni hilo limekwishalipwa na kama bado litalipwa lini?

Tatu, lipo agizo la Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wasizalishe madeni mapya, lakini bado Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi, anaendelea kuzalisha madeni mapya, yakiwemo uhamisho na likizo kwa walimu. Nitashukuru kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itafuatilia tatizo hili na kulipatia ufumbuzi.

Nne, kuhusu mizigo wanayotakiwa kubeba walimu wapya wakati wa uhamisho; kuna Nyaraka mbili zinazopingana. Waraka mmoja unadai walimu wapya wanaweza kulipiwa mizigo yao isiyozidi tani tano. Waraka mwingine unadai wakati wa uhamisho wa walimu wapya waliweza kulipiwa mizigo yenye uzito usiozidi tani moja. Ingefaa Waziri atoe mwongozo kuhusu suala hili ili kuondoa manung’uniko yasiyo ya lazima.

Tano, Madai ya Mzee Sananga Lekule wa Kiraracha Marangu Vunjo wa Halmashauri ya Moshi, alitoa eka nne miaka kumi iliyopita Serikali ikajengwa Shule ya Msingi ya Kijiji cha Kiraracha, Kata ya Marangu Magharibi Vunjo, Halmashauri ya Moshi. Niliwahi kuuliza swali Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu fidia ya eneo alilotoa Mzee Sananga Lekule. Serikali ilitaka kutoa eneo Himo la kumfidia Mzee Lekule, lakini hadi sasa eneo hilo haliwezi kupatikana kwa sababu kuna kesi Mahakamani kuhusu eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mzee Sananga Lekule, ameomba afidiwe shilingi 45,000,000 ili suala hilo limalizike lakini mpaka sasa Serikali inasuasua. Ninaomba ieleweke kwamba, Mzee Sananga Lekule, ana mgogoro mkubwa na watoto wake kuhusu eneo hilo ambalo ni urithi wao. Mzee Sananga Lekule, anatutaka tubomoe Shule hiyo ya Msingi Kiraracha ili achukue eneo lake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba msaada wa Waziri; hebu azungumze tena na Waziri Mkuu anasemaje kuhusu hili?

**MHE. SELEMANI J. ZEDI**: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia suala la upungufu mkubwa wa walimu katika Shule zetu za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu ya kiwango duni cha ufaulu ni uhaba mkubwa wa walimu. Katika halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Jimbo la Bukene, hali ya upungufu wa walimu inasikitisha sana; shule nyingi zina walimu wa masomo yasiyozidi mawili! Darasa linatakiwa masomo saba, lakini unakuta ni masomo mawili tu ndiyo yanayofundishwa. Sasa katika mazingira haya, kwa vyovyote kiwango cha ufaulu kitakuwa chini sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua kama Wizara inajua kuwa Shule ya Sekondari ya Semimbela ina walimu wa masomo mawili tu? Mfano historia na jiografia kwa Kidato cha Nne kwa mwaka mzima, *then* wanafunzi hawa waletewe mtihani wa historia na jiografia tu na wapimwe kwa masomo haya mawili tu. Utawezaje kumletea mwanafunzi mtihani wa *biology, physics* au *mathematics* wakati unajua hukupeleka walimu wa masomo hayo; mwanafunzi atawezaje kufanya mtihani wa somo ambalo hakufundishwa kabisa kwa mwaka mzima?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii, kuomba maombi rasmi ya kupatiwa Walimu wa Sekondari wa kutosha. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina uwezo mzuri wa ku-*retain* walimu wanaopangwa kuja Nzega; kwa mfano, mgao wa mwezi Januari, 2011 ni mwalimu mmoja tu kati ya 45 waliopangiwa ndiyo hakuripoti.

Mheshimiwa Spika, naomba Nzega tupewe upendeleo maalum kupangiwa walimu wa kutosha tuna upungufu wa walimu zaidi ya 700.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Idara ya Ukaguzi. Idara hii ni muhimu sana, lakini inaonekana haijatengewa fedha za kutosha, zitakazowawezesha kufanya ukaguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, shule zetu zilizo maeneo ya mbali vijijini, bila kuwa na ukaguzi wa mara kwa mara, utakuta walimu wachache waliopo hawatekelezi majukumu yao.

Jambo lingine ni kuhusu vitabu vya kufundishia. Shule zetu zina vitabu vichache sana. Shule nyingi za vijijini maeneo ya Jimbo la Bukene hazina vitabu kabisa. Ninaomba Wizara ifanye utaratibu wa makusudi, kuziwezesha Shule za Sekondari za Kata za Jimbo la Bukene ziwe na vitabu vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO**: Mheshimiwa Spika, elimu ndiyo msingi wa maendeleo na hakuna nchi iliyoendelea bila kuwekeza katika elimu. Jambo la kusikitisha ni kuona bado Bajeti ya Elimu imezidi kupunguzwa hata katika Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo haikupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ni nani anayesimamia Bajeti hii wakati kwa zaidi ya mwaka mmoja Waziri ameshindwa kwa kushirikiana na wenzake kupendekeza kwa Rais kuteua Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Mkurugenzi wa Sekondari na Msingi? Je, hakuna wataalam wenye uwezo na sifa au hawajaptikana anaowataka? Haiwezekani Wizara nyeti kama hii, iendeshwe bila Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa Sera Elimu ya Msingi na Sekondari!

Mheshimiwa Spika, wakati tunasherehekea Miaka 50 ya Uhuru, bado watoto wengi wanasoma huku wamekaa chini kama vyura tena kwenye Majiji makubwa kama Dar es Salaam. Mfano, Shule ya Rutihinda iliyokuwa shule bora huko nyuma, sasa hivi zaidi ya watoto 90 wanakaa chini. Hii ni aibu kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa baada ya Sera ya Uchangiaji, Bodi ya Mikopo imekuwa ndiyo suluhisho la kuwapatia vijana wetu wa Elimu ya Juu mikopo. Hata hivyo, Bodi hii imeshindwa kuwabainisha wale ambao kweli wanahitaji mikopo hiyo na wale wenye uwezo wa kujilipia wakiwemo watoto wa Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na kadhalika. Hii inatokana na ukweli kuwa, ukikopa siyo lazima urudishe, kwani ni asilimia tatu tu ya wakopaji wamerejesha mkopo wao. Ukiangalia Bajeti hii, asilimia 46 ya fedha zimekwenda kwenye Bodi ya Mikopo na asilimia 54 tu ndiyo ya matumizi mengine yote ya Wizara katika *Reccurent Budget.*

Mheshimiwa Spika, ninashauri iundwe Kamati ya Wataalam waliobobea, watakaoshauri utaratibu bora wenye kuridhisha nje ya Wizara ya Elimu na kutoa mikopo kwa wanaostahili na kurejesha kama walivyoahidi. Ninataka kujua hii Bodi mpya ya Wakurugenzi imeundwa kwa kutumia vigezo gani?

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna janga kubwa la kuporomoka kwa elimu. Elimu siyo madarasa wala ofisi; elimu ni mwalimu na mwanafunzi. Inasikitisha kuona kuwa, kwa miaka mitano, malengo ya ufaulu kwa Elimu ya Msingi na Sekondari yameendelea kushuka. Mfano, elimu ya msingi (2005), azma ikiwa ni kufikia ufaulu kwa asilimia 70, lakini kuanzia 2005 – 2010 ni mwaka 2006 tu ndiyo ilifika asilimia 70.5 na mwaka 2009 kuwa asilimia 49.38; hii ni aibu kubwa. Katika MMES, lengo lilikuwa kufikia asilimia 50 toka asilimia 32; cha ajabu ufaulu umeshuka hadi asilimia 11.8 kwa Daraja la I – III kwa 2010. Huku daraja 0 ikiwa ni asilimia 50, *Division IV* asilimia 38.

Mheshimiwa Spika, hata Vyuo vya Elimu ya Juu vinasikitisha kuona navyo vinaporomoka kutokana na sababu mbalimbali. Kwa kwa ule utaratibu wa *Webometric Ranking System* unaoweka mkazo kwenye ubora wa kufundisha; utafiti wa 2007 ulionesha kuwa, *UDSM* ilikuwa ya 13 kati ya Vyuo 100 Bora Barani Afrika. Cha kwanza ukiacha vya Afrika Kusini na Misri, Kusini mwa Jangwa la Sahara na juu ya Mto wa Limpopo, lakini mwaka huu Januari kimeporomoka hadi nafasi ya 34 kwa ubora. Je, ni sababu zipi zilizopelekea anguko hili?

Mheshimiwa Spika, lengo la Vyuo Vikuu ni kuwa kimbilio la kupata ukweli ambao hauna mawaa. Cha ajabu ni pale Kitengo cha Utafiti kama cha *REDET* kinapofanya utafiti kwa kushabikia waziwazi Vyama vya Siasa na hivyo kutoa mwelekeo kwa wapiga kura. Hii ni aibu na Waziri atueleze matokeo ya utafiti ya *REDET* yalipatikana kwa utafiti wa kisayansi au la; na kwa nini yalikuwa na kiwango kikubwa hivyo cha makosa *(Margin Error)?*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la mafao kwa Maprofesa wanaostaafu. Wakati wa Bajeti ya Serikali (Utumishi), Waziri alisema kuwa, mafao yao yatajadiliwa ili nao waweze kufaidika na mafao bora. Pia ninataka kuelezwa ni *VCs* wangapi wameshafikia umri wa kustaafu lakini bado wako madarakani; na utaratibu wa uteuzi wao uko vipi?

Maprofesa ni watu muhimu sana, ndiyo waliotufundisha, wametoa Marais, Majaji na kadhalika; ni lazima tuwape heshima na mafao bora hadi watakapofariki kwa michango yao mingi na iliyotukuka kwa Taifa letu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika, ninapenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumko wa madeni mapya ya walimu; ni kweli yapo madeni yasiyoweza kuepukwa kama likizo na malimbikizo ya nyongeza za mishahara au kupanda daraja na yale ya uhamisho. Mwaka 2009/2010, nilisema na ninarudia kusema kwamba, mamlaka wanayopewa Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya kufanya uhamisho wa walimu, yanatumika vibaya, kwa hila na kukomoana; ni vyema madaraka hayo yakasitishwa na kuachiwa uwezo wa kutoa ushauri na mapendekezo tu kwa uhamisho. Tuzingatie ushauri unaotolewa kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, jitihada zimekamilisha ujenzi wa maabara mbili kubwa katika Shule ya Sekondari Kata ya Misozwe. Hata hivyo, maabara hazina umeme wala vifaa tangu Januari, 2011!. Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Elimu juu ya hali hiyo, lakini majibu yake hayakuwezesha kuondoa tatizo hilo. Kwa hali hiyo, majengo ya maabara yatabaki katika hali hii mpaka lini? Nilimshauri Afisa Elimu Sekondari, aombe msaada na kufuatilia barua yangu Wizarani lakini hakuna matokeo mapya! Kufikisha umeme, *TANESCO* wanataka shilingi 12,000,000 na hawana uwezo wa kusaidia.

Kwa kuwa siridhii hali hii kuendelea, nitatafuta msaada popote ili kabla ya Agosti, 2011 umeme ufike katika maabara na tayari mimi binafsi nimeshaweka vifaa vichache na pia vitapatikana kutokana na fedha kidogo sana zitakazotolewa kupitia Halmashauri ya Wilaya na Serikali Kuu. Maabara hii inalenga kuhudumia Shule mbili za Kata ya Misozwe na Kata jirani ya Vucheba.

Shule mpya za Kata zinazotokana na kugawanywa kwa Kata kubwa zilizopo. Kata zinapogawanywa, ikiwa na Shule moja ya Kata inazalisha Kata mpya, ambayo haitakuwa na Shule ya Sekondari ya Kata. Kwa kuwa Wananchi wanaoingia katika Kata mpya walishiriki katika ujenzi katika Kata ya awali; ni vyema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikatoa pendekezo la kuongeza fedha za ujenzi wa madarasa kwa shule hizo mpya ili kuongeza nguvu ya ujenzi wa shule mpya katika Kata mpya, badala ya kuachia mzigo huo kwa Wananchi peke yao. Hata kama usimamizi wa ujenzi wa shule za sekondari uko chini ya TAMISEMI, bado kimsingi Wizara ya Elimu inahusika na Sekta ya Elimu kama chombo cha Taifa.

Kasi ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi wa kati *(VETA)* iongezwe. Kuongezeka kwa Shule za Sekondari za Kata, kunaongeza idadi kubwa ya Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari, ambapo kwa vyovyote haiwezekani wote kuendelea na masomo ya juu hadi Chuo Kikuu. Kwa kuzingatia mahitaji ya watendaji wa nafasi za kati na hasa ufundi, ipo haja kuongeza kasi ya ujenzi wa Vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya. Mfumo huo uende sambamba na kurejesha mfumo wa zamani wa kuchagua baadhi ya Shule za Sekondari katika ngazi ya Kata kuwa na mfumo wa Shule za Sekondari za Ufundi. Mkakati huu unahitaji dhamira ya dhati kutoka katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; tunashauri mkakati mpya uandaliwe na kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR**: Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ninapenda kuchangia eneo la Elimu ya Ufundi *(VETA)*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Serikali kuweka mkakati mzuri wa kuwahamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na mafunzo ya ufundi *(VETA)* ili waweze kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza masomo yao na hasa ikitiliwa maanani kwamba, ajira katika Serikali zimekuwa haba na kwamba, ajira siyo lazima iwe kutoka Serikalini tu bali kazi ni hata ya kujiajiri mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninashauri wanafunzi hao wamalizapo mafunzo yao, waweze kupatiwa mikopo kwa ajili ya kuanzisha biashara zao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Spika, ninashukuru Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nianze moja kwa moja kwa kusema ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Vitengo vilivyopo chini ya Wizara, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii na kwa ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo na nitaanzia na changamoto inayozikabili Wizara hii:-

Kwanza, ufinyu wa Bajeti hasa Bajeti ya Maendeleo. Kati ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa ya bilioni 139.632; ni shilingi bilioni 76.821 ambayo ni sawa na asilimia 55 tu. Hivyo; ni wazi kabisa shughuli za maendeleo zilizopangwa kufanyika, mfano, ujenzi wa maabara, nyumba za walimu na kadhalika, hazikutekelezwa. Inasikitisha kuona sulala la elimu ambalo ni kipaumbele cha kwanza, zaidi ya asilimia 45 za pesa za maendeleo hazikupokelewa na Wizara.

Pili, kinachonisikitsha zaidi ni kuona Bajeti ya Mwaka huu wa 2011/2012, Bajeti ya Maendeleo imepungua na kuwa shilingi bilioni 135.518 toka shilingi bilioni 139.632; tofauti ya zaidi ya shilingi bilioni 4.114. Ninapata mashaka na dhamira ya Serikali ya kuboresha elimu na kama *trend* ya upelekaji fedha za maendeleo katika Wizara hiyo ni shilingi bilioni 74.534 (asilimia 55 tu) zitakazopelekwa.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba, malengo ya mwaka 2011/2012 kama yatatekelezwa, kwa upande wa Mkoa wa Pwani, ninaouwakilisha katika kifungu 4390 *(SEDP)*, Kitabu cha *Vol. IV*, ukurasa wa 155 ni kiasi cha shilingi bilioni 2.061 zimetengwa kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyokuwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2010 Mkoa wa Pwani ni mabaya sana. Kati ya wanafunzi 10033 waliofanya mtihani, wanafunzi 5,889 walipata *Division Zero*, ambao ni asilimia 59 ya wanafunzi waliofanya mtihani huo. Matokeo hayo yanasikitisha sana na yamesababishwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kuna upungufu wa madarasa – Jumla 2,370, asilimia 39 ya mahitaji;

(ii) Kuna upungufu wa nyumba – Jumla 3,961, asilimia 73 ya mahitaji;

(iii) Kuna upungufu wa madawati – Jumla 51726, asilimia 41 ya mahitaji;

(iv) Kuna upungufu wa viti – Jumla 6,156;

(v) Kuna upungufu wa meza – Jumla 6,210; na

(vi) Kuna upungufu mkubwa wa maabara.

Mheshimiwa Spika, kwa Bajeti ya Maendeleo inayofanana na mwaka uliopita, ambayo ukilinganisha na matokeo haya; ni ukweli usiofichika kuwa Mkoa wa Pwani tuna safari ndefu ya kupiga hatua katika Sekta ya Elimu na ukizingatia historia ya Mkoa wa Pwani, ambao ulikosa fursa za elimu. Mkoa wetu wa Pwani una upungufu wa walimu zaidi ya 1,000. Upungufu huo unajitokeza sana kwenye maeneo yenye mazingira magumu hasa ya *Delta.*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niipongeze Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Pwani, eneo la Kibaha, ambacho kinatarajiwa kukamilika Mwaka huu wa Fedha. Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Pwani hususan vijana, ninaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kupitia ilani ya CCM ya Mwaka 2010-2015, kwa mpango wake wa kujenga Chuo cha *VETA* kila Wilaya. Kwa Mkoa wa Pwani, Wilaya zilizochaguliwa ni Bagamoyo na Mafia. Hata hivyo, nina wasiswasi na utekelezaji wa Mpango huo kwa Mwaka huu wa Fedha kwa vile Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu, *Vol. IV*, ukurasa wa 77, kifungu 4397 - *Support VETA*; kwa mwaka huu kiasi kilichotengwa ni shilingi milioni 100, kulinganisha na kiasi cha shilingi milioni 590 (fedha za ndani) na shilingi bilioni 8.102 (fedha za nje). Hivi ni kweli mpango wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* kila Wilaya utaanza kutekelezwa kwa Mwaka huu wa Fedha?

Mwisho Mheshimiwa Spika, niipongeze Taasisi ya *WAMA,* inayoongozwa na Mama Salma Kikwete, kwa uwekezaji wake kwenye elimu ya mtoto wa kike kwa kujenga Shule ya Sekondari ya Mfano iliyopo Kijijini Nyamisati, Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani. Shule hii inafundisha wanafunzi wa kike toka familia duni na yatima kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani; na wanafunzi hao wanasomeshwa bure. Ninaiomba Serikali ione namna ya kuchangia gharama za uendeshaji wa shule hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Naibu Waziri na Watendaji wote waliohusika katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ina matatizo lukuki katika sekta hii ya elimu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Idara ya Elimu ya Msingi haina gari la kuwawezesha kusafiri katika maeneo mbalimbali ndani ya Wilaya ili kukagua Shule za Msingi hivyo kuathiri mwenendo mzima wa ufanisi katika kutekeleza majukumu yao na hivyo kuweza kuinua Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Nanyumbu kuna uhaba mkubwa wa nyumba za Walimu. Tatizo hili ni kubwa sana na hivyo kupelekea Walimu wanaopelekwa Wilayani

Nanyumbu kurudi au kuacha kazi kwa ukosefu wa nyumba za kuishi. Naiomba Wizara isaidie kuongeza bajeti kwa Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Wilaya ya Nanyumbu ina uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa na kwamba madarasa mengi yanayotumika sasa ni ya zamani na yamechakaa na hivyo kudidimiza elimu Wilayani.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine katika sekta hii ya elimu ni uhaba wa matundu ya choo kiasi kwamba shule nyingi hazina vyoo na kufanya wanafunzi kujisaidia vichakani na au kwenye vyoo vya ovyoovyo na hivyo kuhatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa madawati Wilayani Nanyumbu unatisha. Shule nyingi za Msingi zina upungufu mkubwa wa madawati. Hivyo naiomba Serikali ione uwezekano wa kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni tatizo la uhaba wa Walimu katika Shule zetu za Msingi na za Sekondari. Wilaya imekuwa ikipatiwa Walimu wachache na hivyo kuathiri utoaji wa elimu. Naiomba Wizara itupatie Walimu wa kutosha Wilayani Nanyumbu ili wanafunzi wapate elimu inayostahili kwani ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha na maendeleo ya nchi yanaletwa na elimu, iwe *formal or nonformal*. Hivyo ili Tanzania tuendelee, lazima elimu yetu iwe ni ya juu kwa kulinganisha na nchi za jirani kwa kuanzia elimu ya Awali hadi Vyuo Vikuu. Elimu yetu iwe ni bora "*quality education"*.

Mheshimiwa Spika, tuziboreshe Shule za Awali, kwani hapa ndipo tunapopata kuwajenga wanafunzi na kuwatambua '*talents'* zao kwa uzuri zaidi. Ni vizuri Wizara kuangalia yafuatayo na kuyarekebisha:-

1. Walimu wanaofundisha hawana sifa wala vyeti.

2. Hakuna vyuo maalum vya Walimu wa Shule za Awali.

3. Serikali kutotilia mkazo shule hizi kunapelekea elimu hiyo kuwajengea watoto msingi mbovu wa maisha, hivyo ni vyema Serikali kutilia mkazo elimu hii.

4. Uwiano wa wanafunzi na Walimu 54.1 ni mbovu ni vizuri uwiano uwe 20.2, hii ni *international*.

5. Vitabu vya kufundishia viwepo mashuleni.

6. Kuwe na wakaguzi maalum wa shule hizi ambao nao wamesomea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mitaala, yafuatayo yazingatiwe:-

1. Kubadili mitaala mara kwa mara inahatarisha elimu na kuifanya kutokuwa na mpangiilio mzuri, lakini unaweza kubadilisha pale panapohitajika.

2. Mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari ibadilishwe ili iweze kulingana na ajira zinazohitajika ili wanafunzi wakimaliza waweze kujiajiri wenyewe.

3. Masomo yasiendeshwe kinadharia tu bali kwa vitendo kwani itawasaidia katika soko la ajira.

4. Umefika wakati wa kubadilisha mfumo wa elimu kwa kuzihusisha sekta za viwanda na biashara katika kutayarisha mitaala itakayotumika katika kufundisha wanafunzi katika vyuo vyetu. Lengo ni kuelekeza mitaala hiyo katika mahitaji ya sekta hizo. Soko linahitaji ujuzi na umakini wa kutenda badala ya elimu ya maarifa.

5. Tubadilike na kuangalia mitaala yetu na soko la ajira linahitaji nini. Vijana wengi wanaomaliza vyuo hukosa ajira kwa sababu hawana sifa hizo.

Mheshimiwa Spika, tuwe na Walimu bora na sio bora Walimu. Walimu wengi wanaajiriwa lakini wengi wao huifanya kazi ya Ualimu kama ni *"Steping–stone"*. Hivyo Wizara iangalie kwa makini na iwe na mikakati mizuri ambayo itaweza kuwadhibiti Walimu hawa. Walimu wapatiwe mahitaji yao mapema ili wafanye kazi kwa uangalifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, maktaba, shule ziwe na maktaba ambazo zitaweza kuwasaidia wanafunzi kwa kujiendeleza katika kusoma. Walimu zitawasaidia katika kupata *references*.

Mheshimiwa Spika, maabara, Shule za Sekondari zipatiwe maabara zenye vifaa ambavyo wanafunzi wataweza kufanya mazoezi kwa vizuri na uangalifu. Walimu watakaofundisha wawe wengi na wa kutosheleza kwa masomo ya *Physics*, *Biology* na *Chemistry* na sio kuwe na maabara, vifaa lakini Walimu wa kufundisha masomo hayo hawapo.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi, kutokana na hotuba ya Waziri imeonesha upungufu mkubwa katika Idara ya Wakaguzi hasa pale wanapohitajika kwenda kukagua. Katika *data* zilizooneshwa, shule 14,983 ndizo zilikaguliwa kati ya shule 62,025. Ni vyema Idara hii ikaangaliwa vizuri ili Walimu wafanye kazi zao vizuiri, kwani shule zikikaa bila ya kukaguliwa hupelekea wanafunzi kufeli na Walimu kutofanya kazi zao vizuri. Ukaguzi huwa wa aina mbili, ule wa jumlajumla na ule wa siku moja. Je, wakaguzi hawa wamefanya ukaguzi upi? Naomba Waziri utakapokuja kufanya majumuisho alieleze Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya Wahadhiri, Sheria ya Mikopo kwa Wahadhiri inabanwa kwa baadhi ya Vyuo Vikuu, ingawa Wahadhiri wanaofundisha katika Vyuo vya Umma hupewa nafasi ya kupata mkopo na kuendelea na masomo. Kwa upande wa Zanzibar hasa Chuo Kikuu cha SUZA ni Wahadhiri wangapi mpaka sasa (*Post-graduate or Tutorials)* wamepata nafasi hiyo na kama hawakupata kwa nini? Naomba Waziri utakapofanya majumuisho alieleze Bunge hili juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa wanafunzi, kuna wanafunzi waliopata nafasi ya kwenda nje na baadaye hutaka kuendelea kwa *postgraduate*, Serikali huwakatalia lakini chuo huwakubalia. Je, Serikali haioni umefika wakati kwa wale waliopo nje wakapewa mkopo na kuendelea na masomo yao? Kama sera hii haipo au utaratibu huu haupo, kwa nini hauanzishwi na mkawaruhusu kuendelea na kuwapa mkopo? Je, kama Wizara mnalionaje hilo? Naomba atueleze utakapokuja kujumuisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na timu ya wataalam kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sekondari za Kata zipewe kipaumbele ili Walimu, vitabu, madawati na vifaa vya kufundishia vyote viongezwe.

Mheshimiwa Spika, Walimu walipwe madai yao yote, ili madai ya stahili zao yasiendelee kuwa sababu ya vurugu katika shule na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa zote za ajira na kupandishwa vyeo, usimamizi na udhibiti wa Walimu ufanywe katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa Walimu hewa ukamilike na Wizara iandae *monitoring instruments* kuweza kubaini mabadiliko ya idadi ya Walimu na mabadiliko hayo yaingizwe kwenye kumbukumbu za utumishi kila mwezi na kila mwaka.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, naomba kuelezea masuala kadhaa ambayo naona Serikali yetu inahitaji kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kila mzazi anapenda mtoto wake asome vizuri na kupata maisha bora kutokana na elimu anayotarajia kupata lakini ili mtoto apate elimu bora tunawategemea Walimu watufundishie watoto wetu. Serikali bado haijawawekea Walimu mazingira bora ya kufundishia hasa Walimu wa vijijini ambao wanakumbana na mazingira magumu sana kwa kukosa nyumba za kuishi, kukosa usafiri wa uhakika, kukosa umeme hata mtandao ni tatizo katika maeneo mengi ya vijijini vilevile maji nalo ni tatizo sugu. Pia Walimu kwa ujumla wanadai Bilioni 29. Naishauri Serikali ilipe madeni haraka iwezekanavyo tusiandae na kukaribisha Migomo ya Walimu, kama mgomo wa Walimu ukitokea kwanza ni aibu kwa Serikali lakini pia wananchi watakosa imani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ione uwezekanao wa kuwapa motisha/posho Walimu wa Vijijini ili wawe na morali ya kuendelea kuishi na kufundisha vijijini. Pia mishahara ya Walimu iongezwe ili tujenge Taifa imara kwa kupata watoto wengi wenye elimu bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapoteza fedha nyingi kwa Walimu watoro, kuna wengi wanagharamiwa kwenda kituo cha kazi na hawafiki na kuiingizia Serikali hasara. Naomba Walimu kama hao wafuatiliwe na kuadhibiwa ili wasiwashawishi wengine kuiga mfano wao. Nashauri Walimu wachambuliwe kama kuna Mwalimu wa eneo ambalo anakotoka mfano Mwalimu wa Tabora kwanza apangiwe Tabora ili iwe rahisi kujua kama amefika kituo cha kazi na hivyo tuweze kuwa na uhakika wa Walimu kuwepo kituo cha kazi. Aidha, Halmashauri zetu zipewe uwezo wa kuajiri Walimu waliopo katika Wilaya husika ili pengo la ukosefu wa Walimu liweze kujazwa.

Mheshimiwa Spika, siasa Vyuoni, kuna Walimu vyuoni ambao badala ya kufundisha masomo wanahubiri siasa. Naomba Serikali itumie vizuri vyombo vyake ili iwabaini wasaliti hao na kuwachukulia hatua kali. Pia kuna wanafunzi ambao wanatumiwa kuchochea migomo na maandamano, siamini kama kila mwanafunzi anapenda kushiriki katika migomo. Wanafunzi walio wengi wanapenda kusoma na si kushiriki katika fujo au migomo. Katika hili, nashauri kwa nguvu zote Serikali itumie uwezo wake wote kuzuia na kudhibiti wanafunzi wachache ambao wanatumiwa na wanasiasa kufanya fujo na migomo. Kila mwanafunzi ana malengo yake ya baadaye na uwezo wake wa kusoma na siamini kila Chuo na kila mwanafunzi anapenda kujiendeleza katika fani ya Siasa lakini wanalazimishwa na hata kupigwa kama asipokubaliana na matakwa ya wachache kufanya fujo. Hali hii ikiruhusiwa watoto hawatasoma hata wazazi wataogopa kupeleka watoto vyuoni.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa kwa wanafunzi ni bora irejeshwe pindi huyo mtoto anapotakiwa kurejesha. Katika hili, nashauri Serikali ianzishe "*Website*" ya watahininiwa wote wenye madeni na vyeti vyao viwekewe alama na pia katika *"Website"* hiyo ionyeshwe jina, namba ya cheti na suala la deni ili mwajiri aweze kutambua historia ya mwanafunzi na deni lake pia mwajiri awajibike kupunguza mshahara wa mwanafunzi ili deni hilo liweze kulipwa kama ilivyokusudiwa. Pia Serikali kupitia mtandao huo *"Website"* iweze kujua "*Track*" ya huyo mwanafunzi kuwa yuko wapi kwa maana ya kazi anafanyia wapi, mshahara wake ni kiasi gani na deni linavyolipwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayofanya kuwaelimisha vijana wa Kitanzania ili Taifa hili liwe na idadi kubwa ya wasomi na lipige hatua katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, MMEM na MMES, miradi hii miwili ni ya muhimu sana katika kupata vijana wengi wenye elimu hasa vijijini. Tatizo lake ni kuwa, mipango hii

haikwenda sambamba na idadi ya Walimu watakaohitajika pamoja na vifaa vya maabara, matokeo yake kiwango cha elimu kinashuka kutokana na vijana kumaliza masomo bila Walimu wa kutosha na hasa wa masomo ya Sayansi. Ushauri wangu ni kuwa tuendelee kuajiri Walimu kwanza katika shule zilizopo na kujenga maabara ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu, ubora wa elimu ya juu utategemea ubora wa shule za msingi na sekondari. Uzoefu unaonesha kuwa shule za kidini (hasa za Wakristo) zinafanya vizuri zaidi katika mitihani yao ya mwisho. Hili siyo jambo zuri sana maana tunajenga matabaka ya itikadi katika elimu.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, bado kuna tatizo la uhaba wa mikopo ya wanafunzi na pia tatizo la kupewa mikopo wanafunzi ambao wazee wao wana uwezo na wananyimwa wanafunzi ambao wazee wao hawana uwezo. Naiomba Serikali ifuatilie vigezo vinavyotumika ili haki itendeke na watoto wa wanyonge waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, madai ya Walimu, Walimu ndio wafanikishaji wa shughuli za ufundishaji. Ili kazi zao zifanywe kwa ufanisi, ni lazima mishahara yao iwe mikubwa kiasi cha kukidhi mahitaji ya msingi vinginevyo watafundisha kwa ajili ya kupata mshahara tu na sio kwa kuwaelimisha wanafunzi. Hivyo Walimu walipwe madai yao yote ili isiwe hoja baadaye ya matokeo mabaya ya mitihani.

Mheshimiwa Spika, Masomo ya Sayansi, hakuna nchi iliyoendelea bila kuimarisha masomo ya Sayansi. Mfumo wetu wa elimu unawalazimisha vijana kupendelea kusoma masomo ya "*Arts*" hata Walimu wa Sayansi wanakuwa wachache. Kama kweli tunataka maendeleo ya sayansi katika nchi hii, wanafunzi wanaosoma Sayansi wote wasome bure mpaka Chuo Kikuu lakini pia wahakikishiwe ajira katika viwanda na taasisi mbalimbali ili wapate moyo wa kusoma kwa bidii.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nampongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumizia suala la elimu ya awali. Elimu ya awali ni muhimu sana kwa maandalizi ya watoto. Hivyo nashauri mafunzo ya Walimu wa elimu ya awali itolewe (*early childwood development training)* yaendelezwe na kozi hii ianzishwe toka ngazi ya cheti.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie chakula mashuleni. Wakati nachangia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, niliongelea umuhimu wa chakula mashuleni ili kupunguza tatizo kubwa la utapiamlo linalolikabili Taifa hili. Nilieleza tatizo kubwa la upungufu wa chakula lililoletwa na ukame tarafa ya Pawaga, Ismani, Idodi Wilaya Iringa. Niliomba watoto wa shule wanaotoka maeneo haya ambayo yanapakana na Mkoa wa Dodoma wenye programu ya chakula mashuleni, wapewe chakula mashuleni. Naomba

Waziri anijibu kuna mpango gani? Watoto hawa hawawezi kusoma vizuri mashuleni hivyo kuhangaika kutafuta chakula.

Mheshimiwa Spika, watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Wizara ya Elimu iweke asilimia (%) ya watoto hawa kuanzia wale wanaomaliza Darasa la Saba kujiunga na Sekondari pia wale wanaojiunga Vyuo Vikuu ili wapate mikopo asilimia mia moja (100%). Hii pia iendane na upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa nyumba za Walimu na hasa vijijini litiliwe umuhimu unaostahili, ikiwa ni pamoja na kuwapa *Hardship Allowance* kwa wale wanaofundisha katika maeneo ya mazingira magumu. Walimu hawa pia waangaliwe kukopeshwa vyombo vya usafiri hasa kwenye maeneo ambayo usafiri ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanaofundisha watoto wenye ulemavu wapewe motisha kwani wanafanya kazi ngumu inayohitaji kutiwa moyo.

Mheshimiwa Spika, madai yote ya Walimu yaliyohakikiwa yafanyiwe kazi ili kuondoa kero na kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze juhudi kubwa inayofanywa na Serikali kuinua kiwango cha elimu nchini kwa kuongeza idadi ya udahili na pia bora wa elimu. Napenda kuihamasisha Wizara kwa ushirikiano wa Wizara ya TAMISEMI kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika kujenga na kuchangia uendeshaji wa shule zetu.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM inaelekeza kujenga shule za Kidato cha Tano na Sita kwa kila Tarafa. Katika Jimbo langu la Busega hakuna shule ya aina hiyo hata moja. Naomba Waziri anipe maelezo ni lini kutajengwa shule hizo katika Tarafa mbili za Busega na Kivukoni? Shule za Mkula na Kabita zilipendekezwa, naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Busega wamehamasika kupanua Shule ya Sekondari ya Sogesca ili kuchukua Kidato cha Tano na Sita. Hata hivyo, upanuzi wa shule hii unatatizwa na utapeli wanaofanyiwa wananchi kwa sehemu ya ardhi ya kiwanja chao kugawiwe na Watendaji wa Wizara ya Ardhi kwa mtu anayejiita Mwekezaji. Wananchi ambao ndio wenye ardhi hawaafikiani na ardhi yao kugawiwa kwa mtu, hatutaki Nyamongo nyingine izaliwe Jimboni kwangu, nahitaji maelezo ya uhakika katika suala hili ili wananchi wasikwazwe juhudi zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Magu yenye Majimbo mawili ya uchaguzi, yaani Magu na Busega hakuna Chuo cha Ufundi *VETA*. Mwaka huu tunategemea Busega itaanza kuwa Wilaya mpya. Naona sasa hili ni eneo kubwa mno linabaki bila huduma ya Chuo cha Ufundi. Mwaka jana, mfano wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba walikuwa zaidi ya 7,000 katika Jimbo la Busega. Waliochaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari

ni takribani 3,200 tu. Sasa idadi ile kubwa ya vijana wanaobaki bila elimu zaidi wataenda wapi? Tunahitaji kusaidiwa haraka kwa kujengewa Chuo cha Ufundi Busega.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kupandisha hadhi Vyuo vya Kati kuwa Vyuo Vikuu kufuatana na mahitaji ya nchi. Hata hivyo, uteuzi wa Vyuo hivyo huangalia uwezekano wa miundombinu stahili. Katika Mkoa wa Mwanza kuna Vyuo vikongwe kama vile Chuo cha Ualimu Butimba na Liti – Ukiriguru. Mkoa wa Mwanza pia ndiyo Mkoa wenye idadi kubwa ya watu nchini baada ya Dar es Salaam. Hata hivyo, inasikitisha kuwa Mkoa huu bado hauna Chuo Kikuu cha Umma. Je, kwa nini Butimba *TTC* isifanywe Chuo Kikuu kama ilivyokuwa kwa Mkwawa na Chang'ombe *TTC*?

Mheshimiwa Spika, Shule na vyuo vyetu vimeingiliwa na siasa, Walimu, Wakufunzi na hata Wakuu wa Vyuo wanatumika kuhamasisha Walimu na wanafunzi kugomea Serikali iliyopo. Sheria inazuia Watendaji wa Serikali kujishughulisha na siasa japo hawazuiwi kuwa na upande wanaoegemea. Tunaomba Sheria hii itumike, Walimu wote wanaochochea migomo wafutwe mara moja ili wasivuruge juhudi za Serikali kutekeleza Ilani ya CCM. Mifano ipo dhahiri Ustawi wa Jamii, Kijitonyama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninalo tatizo la madeni ya mishahara ya Walimu 144 katika Wilaya ya Magu walioajiriwa mwaka 2008 ambapo mishahara yao ya Juni hadi Septemba hawajalipwa. Naomba kupata majibu kwa nini imechukua muda mrefu hivyo kulipa malimbikizo hayo?

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumekuwa tukionekana wazito katika ushindani wa kibiashara Kitaifa na Kimataifa. Hii ni kutokana na kutokuwa na elimu ya ujasiriamali kuanzia hatua ya chini. Nashauri kuwepo masomo ya ujasiriamali katika mitaala kuanzia shule za misingi, sekondari na vyuo kwani kila taaluma inaweza kufanyiwa biashara, kuleta mapato na kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzisha Digrii Maalum ya Kiswahili. Ndugu zangu, Kiswahili ni hazina yetu Watanzania, tuiuze na tujitangaze nayo. Walimu wengi wazalishwe na wafundishwe kuitumia lugha hii kibiashara. Wakafungue vituo vya kufundisha Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani, Maziwa Makuu, *SADC*, Sudan Kusini, wakafanye ukalimani, hata kwenye Mataifa makubwa mfano China, USA, UK n.k. Tusiache fursa hii kuchukuliwa na Wakenya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwa njia ya maandishi nachangia Bajeti ya Wizara ya Elimu. Awali ya yote, napenda nielezee hali ya elimu katika Mkoa wa Kagera na hususani Wilaya ya Muleba. Hali ya elimu katika Wilaya ya Muleba ni mbovu/ina hali mbaya. Kwa kulenga Bajeti hii, hali hii inasababishwa na

upungufu wa Walimu, miundombinu, vifaa vya kufundishia na utawala duni wa sekta ya elimu Wilayani.

Mheshimiwa Spika, kwa kulenga shule za msingi, inasikitisha kuona kuwa Wilaya ya Muleba kuna shule zenye wanafunzi wa Darasa la Saba kwa miaka mingi lakini wakiwa na chumba kimoja cha darasa au viwili. Wilaya hiyohiyo, Shule ya Msingi yenye darasa mpaka la saba inasikitisha kuona ina Walimu wawili au watatu ilihali Chuo cha Elimu Katoke kikiwa katika eneo hili. Wananchi wanashindwa kuelewa busara ya Serikali pale shule zinapokosa Walimu wakati vijana wenye sifa za kujiunga na Chuo wapo na Chuo kipo umbali wa pua na mdomo. Zipo hoja rahisi toka kwa wananchi wa Wilaya ya Muleba wanaohoji kwa nini basi Serikali isidahili wanafunzi Walimu toka eneo hili ili kupunguza gharama?

Mheshimiwa Spika, pamoja na dokezo la madarasa kama sehemu ya upungufu lipo tatizo la Ofisi za Walimu, maktaba na vyoo. Napenda nikiri kuwa kuna kasoro katika kulisimamia suala hili. Wizara ya Elimu na TAMISEMI ipo haja ya kuwa makini na kuangalia kama rasilimali zinazotengwa na Serikali zinatumika kikamilifu. Kama ilivyo kwa miundombinu, kuna upungufu katika utoaji wa vifaa vya kufundishia na hasa vitabu. Baadhi ya shule, hali ya vifaa ni mbaya sana hali inayotusukuma kuhoji kama kweli Serikali hutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na kama zinatengwa, je, kweli inatumika kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, yote hayo yanachangiwa kwa kiasi fulani na utawala duni wa elimu katika Wilaya. Nguvu ya ukaguzi na usimamiaji wa elimu Wilayani ni duni sana. Upungufu huu unaonekana katika mahudhurio na utendaji wa Walimu, nidhamu ya Walimu na wanafunzi, hali duni ya miundombinu na ushiriki na ushirikishwaji wa wazazi na wananchi katika kuendesha shule.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yanayoathiri elimu ya msingi kipekee, Shule za Sekondari Wilayani nazo zina matatizo karibu sawa na hayo. Sekondari Wilaya ya Muleba zina upungufu wa Walimu kwa kiwango cha hali ya juu. Walimu wanaopangiwa kazi Muleba, baadhi yao hawafiki katika vituo vyao hali inayoathiri utoaji wa elimu. Tunapendekeza Serikali hali hii inapotokea, idadi ya Walimu ambao hawakuripoti, Mkurugenzi wa Wilaya apewe ruksa kuajiri moja kwa moja idadi kama hiyo kwani Bajeti yake inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kuhusu ubora wa sekta ya Walimu. Kwa ujio wa kidiplomasia, taaluma ya elimu si nzuri kwa hali ambayo tunastahili. Nomba na kushauri mpango maalumu uanzishwe ili kuinua na kuboresha sekta hii. Haya ni mapendekezo yangu.

(a) Uanzishwe utaratibu wa kutoa leseni kwa Walimu. Kupata leseni Mwalimu awe amehakikiwa na kuona kama anamudu jukumu hili barabara, mfano Zimbabwe miaka 1980 – 1990 walikuwa na utaratibu huu na uliwasaidia sana.

(b) Kulenga Walimu wenye sifa, sasa tulenge kudahili wanafunzi wenye uwezo na sifa siyo wale ambao wameshindwa masomo na kukosa fani bali wale wenye wito na uwezo.

(c) Serikali ijiandae kutoa mishahara na marupurupu yanayovutia kwa Walimu wenye leseni (waliochujwa).

(d) Walimu ambao tayari wako kazini wasaidiwe kuongeza weledi na umakini wao katika kutenda/kutekeleza majukumu yao. Wapo Walimu ambao kwa vyovyote vile hawawezi kupanda daraja na kupewa leseni au kwa maneno mengine hawastahili kuwa Walimu, kwa utaratibu mzuri wapunguzwe kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niishauri Serikali ifikikirie kuanzisha Chuo cha *VETA* sawa na kile cha Chang'ombe Dar es Salaam Mkoani Kagera. Hii itatusaidia kupata Chuo katika eneo letu kwani hali ya kijiografia inafanya usafiri toka Kagera kwenda Mikoa ya nje yenye Vyuo vya *VETA* kuwa ya gharama kubwa. Pamoja na *VETA*, napendekeza kwa Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla shughuli/elimu ya michezo ipewe kipaumbele kama ilivyo kuwa miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja shukrani kwa Muumba aliyetuwezesha kuwa hai na afya njema, shukrani kwa kupata nafasi hii. Kwa niaba ya Warufiji, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali yoyote ile ni kukusanya fedha kutoka kwa wananchi kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi hao bila ya upendeleo wa namna yoyote ile kuhakikisha na kupata haki na fursa sawa za huduma zote za msingi zikiwemo za elimu, afya, maji, nishati, barabara, mawasiliano, ardhi na kadhalika. Ni wajibu wa Serikali kuwa ndogo, yenye uwezo wa kutumia teknolojia ili kutoa huduma bora, bila ya upendeleo wowote, isiyo na urasimu na hivyo kubakiza fedha nyingi zaidi kutumika katika kutoa na kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ya elimu ambayo haimzuru mwanafunzi kuendelea kwa sababu ya kifedha au umbali wa mtu huyo na Taasisi hiyo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, elimu ya umma iliyowekwa kwa mtaji wa kodi ya wananchi ni lazima ipunguze michango yake yote isiyo ya lazima katika kuhakikisha usawa na haki ya msingi kwa kila mtu kunufaika na uwekezaji huo uliowezeshwa na kodi zao. Elimu ni lazima iongozwe na misingi na vigezo vyenye kutoa mikomo au mipaka ya ada zinazowekwa na shule na vyuo vya watu binafsi ili kupunguza mlipuko wa shule au vyuo vyenye kutoza ada za juu mno kuliko uhalisia wa gharama za uwekezaji ikizingatia kuwa majengo ni ya kudumu na sio halali au haki kwa mwekezaji kujilipa gharama zote ndani ya muda mfupi kwa kutoza ada kubwa sana. Inashangaza kuona shule za msingi zikitoza ada ya hadi milioni mbili na zaidi kwa mwaka. Hakuna uhalisia wa tozo ya namna hii kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, majengo ya shule zilizojengwa zamani kule Rufiji yamechakaa na yanahitaji ukarabati mkubwa na kwamba samani zake pia zinahitaji ziwekwe nyingine, majengo haya ya madarasa na nyumba za Walimu na vyuo ni lazima zijengwe upya. Ikienda sambamba na ujenzi wa Shule za Sekondari ambazo baadhi ya watu wamekuwa wakibeza uwepo wa Shule za Kata. Naishauri Serikali kuongeza kasi ya ukamilisha shule hizo za Kata katika Wilaya ya Rufiji, Kata ya Mkongo, Chemchem, Ngarambe na Mgomba ili kupunguza gharama za wanafunzi kwenda mbali na maeneo yao kwa ajili ya kupata elimu hiyo ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa Walimu Rufiji bado ni mkubwa hasa katika shule zilizo mbali na Miji katika Shule za Msingi. Unashangaa kuona Walimu wengi wapo Mijini wakiacha Shule za Vijijini bila ya Walimu. Naitaka Serikali kuhakikisha changamoto hii inarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Sekondari bado kuna uhaba mkubwa. Motisha kwa Walimu wa Vijijini iundiwe Sera kwa Halmashauri zote kutekeleza hayo kwa maslahi ya wote waishio Vijijini. Tabaka la wenye fursa ya elimu bora kwa wenye nacho na ukandamizaji kwa wasionacho ni tatizo kubwa, ni lazima sera ya kurekebisha hili iundwe na kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vitabu ni changamoto isiyo ya lazima. Nashauri Serikali kuboresha *Library* za Sekondari na kuziwezesha kufanya kazi kisasa zaidi na hivyo kupunguza matumizi ya kila siku ya ununuzi wa vitabu na kuzuia kuibiwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rufiji haina Chuo cha *VETA*, naishauri Serikali kutuwezesha katika hili ili vijana wanaomaliza Kidato cha Nne waweze kupata fursa ya masomo zaidi katika Chuo cha VETA. Nipo tayari kushirikiana na *VETA* na Wizara ili Chuo hicho kijengwe Mkongo Rufiji na eneo litapatikana bila ya shida yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kuleta Hotuba nzuri hapa Bungeni na kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, elimu yoyote duniani ina maana pale elimu inapoelekezwa katika maarifa vinginevyo elimu hiyo ni kazi bure. Wahitimu wetu kuanzia Shule ya Msingi, Sekondari, *VETA* na Vyuo Vikuu wanapata elimu lakini wamekosa maarifa. Hivyo wanabaki na elimu yao vichwani bila ya kuwasaidia wahitimu wetu. Mfano, mhitimu anayemaliza Digrii ya Kilimo na Mifugo, Chuo Kikuu cha Sokoine bila ya kuwezeshwa kupata ardhi nzuri ya kilimo, mkopo wa fedha za mtaji ili elimu yake aiweke katika maarifa na aweze kuzalisha na impatie faida, elimu yake itakuwa haina faida. Hali kama hii ni sawa na taaluma nyingine, Udaktari, Uhasibu, Ualimu, Uandishi, Uhandisi, na kadhalika. Pendekezo langu, Serikali ifanye utafiti wa kuwasaidia wasomi wetu mara baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa Walimu Wilayani Karagwe na hasa Jimbo la uchaguzi Karagwe. Wilaya hii ya Karagwe ipo mpakani mwa Tanzania na Rwanda na Uganda. Watumishi walio wengi wanakimbia kwenda huko kwa kisingizio kuwa ni mbali "*remote area*". Serikali ibuni mbinu za kuwashawishi Walimu waende Karagwe. Shule nyingi za Msingi na Sekondari hazina Walimu mfano, Shule ya Sekondari Ihembe ina Mwalimu mmoja tu. Sekondari hiyo ina Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Mheshimiwa Spika, hosteli za shule za sekondari Jimboni Karagwe ni lazima zijengwe kwa ajili ya kulinda watoto wetu wote wa kike na kiume. Mimba zitapungua kwa watoto wetu wa kike kuacha kupanga nyumba mtaani.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa nyumba za Walimu ni tatizo kubwa sana. Mfano wa Shule ya Msingi Kabale katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Walimu na familia zao wote wanaishi kwenye nyumba moja tu! Hii ni hatari sana kiafya na ustawi wa familia hizi. Ni lazima Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu Jimboni Karagwe na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, shule za Kiingereza ni nzuri lakini zina matatizo makubwa sana. Baadhi ya shule hizo hazina viwango vya kutosha kwa ajili ya kutoa elimu inayostahili kwa watoto wa Taifa hili. Baadhi ya shule hizi zinazoitwa "*English Medium*" zinatuibia fedha zetu wakati hazitoi elimu inayokidhi haja. Serikali isimamie kwa karibu sana shule hizi kuanzia Shule za Awali, za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi tunazo Shule za Sekondari kila Kata na tayari watoto wetu wamehitimu Kidato cha Nne lakini kuna uhaba wa Shule za Kidato cha Tano na Sita, ni muhimu Serikali ikajipanga kuanzisha Shule za Kidato cha Tano na Sita angalau moja kila Kata nne kwa kuanzia, baadaye mbili na baadaye moja kwa kila Kata.

Mheshimiwa Spika, aidha, uhaba wa madawati na vyoo shule za msingi ni tatizo lisilostahili kufumbiwa macho.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha *VETA* kwa Mkoa wa Kagera, Wilaya zote hazina Chuo cha *VETA*. Tunaomba sana kwa kuanzia Mkoa wa Kagera upewe Chuo cha *VETA* cha Mkoa mzima, baadaye Serikali iingie Wilayani.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Walimu na malimbikizo mengine yalipwe kwa wakati na Serikali iache kuwakopa haki zao. Hadi Juni 2011, madeni ya Walimu kwa nchi nzima yanakadiriwa kufikia shilingi za kitanzania 29,237,007,865.64.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba nzuri kabisa. Aidha, niwapongeza Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu ni sekta muhimu sana kwa sababu elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Bila elimu hakuna yeyote ambaye angekuwa katika nafasi aliyonayo leo. Najua mafanikio katika sekta hii yapo lakini kadri mafanikio yanapokuwepo na changamoto pia zinaongezeka.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa Sekondari za kila Kata, zimeongeza nafasi kwa watoto wengi kupata elimu ya sekondari. Changamoto iliyopo ni upungufu wa Walimu hasa katika shule zilizopo kijijini. Walimu wanapopangiwa wengi lakini huripoti tu na hatimaye kutoweka. Sasa basi ushauri wangu kwa shule hizi ni kuziboreshea mazingira na miundombinu ya kufundishia, nyumba za Walimu, madarasa na kuhakikisha vifaa vyote muhimu vya kufundishisa vinapelekwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, tunaiomba Serikali iangalie namna ya kuboresha maslahi ya watumishi wanaopangiwa vijijini. Watumishi hawa wawe na *special package* itakayowafanya wawe na *morale* ya kufanya kazi vijijini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu watumishi ni madai. Watumishi wengi katika sekta ya Walimu wanapopandishwa daraja wanakaa muda mrefu bila kupewa stahili zao kulingana na madaraja mapya mwisho wa siku kunakuwa na madai. Niiombe Wizara itafute namna ya kurekebisha upungufu huu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule, ni Idara muhimu sana. Kama ilivyoanishwa katika Hotuba hii, majukumu yake makubwa ni kuhakikisha kuwa Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa kwa ufanisi katika ngazi zote za elimu. Ili kuweza kufanikisha majukumu ya Idara hii muhimu inatakiwa wapatiwe vitendea kazi vya kuwawezesha kutimiza majukumu yao. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, yako mapungufu makubwa katika Idara hii, waongezewe bajeti ili waweze kuendesha shughuli za ukaguzi katika Wilaya yote. Wilaya hii ni kubwa sana, Shule za Msingi ni zaidi ya 200 na Sekondari ni zaidi ya 45. Naomba Serikali iongeze fedha za uendeshaji ili kuimarisha Idara hii kwa ufanisi zaidi katika Halmashauri ya Geita.

Mheshimiwa Spika, sina la ziada, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kukabiliana na changamoto nyingi za elimu. Naomba yafuatayo:-

1. Kuna ahadi ya kujenga Chuo cha Ufundi cha Madini Kahama iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Kahama tarehe 10/10/2010, sijaona kwenye Hotuba. Naomba kijengwe.

2. Serikali iongeze idadi ya Walimu wa Sekondari.

3. Naomba Serikali ianze kuendesha *Hostels* kwenye shule tano za Msalala (Mwalimu Nyerere Sekondari, Isaka, Mpewa, Busangi na Bahaha) ambazo wananchi wamejenga. Serikali ilete watumishi Walimu na wasio Walimu.

4. Shule za Msalala zipatiwe umeme.

5. Serikali ijenge kwa ushirika na wananchi, Shule za *'A level'* za kutosha Kahama. Wilaya ya Kahama ina shule za Sekondari 46, zote za *'O Level'*, shule za *'A Level'* za Serikali ni mbili tu. Naomba zijengwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuweka mikakati ya kuboresha elimu. Napendekeza yafuatayo:-

(1) Ujenzi wa nyumba liwe ni jambo la kipaumbele, Walimu wote wanahitaji mazingira bora ya kuishi ili wapate hamasa ya kuwajibika.

(2) Walimu wapatiwe vyombo vya usafiri, kipaumblele ni pikipiki.

(3) Naomba Serikali iweke mkakakti wa kutosha wa kurejesha nidhamu shuleni. Nidhamu imekuwa ni tatizo kubwa kwa wanafunzi wetu wa sasa wa Sekondari.

(4) Naiomba Serikali iimarishe Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya *VETA* kwa haraka sana. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kibadilishwe kuwa cha *VETA*.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi kiongezewe nguvu kwa kukipatia vitendea kazi vya kutosha. Kitengo cha Ukaguzi Wilaya ya Kisarawe hakina gari. Gari iliyokuwepo awali iliibiwa na majambazi lakini mpaka sasa hakuna gari lingine lililoletwa na Wizara ili kuwezesha Idara ya Ukaguzi ifanye kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, haki za Walimu. Walimu bado wanadai madeni mengi haswa Walimu wa Jimboni kwangu Kisarawe. Naomba Serikali iwalipe Walimu wote wanaodai madeni mbalimbali katika Tanzania nzima kwa kuanzia Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, kupandishwa kwa madaraja kwa Walimu bado limekuwa changamoto kubwa. Naiomba Serikali isimame kidete katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Wizara kwa kufanya kazi kubwa. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu wengi nitoe pongezi za dhati kwa Wizara nzima. Nikianza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanazofanya. Tunawashukuru kwa elimu ya msingi bure, ukaguzi, elimu kwa

Walimu, vitabu mashuleni, maabara na kile ambacho Serikali imeweza kutoa imetoa, hongereni!

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina Sekondari 29 lakini ina shule ya *'A level'* moja tu na ni ya wasichana tu na tena ni chakavu mno inahitaji ukarabati. Maombi kwa Wizara ni kama ifuatavyo:-

*1.* *Ifakara Secondary School* ikarabatiwe, ni ya siku nyingi. Ni hatari!

2. Wananchi wa Kilombero tunaomba sekondari mbili zipandishwe hadhi ziwe za *A Level*, Sekondari hizo ni Kidatu *secondary school* na Nakaguru *Secondary School.*

3. Wilaya inahitaji Chuo cha VETA.

4. Tunaomba Chuo cha Walimu *TTC.*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni:-

(1) Walimu wasikopwe. Walipwe haki zao kupunguza migomo.

(2) Lishe bora mfano kikombe cha uji kwa wanafunzi. Hii inazuia utoro mashuleni. Mimba za utotoni na kusinzia madarasani.

(3) Mishahara ya Walimu iongezwe wale wanaoenda Vijijini waongezewe 25% zaidi ya Walimu wa Mijini.

(4) Kufanyike harambee za kununua madawati kila Wilaya.

(5) Elimu ya awali izingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mungu kwa nafasi hii ya kuchangia. Pia nimshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na timu yake, niishukuru Kamati ya Huduma za Jamii kwa kazi yao kubwa ya kusimamia na kumshauri Waziri na timu yake namna ya kuboresha elimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa mitaala ya elimu inayokuwa na mwelekeo ya kuboresha elimu kwa Watanzania. Nipongeze utaratibu mzima wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na Shule za Sekondari za Kata. Shule hizi zimeleta ukombozi mkubwa kwa vijana wetu hasa pale ambapo vijana waliofaulu Darasa la Saba, wengi walikuwa hawashukuliwi kujiunga na Sekondari kwa sababu shule zilikuwa chache, hivyo basi waliishia kwenda kufanya kazi za majumbani na kuchunga ng'ombe

Mijini kama Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Arusha, Moshi, Mwanza na kadhalika. Hivi sasa wanafunzi wanajiunga na Sekondari na wanafanya vizuri kwenda '*A level'* hata Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni kwamba Walimu katika ngazi zote za shule ni wachache, Shule za Msingi, Shule za Sekondari *(O-Level),* Shule za Sekondari *(A-Level),* Vyuo vya Ufundi *(VETA)* na Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa majengo, majengo yote ya shule ni machakavu hasa vijijini. Aidha, nyumba za Walimu hazitoshi badala yake wanawajibika kupanga kwa wananchi mara nyingine kubanana na wapangaji tena mbali na shule.

Mheshimiwa Spika, mishahara, posho na vyeo. Walimu Wanakaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo, lakini pia wamesahaulika kupandishwa vyeo na kuongezewa mishahara. Pia wanadai posho mbalimbali likizo, uhamisho, kujikimu na kadhalika. Walimu wapewe stahili zao ili iwaongezee motisha ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi iangaliwe kwa upya, ina tatizo gani, kwa nini Idara hii haifanyi kazi kama inavyotakiwa. Idara iongezewe idadi ya Wakaguzi, usafiri, posho za usimamizi na ukaguzi. Wakati mwingi wanafunzi kutofanya vizuri kunatokana na ukaguzi duni ndiyo maana, majengo ni mabovu, Walimu ni wachache, madawati, vitabu na chaki (vitendea kazi) ni changamoto ambazo Wakaguzi wangefanya kazi zao ipasavyo wangezigundua na kuzifanyia kazi, ufundishaji ungefanyika kwa kiwango cha juu katika ngazi zote na hatimaye elimu ingekuwa bora kuanzia ngazi ya Chekechea hadi Chuo Kikuu na Vyuo vyote vya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wazazi, wanafunzi na wadau wengine wa elimu wajidhatiti ili kuinua kiwango cha ufaulu na kuboresha elimu ilingane na wenzetu wa nchi nyingine za Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka (2011-2012).

Mheshimiwa Spika, Katika dunia ya leo, ili binadamu aweze kuboresha maisha yake, ni lazima awe na elimu. Elimu ndiyo inayomwezesha kujitambua na kujimiliki mwenyewe kwa kuyatawala na kuyatumia mazingira yanayomzunguka ili kuboresha maisha yake. Ndani ya utandawazi, elimu kidogo tafsiri yake ni umaskini zaidi na elimu zaidi tafsiri yake ni maisha bora zaidi. Naomba nimnukuu Mzee Nelson Mandela aliyekuwa Rais wa South Africa mwaka 1991 alisema hivi juu ya elimu, "Elimu ni injini kubwa ya maendeleo ya mtu. Ni kupitia elimu ndipo binti wa mkulima mdogo ataweza kuwa Daktari Bingwa, mtoto wa kibarua mgodini anakua Mkuu wa Mgodi na mtoto wa kibarua wa mashambani anakuwa Rais wa Taifa kubwa" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hadi hapo umeeleweka umuhimu wa elimu ni nini na kama tunataka kuwa na Tanzania bora, tuanze mapema kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu bora na inayoendana na hali halisi ya sasa. Pia iwe ni elimu yenye mshiko yaani ni elimu ajiri, *which means* hata mtoto akimaliza shule leo anaweza kutumia elimu na ujuzi wake alioupata shuleni kujipatia kipato au hata kutumia elimu hiyo kuwanufaisha au kuwasaidia wenzake wanaomzunguka na wao waone kweli elimu ina umuhimu na wao kupata wivu wa kuitafuta hiyo elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuchangia katika suala la *capitation grants*, hela ambazo zimetengwa na Serikali kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya elimu katika Shule za Sekondari za Serikali hapa nchini. Hela hizi hutolewa kwa kila mwanafunzi wa Sekondari anayesoma katika Shule za Serikali. Kiasi cha Shs.10,000/= huenda shuleni kwa ajili ya kuboresha mfumo mzima wa elimu ikiwa ni pamoja na kununua vifaa mbalimbali kama vile chaki, vitabu n.k.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za mwaka 2010, kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi kulikuwa na jumla ya wanafunzi 1,600,000 kwenye Shule za Sekondari na hii ni kwa kuanzia Kidato cha I – VI na kwa kuwa Sera ya Serikali ni kutoa Sh.10,000/= *per head, so* Serikali ilipaswa kutoa Shs.160 Billions, lakini Serikali ilipeleka kiasi cha Shs.546 millioni tu tofauti na Sera inavyosema na hii inaondoa zana nzima ya elimu bora. Kutokana na hela hizo pungufu kupelekwa mashuleni kwa mwaka 2010 ilibidi kila mwananfunzi apate Shs.390 tu badala ya Shs.10,000/= kama ilivyopitishwa kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza, Serikali iweke utaratibu wa wazi wa namna gani inapeleka fedha hizo kwenye Halmashauri na Halmashauri kwenda katika shule. Pia, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kila inapokutana iwe inapokea taarifa ya fedha hizo na hii itapelekea fedha hizi kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala la elimu kwa mtoto wa kike. Kidunia licha ya mataifa kuongeza fursa za watoto wote kupata elimu, wasichana ndio waathirika wakubwa wa changamoto zozote zinazozikabili nchi maskini mfano, nchi zinazoendelelea kama Tanzania n.k. Kwa takwimu za *(UNESCO 2008),* kati ya watoto milioni 100 wenye umri wa miaka (6-11) ambao hawako shule 60% ni wasichana na kati ya watoto 150 milioni wanaokatishwa masomo na kuacha shule, wasichana ni milioni 100.

Mheshimiwa Spika, nchini Tanzania jitihada za kuboresha elimu zinasongwa na wimbi la wasichana wengi kuacha shule, kukatisha masomo au kudondoka. Baadhi ya sababu ambazo zinasababisha hali hii hizi zifuatazo:-

(1) Wazazi kushindwa kumudu gharama za maisha na mahitaji ya mtoto. Kutokana na hali ngumu ya maisha, mzazi inabidi ajali mahitaji ya familia kwanza kama chakula na mavazi kuliko kulipa karo kwa mtoto au kumpa nauli kwa wale wanaokaa mbali na shule.

(2) Mimba za utotoni ambazo kwa kweli ni tatizo kubwa sana na hili halijapatiwa ufumbuzi rasmi au unaoeleweka hadi sasa kwani imekuwa inamuonea binti tu na mwanaume kuendelea kupeta na *either* na maisha yake ya kazi au elimu bila kubugudhiwa.

(3) Watoto wa kike wanabebeshwa mizigo mikubwa ya kazi za nyumbani/familia hivyo kukosa muda wa kwenda shule na kujisomea na hivyo kufanya vibaya shuleni au kutokumaliza shule au kutokwenda shule kabisa.

(4) Kutokana na hali duni ya uchumi, wazazi wanachangia katika kumnyima mtoto wa kike elimu kwani wamekuwa wakiwatumia katika biashara zao au kuwaoza wakiwa wadogo ili kujipatia kipato au mali yaani posa au kudhani kuwa wakwe zao watawasaidia kwa chochote. Pia wasichana wenyewe wanashawishika kufanya ngono ili waweze kupata angalau hela ya kujikimu kimaisha mfano, kununua sabuni kwa ajili ya kufulia nguo zao hasa wakati wanapobalehe wengi wanakuwa wanajali usafi sana.

Mheshimiwa Spika, elimu ya Tanzania imekuwa inadidimia badala ya kusonga mbele, hii inatokana na kubadilisha mitaala mashuleni mara kwa mara bila kujali uhalisia wa maisha. Mfano, vijijini hali ni ngumu zaidi kwani Dole Gumba limetawala saini za wakulima kwenye vocha za pembejeo. Vilevile ufaulu wa kidato cha IV umeporomoka sana. Imeonekana dhahiri mwaka jana wakati wa matokeo ya Kidato cha IV, ni 50.4% tu walifanya vizuri tofauti na kipindi cha nyumba ambapo mwaka 2007 walifaulu kwa 90.3%. Pia kama aliyosema Mheshimiwa Chilolo Kiwango hiki kimeshuka hata kwa idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwani takwimu zinaonyesha mwaka 1986 kati ya watu 10 waliokuwa hawajui kusoma alikuwa mmoja na mwaka 2010 kati ya *same* idadi ni watatu ndio walikuwa hawajui kusoma na kuandika hivyo bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha elimu inaendelea kuwa bora na sio bora elimu tu.

Mheshimiwa Spika, Walimu wamekuwa wakikata tamaa kutokana na kuvurugwa kwa taratibu za maslahi yao na motisha ndogo toka kwa mwajiri Serikali au jamii husika. Kama alivyosema Mheshimiwa Chiku, mishahara midogo wanayolipwa inafanya wapoteze muda mwingi kutafuta njia mbadala ya kujiongezea kipato ili kujikimu kimaisha na hivyo kukosa muda wa kusoma miongozo na silabasi zao na hivyo kuto-*deliver* vizuri kwa wanafunzi wakati wa kufundisha. Walimu pia wamekuwa wakijitahidi kumaliza silabasi tu badala ya kumaliza ujinga kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya taaluma ya utu nayo imefifia. Jamii inaona huenda Ualimu ni kama kupotea au mbadala wa mwisho. Naomba kumnukuu mtu anaitwa Smith, 2010, "Nilichagua Ualimu na mpaka sasa watu wanadhani nimefeli. Watu wanasema, nataka mtoto wangu awe Daktari au Mwanasheria, si Mwalimu. Ni aibu kuwa Mwalimu kwani kila mtu anakimbia taaluma hiyo".

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku tunakuwa na Walimu wasiofaa 10,000 na wanaoofaa 400 tu. Kati ya utafiti wa Walimu nchini Tanzania ni 10% tu ya Walimu wa kiume na 15% ya Walimu wa kike wamesema kuwa Ualimu lilikuwa chaguo la kwanza

la kazi na 37% walishindwa kupata chaguo la kwanza sababu alama zao zilikuwa chini. *So*, Ualimu unaelekea kuwavutia wasio na sifa za kutosha. (Mulkeen na wenzake, 2005, ukurasa wa 11).

Mheshimiwa Spika, napendekeza Walimu waangaliwe katika suala zima la maslahi ili waweze kujikimu na kuwafanya wapende kazi yao na pia kutoa motisha kwa Walimu wa pembezoni, utakaowavutia kwenda maeneo ambayo ni ya mbali au yenye miundombinu mibovu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawamba (Mb).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu makubwa ya kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi kuanzia ngazi ya chini ya elimu ya awali na msingi hadi elimu ya juu, uwajibikaji mkubwa kwa Watendaji wa Wizara hii pamoja na kutengewa mgao wa fedha zinazotosheleza vinahitajika ili kuzikabili changamoto ambazo zimeorodhweshwa katika Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawawezi kuendelea kuwa na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya ufundi. Serikali ichukue hatua madhubuti endapo tunataka kuwa na Taifa lililoelimika kikamilifu. Ni lazima watoto wetu wafundishwe kwa kutumia vifaa vilivyo bora na vya kisasa. Walimu wataipenda kazi, pale tu vifaa vya kufundishia na kujifunzia vitakapokuwa vinapatikana bila tatizo.

Mheshimiwa Spika, haipendezi kuona watoto wetu/wanafunzi wakiendelea kupatiwa elimu huku wakiwa wamekaa chini sakafuni. Tanzania ni nchi tajiri kwa upatikanaji wa rasilimali nyingi pamoja na misitu mikubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, kwa mfano huko Iringa na katika maeneo mengine pia. Tanzania hatuhitaji kununua mbao kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kutengeneza madeski na viti. Tujitume, tuwe wabunifu na ikiwezekana wafanyabiashara wenye moyo wa uzalendo waendelee kuhamasishwa ili watoe mchango wao katika maendeleo ya watoto wetu kwa kuwatengenezea mazingira mazuri ya kusomea, ikiwa ni pamoja na viti, madeski na hata ikiwezekana kompyuta kwa baadhi ya shule.

Mheshimiwa Spika, imefahamika kwamba wananchi wengi hawaandikishi watoto wao wenye umri wa kuanza shule. Hata Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo imethibitisha kwamba kiwango halisi cha uandikishaji wa rika lengwa *(Net Enrolment Ratio [NER])* katika elimu ya msingi imeshuka kutoa 95.9% mwaka 2009 hadi 95.4% mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ni vema uongozi wa Serikali za Mitaa ukawajibika katika kuhakikisha unafuatilia wale wote ambao wana watoto wenye umri wa kuanza shule

lakini bado wanaonekana wapo nyumbani. Hii itasaidia kupunguza ongezeko la idadi ya watoto wanaojiingiza katika shughuli za ajira katika umri mdogo au uzururaji na kuombaomba mijini/barabarani.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa, Serikali iweke kipaumbele kwa taaluma ya Ualimu kwa kuwapatia Walimu mazingira mazuri ya kazi yao kama kuwalipa mishahara yao kwa wakati, kuwapatia nyumba za kuishi na kupewa kozi fupi fupi ndani na nje ya nchi. Walimu wapate fursa ya kushiriki katika semina na makongamano mbalimbali hapa nchini ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, pindi Walimu au Watumishi wengine wa sekta hii wanapokuwa wamefariki, basi Serikali iajiri wapya na wote waliofariki waondolewe katika orodha ya malipo. Kwa kufanya hivyo, tatizo la mishahara hewa litakuwa limedhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono mia kwa mia Bajeti ya 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *VETA*, natoa shukrani nyingi sana kwa Serikali kuanza ujenzi wa *VETA* Lindi, ahsante sana. Tatizo linalokuja sasa ni kutomalizika kwa ujenzi huo, utaisha lini? Naomba *VETA* iishe kujengwa Lindi.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kwa makusudi kabisa kuiendeleza elimu katika Mkoa wa Lindi, kwani elimu Mkoa wa Lindi ipo nyuma sana katika nyanja zote, Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, *Form V-VI* na Chuo Kikuu. Hakuna majengo ya kutosha, hakuna Walimu wa kutosha, hakuna zana za kufundishia za kutosha, hakuna nyumba za Walimu za kutosha, hivyo kufanya elimu kuwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, kutokana na mila na desturi za Mkoa wa Lindi, watoto wa kike si wengi waendao shule, *dropouts* ni nyingi sana, tunahitaji elimu ya wasichana katika hatua za sekondari wawe na mabweni ili wakae shuleni. Mila na desturi za kikoloni za mfumo wa elimu wa kuwaendeleza watoto wa kiume tu umewaathiri watoto wa kike na kudhani kuwa elimu ni kwa watoto wa kiume tu. Hivyo kufanya watoto wa kike kutopelekwa shule, tunahitaji mabweni. Tuongezewe fedha kwa ajili ya kuendeleza mashule, nyumba za Walimu na ujenzi wa mabweni kwa MKOA wa Lindi. Pia kuendeleza *High School* kwani zilizopo ni chache tu.

Mheshimiwa Spika, shule za Ufundi za Msingi Lindi. Je Serikali haiwezi kufufua Shule za Ufundi za Msingi zilizopo Mkoani Lindi ili watoto wamalizao Shule za Msingi waende kujifunza ili kupunguza tatizo la ukosefu ajira binafsi kwa vijana, wakati watoto hao wakisubiri *VETA* Lindi kumalizia ujenzi. Shule za Msingi za Ufundi Mkoani Lindi ni hizi:-

Wilaya ya Lindi — Shule ya Msingi Mpilipili

| | |
|---|---|
| Halmashauri ya Lindi Vijijini | Shule ya msingi Mtama |
| Ruangwa | Shule ya Msingi Mbekenyera na Mkowe |
| Nachingwea | Shule ya Msingi Kilimarondo<br>Shule ya Msingi Mnero Ngongo<br>Shule ya Msingi Marambo Shule ya Msingi Nachingwea Mjini |
| Wilaya Liwale | Shule ya Msingi Liwale Mjini<br>Shule ya Msingi Mwarikiwa<br>Shule ya Msingi Chimbuko |
| Wilaya ya Kilwa | Shule ya Msingi Singino<br>Shule ya Msingi Njinjo<br>Shule ya Msingi Kipatimu<br>Shule ya Msingi Kilwa Masoko |

Mheshimiwa Spika, naomba Shule hizo za Msingi za Ufundi zifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira Mkoani Lindi ni kubwa sana, hivyo kuwafanya watoto wa Shule za Msingi wamalizapo Shule kwenda Dar es Salaam kutafuta ajira. Karibuni asilimia 45% za Wamachinga wa Dar es Salaam hutokea Lindi. Nani alaumiwe kwa tatizo hilo? Mtuangalie kwa jicho la huruma Lindi. Hatukuwa nyuma kwa makusudi, ni sababu ya ukombozi wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa Shule wa Elimu, tunaomba wawezeshwe kwa kupewa usafiri, mafuta ya kutosha ili waende kufanya kazi za ukaguzi mashuleni.

Mheshimiwa Spika, mimba mashuleni, Serikali ijenge mabweni wakishirikiana na wananchi ili wanafunzi walale mabwenini kwani mimba zimezidi. Tunamshukuru mama Kikwete kwa kujenga mabweni katika Shule ya Sekondari (Ngongo), Lindi mjini. Pia ameleta vitanda na magodoro. Ahsante sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja nilizochangia kwa kuongea lakini bado kuna tatizo la Maafisa Elimu kuchagua au kupendekeza Waratibu Elimu Kata kwa upendeleo mkubwa. Aidha, hali hii inapelekea Walimu kutofanya kazi yako kwa ari na moyo wa kujituma. Kuna Walimu wana elimu kubwa lakini hawapewi nafasi kulingana na elimu waliyonayo na aidha kutokana na utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la uanzishwaji wa Kidato cha Tano na Sita katikaS zetu za Kata liangaliwe kwa undani zaidi. Shule hizi hazina umeme, hakuna maji na vifaa vya

kufundishia. Suala hili si la maudhi kwa wanafunzi tu bali hata Walimu. Inakuwa vigumu kwa Walimu hawa kuwa na maandalizi mazuri ya vipindi kwani kukosa umeme hata wanafunzi wanakosa muda wa kujisomea jioni. Naishauri Serikali kutoa vipaumbele katika shule hizi walau wapate nishati ya umeme wa mwanga wa jua kama utatuzi wa muda, lakini baadaye wapate umeme wa muda wote.

Mheshimiwa Spika, suala la wazazi kutoshirikishwa baadhi ya maamuzi katika maendeleo ya Shule hizo za Kata liangaliwe upya. Leo hii Walimu wakishirikiana na baadhi ya Wenyeviti wa Bodi wanapitisha michango ambayo inakuwa ni ya manyanyaso kwa wananchi. Aidha, wanaweza kuamua kubadili sare ya shule na wazazi wakapewa tu utekelezaji. Haijalishi kitambaa kilichopendekezwa kama kinapatikana kwenye mazingira yao au laa! Pili, je, rangi hiyo imeridhiwa na wananchi au wazazi kwa ujumla wao? Nashauri kupitia vikao mbalimbali suala la ushirikishwaji lipewe kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la uanzishwaji wa Vyuo vya *VETA* ni la msingi sana. Leo hii vijana wengi hawana stadi za kazi za kuweza kuwasaidia katika maisha yao. Jimboni kwangu hakuna Chuo cha *VETA*, kilichopo ni chuo cha mtu binafsi na ambaye anajitahidi sana. Anachukua vijana wachache na ambao anahangaika sana kuwafundisha. Vijana hawa wanastahili kupata sehemu nzuri ya kupanga, madarasa mazuri na Walimu weledi. Ukifika hapo chuoni utakuta wanafunzi wanafundishana wao kwa wao, hakuna Walimu wa kutosha, hakuna vifaa vya kutosha na mbaya zaidi kijana anapohitimu hana nyenzo za kufanyia kazi. Sasa tunategemea kijana huyu ataenda kufanya nini huko kijijini kama siyo kurudi mjini na kuwa kijiweni tu? Naishauri Serikali kuharakisha mchakato huu wa kujenga vyuo hivi na nawasihi waanzie Jimbo la Biharamulo Magharibi. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu bali hata Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, naomba nalo liangaliwe na suala la mitaala liwekwe bayana ili vyuo hivi viweze kufanya kazi nzuri ya kuijenga jamii yenye uwezo mkubwa na mzuri.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mzima na kuweza kuchangia Bajeti hii. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Hotuba yake mahiri ambayo imejaa matumaini kwa Watanzania ambao wanasubiri maendeleo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia upande wa Walimu. Walimu katika nchi yetu ni watu ambao wamezarauliwa, maisha ya Mwalimu yamekuwa duni kiasi kwamba hata utendaji wao unapelekea kuwa sio mzuri. Walimu hao hata baadhi ya mafao yao bado yanasuasua. Je, kama Walimu hali yao ndio kama hiyo na posho zao hazipatikani kwa wakati, Wizara inategemea nini katika utendaji wao wa kazi? Hivi unamtegemea Mwalimu huyo kwa hali hiyo asichelewe kazini na pia afundishe darasani kwa ufanisi? Matokeo ya mitihani yanapokuwa mabaya ndio Walimu wanapoonekana kuwa hawafundishi vizuri, sababu kubwa ni matatizo hayo. Napendekeza ili tuweze kupata wanafunzi wazuri katika shule zetu, tunahitaji Walimu wazuri ambao wanapata mafao yao kwa muda muafaka ndipo tunaweza kupata vijana wazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie uhaba wa Walimu katika nchi yetu, tatizo hili limekuwa sugu. Imefikia hadi shule moja ambayo ina watoto zaidi ya mia tatu (300) inahudumiwa na Mwalimu mmoja au wawili, kwa mpango huu ndio tunaeneza elimu au tunapunguza elimu? Napendekeza Serikali ifanye haraka kuongeza Walimu katika Shule za Kata hadi vijijini ili tuweze kuongeza ufanisi katika elimu na pia kuwe na motisha kwa Walimu ambao watajitolea kufundisha katika shule za vijijini kutokana na mazingira ya vijiji husika. Kama tunavyojua vijijini hakuna huduma nzuri, kama maji, nyumba ya kukaa hata umeme ni mtihani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Bajeti hii ambayo mwelekeo wake ni kupunguza matatizo ya wananchi kuhusu suala la elimu. Aidha, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia Wizara hii ambayo imepata mafanikio makubwa. Baada ya utangulizi huo nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Wazima, Kitengo hiki ni muhimu kwani bado kuna watu wengi hawajui kusoma na kuandika. Naomba Serikali iweke utaratibu wa kuwaelimisha ili waweze kujisomea na kujielimisha. Vilevile elimu hii iongezewe mitaala ya kilimo, afya na taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi ni muhimu sana hasa kwa vijana wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari kwani vijana hawa wakipata elimu ya ufundi itawasadia kujiajiri. Naiomba Serikali itueleze imejipangaje ili kuwapatia mtaji ili wajiajiri.

Mheshimiwa Spika, madeni ya Walimu na kupandishwa vyeo. Niombe Serikali ianzishe dawati la kuhakikisha madeni haya na kupandisha vyeo yanashughulikiwa ili kuondoa malalamiko ya siku zote. Naomba Serikali itoe maelezo kwa nini matatizo haya yapo kila Bajeti? Madai mengine ni ya muda mrefu. Naomba Serikali ieleze ni vipi inafuatilia malipo haya ya Walimu katika Halmashauri kuhakiki ulipwaji wa madeni hayo?

Mheshimiwa Spika, majengo ya madarasa, nyumba za Walimu, majengo ya hostel, ujenzi wa maabara n.k. Kwanza niishukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kujenga majengo hayo, ila kwa sasa ni vyema mpango uliopo usimamiwe ili kupunguza matatizo makubwa yaliyopo. Ujenzi wa vyuo umefanikiwa sana ila utaratibu wa kuviendesha, naiomba Serikali ilete Sheria ya Kupiga Marufuku Siasa Mashuleni na kwenye Vyuo kwani inawapotezea muda wa masomo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata wasaa huu wa kuweza kuchangia Wizara hii kwa njia ya maandishi. Kwanza kabisa, naomba nichangie juu ya uchangiaji wa ada za mitihani ya kitaifa ya Kidato cha Nne na Sita.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko kabisa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haikuwatendea haki wanafunzi na Watanzania kwa ujumla wao kwa kuwabagua wanafunzi hao katika masuala ya ulipaji ada za mitihani ya Kitaifa. Kitendo cha Serikali kuamua kuwalipia ada za mitihani ya kitaifa wananfunzi wanaosoma shule za Serikali tu na kuwaacha wa shule binafsi kuendelea kulipia ada hizo, ni ubaguzi wa wazi.

Mheshimiwa Spika, siku za nyumba kila mtahiniwa alilipa ada hiyo bila kujali anasoma shule ya Serikali au binafsi. Tunamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni sababu zipi za msingi zilizopelekea mabadiliko hayo, ilihali Serikali hiyohiyo imehimiza uanzishwaji wa shule binafsi ili kukabiliana na wimbi la ongezeko la wanafunzi wanaomaliza Shule za Msingi kujiunga na Sekondari. Pia hali hii imesababisha kuwapo na manung'uniko makubwa kwa shule za binafsi.

Mheshimiwa Spika, Walimu ni nguzo muhimu sana katika ujenzi wa Taifa hili, lakini Walimu hawa nadiriki kusema wametelekezwa. Tumeshuhudia malalamiko mengi sana kuhusu stahili zao, kama wanavyofanya kazi zao kwa uaminifu na uvumilivu mkubwa basi Serikali nayo ionyeshe uungwana iwasikilize Walimu hawa. Walipwe mshahara yao kwa muda muafaka sambamba na kupandishwa madaraja yao yanayostahili na si kwa mazoea kwa maana kwamba kila Mwalimu anajulikana ameanza kazi lini na hivyo stahili yake ni ipi.

Mheshimiwa Spika, Walimu hawa wameonewa hata wanapoamua kujiendeleza kielimu. Mwalimu mwenye ngazi ya Diploma mwenye ngazi ya mshahara *TGTS E* na kuendelea anapohitimu na kupata *degree* arudipo katika kituo chake cha kazi hushushwa daraja hadi *TGTS D* kwa madai kwamba kwa mhitimu wa Chuo Kikuu ni lazima aanzie na ngazi ya *TGTS* D, hii ni haki? Je, Mwalimu kujiendleza kielimu ni kosa? Je, ni nia ya Serikali kudhoofisha kada ya Ualimu? Je, ni mbinu ya kuwatisha Walimu tamaa ya kujiendeleza kwa maana kwamba wasitoke vituoni mwao? Namwomba Waziri aje na majibu ya maswali hayo.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imelenga kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kilolo ni kati ya Wilaya mpya hapa nchini na ina kiu ya maendeleo. Pamoja na upya wake Wilaya ina jumla ya shule za sekondari 37 na ina jumla ya shule za sekondari 25 zimejengwa katika miaka mitano iliyopita. Wahitimu wengi wa kidato cha nne na sita wanakosa nafasi ya kujiendeleza. Tumekwisha omba

ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Kilolo. Je, ni lini sasa chuo hicho kitajengwa Wilayani Kilolo?

Mheshimiwa Spika, suala la kufuta mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili liangaliwe upya. Aidha, mwanafunzi akidahiliwa kazi yake kubwa ni kusoma na kufanya mitihani tu na ni zeozi zuri kwa wanafunzi ili wasiogope mitihani.

**MH. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango pamoja na ushauri ufuatao katika utoaji wa elimu ya ufundi katika nchi hii hasa ukichukulia maanani ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Ufundi, Serikali ichukue msisitizo wa kuboresha Vyuo vya Ufundi ili kuwafunza wataalam zaidi katika fani ya ufundi ili Watanzania waweze kuwa na wataalam wenye uwezo unaofanana na washiriki wenzake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Kwa vile lugha ya Kiingereza na Kifaransa ndio inayotumika katika Afrika ya Mashariki na Afrika nzima hadi duniani kote nashauri Serikali ichukue uamuzi wa makusudi wa kusomesha Kiingereza kuanzia darasa la kwanza hadi Chuo Kikuu ili Tanzania iwe na uwezo wa kuwasiliana kikamilifu na wenzake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waratibu wa Elimu Kata hadi sasa haijulikani vigezo vya uteuzi wa waratibu hawa. Mara kwa mara inatumiwa upendeleo wa kisiasa kwa sababu ya Chama Tawala kinawatumia Maafisa hawa kama *political agents.* Nashauri Serikali itoe vigezo vya kielimu vya kuteua maafisa hawa.

Mheshimiwa Spika, adhabu za viboko, pamoja na kwamba sheria ya elimu imekataza, walimu bado wanachapa wanafunzi hadi kuwajeruhi na wengine kusababisha vifo. Nashauri adhabu hiyo ifutwe shuleni mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya awali nashauri iwe sehemu ya mtaala wa shule ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Philipo Mulugo na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kurudisha elimu ya awali katika shule ya msingi lakini kwanza ningeshauri elimu hii ya awali ianzishwe katika shule zote za msingi na elimu hii ya awali iboreshwe ili iweze kujenga msingi bora wa mwanafunzi kuna msemo unaosema nyumba bora hujengwa msingi imara.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwa shule za kata, shule hizi zimeweza kusaidia sana watoto wanaomaliza elimu ya msingi kuweza wote waliofaulu kujiunga na elimu ya sekondari. Ushuri wangu shule hizi kwanza ziboreshwe kwani kuna baadhi ya shule hizi zilijengwa kwa uharaka kiasi kwamba nyingi zao hazina ubora unaotakiwa na nyingi hazina maabara, hazina walimu wa kutosha na vifaa vya kujifunzia na vitabu.

Mheshimiwa Spika, pia shule hizi kama tunataka kweli kuwasaidia vijana wetu hasa wa kike katika shule hizi mabweni yajengwe, watoto wengi kutokana na umbali wa shule hizi wanapanga mtaani na shule kama za Dar es Salaam wanafunzi wanapta taabu sana usafiri. Ninaomba jambo hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningeomba liangaliwe na Serikali ni kuhusu hawa vijana ambao wamekosa nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari wanapewa utaratibu gani? Yaani vijana ambao hawakufauli kuendelea na sekondari na ambao katika Wilaya zao hakuna Vyuo vya Ufundi *(VETA)* tunawawekea mkakati gani? Ningeshauri pengine sasa elimu ifikie mpaka darasa la 12 ili hawa vijana wote wapate hiyo elimu na umri uongezeke.

Mheshimiwa Spika, pia uwepo mpango mzuri wa kuwasaidia hawa vijana wanoamaliza elimu ya Vyuo vya *VETA* kuweza kupatiwa mikopo. Ushauri wangu ni kuwa Halmashauri zipewe jukumu la kuwapatia mikopo hawa vijana na ikiwezekana watengeneze vikundi kutokana na taaluma mfano waliohitimu useremala wapewe jukumu la kutengeneza *furniture* za mashule na Halmashauri isimamie hiyo mikopo watakayopewa. Hapo tutakuwa vijana pia tumewawezesha kielimu ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iongeze kasi ya kuhakikisha walimu wanaoidai Serikali walipwe, kwa sababu walimu wetu wamepoteza ari ya kufundisha kwa sababu madeni yao yamekuwa sugu mno.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu ya madai ya Walimu wa Mkoa wa Iringa. Walimu wanaoidai Serikali hadi Juni, 2011 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeona ni vizuri nilete kwako takwimu ya madai ya walimu wa Mkoa wa Iringa, sababu walimu wengi sasa hawana ari ya kufanya kazi. Naomba Wizara jambo hili litolewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, siku zote huwa najiuliza hivi elimu ikishuka Wizara gani ilaumiwe ni Wizara ya TAMISEMI au Wizara ya Elimu? Kwa sababu sera zote zipo chini ya Wizara ya Elimu na shule zinasimamiwa na TAMISEMI, naomba nipatiwe ufafanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloomba kuchangia ni kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Naomba kuishauri Serikali kuwa wangekabidhiwa taasisi za fedha yaani mabenki ndiyo yashughulikie hiyo mikopo badala ya Bodi ya Mikopo,

sababu ikishugulikiwa na benki zetu hata ukusanyaji wa pesa hizi utakuwa rahisi sana. Kumekuwepo na migomo mingi sana ambayo inahusishwa na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Philipo Mulugo, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa waliyonayo ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu iliyo bora na si bora elimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya Wizara, nashauri Idara ya Ukaguzi wa Shule iwezeshwe vya kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika Halmashauri zetu Idara ya Ukaguzi wa Shule wameshindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na ukosefu wa usafiri matokeo yake walimu wasiokaguliwa hujisahau kufikia malengo waliyowekewa. Walimu kutokukaguliwa kunaweza kusababisha pia mdororo wa elimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi hao watatoaje ushauri wasipokwenda kwenye shule husika? Watasimamiaje viwango vya utoaji elimu? Wakaguzi wapewe vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kama kuna chombo kinachosimamia uendeshaji wa shule binafsi kwa kuhakikisha kuwa ada zinazotozwa na wamiliki wa shule hizo za binafsi zinaendana na huduma zinazotolewa na wamiliki wa shule hizo kwa wanafunzi husika. Tumeshuhudia jinsi wamiliki wa shule binafsi wanavyopandisha ada bila kuongeza huduma yoyote kwa wanafunzi. Kama hakuna chombo cha kuwasimamia wamiliki wa shule/vyuo binafsi kwamba kila mwenye shule/chuo afanye atakavyo je, huko siyo kutowatendea haki Watanzania? Naomba ufafanuzi katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma shule zetu zilikuwa na redio na wanafunzi walipata elimu ya ziada kupitia redio. Kwa sasa walimu hawatoshi na redio hazipo katika shule zetu. Nashauri Wizara itumie teknolojia za kisasa kama vile redio, *TV* na kadhalika katika shule zetu ili kusaidia kutoa elimu kwa njia ya masafa kuziba pengo la ukosefu wa walimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma shule za sekondari zilikuwa za Kitaifa, wanafunzi walitoka Mtwara na kusoma Kagera na kadhalika hali hiyo iliweza kuwajengea Utaifa na kuwawezesha vijana kubadilishana uzoefu wa kujua tamaduni za jamii mbalimbali, kutembea pia ni kujifunza. Kwa sasa mtoto anapomaliza shule ya msingi kwenye Kata, anakwenda kusoma shule ya sekondari ya Kata, anakwenda *A - Level* ya Taifa akifanikiwa kwenda chuo hapo ndipo atakapobadilisha na kuona ulimwengu mwingine kwake. Naiomba Serikali itafakari hili. Kuna haja ya kujenga shule za sekondari za Kitaifa zitakazowachukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali kwa nia ya kujenga Utaifa, umoja na tamaduni za jamii mbalimbali za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kama kuna mfanyakazi Mtanzania anayeonewa ni mwalimu. Mwalimu akipandishwa cheo, mshahara wa cheo kipya halipwi kwa wakati, posho za

walimu hazilipwi kwa wakati, mishahara wanafuata mjini na hawapewi nauli kwa kufuata mishahara, halipwi posho ya kujikimu wanapopeleka taarifa za kazi Wilayani na kadhalika. Ni lini Serikali itakapomthamini mwalimu kwa kulipa kila stahili ya mwalimu kwa wakati muafaka? Mwalimu ni mfanyakazi kama mfanyakazi yeyote wa Serikali wathaminiwe na kutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza posho kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu hadi shilingi 7,500/=. Nawaomba Wakuu wa Vyuo Vikuu nchini kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya wanafunzi kupunguza malalamiko yasiyo na msingi kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja kwa kuiomba Serikali kuweka utaratibu wa kuwaendeleza wanafunzi wanaokosa nafasi ya kujiunga na kidato cha tano na kubaki wakiranda randa mitaani bila taaluma yoyote ya kuwasaidia kimaisha. Wanafunzi hao kwa sasa wapo wengi sana kutokana na shule za sekondari za kata. Wanafunzi hao wanaweza kufundishwa utaalamu wa ufugaji wa kisasa, kilimo cha kisasa na kadhalika katika vituo maalum vitakavyoanzishwa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, kwa huo tutapunguza wimbi la vijana kukimbilia mjini kwa lengo la kutafuta kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kuwaruhusu wasichana wanaopata mimba mashuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua lakini kwa kupunguza kuwa wanafunzi mama ni vizuri fursa hiyo ikatolewa kwa wale walio katika *A-Level*.

Mheshimiwa Spika, tukitaka tuwe na elimu bora ni lazima mwanafunzi atahiniwe kujua uwezo wa mwanafunzi na ni wapi mwalimu atilie mkazo kwa mwanafunzi wake. Serikali yetu imefuta mtihani wa kidato cha pili na kukariri darasa kwa mwanafunzi wa kidato cha pili.

Mheshimiwa Spika, wazazi tungependa watoto wetu watahiniwe na kama mtoto hana uwezo akariri darasa ili iwe fundisho kwa walio nyuma yake kusoma kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa walimu, ni vyema kwa sasa mgao wa walimu ukazingatia hali halisi ya maeneo na mazingira, kwani kwa hali ilivyo si rahisi kuchukua uwiano wa walimu na wanafunzi kwa hakika vijijini walimu watakuwa wachache na mjini watakuwa wengi kwani zipo haki za kimsingi ambazo huwezi kuwaondoa walimu hao mijini.

Mheshimiwa Spika, suala la uhamisho wa walimu haliepukiki kwani yapo matatizo na mazingira ambayo wakati mwingine huwezi kuzuia walimu hao wasihame, lakini linaendana na tatizo la kupanda vyeo na malipo kutopatikana. Kwa nini Serikali isitenge fungu hilo kila mwaka ili kuhakikisha tatizo hilo linazidi kupungua au kwisha kabisa? Malimbikizo mengi ni ya uhamisho na mapunjo. Jamani tutafute namna ya kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa wa walimu katika maeneo yote nchini, shule zetu za sekondari na za Mmingi hazina walimu kabisa na kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu katika randama hakuonyeshi mgao wa walimu na uwiano wao katika nchi nzima je, Serikali iko tayari kutuletea mgao huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka huu wa fedha Serikali imeahidi kujenga maabara kote nchini ni maabara ngapi zitajengwa katika Jimbo la Peramiho?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanasaikolojia waliokwishafanya utafiti wamegundua kuwa ubongo wa binadamu hukua kwa asilimia 80 toka umri wa binadamu wa miaka 0 mpaka miaka mitano na kwa kuwa msingi mzuri wa elimu hutakiwa kuwekwa kipindi hicho. Ninapenda kujua katika mpango maalum wa elimu, elimu hii inayowaandaa watoto toka miaka ya chini kabisa inapewa kipaumbele gani nchini?

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameelezea kwa kirefu sana katika ukurasa 73 na ameainisha umuhimu na mipango ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Katika kipengele (b) programu ya Vituo vya Ufundi Stadi vya Wilaya *(District Vocational Training Centres Programme)* ameeleza umuhimu wake, nisisitize tu kwamba programu hiyo ndiyo jibu la matatizo makubwa ya upungufu wa ajira kwa vijana maana ufundi stadi unasaidia kuandaa vijana kujiajiri wenyewe, pamoja na umuhimu huo nina maoni yafuatayo:-

Kwanza kama kila Wilaya itakuwa na Vyuo vya Ufundi Stadi ambapo tujitahidi kuvianzisha hata kwa fani chache tu vitoe matumaini kwa vijana wetu wanaomaliza Kidato cha nne, hilo ndilo jibu kwa kundi hili, tusisababishe wazazi wakakata tamaa maana kila mtu leo anadhani mtoto aliyefaulu ni yule anayekwenda Kidato cha tano.

Pili, vyuo hivyo vikazanie na vianze na fani ambazo hazihitaji uwekezaji mkubwa, mfano fani za huduma mahotelini, ukatishaji tiketi za mabasi na ndege, utengenezaji wa nywele *(saloon)* za kiume na kike, usafi na *TEHAMA*, hizo ndizo zinazotoa ajira kwa kiasi kikubwa kwa vijana wetu.

Tatu, Idara hii ya ufundi stadi iangalie uwezekano wa kutoa mafunzo ya uchimbaji, na *processing* ya madini ya kawaida, ipo ajira kubwa kwa *level* hiyo katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, *VETA* ndiyo mkombozi wa vijana wetu, Serikali ijipange ianze vyuo hivi kila Wilaya. Naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza kwa jitihada zenu za kuwaelimisha Watanzania na haswa watoto wa maskini.

Mheshimiwa Spika, kama kuna kitu kimoja mnatakiwa kukiangalia basi ni kutoa usawa katika elimu kwa watoto wa Tanzania. Ili kufikia kutoa usawa *(equality)* katika elimu ni lazima mpeleka walimu wa kutosha kwenye shule za Serikali za vijijini na ni lazima mhakikishe walimu hao wanaishi kule. Ni nini hasa kifanyike sasa? Wenzetu katika Serikali mnatakiwa mfanye jitihada za makusudi kabisa katika kubuni *incentive schemes* zitakazowafanya walimu wakubali kwenda kufanya kazi na kukaa vijijini. Baadhi ya mambo mnayoweza kuyafanya ni pamoja na kutoa mikopo ya vyombo vya usafiri kwa walimu wa vijijini, kuwajengea nyumba za kisasa na kupeleka umeme na kadhalika. Naomba maelezo ya kiutekelezaji katika hili.

Mheshimiwa Spika, niwashauri myafute matawi yote ya vyama vya siasa vyuoni, hata yale yaliyo nje ya vyuo (jirani). Hili litatupunguzia migomo na vurugu kwenye vyuo vyetu na ikiwezekana mzuie kabisa viongozi wa vyama vya siasa kufanya shughuli za siasa vyuoni humo na muwe wakali kwa watakaokiuka.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatujengea Chuo cha *VETA* kule kwetu Nzega? Ni vipi mmejipanga kukusanya pesa za mikopo ili mfuko huo uwe *revolving?* Naomba maelezo ya kina katika hili. Ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Bajeti hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Bajeti kwa mikakati yake mizuri ya kuboresha elimu nchini kwa idara zake zote.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiojificha kwamba Bajeti hii ni ndogo sana ukilinganisha na kero nyingi katika Wizara hii. Hivyo ninaishauri Serikali kuangalia namna ya kusaidia fedha kupitia Mfuko Maalum wa Hazina ili kupunguza kero zilizoko hususan madai ya walimu, ujenzi wa hosteli za shule za sekondari za kata, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi kulipa madai mbalimbali ya walimu bado kuna madai mengi sana ya walimu mfano mdogo tu wa Mkoa wa Singida ni jumla ya shilingi za Kitanzania 580,996,003.60 na kwa nchi nzima ni jumla ya shilingi za kitanzania 29,237,007,865.64.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na watendaji kuzalisha madeni bila utaratibu kwa mfano uhamisho wa mara kwa mara, likizo bila malipo, safari za kikazi bila malipo na kadhalika hatimaye malimbikizo yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unapunguza moyo wa kazi kwa walimu kwa kiasi kikubwa na hatimaye husababisha migogoro ya walimu na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauru Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha madai haya yanalipwa yote haraka iwezekanavyo;

(b) Kuacha kuwahamisha walimu wakati Serikali haina fedha; na

(c) Watendaji waache kabisa utaratibu wa kulimbikiza madai ya walimu.

Sasa ni wakati wa kutekeleza kauli mbiu ya walimu isemayo haki sawa na wajibu, hiii itasaidia sana kurudisha ari ya kazi kwa walimu. Ninasubiri majibu yenye maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa angalizo kama mwalimu mzoefu kuwa utaratibu wa Serikali kuunganisha idara zote zilizoko mkoani kuwa kwenye klasta moja sio nzuri kwani inamfanya Afisa Elimu wa Mkoa kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa haraka kwani mpaka aombe fedha kwa Meneja wa Klasta. Kwa kuwa Idara hii ni kubwa na pana ni vema iendelee kuwa na *OC* yake ili iweze kujiendesha kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliwahi kuandika barua kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kuwa Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kurudishiwa tangu mwaka 2009. Inashangaza hadi sasa Idara hii Maafisa Elimu Watu Wazima wapo majina tu, mafungu hawana pamoja na mikakati yao mizuri ya kuondoa kabisa kada ya watu wasiojua na kusoma.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuhakikisha idara hii inatengewa fedha ili iweze kujiendesha pamoja na kuwalipa posho walimu ambao wanafundisha madarasa ya Elimu ya Watu Wazima mfano, MEMKWA, MUKEJA, Elimu Masafa na ana kwa ana.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa azma yake ya kujenga vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya ikiwemo Manyoni Kata ya Njirii ambayo tayari majengo yapo tuliyopewa na wakandarasi wa barabara toka Manyoni hadi Singida. Vilevile ujenzi wa *VETA* Wilaya ya Iramba kata ya Ulemo ambako kuna majengo tumepewa na wakandarasi waliojenga barabara ya Singida hadi Shelui.

Mheshimiwa Spika, ninaogopa sana endapo majengo hayo hayatapata matumizi mapema yataharibika na kufanya gharama kuwa kubwa ya kujenga *VETA* kwa Wilaya hizi mbili. Nategemea Waziri atapokea ombi langu na atatoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali wajibu wake wa kukarabati Vyuo vya Ualimu vingi vimechakaa sana. Ukizingatia Vyuo vya Ualimu ndivyo ambavyo vinawapika walimu wetu ambao Taifa linawategemea kutoa taaluma katika shule za msingi na sekondari. Ninashauri fedha zitengwe kuzikarabati kikiwemo Chuo cha Kinampanda. Ninasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya katika zile shule za kata hadi kuja hapa Bungeni walitoka kwenye sekondari hizo za kata.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali kuongeza juhudi za kujenga maabara katika sekondari za kata, ili tuweze kuongeza idadi ya walimu wa sayansi, kujenga nyumba za walimu za kutosha ili walimu wakubali kwenda vijijini, kujenga hosteli hasa shule za vijijini na zianze hosteli za wasichana ili kuepuka mimba za utotoni na mmomonyoko wa maadili, vitabu vya kufundishia na kadhalika. Nina matumaini taaluma itapanda kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana mitaala ya elimu inapobadilika mara kwa mara wakati sera ya elimu ipo. Hili ni tatizo kwa sababu sio rahisi kusomesha walimu na kununua vitabu vipya mara kwa mara ni uharibifu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii.

**MHE. GOODLUCK J. OLE- MADEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mheshimiwa Phillipo Mulugo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga na watendaji wote kwa jitihada wanazofanya kuboresha na kuendeleza sekta ya elimu. Natambua changamoto zinazoikabili Wizara hususan katika elimu ya juu na kero zinazoikabili elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya elimu.

Mheshimiwa Spika, jimbo ninalowakilisha Bungeni ambalo ndiyo Halmashauri ya Wilaya ya Arusha lina upungufu mkubwa sana wa walimu. Naomba Halmashauri hiyo iongezewe walimu. Kufuatia ziara niliyoifanya kwenye Wilaya nilibaini kuwa chanzo cha tatizo ni kukosekana kwa nyumba za walimu. Mheshimiwa Rais wakati wa mkutano wa kampeni za uchaguzi aliwajulisha wananchi kuwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 230 zitakazotumika kujenga nyumba za walimu kwenye shule za msingi na sekondari nchini kote. Naomba nijulishwe kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu Wilayani kwangu. Aidha, naomba nijulishwe tarehe ambayo fedha hizo zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, nilitembelea shule kadhaa kwenye Wilaya yangu na kuona hali inayoashiria kuwa huenda ukaguzi haufanyiki au ikiwa unafanyika huenda taarifa hazifanyiwi kazi. Nashauri kuwa Idara ya Ukaguzi wa Shule uimarishwe na utendaji wa wakaguzi ufuatiliwe ili kuhakikisha kuwa wanatimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, elimu ya ufundi stadi ni haki ya Kikatiba ya wananchi wetu, Serikali kupitia Mamlaka ya Ufundi Stadi *(VETA)* imeweka mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi kwa kila Wilaya. Kwa kuzingatia hali halisi ya utekelezaji wa mpango huo, inaelekea kuwa baadhi ya Wilaya zitafikiwa baada ya mwaka 2015. Kwa kutambua na kuzingatia malengo yaliyowekwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 nashauri kuwa Chuo cha Ufundi Stadi Arusha ambacho ni cha Kitaifa kitenge asilimia 50 ya wanafunzi wanaodahiliwa kila mwaka kwa ajili ya Wilaya ya Arusha *(Arusha District Council).* Uteuzi wa wanafunzi kujaza nafasi hizo ufanyike na kamati itakayojumuisha wawakilishi wa wananchi (Madiwani na Mbunge) ili kuhakikisha kuwa nafasi hizo zinatumika kikamilifu kwa ajili ya wananchi wa Wilaya hiyo. Aidha, nashauri kuwa ili kuziba pengo kubwa la vijana wasio na ajira na mahitaji ya jamii, *VETA* Arusha ianzishe vituo vya mafunzo kwenye ngazi ya tarafa kwa kutoa mafunzo ya stadi zinazohitajika na jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ieleze kazi zinazofanywa na Idara ya Elimu ya Watu Wazima. Tathmini ya hali ya watu katika jamii inaonesha kuwa kiwango cha kujua kusoma na kuandika kinaendelea kushuka. Katika Jimbo langu sijaona wala kusikia kuwa kuna kituo cha elimu ya watu wazima. Nashauri idara hiyo iimarishwe kwa kuweka viongozi na watendaji kwenye kujituma.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri imeonesha kuwa moja ya majukumu ya ofisi ya Kamishna ni kuweka viwango vya elimu nchini. Kwa uelewa wangu juu ya viwango ni pamoja na uwiano baina ya mwalimu na wanafunzi darasani na kadhalika. Je, Kamishna wa sasa anafanya mikakati ipi ili kutekeleza viwango vilivyowekwa katika shule za msingi na sekondari nchini? Tutaboresha ubora wa elimu nchini?

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari kwenye Jimbo langu hazina maabara. Hotuba ya Waziri haoneshi kama kuna mpango wowote walau kupitia MMES II wa kusaidia shule za sekondari nchini kujenga maabara na kupata vifaa vinavyohitajika. Kufundisha masomo ya sayansi kwa *simulaltion* kutapotosha wanafunzi. Naomba Wizara isaidie shule za sekondari kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kupata maabara.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara isaidie shule za sekondari kwenye Jimbo kuanzisha maktaba ili wanafunzi wapate vitabu muhimu vya rejea na kiada kwa ajili ya masomo yao.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari leo vilionesha kuwa walimu wanaidai Serikali kiasi cha shilingi 29,237,007,865.64 na katika Wilaya ya Arumeru walimu wanadai shilingi 195,263,948.00 naiomba Serikali ihakiki na kulipa madeni hayo ili kuwatia moyo walimu wazidishe bidii katika kufundisha.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa shule ya sekondari Ilboru wameiomba Wizara iwasaidie wapate angalau basi moja kwa ajili ya kusafiria wanapokwenda shule za kimasomo, michezo na matibabu. Naomba sana Wizara isaidie ombi hili.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi kwenye kata ya Oljoro ambao husoma kwenye shule za kutwa ikiwemo Chuo cha *VETA* hutumia malori ya mchanga kwa usafiri wa kwenda shule na kurudi nyumbani. Usafiri huo ndio pia hutumiwa na walimu na watumishi wengine. Kata hiyo, ina shule mbili za sekondari na chuo kimoja cha *VETA.*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara inunue walau basi moja lihudumie shule zote.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia hoja hii kwa maandishi, kwanza kabla ya kuchangia nampongeza sana Waziri, watendaji wote wa Wizara hata Serikali kwa kuweza kuleta Bajeti nzuri. Kabla sijachangia nina *declare interest* kuwa mimi ni mdau na nina shule.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa Bajeti hiyo ninawiwa kuchangia baadhi ya maeneo ili kukamilisha uwakilishi mzuri wa wananchi wa Jimbo la Ukonga. Mimi nitachangia kuhusu upungufu wa shule za awali, utoaji wa chakula mashuleni na uboreshaji wa madarasa.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha mafunzo hayo kwa watoto wadogo. Elimu hii ni nzuri kwa ajili ya kuwaandaa watoto hawa. Naishauri Serikali kuliweka jambo ili rasmi zaidi ili shule hizi ziweze kuwepo katika nchi nzima na kwa kiwango kinachofanana. Lakini pia Serikali iandae walimu watakaoweza kuwalea na kuwafundisha maana Serikali imeanzisha elimu hii kabla ya kuwatayarisha walimu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia hasa ukizingatia upya wa shule hizi na kundi lenyewe la watoto wanaohitaji zaidi kujifunza kwa kuona na kutenda zaidi.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa chakula cha mchana, naishauri tena kwa mara ya pili kuwa mpango wa kuwapatia watoto mlo wa mchana. Wanafunzi waliotoka familia zenye kipato cha chini hawana uhakika wa kupata mlo wa asubuhi, mchana na usiku, hivyo iwapo chakula cha mchana kitapatikana basi Serikali inamhakikishia kupata angalu milo miwili, mmoja wa Serikali na mwingine kutoka katika familia. Pia itapunguza utoro na kuchochea watoto kupenda shule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa majengo. Majengo mengi hasa madarasa yamechakaa mno, hakuna sakafu chini na angalau watoto hawa wakikaa chini kwenye vumbi. Hili linakwenda sambamba na uhaba wa madawati. Katika jimbo la Ukonga ambalo lipo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam zipo shule zenye wanafunzi wengi na madawati machache mno. Mfano shule ya Viwege ina wanafunzi 900 madawati 60, shule ya Mwagati kuna uhaba wa madawati 789 na kadhalika. Nashauri Serikali kuwa na mkakati kabambe wa kutafuta madawati ya kutosha kila mwaka kabla ya kandikisha wanafunzi wapya.

Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha na kuongeza Vyuo vya Ufundi, jumla ya wanafunzi waliopo sekondari nchini ni 1,638,699 kati ya wanafunzi hawa wanafunzi wanaohitimu ni 639,700 wanafunzi 72,014 wanaingia kidato cha nne, nafasi za mafunzo ya ufundi ni 84,000. Kwa mahesabu haya utaona kuwa wanafunzi wanaobaki bila kuendelea na chuo au shule ni kubwa. Nielezee masikitiko yangu kuwa Serikali inasema kila Wilaya iwe na Chuo cha *VETA* wakati katika Bajeti ya Wizara ni shilingi 100,000,000 tu. Sasa hii inanitatiza kuwa kiasi hiki hakiwezi kutekeleza azma ya Serikali ya kuendeleza vyuo kama iliyotarajiwa. Naomba Serikali iangalie hili kwa upya na kwa umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa ufaulu wa kidato cha nne mwaka 2010. Kiwango cha ufaulu kilishuka kutoka 72.5% mwaka 2009 hadi 50% kwa mwaka 2010. Naomba sana Serikali iangalie kwa umakini kuporomoka kwa ufaulu ambako kuliwashtua wanafunzi na wazazi wengi, hata ilifika kiwango watoto wawili kujinyonga kwa kufeli mitihani yao. Pamoja na kutokuwa na utafiti wa kutosha Wizara ifuate utaratibu wa kutumia *continues assessment* za wanafunzi katika kuamua kama mwanafunzi amefaulu au la. Hii itasaidia sana kupata ukweli wa wanafunzi wanaoibia mitihani na wale walio na uwezo wa kielimu. Ninaamimi kuwa kama hii ingetumia wanafunzi au elimu isingeweza kuporomika kwa kiwango hicho. Hali hii ya kufeli kwa wanafunzi hapo dalili kuwa wanapimwa kwa mitihani ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malimbikizo ya madai ya walimu, kwa taarifa zilizopo watumishi na walimu 3050 wanaidai Serikali na Serikali ilitegemea kuwa ifikapo Juni, 2011 madai hayo yatakuwa yamehakikiwa, naomba sana kama Serikali imemaliza zoezi hilo walimu na watumishi hao wapewe taarifa ya kuweza kulipwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Wilaya yangu ya Ilala. Katika Manispaa hii walimu 562 waliopandishwa daraja tarehe 19/10/2010 hawajarekebishiwa mishahara yao. Kutowalipa walimu hawa stahili zao ni kuendelea kulimbikiza fedha/madai mengine jambo litakaloendelea kuongeza mduara wa madai ya walimu. Naomba Serikali fedha hizi zilipwe kwa walimu hawa ili waweze kufanya kazi kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri lakini pia kwa utendaji mzuri ukiachilia mbali malalamiko mengi ya walimu kuhusu mafao na malimbikizo ya mishahara yao, naamini kabisa kuwa matatizo haya mtayashughulikia kwa haraka ili walimu wapate stahili zao kwa wakati. Naomba sana matatizo haya ya malimbikizo ya madai ya walimu katika Wilaya ya Kinondoni yashughulikiwe haraka kwani walimu wangu wanataabika sana.

Mheshimiwa Spika, naomba katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri atueleze ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari ramani inayofuatwa ni ipi yaani ya Wizara au kila Halmashauri wanajenga kwa ramani zao? Pia naomba atueleze kwa

mujibu wa ramani za ujenzi wa madarasa ya sekondari na ya msingi gharama za ujenzi ni kiasi gani kwa darasa la sekondari na la *primary*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuruhusu michezo mashuleni, bado mwitikio ni mdogo sana. Naiomba Wizara iendelee kuhamasisha na kusimamia michezo mashuleni ili tuweze kuinua vipaji vya vijana wetu na hatimaye kupata wachezaji wa michezo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la watu kutopandishwa madaraja na kutokulipwa haki zao kwa wakati. Mfano mwaka 2005 kuna watu wameajiriwa, wamepandishwa daraja mwaka 2010 mpaka leo huo mshahara bado haujarekebishwa kwa Tabora wapo wengi. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atupe ufafanuzi wa hilo suala maana linagusa sana maisha ya walimu na familia zao.

Mheshimiwa Spika, suala zima la uboreshaji elimu Serikali inajipangaje kuhusu kupeleka *computer* katika shule zetu zote hasa sekondari.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwa nini wanafunzi wanakatazwa kurudia kidato cha nne tatizo ni nini? Na Serikali haijui kwamba suala hili la kuwakatalia na kuwambia wafanya mitihani katika vituo vya watu wazima hamuoni kama wanafeli na kuharibikiwa kabisa? Naiomba Serikali ifute uamuzi wake wa kuzuia watoto wasirudie kwa kuwa hakuna tija yoyote. Maana kuna maradhi, kucheleweshwa ada na kadhalika hivyo inapelekea mtoto kufeli sana Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Serengeti ilipata msaada wa kompyuta 165 na nyenzo nyingine ambazo zilisambazwa katika shule za sekondari 21 mwaka 2009. Lakini hadi leo hii Julai, 2011 hazijaanza kufanya kazi sababu ya kutokuwepo umeme. Hivyo ni vema kupewa umeme katika shule hizo ili kompyuta hizo zifanye kazi kama ilivyotarajiwa kueneza *TEHAMA* hasa elimu ya sekondari. Umeme wa jua ni vema upelekwe kwa haraka katika hizo sekondari 21. Upo uwezekano mkubwa kompyuta hizo kuharibika, kupitwa na wakati au hata kuhujumiwa na kuibiwa. Hivyo ni vema kompyuta hizo zifanye kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, taaluma na elimu vinashuka kwa sababu ya usimamizi na ukaguzi hafifu. Ni vema Halmashauri na Serikali iimarishe sehemu hii ya ufuatiliaji kwa njia ya usimamizi na ukaguzi mashuleni.

Mheshimiwa Spika, wananchi washirikishwe kikamilifu na Halmashauri ili chakula kitolewe mashuleni ili kusaidia uboreshaji wa utoaji elimu. Maelekezo maalum yatolewe ili Halmashauri iwajibike na maelekezo hayo yaimarishwe katika makuzi ya kimwili na kiakili kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, mtihani wa kidato cha pili na darasa la nne irudishwe ili isaidie kupandisha kiwango cha ufaulu. Mitihani hii isipokuwepo wanafunzi wanakosa msukumo chanya wa kujisomea.

Mheshimiwa Spika, mitaala na vitabu vya kiada na ziada itazamwe upya ili kuzuia upenyo wa kutoa zabuni ambazo zinasababisha kubadilika badilika kwa aina za vitabu vya kiada na ziada.

Mheshimiwa Spika, maelekezo yatolewe madhubuti juu ya udhaifu uliopo wa kuwafukuza ama kuwasimamisha shule wanafunzi kwa vile tu hawajalipa karo ama michango ya shule hii si sahihi ni vema wanafunzi wasibugudhiwe.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ugatuaji madaraka, uendeshaji wa elimu utazamwe upya ili kuondoa mkanganyiko wa uwajibikaji katika Halmashauri na mikoa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mengine ambayo sikupata kuyasema wakati nachangia kwa mdomo.

Mheshimiwa Spika, tunazo shule nyingi ambazo hazina na hazijaunda Bodi za Shule hivyo kufanya fedha zinazopelekwa kuibiwa wakati wa utekelezaji wa miradi, pili kushindwa kuendesha shule vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya kujiunga na vyuo vya ualimu, ombi ni kupeleka maombi Wilayani halaru yapelekwe wizarani, kurahisisha, tathmini na kutoa uwiano.

Mheshimiwa Spika, naomba Jimbo la Manyovu, tufungiwe *solar* kwenye shule za kata ili wanafunzi waweze hata kufanya *homework* zao na kujisomea.

Mheshimiwa Spika, naomba walimu katika Jimbo la Manyovu, watakapomaliza mafunzo tupewe upendeleo ili walimu wengi wachaguliwe toka Kigoma waingie Vyuo vya Ualimu Kasulu ili waweze kubakia huko kwa wingi kwa sababu mazoea ya eneo na posho za mazingira magumu hayatakuwa na umuhimu kwani ni nyumbani.

Mheshimiwa Spika, mengi nimechangia kwa mdomo.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba ya Waziri katika ukurasa 58 ameeleza juu ya umuhimu wa Elimu ya Watu wazima, kwani Taifa letu sasa lina changamoto nyingi kama vile mimba za utotoni, uelewa mdogo wa jamii juu ya Katiba, umuhimu wa upigaji kura, afya ya jamii na zaidi Kilimo Kwanza, tukiendeleza umuhimu wa Elimu ya Watu Wazima tutasaidia sana kuondoa matatizo yote katika jamii.

Mheshimiwa Spika, pesa za miradi ya maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima katika ukurasa 78 wa kitabu cha Bajeti ya Maendeleo pesa za kuendeleza *CBAE/COBET* zipo fungu la *Commissioner* wa Elimu. Nashauri pesa hizo zipewe fungu lake katika Idara ya Elimu ya Watu Wazima kama ilivyo kwa Matumizi ya Kawaida ya Wizara ukurasa wa 245 *subvote 3002* ili ufanisi uwe kwa haraka na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, posho ya shilingi 20,000 kwa *honorarium* ya walimu wa EWW na MEMKWA haitoshi kabisa hasa kwa sasa na hivyo inavunja moyo walimu wa EWW. Napendekeza posho hii ipandishwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2011/2012. Katika kuandaa Bajeti hii inadhihirisha wazi kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anajitahidi sana katika kuainisha mipango mizuri ya kuendeleza na kuboresha elimu hata mafunzo ya ufundi ambayo yatawezesha vijana wetu si kupata elimu tu bali elimu itakayowawezesha kujiajiri wenyewe. Hii inazingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyodhamiria kuinua vijana wake kielimu na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kuna malalamiko mengi ya wananchi yanayotokana na kushuka kwa kiwango au ubora wa elimu ambapo wanafunzi wengi wamekuwa wakifeli na hata wale wanaohitimu darasa la saba kutojua kusoma na kuandika, wanaohitimu kidato cha nne na cha sita kutojua kusoma na hata kuandika lugha ya Kiingereza. Wanaohitimu vyuo mbalimbali hapa nchini kushindwa kupata ajira kwani wanaposhindanishwa katika *interview* za kuajiriwa wanaonekana wana kiwango kidogo sana cha uelewa wa mambo. Unategemea kwa msingi mzuri kiwango cha elimu katika ngazi hizo kingewawezesha wanafunzi wanaohitimu kufanya vizuri katika masomo yao na baadaye elimu hiyo iwasaidie katika kupata ajira na maisha bora tujiulie ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, katika kupita kwangu Jimboni nimepata malalamiko mengi ya walimu. Wanafunzi, wazazi na pia kujionea hali halisi ya mazingira duni ya shule zetu kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari za kata, sekondari za Serikali na shule zinazomilikiwa na watu binafsi. Shule zetu kwa kweli nyingi haziko katika hali nzuri, unaweza kukuta madarasa ambayo hayana madawati, hakuna vitabu vya kusomea na kufundishia, vitabu vichache vilivyopo vinatumiwa na walimu na hata hivyo vingi ni vya masomo ya kawaida kwa maana hakuna vya masomo ya sayansi. Serikali iweke mipango mizuri ya kuhakikisha kila shule kwa madarasa yana vitabu na walimu wanapatiwa vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya shule ni chakavu na huduma kama za choo ni duni, mwanafunzi anataabika mahali pa kujisaidia ama aende porini au atumie vyoo vilivyoko mashuleni ambavyo matundu yake ni machache na hayana uwiano na idadi ya wanafunzi. Hii inampa mwanafunzi adha kubwa ya kuona shule kama mahali pa

adhabu kwani anapojihisi haja akiwepo shuleni inakuwa mzigo mzito kwake kufikiria atajisitiri vipi. Serikali iangalie tatizo la huduma ya vyoo mashuleni na kuhakikisha kwamba shule zote zina idadi ya vyoo vyenye matundu yanayowiana na idadi ya wanafunzi waliopo shuleni.

Mheshimiwa Spika, huduma ya chakula mashuleni ni jambo lingine linalomuathiri mwanafunzi asiweze kufuata masomo yake kikamilifu kwani mtu yeyote anapokuwa na njaa akili yake haiwezi kufikiria vizuri, hivyo hata maendeleo ya mwanafunzi huyu hayatakuwa mazuri, nashauri Serikali ifanye jitihada kurudisha mfumo wa kutoa chakula mashuleni ili kujenga miili na akili ya wanafunzi ambao ni vijana wetu wa Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, majengo ya shule zile ambazo yamechakaa na yako katika hali mbaya Serikali iweke mipango ya kuyakarabati. Hii ni pamoja na kuboresha huduma za maabara na kujenga hosteli za wasichana na wavulana ili watoto wasitembee umbali mkubwa kwenda mashuleni, kuwalinda wanafunzi wa kike na mimba zisizotakiwa na pia kuwalinda na vishawishi vya kuoa/kuolewa mapema.

Mheshimiwa Spika, walimu nao wana malalamiko na kero lukuki kuhusu mazingira wanayofanyia kazi pamoja na madai yao ya nyumba bora za kuishi, mishahara, marupurupu ya posho, malipo ya likizo, usafiri na hata malipo ya uhamisho. Kutokana na madai ya walimu hawa ambayo yanapigiwa kelele na chama chao (CWT), imekuwa chimbuko la kuwakatisha tamaa walimu kwa hiyo nao kupunguza morali ya kufanya kazi kwa bidii. Kazi ya ualimu pamoja na kwamba ni kazi ya wito, wengi wetu tumefikia tulipo kwa juhudi za walimu ambao wamevumilia na kutupa elimu japo wao wako katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu na ugumu wa kazi ya mwalimu, Serikali katika Bajeti hii itawalipa walimu wote madeni yao halali na pia iwaboreshee hali ya kufanyia kazi kama kufikiria kuwakopesha pikipiki au kuwapa baiskeli za kuwawezesha kwenda mashuleni na kurudi majumbani kwao. Pia katika kila shule zijengwe nyumba bora za walimu ili waweze kukaa mahali salama penye hadhi ili kuwapa moyo wa kufanya kazi vizuri. Katika jitihada za kuboresha elimu, Serikali ipige marufuku masomo ya ziada yanayofundishwa na walimu kwa malipo kwa jina la *tuition*, mfumo huu umefanya walimu wengi kutofundisha vizuri darasani na kuwataka wanafunzi wabaki mashuleni kwa masomo ya *tuition* na kuwatoza wazazi fedha na mzazi ambaye hana pesa za kulipia *tuition* mwanae anabaki nyuma. Hii si haki kabisa na wala sio mfumo mzuri katika kuendeleza masomo kwa watoto wa jamii nzima ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ufundi yamesaidia sana vijana wengi ambao walipata ujuzi mbalimbali katika shule za ufundi na kufanikiwa kujiajiri wenyewe. Kwa kuwa shule hizo zimeonekana kuzaa matunda mema, Serikali ipange kutoa mafunzo ya ufundi katika baadhi ya shule za kata, ili vijana waweze kupata ufundi kulingana na mahitaji ya pale walipo. Hii itasaidia vijana kuwa na ajira vijijini badala ya kukimbilia mijini kufanya biashara za umachinga.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuangalia kwa jicho la huruma shule zilizoko katika Jimbo la Kibaha Vijijini kwani kwa jumla nyingi zipo katika hali mbaya sana. Naomba kijengwe Chuo cha Ufundi kusaidia watoto wa wafugaji na wakulima kupata stadi za kuwawezesha kujiajiri kwa shughuli mbalimbali. Vijana wa Jimbo la Kibaha Vijijini ni vijana wachapa kazi na wapo tayari sana katika kujifunza, kunachowapa shida ni muongozo. Hata ufugaji unahitaji stadi za kujua kufuga kisasa ili kuweza kupata mifugo na nyama bora na pia maziwa ya kutosha. Kilimo nacho kina stadi yake kujua misimu, mbegu bora, mazao yanayostawi na kwa wakati gani. Wakijengewa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi kwa hakika watainuka kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, zama hizi ni za karne ya *TEKNOHAMA*, ni lazima masomo na mafunzo yanayotolewa kwa vijana wetu yaendane na mabadiliko yanayotokea duniani, nashauri shule zetu ziimarishwe zaidi kuhakikisha vijana wanapata masomo ya kompyuta na mawasiliano ili kuendana na mabadiliko yaliyopo duniani katika mfumo wa elimu na uchumi. Ni kweli kwamba shule nyingi na hasa zile zilizoko vijijini hakuna umeme na kwa maana hiyo mafunzo ya vitendo ya kutumia kompyuta yanaweza kushindikana. Lakini Serikali inaweza kujipanga vema na kununua *solar* ambazo zinatoa nishati ya jua na kutumika mashuleni kwa ajili ya kufundishia teknolojia hii. Masomo haya yaanze katika Vyuo vya Elimu ili walimu wanapokuwa na ujuzi huu ni rahisi kuwafundisha vijana walioko mashuleni.

Mheshimiwa Spika, miaka ya karibuni wanafunzi hasa wale walioko katika Vyuo vya Elimu ya Juu wanapata shida sana kuhusu sehemu ya kufanyia majaribio *(Practical Training)* Mashirika na Makapuni mengi yamekuwa yakikataa kuchukua wanafunzi kufanya masomo ya vitendo katika taasisi hizo. Serikali ichukue jukumu hili na endapo wanafunzi wanatakiwa kwenda kufanya masomo ya vitendo inawawia vigumu kupata kazi kwani wanakuwa hawana uzoefu wowote katika ujuzi wa taaluma waliyosomea.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba Bajeti hii, itaondoa kero za walimu na wanafunzi na kwamba hatutaona tena maandamano ya kundi hili mabarabarani wakidai haki zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo; pale Wizarani kuna nafasi nyingi sana zinakaimiwa kuanzia Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi na kadhalika. Je, nafasi hizo zitakaimiwa mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza Watanzania wote kwa kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na sekondari kila kata na hata kijiji. Serikali iliwaahidi Watanzania suala la walimu, vifaa vya maabara, vitabu na kadhalika. Ili kuboresha elimu, Serikali inapaswa kuchukua hatua za makusudi kupata walimu, zipo shule za kata zenye walimu wawili, mkuu wa shule na

mwalimu wa taaluma. Hii ni hatari sana kwa elimu yetu, mwisho tutazalisha watu ambao hawana *skills* na hivyo kushindwa kupambana na mazingira yao, badala ya kupata elimu bora itakuwa bora elimu.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua na kupambana na tatizo la walimu ni kuanzisha Vyuo vya Elimu kwa ngazi ya Cheti kwa walimu wa shule ya msingi na Stashahada kwa shule za sekondari, Mheshimiwa Waziri, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa kujua hilo imejenga Chuo cha Elimu Karatu kwa malengo ya kutoa mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Cheti na Stashahada, miundombinu ni tayari. Tunaomba Serikali isajili Chuo hicho na kukiendesha kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu hii inasadia sana kupunguza au kufuta kabisa tatizo la walimu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa kwa uzito wake ni Wizara kutokuwa na sera za uhakika. Nina maana kuwa kumekuwa na tabia ya kubadilika badilika kwa mitaala ovyo na kufanya elimu iwe ikiyumba. Tumeona kuwa kila Waziri anakuja na namna yake kama ajuavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha, tatizo kubwa kwa shule nyingi za kata hakuna wahasibu hivyo wakuu wa shule wamekuwa wakifanya kazi hizo, hii ni hatari sana, Wizara ishughulikie hilo. Aidha, kwa kutoa mwongozo kwa wakuu wote wa shule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugatuaji wa madaraka ni kweli shule za sekondari zipo chini ya Halmashauri zetu kiutawala na sera zipo kwa Wizara ni sawa inapaswa kufanyika utaratibu mzuri ili kuwe na mawasiliano mazuri kati ya Halmashauri na Wizara katika utendjai wenye tija kwa shule zetu. Mfano shule zinaingia mkataba wa zabuni za vyakula na Halmashauri na mlipaji wa zabuni hii ni Mkuu wa Shule bila ya Halmashauri (Mkurugenzi) kuhusika, inapotokea shida ya malipo mzabuni huishitaki Halmashauri hii inaleta mkorogano kati ya Halmashauri na Wakuu wa Shule.

Mheshimiwa Spika, Wizara iimarishe Idara ya Ukaguzi wa Shule hasa taaluma, ufundishaji kwa walimu na hata wanafunzi. Ukaguzi umelega lega sana na inawezekana pia haupo katika maeneo fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, kuboreshwe mahusiano kati ya wananchi (jamii) na walimu. Jamii inapaswa kufahamu nafasi na wajibu wao kwa walimu. Wanafunzi katika kutoa elimu bora.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naaza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika kutusaidia sisi

kama Wabunge, lakini pia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kiutendaji kwa Serikali na wananchi kwa ujumla bila kuchoka na bila woga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii kujumuisha mengi ambayo naomba nichangie machache kufuatana hali halisi ya jimbo la Kilwa Kaskazini na nchi kwa ujumla. Lipo tatizo kubwa sana katika ajira za watumishi Sekta ya Elimu haswa katika upandishaji madaraja, mafunzo kazini na semina.

Mheshimiwa Spika, upandishaji madaraja kwa walimu unachukua muda mrefu sana kiasi kupelekea kukosa hamasa ya kufanya kazi lakini pia pale wanapopandishwa huchukua muda mrefu sana mishahara yao kulipwa kufuatana na madaraja yao. Hili inapelekea kuwa na malimbikizo makubwa sana na ucheleweshwaji wa kulipwa malimbikizo husika. Katika malipo pia walimu wanachelewa sana kupata pesa za likizo kiasi ambacho hata malengo yao ya kujikimu kwa safari ama likizo huwa za kusuasua.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani ipo haja ya Serikali kutoa motisha kwa wale wanaofanya kazi maeneo ya vijijini kwa maana wapo katika mazingira magumu sana. Viwango vya mishahara haina tofauti na wanaoishi mijini hivyo inapelekea wengi kukimbilia mijini na wale walio vijijini kuhisi kuwa wanaonewa na wamepoteza thamani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuangalie kwa makini katika ucheleweshaji wa malipo inapelekea walimu kuingia katika mikopo ambayo inawafanya walipe riba kubwa sana kutoka katika taasisi binafsi za fedha. Lakini jitihada za makusudi zifanyike ili kuelimisha walimu na watumishi wengine katika sekta kuhusu mikopo hii ambayo imekuwa ni janga kubwa kwao na kwa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kazini ni kikwazo kikubwa sana maana toka siku anaajiriwa hadi anahamishwa au vinginevyo anakuwa hajapata kuhudhuria hata mafunzo ya siku mbili ambapo ni kinyume cha sheria za kazi lakini pia tunahuisha ujuzi na kuwafanya wasiwe na ujuzi endani na wakati. Serikali igharamie masomo kwa wale wote ambao watakuwa wanajiendeleza wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya kufundishia, maabara, madawati, nyumba, maji, usafiri na hata mazingira bora ya ufundishaji sasa ni wakati muafaka Serikali iangalie zaidi maeneo ya vijijini ambapo kwa kipindi kirefu wamekuwa wahanga, ambao hawana kimbilio.

Mheshimiwa Spika, pengo lililopo sasa katika utoaji elimu kutokana na upungufu wa walimu ni kubwa sana ni vema tukaangalia uwezekano wa kubadili sheria zetu ili tuweze kuleta walimu kutoka katika nchi nyingi kama India, Pakistan na Bangladesh haswa katika masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi. Wakati tukiwa tunajipanga wenyewe kupata ufumbuzi wa kudumu katika tatizo hili kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo katika makato kwa watumishi wa sekta ya elimu kwa maana hawana furaha na mfuko wa bima ya afya na hata bima ya maisha ambayo

kwa muda mrefu wamekuwa wakichangia lakini pale ambapo wanastahili kulipwa stahili zao basi inakuwa kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ifike wakati sasa Serikali itoe suluhisho la migogoro katika Vyuo Vikuu kwa maana nalo linaleta usumbufu mkubwa kwa jamii nzima. Hili ni jambo ambalo limekuwepo kwa miongo kadhaa, hivyo ni vema likapata ufumbuzi wa kudumu. Njia pekee ni Serikali kuwa wazi katika kila hatua ya utekelezaji na utatuzi wa matatizo kwa wanafunzi na walimu. Hii nina maana kuwa huwa muda mrefu unapita toka tatizo linapojitokeza mpaka kufikia hatua ya ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kusikia Serikali inatoa tamko sasa ni jinsi gani matatizo ya walimu yamepatiwa ufumbuzi na kwamba Wizara gani itahusika moja kwa moja na masuala yao ikiwa ni TAMISEMI au Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Natakutakia kila la kheri. Namuomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na nNaunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ya Wizara yake kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mvomero haina Chuo cha *VETA* na hivi karibuni niliuliza Serikali ina mpango gani wa ujenzi wa chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Mvomero maelezo ya Naibu Waziri yanaonyesha kuwa Wilaya ya Mvomero ipo katika Wilaya 28 za mwanzo katika mpango wa kujengwa Chuo cha *VETA.* Je, ni lini mpango utatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka 13 shule hii haijasajiliwa. Mwaka 2009 nilichangia ukarabati wa madarasa, ujenzi wa vyoo ili kukamilisha vigezo kwa ajili ya usajili. Nataka kujua ni lini shule itasajiliwa?

Mheshimiwa Spika, kuna uhaba wa walimu shule za msingi na sekondari katika Jimbo la Mvomero katika Jimbo la Mvomero. Naomba Serikali iangalie tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna walimu wengi wana malalamiko ya kutopandishwa madaraja Serikali inatoa tamko gani?

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawamba pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Philipo Mulugo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia kwa makini uandaaji wa Bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Pia shukrani za dhati zimfikie Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa juhudi zao za kuiendeleza sekta hii ya elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi mchango wangu utakuwa kama ifuatavyo:-

Shule za Sekondari za Kata, tunaipongeza Serikali kwa juhudi zote hizo zilizosaidia kufanikisha ujenzi wa shule za kata. Naishauri Serikali pamoja na Wizara kwa pamoja ihakikishe kuwa inaboresha shule zetu za kata kwa kupeleka walimu wa kutosha, kuzinunulia vitabu, vifaa vya maabara, kujenga nyumba za walimu pamoja na kuziwekea umeme hata kama ni ule wa *solar*. Hali hii itasaida kwa kiasi fulani kuleta ufanisi kwa wanafunzi wa walimu wanaofundisha katika shule hizo. Katika jimbo langu la Tarime, wazazi wamejitahidi kujenga shule za sekondari zipatazo 35. Tatizo kubwa linalozikabili shule hizi ni ukamilishaji wa maboma ya majengo ambayo bado hayakuezekwa. Hivyo naiomba Wizara isaidie kwa dhati Wilaya ya Tarime msaada wa bati zipatazo 10,000 tu ili kukamilisha zoezi hili. Hii itawatia moyo wananchi wa Tarime ambao juhudi zao zinaonekana dhahiri kuwa wanapenda watoto wao wasome na kujiendeleza ili kutekeleza sera ya elimu nchini Tanzania inayotutaka elimu ya kidato cha nne iwe ya lazima kwa kila mtoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sera ya elimu, mfumo wa sera ya elimu nchini Tanzania wa $1:6:2:3^+$ binafsi naunga mkono ikiwa utatekelezwa kwa vitendo. Kwanza mfumo huu utapunguza suala la miaka mingi mwanfunzi kukaa shuleni/vyuoni na matokeo yake anapohitimu elimu yake ya Chuo/Vyuo Vikuu huwa umri umeenda na hivyo zaidi huwaza maisha kuliko ufanisi wa kazi. Naishauri Serikali iharakishe mfumo huu na ihakikishe kuwa sera hii inaanza kutekelezwa mara kwa mara.

Mheshimimiwa Spika, kuna tetesi za dhahiri kuwa kutokana na kushamiri kwa ongezeko la Vyuo Vikuu katika nchi yetu, elimu inayotolewa katika vyuo hivi hasa vyuo vya binafsi haikidhi haja ya kumuandaa mwanafunzi kuzimudu stadi za maisha. Hali kadhalika kuna tetesi za wazi kuwa hakuna wataalam katika vyuo hivyo. Pia kuna tetesi kwamba vyuo hivi vimeanzishwa kwa lengo la kujipatia utajiri kwa baadhi ya watu au taasisi zinginezo; hivyo basi lengo kubwa si kutoa huduma ya elimu ila ni utajiri wa haraka haraka! Jambo hili pia naiomba Serikali pamoja na Wizara kulifuatilia ili kujua uhakika wa tetesi hizo. Mitaala inayofundishwa katika vyuo hivyo ihakikiwe na wataalam waliobobea.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha *EMAC* katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hakina budi kutazamwa kwa jicho yakinifu kwani kimekuwa kikitumiwa kwa muda mrefu na baadhi ya wachapishaji wa vitabu toka nje ya nchi na hivyo kuwa kikwazo kwa wachapishaji wazalendo. Aidha, lugha za kuudhi na hata rushwa ni jambo la kawaida katika kitengo hiki. Hali hii ya upendeleo imepelekea baadhi ya wachapishaji hasa wazalendo washindwe kuchapisha kazi zao na hivyo kukwamisha suala zima la upatikanaji wa vitabu katika shule zetu! Naishauri Serikali ipange wataalam waliobobea katika kitengo hiki ambao hawana tamaa, ubinafsi, chuki na hata uzembe ili kuhakikisha kuwa *EMAC* inaleta ufanisi katika sekta ya elimu na si karaha!

Pia Serikali ihakikishe kwa dhati kuwa inawaendeleza wachapishaji wazawa kwa kuwapatia ushauri, semina, mikopo na hata ruzuku. Hali hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuinua kiwango cha elimu hapa nchini Tanzania. Hii ni kwa sababu wachapishaji toka

nje ya nchi hawawatumii waandishi wa vitabu wazalendo na matokeo yake huagiza vitabu toka nchini kwao ambavyo huuzwa kwa gharama kubwa na wakati huo huo haviendani na mazingira halisi ya Tanzania. Jambo hili lahitaji fikra zaidi kuliko ubinafsi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi ihakikishe kuwa inatekeleza Ilani ya CCM kwa kutimiza ahadi zote zilizoorodheshwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010. Wizara ihakikishe inajenga Chuo cha *VETA* kwa kila Wilaya na msisitizo nauweka kuwa Serikali ihakikishe kuwa inajenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Tarime. Vyuo vya *VETA* vitasaidia kwa kiasi kikubwa kuziba pengo la ajira katika nchi ya Tanzania. Nina imani na Serikali ya CCM na naamini itatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara/posho/maslahi ya walimu. Hili jambo lizingatiwe na kufuatiliwa kwa ukaribu zaidi. Baadhi ya walimu wanashindwa kutekeleza wajibu wao wa kufundisha kwa ajili ya ujira mdogo. Hivyo basi naishauri Wizara ya Elimu ihakikishe inaboresha mishahara, posho, maslahi pamoja na stahili nyingine za walimu ili kuwatia moyo katika utekelezaji wa kazi na wajibu wao katika jamii. Hali hii iende sambamba na uboreshaji wa nyumba za walimu wa kada zote wa shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu hadi vyuo vikuu. Natumia nafasi hii kuikumbusha Wizara kuwa ihakikishe inaboresha miundombinu ya Chuo cha Ualimu Tarime kwa kukifanyia ukarabati mkubwa kwani chuo hicho kimezeeka sana na hivyo kuhatarisha maisha ya wanachuo, walimu/wakufunzi pamoja na watumishi wengine wa hapo chuoni.

Upungufu wa walimu na watumishi wengineo katika sekta hii ya elimu ni jambo ambalo si la kupuuza katika nchi yetu. Ni dhahiri na wazi kuwa tukiboresha mazingira ya walimu, tukiongeza mishahara na posho nyinginezo ni wazi na dhahiri kuwa Wizara hii itapata watumishi wengi sana kwani kwa sasa vyuo vingi vinafundisha kozi ya ualimu na wanafunzi wanaosomea fani ya ualimu ni wengi ila wanapohitimu hushindwa kuajiriwa katika sekta hii ya elimu kwa visingizio kuwa hakuna maslahi bora.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, binafsi naishauri Serikali ihakikishe kuwa inatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya umma kwanza. Pia iangalie na historia ya mwanafunzi kwa utafiti wa kina zaidi. Utafiti uhusishe uwezo wa wazazi wa mwanafunzi, shule alizosoma mwanafunzi (elimu ya awali, msingi, sekondari na hata vyuo vya *diploma* au cheti). Serikali itoe elimu kwa Watanzania ili watambue umuhimu wa kuchangia elimu. Binafsi nitafarijika sana ikiwa tutawafundisha umuhimu wa Watanzania kujitambua na kuanza kutoa michango katika elimu na huduma nyingine za kijamii kuliko kuegemea kuchangia harusi na starehe nyingine ambazo hazina tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bodi ihakikishe inashirikisha wadau mbalimbali wa elimu ili kubuni mbinu shirikishi ya kuchangia elimu na kuwafundisha Watanzania kuwa vitu vya bure katika dunia ya sasa vimepitwa na wakati! Bodi ihakikishe kuwa watoto wanaonufaika na mikopo ni wale tu ambao wazazi wao hawajiwezi. Wanafunzi ambao

wazazi wao wanajiweza bodi ihakikishe kuwa inawajulisha ili watoe gharama za kuwasomesha watoto wao. Naamini kuwa tukiamua tutaweza na sasa tuamue.

Mheshimiwa Spika, mitaala kubadilika badilika kila mara katika nchi yetu kumeathiriwa kwa kiasi kikubwa sana maamuzi ya kisiasa. Jambo hili kwa kiasi fulani limeathiri wanafunzi, walimu, wazazi na hata wachapishaji wa vitabu. Naishauri Serikali ihakikishe kuwa kabla ya kutoa tamko rasmi la kubadilisha mitaala iwe inatoa semina kwa walimu watakaofundisha mitaala hiyo pamoja na wachapishaji wa vitabu ili nao waandae waandishi wao kukabiliana na hali hiyo. Pia mitaala hiyo ibadilishwe kulingana na matakwa ya kijamii katika fani za utamaduni, siasa na uchumi. Mitaala isibadilishwe kutokana na utashi wa kisiasa wa mtu mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kidato cha nne mwaka 2010 yanaonyesha dhahiri kuwa elimu yetu inayotolewa katika shule zetu bado ina walakini. Walakini huu umetokana na baadhi ya walimu kukata tamaa kutokana na maisha duni/mishahara duni/posho duni wanazopata. Pia mazingira duni ya wanafunzi kujifunzia nayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuathiri matokeo ya kidato cha nne kwa mwaka 2010. Pia ubadilishaji wa mitaala bila kufanya ushirikishaji wa wadau hususan walimu nao uliathiri kwa kiasi kikubwa matokeo hayo kuwa mabaya sana. Mitaala ilibadilishwa lakini vitabu vilichelewa kuchapishwa. Pia ukosefu wa walimu, vifaa vya kufundishia kama vile vitabu, vifaa vya maabara na vielelezo vinginevyo kama vile tufe na ramani navyo ni baadhi ya vitu vilivyochangia matokeo hayo kuwa mabaya. Naishauri Serikali ijipange ipasavyo ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizosababisha matokeo ya mwaka 2010 yawe mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, suala la migomo ya wanafunzi vyuoni, ni dhadhiri na wazi kuwa wanasiasa uchwara wanachangia kwa kiasi kikubwa suala hili katika vyuo vyetu. Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuwa wanasiasa wapigwe marufuku na shuguli zote za kisiasa kama vile wanafunzi kujiunga na vyama vya siasa vipigwe marufuku, pia Serikali itumie sheria kudhibiti hali hii. Mwanafunzi yeyote anayeshawishi wenzake kugoma akibainika afukuzwe mara moja bila kubembeleza na wale waliogoma wakifukuzwa wakati wa kurudishwa, warudishwe kwa masharti makali kama vile barua kutoka kwa mzazi/mlezi, barua kutoka kwa Balozi, Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji, Katibu Tarafa, Kata, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa hadi barua ithibitishwe na Waziri na mwanasiasa yeyote anayejitafutia umaarufu kupitia Vyuo Vikuu apewe adhabu kali sana.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya JKT yawe ya lazima kwa kila mwanafunzi anayehitimu kidato cha nne, sita au *diploma* au cheti ajiunge na JKT kwa muda wa mwaka mmoja au miezi sita. Katika mafunzo hayo mwanafunzi afundishwe juu ya uzalendo pamoja na ukakamavu! Ili hili liweze kufanikiwa; sifa kuu ya kumruhusu mwanafunzi kujiunga Chuo Kikuu iwe ni mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa umuhimu wa Wizara hii na hivyo pia changamoto nyingi inazokabiliana nazo. Ni kweli kazi kubwa imefanyika lakini tukifanya tathmini tutabaini kuwa tunao uwezo wa kufanya vizuri zaidi. Ujenzi wa Chuo cha *UDOM* ni mfano mzuri sana na nampongeza Mheshimiwa Rais na wale waliofanikisha uanzishwaji wa chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, zile fedha zinazokuwa zimetolewa kwa kila mtoto sasa zinafika kwa kiwango kidogo sana hakikidhi haja kabisa. Upo pia upungufu mkubwa wa walimu, madawati, nyumba za walimu na madarasa.

Mheshimiwa Spika, katika karne tuliyonayo ni aibu kuwa na matatizo hayo. Hivyo Serikali ije na mpango wa kusaidiana na Halmashauri ili kumaliza shida hizi. Nyumba za walimu ziwekwe *solar*. Kila shule ya msingi iwe na mwalimu wa michezo. Ili kukabilina na tatizo la uhaba wa walimu naomba Serikali ifikirie kujenga Chuo cha Ualimu Mbinga au kukifufua cha zamani kilichogeuzwa kuwa sekondari ya *Mbinga day*.

Mheshimiwa Spika, bado tunahitaji kubuni mbinu mpya ya kudhibiti fedha zinazopelekwa katika sekondari hizi ili thamani ya fedha ionekane. Naamini pia *VETA* wanaweza kusaidia kutoa vifaa vya kufundishia hasa masomo ya sayansi, hivyo wahusishwe zaidi. Ombi maalum ni kuona sekondari za Mbinga nazo zinashirikishwa katika kupewa kompyuta, mabweni na kadhalika. Kama inavyoonekana kufanyika Wilaya nyingine kwa kusoma ni majaribio.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukigeuza Chuo cha Maendeleo Mbinga kuwa *VETA* uharakishwe. Jimbo la Mbinga Mashariki limefanikiwa kuwa shule moja ya *High School*. Wizara itusaidie tuongeze sekondari ya Ruanda na Hagati hasa katika maeneo ya hosteli, maabara, maktaba na *Assembly Halls*.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la wanafunzi hapo kusoma masomo ya sayansi lakini pia walimu wa sayansi. Naomba sasa tuamue kupandisha mishahara ya walimu kwa kuongeza mishahara walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu tumepiga hatua hasa kwa kuangalia soko linahitaji nini. Jambo hili lifanyike kwa *VETA* pia. Tukarabati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuongeza *facilitaties* ili kiendelee kuwa chuo chetu cha kujidai nacho. Nawasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, elimu ya awali bado kuna *gap* juu ya elimu ya awali. Sio shule zote zina darasa la elimu ya awali. Je, Serikali inasema nini juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, *milk feeding programme* ya shule za msingi, Serikali iliamua shule za msingi ziwe zina *milk feeding programme* angalau *once a week*. Je, agizo hilo limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, shule za msingi za Ludewa zilikuwa zinapewa *capitation subsides* na sasa tangu Machi shule hazijapewa *capitation grant.* Aidha viwango vya *capitation grant* pia vinaenda vinabadilika badilika havieleweki, *formula* inasemaje.

Mheshimiwa Spika, kata ya Maranga Wilaya ya Ludewa inapaswa kuongeza shule ya msingi kutokana na idadi ya watoto kuwa wengi. Je, Serikali ipo tayari kusaidia shule hiyo na pamoja na mchango wangu huu naambatisha maombi ya shule ya msingi ya Mbugani ili Serikali ichangie kupitia Halmashauri kwa *capitation grant* maana ni jukumu la Serikali kwa kushirikiana na sisi wananchi wa Ludewa kujenga shule na kutoa elimu. *Right to education universal education to all.*

Mheshimiwa Spika, elimu ya sekondari nashauri iwe ni agizo liende kila *RCC* na *DCC* kuwa kila tarafa iwe na *A -Level* kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wakimaliza *form four* hawapati nafasi ya kwenda *form six* na hivyo inatarajiwa waende elimu ya ufundi lakini bado vyuo vya ufundi haupo kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Wilaya ya Ludewa eneo la Shaurimoyo tutapatiwa Chuo cha *VETA* maana tumekwishatenga eneo la chuo. Serikali ina mpango gani wa kuchagua vyuo vya *private but qualified* kwa mfano, vyuo vya dini ili kuingia ubia kama hospitali za *DDH* na Serikali?

Mheshimiwa Spika, nashauri mikopo ya elimu ya juu ipitie benki ambazo 100% *owned by Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, nashauri vyeti vya wanafunzi waliofadhiliwa na mikopo viwekwe alama za *dot* na wanafunzi wanapoanza kazi waajiri wakiona vyeti waelewe kuwa hao waajiriwa wanapaswa kukatwa fedha.

Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu vijijini ni kubwa kuwepo na *teachers retention scheme*, posho ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, suala la wanafunzi kuachishwa masomo baada ya kupata ujauzito limefanyiwa utafiti wa hali ya juu na wataalam husika, utafiti ulionesha nini? Lakini Zanzibar ina utaratibu unaomruhusu msichana wa aina hiyo kuendelea na masomo. Huku Tanzania Bara kuna mpango gani kwani tunapoteza wasichana wengi na kwa bahati mbaya sana huwa wenye uwezo mkubwa kimasomo.

Mheshimiwa Spika, nafasi zilizowazi na zinakaimiwa na maafisa wengine kwa muda mrefu sasa zipate maafisa kamili ili wafanye kazi kwa kujiamini.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ufundi yatiliwe mkazo kunusuru vijana wanaobaki vijijini baada na kushindwa kuendelea na masomo ya baada ya darasa la saba na kidato cha nne.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika Bunge hili ikiwa ni kuendelea kuungana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupokea hoja zote za Walimu na hii ni kwa sababu TAMISEMI inafanya kazi sambamba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenye masuala ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Serikali hii makini haiwezi kumdharau Mwalimu, haiwezi kumfanyia jambo ambalo haliwezi kumtendea haki Mwalimu wetu kwa sababu tunatambua mchango wake mkubwa na tumeeleza sana hapa jinsi ambavyo tunatambua mchango wa Mwalimu na kazi kubwa wanayoifanya ya kuelimisha Watanzania sisi wenyewe Wabunge tukiwemo. Kwa maana hii nataka niwahakikishe kwamba hata Mheshimiwa Rais ameendelea kusisitiza kwamba pia anawatambua Walimu na nakumbuka mwaka 2007 tukiwa Dar es Salaam alipokuwa anafungua Jengo la Chama cha Walimu pale Ilala aliwaambia "Walimu nawaheshimu sana, nawathamini sana, nautambua mchango wenu na mimi ni Mwalimu mwenzenu". Sasa sisi hatukuhoji lakini Walimu wanajua kwa nini alisema yeye ni Mwalimu mwenzao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba elimu imepata mafanikio makubwa kutokana na mipango ya elimu. Tunao mpango wa elimu ya MMES kwa upande wa sekondari, lakini tuna mpango wa elimu ya msingi ambao unatambuliwa kwa jina la MMEM ambayo kwa mipango hii imeweza kutufikisha mahali pazuri sana. Moja kati ya mafanikio mazuri ambayo kwa kweli tumeyapata kupitia mipango hii, kwanza tumeongeza idadi ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza nchini katika shule zetu za msingi lakini pia tumeweza kuweka na mipango ambayo inawezesha Walimu kwenye maeneo yao kufanya kazi yao katika mazingira rahisi ili kuweza kuboresha sekta ya elimu na hii inaenda sambamba na ongezeko la shule za sekondari kwenye Kata zetu. Haya ni matokeo mazuri ya mpango wa MMES ulioweza kushirikiana na wananchi kujenga shule zetu za Kata nchini na kwa kweli tumepata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano kuanzia mwaka 2005, tulikuwa na shule za msingi 14,440, lakini sasa hivi tunazungumzia shule 15,816, hayo yote ni mafanikio ya elimu yanayotokana na mipango mizuri. Kwa upande wa sekondari hizi za "*O Level*" awali tulikuwa na shule 1,603, lakini baada ya kuongeza shule za kata sasa hivi tunazungumzia kuwa na shule 3,397, lakini kwa mipango hiyohiyo kwa sera ya kupanua shule za *A Level*, tulikuwa na shule za *A Level* 57 leo hii tunazungumzia kuwa na shule za *A Level* 543. Kwa hiyo, ni mafanikio ambayo tumeyapata na lazima tushirikiane, tuweze kuunga mkono jitihada hizi na mafanikio haya yote yanayotokana na mshikamano uliokuwepo kati ya Serikali na wananchi wake kwenye maeneo yao. Bado tutaendelea kusisitiza wananchi wajitokeza katika kuchangia mipango mbalimbali ya elimu ili tuweze

kuboresha sekta ya elimu na tupate mafanikio zaidi na hiyo sasa imesaidia sana kuongeza hata idadi ya wanafunzi ambao wanasajiliwa kwenye elimu ya msingi na sekondari, lakini pia hata vijana ambao wanaenda *A Level*, sasa ni wengi sana kufuatia mipango mizuri ya Serikali hii ili kuweza kupata matokeo mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu mwenzangu tumewasikiliza kwa umakini sana na sasa tumegawana kazi za kufanya. Mimi yako maeneo ambayo nitatoa ufafanuzi yale ambayo yanahusu Ofisi ya Waziri Mkuu na Naibu mwenzangu atatoa mchango wake na Mheshimiwa Waziri atakuja kukamilisha hoja zote ambazo tumeweza kuzipokea kutoka kwenu na kwa Serikali hii makini, tuko mbele yenu na mwisho tutakuja kuomba sasa tuweze kuridhia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili tuungane pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kama ambavyo mlivyopitisha bajeti yake tuweze kufanya kazi ya kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, jana tulipata mchango kutoka kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, pale alipozungumzia fedha nyingi inayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia makabrasha yake ambayo yanaonekana mbele yetu kwamba tumepeleka fedha nyingi lakini Ofisi ya Waziri Mkuu imerejesha fedha na hazikutumika na akaomba fedha zile sasa zirudishwe ziweze kuongeza miundombinu tuliyonayo badala ya kuwapa tabu wananchi kuchangia michango hiyo kwa ajili ya majengo hayo. Nataka nimwambie kitu kimoja kwamba fedha hizi tunapozionyesha kwenye makabrasha yetu kama fedha ambazo tumezitenga kuzipeleka kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kufanya kazi husika, si kwamba fedha zote ziko mahali na kwamba tunataka kuzipeleka zote, zinatokana na makusanyo ambayo *TRA* wanajitahidi kukusanya fedha zile na kadri zinavyopatikana na bajeti zinavyoonyesha tunazipeleka kulingana na makusanyo yetu. Sasa inaweza ika-*happen* mpaka mwishoni hatujakamilisha kupata fedha yote na kuipeleka, kwa hiyo, *deficit* si fedha ambayo imerudishwa tena ili kupunguza matumizi kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nililazimika nitamke hili ili pia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote ambao walikuwa hawajui utaratibu huu, waweze kufahamu kwamba ingawa tunasema tunapeleka shilingi milioni 400 kwa ajili ya maendeleo yetu lakini upelekaji wa fedha unakwenda kwa awamu, mara nyingi tumejiwekea utaratibu, huwa tunapeleka *quarterly* ili kufanya kazi zilizokusudiwa lakini kutokana na makusanyo hayo na jinsi ambavyo tunapeleka fedha hizi kwenye maeneo yale unaweza ukakuta tumemaliza kipindi, makusanyo hayakuweza kutosha kuweza kupeleka fedha zile, lakini si kwamba fedha zote zilipelekwa kwenye mamlaka halafu tukaziagiza kuzirudisha. Hata kama hilo lingefanyika, kama tunapeleka fedha hizi kwa Mkurugenzi na kama zitatakiwa kurudishwa au zimekaa kwa kipindi chote na hazijatumika lazima Mkurugenzi na wataalamu wake wa fedha wangezirudisha Hazina na kuzikatia risiti. Kwa hiyo, tungetegemea pia kupata risiti ya marejesho ya fedha hizo ili kuthibitisha kama zile fedha hazikutumika na badala yake zimerudishwa kwa shughuli nyingine ambayo sio rasmi. Kwa hiyo, nilitaka nitumie nafasi hii kutoa maelezo juu ya hili ili pia watu waweze kufahamu na tuweze kuungana pamoja ili kuhamasisha wananchi kuendelea kuchangia

miradi yetu kama ambavyo utamaduni wetu ulivyokuwa na huku Serikali ikiunga mkono jitihada hizi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, sisi tunapeleka fedha katika maeneo mawili. Tuna fedha ya ruzuku ya maendeleo ambayo inatumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwenye elimu, tuna fedha ambazo tunapeleka kwa ujenzi wa nyumba za Walimu, maabara, madarasa pia, lakini zote hizi tunaunga mkono jitihada za wananchi ambazo zinaendelea kwenye maeneo yetu. Tuna fedha ya uendeshaji, tunaita *capitation grant* ambayo tunaipeleka shuleni na kwa bahati nzuri mwaka huu viwango vya c*apitation* vimeongezeka. Kwa shule ya msingi tunapeleka *capitation* kwa kila mwanafunzi kwa shilingi 10,000/= lakini kwa shule za walemavu ni shilingi 20,000/= kama ambavyo Naibu Waziri asubuhi ametoa maelekezo na kwa sekondari sasa tumeboresha, tumezipandisha mpaka shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo ambalo linajitokeza kwenye eneo hili la ukosefu wa takwimu sahihi zinazoagizwa kwa Walimu Wakuu kwenye maeneo yetu, jambo ambalo tayari tumeshaliagiza na kuimarisha upokeaji wa Takwimu hizi ili tuweze kupeleka fedha sahihi kwa Wakuu wa Shule au Walimu Wakuu ili waweze kufanya matumizi ya fedha hizi. Katika hili, napenda pia kutoa ufafanuzi wa viwango vile ambavyo tumeviweka kwenye ile *capitation,* tumeigawa kwenye *percentage* ili Mwalimu Mkuu au Mkuu wa Shule aweze kutumia kama amavyo imekusudiwa. Kwa elimu ya msingi ile shilingi 10,000/- asilimia arobaini ya ile shilingi 10,000/- tuliyopeleka itamsaidia Mkuu wa Shule kununulia vitabu vile ambavyo anaona sasa ni muhimu kuweza kusaidia ili aweze kufundishia au kujifunzia na asilimia ishirini ni ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vile ambavyo anaona ni muhimu sasa kuweza kuvinunua. Halafu kuna asilimia ishirini nyingine itasaidia kufanya ukarabati mdogomdogo pale wa miundombinu ambayo ipo ili kuweza kuiweka imara badala ya kwenda kwa Mkurugenzi kuomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo mbalimbali. Tumetenga asilimia kumi kati ya zile kwa ajili ya mitihani ya ndani ya shule ya msingi na asilimia kumi nyingine inamsaidia kwenye utawala, anaitwa kwa Afisa Elimu, anaweza pia akakimbia haraka sana na kurudi. Huo ndiyo mgawanyo wa *capitation* wa shule za msingi kutokana na ile shilingi 10,000/- ya kila mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekondari, tumeigawa kwa asilimia hamsini. Asilimia hamsini ni kununua vitabu ambavyo vitamsadia yeye katika kufundishia na kujifunzia ambavyo yeye ana mamlaka pamoja na Bodi yake kwa pamoja ili aweze kuamua ni vitabu gani sasa vinatakiwa vinunuliwe kwa ushauri wa Walimu ili waweze kufanya matumizi na asilimia 50 ile ni vifaa mbalimbali lakini kama kuna vifaa vya maabara, kununua *chemicals,* kwa haraka sana ili *experiment* ziweze kuendelea inakuwa ni asilimia hamsini. Mgawanyo huu nao ulitakiwa na Mheshimiwa Masele, aliomba sana apate mgawanyo huu lakini pia Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yake sasa tutakuwa tumenufaika kujua mgawanyo wa fedha hizi unakuwaje.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lissu pia alitaka kujua baadhi ya Walimu wasiolipwa mishahara na Serikali inatoa tamko gani? Tatizo hili liko kwa Walimu wapya

lakini kwa sasa nataka niwahakikishie sehemu kubwa ya Walimu, zaidi ya asilimia tisini wanalipwa mishahara yao na tunakiri kwamba wale asilimia kumi wapo ambao hawajalipwa mishahara hiyo kutokana na matatizo mbalimbali. Utaratibu ambao Wizara ya Elimu na TAMISEMI unao, baada ya kumaliza mitihani imekubalika tunaajiri Walimu kiasi fulani, Walimu wote wanapangwa kwenye Wilaya mbalimbali nchini na tukishapeleka mgao wa Walimu kwenye Wilaya husika Walimu mia moja na fedha zote za stahili zao zinapelekwa kwenye Wilaya ile. Majina yanapotolewa kwenye mbao za matangazo na kwenye mtandao kwamba Mwalimu unatakiwa kwenda Wilaya fulani na fedha yako iko pale. Tatizo kubwa hapa, Walimu baadhi wanapopata taarifa ya kwenda kuripoti kwenye Wilaya hiyo hawataki kwenda kuripoti huko anataka akaripoti kwenye Wilaya nyingine. Akienda kuripoti Wilaya nyingine hawezi kupata mishahara mpaka arudi kwenye Wilaya husika ndiyo aweze kupata mishahara yake. Kwa hiyo, utakuta ucheleweshaji wa mishahara kwa Walimu wapya inatokana na hiyo kama sababu mojawapo.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili ni kwamba sasa hivi tuna utaratibu wa kujaza fomu ya Udhibiti wa Ajira ili kuachana na ajira hewa. Ile fomu maalumu utaijaza pale unaporipoti. Walimu wengine wanachelewa kwenda kuripoti, akichelewa kuripoti atachelewa pia na taratibu zote za kimsingi za kifedha ili kukamilisha kupata mshahara wake. Kwa hiyo, utakuta malalamiko ya Walimu yanayochelewa yanatokana na hilo. Tuna kesi moja ya Rungwe kule Mbeya, tuna Walimu wetu 22 mpaka leo walikuwa hawajapata mishahara yao. Tatizo lililojitokeza ni kwamba tulipokuwa tunapeleka orodha ya Wilaya ya Rungwe, iko ukurasa mmoja wa karatasi, hakuweza kwenda kule Rungwe kwa hiyo taratibu zilichelewa na Walimu wenyewe hawakupata taarifa mapema, hawa wote tunawatambua na taratibu zao zinaendelea na tunahakikisha kwamba wanapata mishahara yao kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Simbachawene Mbunge wa Kibakwe jana alitaka kujua hawa Walimu wa leseni walioruhusiwa kwenda masomoni. Mwaka 2007 tulipokuwa tunaaza utaratibu huu wa Shule za Kata, tulitafuta njia ya dharura ya kuweza kunusuru shule zetu hizi ili pia watoto wetu wapate kufundishwa na ndipo ambapo tuliamua kuchukua vijana wa Kidato cha Sita ambao tunaamini wana uwezo mkubwa wa kimasomo, maana kufundisha nako ni taaluma mpaka uwe na *methods* za kufundisha. Tulichofanya ni kwamba waliingia kwenye utaratibu wa kawaida kwenye mikataba na walikuwa wanapata asilimia themanini ya mshahara *basic* wa Mwalimu anayeanza ajira na hiyo ndiyo fedha ambayo walikuwa wanapata. Baada ya kipindi cha mwaka na miaka miwili, walilazimika wote waende vyuoni wakapate taaluma ya ufundishaji. Sasa eneo hili ndilo ambalo Mheshimiwa Simbachawene alikuwa anata kujua kwa nini tuliwapeleka masomoni.

Mheshimiwa Spika, Walimu hawa wanapokuwa kwenye mkataba, mikataba yao mwisho ni miaka miwili, zaidi ya hapo anakuwa sio Mwalimu. Kwa hiyo, lazima watafutiwe utaratibu wa kupata leseni ya kufundishia na ndipo ambapo tukaamua kuwapeleka vyuoni ili wakapate ile leseni ya kufundishia kwa kuhudhuria mafunzo ya Ualimu halisi. Kwa hiyo, pale ndiko ambako kulionekana kuna *gap* kati ya Walimu waliotakiwa kubaki shuleni na wale kwa sheria ile ilikuwa ni lazima kuwapeleka vyuoni.

Kwa hiyo, ndilo ambalo lilikuwa limejitokeza na sasa Walimu wale wameshapata taaluma hiyo na wako mashuleni wanaendelea kufundisha na waliingia kwenye ajira na wakiwa chuoni walikuwa wanaendelea kupata ile asilimia themanini kwa hiyo Serikali ilikuwa inaendelea kujali mchango wao ili waweze pia kufundisha.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanaojiendeleza kupangiwa vituo vipya. Mwalimu yoyote aliyetoka kazini, *in service training* lazima anapomaliza masomo anarudi kwenye kituo chake na Walimu wote ambao wanaanza ajira wanapokwenda kusoma kwenye kozi kama digrii, yule ndiye anapata fomu ya kujaza kituo ambacho angependa kwenda kuanza nacho na baada ya hapo Wizara ya Elimu inafanya *consideration* yake kwa ajili ya kuendelea na kazi ya Ualimu.

Mheshimiwa Godfrey Mbilinyi, jana alitaka kujua madeni ya wazabuni wa chakula katika Mikoa mbalimbali ikiwemo na Mbeya. Nataka nimhakikishie kwamba kulitokea tatizo kubwa la wazabuni wetu kwenye shule zetu za *boarding* ambazo zinalisha chakula lakini Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ilipita kila shule kufanya uhakiki wa madeni yale na tulilipa kwa kiasi kikubwa na tukawaagiza na tukawapa utaratibu Wakuu wa Shule namna ambavyo hawatakiwi kuzalisha tena madeni. Tumeshafanya uhakiki na madeni yote yameshalipwa. Kama kuna maeneo ambako bado tunatakiwa kulipa madeni na kuna tatizo hilo, tupeni taarifa ili twende na tumeshaanza kutuma Tume mbalimbali za kwenda kuhakiki madeni hayo ili tuweze kuwalipa wazabuni wetu waendelee kutoa huduma kwenye shule zetu za *boarding*.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Mbunge ambaye jana sikuweza kupata jina lake kwa haraka aliweza kuonyesha wasiwasi juu ya wanafunzi ambao tuliwaleta hapa na tukawapa zawadi kwamba inawezekana ni mchezo tu ambao Serikali ulicheza, kwa hisia zake kwamba wale vijana saba waliotoka kwenye shule za Kata sio jambo halisi. Mimi nasema hivi, Watanzania tujenge tabia ya kuaminiana. Serikali hii haiwezi kuleta kijana hapa ikamtafutia jina la Shule ya Kata kwamba ndiye aliyefaulu huku akiwa hajafaulu. Suala la mitihani linaratibiwa na Taasisi Maalum, Baraza la Mitihani na matokeo yake yanaratibiwa na wao. Sisi tulipopata majina, bahati nzuri vijana wetu kutoka Shule za Kata wame-*perform* vizuri, kwa hiyo lazima tujipongeze. Tushikamane katika kupongeza na kuunga mkono jitihada hizi ili Shule za Kata ziweze kufanya vizuri na mimi nawahakikishia shule hizi zinaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimefanya ziara Mkoa wa Ruvuma, nimeenda Shule ya Londoni ya Wasichana, wameweza ku-*perform* vizuri kwa asilimia 100. Nililazimika kwenda kuwapongeza na kuwaunga mkono na kuzungumza na Walimu na hapa sasa tunatafuta utaratibu wa kwenda kuwapongeza Walimu wale kwa kuwafaulisha vijana wale wa Kidato cha Sita kwa asilimia mia moja. Hizo ndizo jitihada za Serikali. Kwa hiyo, tuungane Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuzipa nguvu shule hizi ili ziweze kuongeza uwezo.

Mheshimiwa Spika, changamoto yetu ni kuongeza Walimu na nilishasema mara nyingi hapa kwamba sisi tunaweza ku-*cover* Walimu, *by* mwaka 2013 tutakuwa tumefikia zaidi ya asilimia themanini na tano na nimeweka hiyo kwa sababu najua kuna

dharura, kuna matatizo mengine sasa hivi kwenye shule za msingi mahitaji yetu sisi ni Walimu 214,468 waliopo ni 167,000, upungufu ni Walimu 46,000 lakini kwenye sekondari mahitaji yetu ni Walimu 81,800, waliopo 44,000 upungufu ni Walimu 37,000. Mwaka huu kama Walimu wote waliomaliza kozi zao watafaulu vizuri, tunakusudia Walimu 19,000. Tukifanya mara mbili, tatu tuna-*cover*. Kwa hiyo, hatuna shida ya Walimu, tunaamini shule zetu zote zitapata Walimu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, msiwe na mashaka popote mlipo, tutaweza kushirikiana vizuri katika ku-*cover* upungufu wa Walimu uliopo. *Seriousness* ipo na tutahakikisha kwamba jambo hili linaweza kumalizika vizuri.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo mimi nilitakiwa kuchangia ni haya kwa sababu Naibu Waziri atakuja hapa kuja ku-*cover* maeneo yote ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge lakini mwisho Mheshimiwa Riziki Omar Juma jana alitoa mchango wake hapa wa namna ambavyo tunadharau kuboresha sekta mbalimbali ikiwemo na Vituo vya Walimu kwa ajili ya kuendeleza Walimu na akaonyesha jarida ambalo lilionyesha Kituo cha Walimu kilichoholela kule Rufiji, nasikitika sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Marombwa jana alikataa na mimi nakataa kwa sababu nimewahi kuwa Mkuu wa Wilaya pale na tarehe 14 Mei, 2010, mimi nilikuwa Bungu kufanya kikao cha Walimu madarasani, wote tukiandaa mpango thabiti wa kuweza kuwafanya Walimu waweze kufanya vizuri ikiwemo kufanya zile kozi za kupitia mada mbalimbali. Tatizo pale Bungu hakuna Kituo cha Walimu na mimi mwenyewe ndiye nilipendekeza kwamba moja kati ya darasa la shule ya msingi pale litumike kama Kituo cha Walimu ili Mratibu wa Kituo cha Walimu aweze kukutana na Walimu pale kujadili mada mbalimbali. Nilishtuka kuona picha na nilipoiangalia ile picha, sijui wale ndugu zetu wa HakiElimu waliitoa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini Mkurugenzi wa HakiElimu yuko hapa, hebu tushirikiane katika kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuboresha miundombinu. Jambo hili linawafanya Watanzania waone kwamba Serikali haifanyi jambo lolote. Hii picha nadhani Mkurugenzi anaweza kuifuatilia aone yule mpigapicha aliitoa wapi na kuja kuiweka kwenye gazeti. Jambo hili linatuhuzunisha, tuungane pamoja kuunga mkono jitihada hizi na kama tunatoa jambo liwe la kweli ili pia tuweze kuendelea na kushikamana vizuri na tuweze kuendelea na taarifa zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu umeniishia, nimepata marekibisho na jina la Mheshimiwa Mbilinyi, yeye ni Joseph Mbilinyi na sio Godfrey. Kwa hiyo, atambulike kwa jina la Joseph Mbilinyi. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimemkopesha muda wangu. Waheshimiwa Wabunge kama tulivyosema asubuhi, saa saba na nusu kutakuwa na uzinduzi wa maabara inayotambea yaani *Mobile* Maabara. Waziri Mkuu atakuwa Mgeni Rasmi, kwa hiyo, atakayekuwepo *around* anakaribishwa pale kwenye viwanja vyetu vya maonyesho ndipo shughuli hiyo itafanyika.

Mimi binafsi sina jambo lingine la kutangaza, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.53 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge asubuhi, tulikuwa tumepanga kwamba mchana huu utatumika kujaribu kufafanua hoja na kuingia kwenye Kamati ya Matumizi. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia afya njema ya kuniwezesha kusimama leo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa imani yake kubwa aliyoionyesha kwangu, kwa kuniamini na kuniteua kwa nafasi hii ya Naibu Waziri katika Wizara hii. Napenda kumuahidi kwamba nitajitahidi sana kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonisaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Songwe, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana tena za kishindo na kwa kupita bila kupingwa na kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia kwa kazi za maendeleo Jimboni. Nami naahidi kuwatumikia ili kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru mke wangu mpenzi Elizabeth Kirigha Mulugo, watoto wangu Nickson, Menrad na Maurine, kwa uvumilivu wao mkubwa wakati wote nisipokuwepo nyumbani. Pia nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipomshukuru sana Dereva wangu Bwana Msafiri Mkuyawa, kwa ushirikiano anaonipa kwa kunifanikishia safari zangu na kulinga uhai wangu. Mungu ampe afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa ushirikiano mkubwa wakati wote anaonipa pale Wizarani. Mimi kama Naibu Waziri kwa mara ya kwanza, namshukuru sana kwa ushirikiano anaonipa na nimejifunza mengi kutoka kwake kwa kipindi hiki kifupi. Aidha, napenda kuwashukuru Katibu Mkuu Prof. Hamis Omar Dihenga, Naibu Katibu Mkuu Celestine Muhochi Gesimba, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Taasisi za Elimu kwa ushirikiano wao wanaonipa pale Wizarani.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, napenda nikupongeze kwa mara nyingine tena wewe binafsi kama mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa Spika katika Bunge hili. Pia, nataka kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa

kuchaguliwa kwake kushika nafasi hiyo. Aidha, napenda kumpa pole kwa kufiwa na mlezi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwake kwa awamu ya pili kuliongoza Taifa letu hili la Tanzania. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Peter Pinda kwa umakini wake alionao katika kusimamia shughuli zote na nyingi sana za Serikali hii. Aidha, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wenzangu wote kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Napenda pia niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa katika Majimbo yenu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mizuri na iliyosheheni busara, hekima na changamoto. Aidha, siyo rahisi kujibu kwa kina na utoshelezi hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi. Tunaahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuzituma kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia.

Mheshimiwa Spika, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zilikuwa zimelenga katika kuelekeza namna bora zaidi ya kushughulikia masuala ya elimu kwa wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa basi, naomba nijikite katika kujibu hoja mbalimbali zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakijadili hoja iliyo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hoja, nikianza na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, alikuwa anataka kujua nafasi zinazokaimiwa kwa muda mrefu pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Namjulisha tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za kujaza nafasi zimeshawasilishwa kwenye mamlaka husika, kwa sababu namna ya kuwapata Wakurugenzi upo utaratibu maalum wa Kiserikali ambao unafanywa. Sisi kama Wizara tayari tumeshapeleka mapendekezo kwenye mamlaka husika na tunategemea wakati wowote tutapata majina ya uteuzi wa Wakurugenzi wetu pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki angependa kujua kwa nini Walimu wasipewe mikopo ya vyombo vya usafiri ili viwasaidie katika kazi za kila siku. Hoja hii ni kwamba, utaratibu wa mikopo unategemea uwezo na uamuzi wa mtumishi mwenyewe. Aidha, mtumishi anatakiwa abakiwe na si chini ya theluthi moja ya mshahara wake baada ya kukatwa makato. Hivyo basi, kutokana na kuwepo kwa taasisi nyingi za fedha, Wizara yangu imekuwa ikiidhinisha mikopo kwa Walimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Hivyo, nashauri Walimu wote pamoja na watumishi wengine Serikalini, waombe mikopo kulingana na uwezo wa vipato vyao (mishahara yao). Benki zetu ziko tayari na hasa Benki za *NMB, CRDB, NBC* na Benki zingine.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kujikita kujibu hoja ya Mheshimiwa Antony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo, yeye alitaka kujua kwamba baadhi ya Walimu

wanaomba ruhusa ya kwenda kusoma kwa kujiendeleza na waajiri wamekuwa wagumu sana kutoa ruhusa hizo kwa Walimu hao wanapotaka kwenda kujiendeleza. Nataka tu niseme kwamba taratibu za Utumishi wa Umma zinaeleweka. Pale wanapotoa ruhusa za kwenda masomoni, wanatoa bila ubaguzi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunakuwa tunapata matatizo ya upungufu wa Walimu kwenye shule zetu za Kata. Unapofanya ziara, unakuta shule ile ina Walimu 30, ina Walimu 20 lakini nusu ya Walimu wamekwenda kusoma. Taratibu zinasema kwamba angalau basi Mwalimu afike pale kituo cha kazi, akikaa angalau miaka miwili mpaka mitatu, anaweza sasa akapata ruhusa ya kwenda kusoma lakini, nataka tu nitoe masikitiko yangu kwamba kuna baadhi ya Walimu wakifika maeneo ya kazi hawawezi kuomba hata ruhusa kwa Mwalimu Mkuu, hawawezi kuomba ruhusa hata kwa Mkurugenzi, wanaandika barua na vyuo vinawadahili na wanakwenda kusoma. Sasa, anaporudi kwenye kituo chake cha kazi kwa mwajiri ambaye ni Mkurugenzi anakuta ameshamwandikia barua ya kusimamisha mshahara, inakuwa ni tatizo na hawa Walimu wanaanza kusema kwamba labda Serikali inatunyanyasa.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mwito kwa Walimu wote nchini au na wafanyakazi wengine wa Serikali kwamba wafuate utaratibu wa kuandika barua kuomba ruhusa kwa mwajiri ili waweze kupata ruhusa ya kwenda kusoma. Kwa sababu yule mwajiri atakuwa anaangalia ikama ya Walimu maeneo husika, kwa sababu sidhani kama Mkurugenzi wa Wilaya atatoa ruhusa ya kwenda kusoma wakati kituo kina Walimu watatu, wanaondoka Walimu wawili, Mwalimu mmoja anabaki ambaye yeye ndiye Mkuu wa shule, nadhani Mkurugenzi hawezi kufanya kazi kama hiyo. Kwa hiyo, nawashauri tu Walimu wafuate utaratibu, hawatapata matatizo na kama ilivyoelezwa kwamba waajiri ni wagumu, siyo waaajiri bali Walimu wetu wafuate utaratibu na siyo Walimu tu na wafanyakazi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, angependa kujua Walimu wanaohitimu, angependa kwamba zoezi hili la ajira lifanyike mara moja. Namthibitishia Mheshimiwa kwamba Walimu wote waliohitimu na kufaulu, watapangiwa vituo vyao vya kazi mara baada ya bajeti ya mwaka 2011/2012 itakapokamilika. Hata katika uzoefu wa huko nyuma, ni kweli Serikali, kupitia Wizara hii ya Elimu ina bahati kubwa sana kwamba Idara ya Walimu ndiyo wanaajiriwa baada tu ya kumaliza mafunzo, Serikali inathamini sana upungufu wa Walimu kwenye shule zetu. Kwa hiyo, wanapata ajira moja kwa moja. Hata watakaohitimu mwaka huu ilimradi wakifaulu, Serikali inaahidi kwamba itawaajiri hata kama watakuwa namba kubwa. Hata mwaka jana tumeajiri Walimu 9,226 na mwaka huu tunategemea angalau kuajiri Walimu kuanzia 15,000 mpaka 16,000 ili waende huko kwenye Shule zetu za Kata wakapigane na masuala ya elimu. Baadhi ya Walimu wanalalamika kwamba hawajaajiriwa. Wale Walimu hawakufaulu mitihani yetu, walipata *supplementary*, kwa hiyo tukaagiza kwamba wafanye mtihani na tarehe 4 Aprili, 2011 walifanya *supplementary* zao na majibu yameshatoka, tunasubiri tu kuwapangia vituo waje wajumuishwe na hawa ambao tutawaajiri mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, wawe na amani huko wanakonisikia kwamba wataajiriwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, anasema somo la Kiingereza liwe somo la kufundishia katika ngazi ya elimu ya msingi. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 1995, shule za msingi zilizopo nchini hutumia lugha ya Kiswahili kwa shule za msingi za Serikali na Kiingereza kwa shule zisizo za Serikali ambazo ni chache sana. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatumia lugha ya Kiswahili kwa kufundishia masomo ya awali na shule za msingi lakini somo la Kiingereza linasimama kama somo. Naomba tu Mbunge aelewe hivyo, iko kwenye Sera yetu ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Nyambari Nyangwine Chacha, angependa kuelewa elimu ya biashara kama inafundishwa katika shule zetu ili kuwawezesha vijana wamalizapo masomo waweze kujitegemea. Tena Mheshimiwa Nyambari ni mtunzi mzuri tu wa vitabu, anaelewa mambo haya na naona yeye mwenyewe anatunga vitabu hata vingine vya kilimo, vya sayansi, vya biashara. Namhakikishia kwamba elimu ya biashara inafundishwa katika shule za michepuo ya biashara kwa lengo la kuwawezesha vijana kujitegemea wanapomaliza masomo yao. Hata hivyo michepuo ya ufundi, kilimo na sayansi, hayo masomo hufundishwa katika baadhi ya shule za sekondari nchini. Michepuo yote ni muhimu kwa maendeleo ya wanafunzi kwani huwawezesha wamalizapo shule kuweza kujitegemea. Tunapokuwa tumeweka masomo kama ya kilimo kwenye sekondari, lazima kwenye vitendo utakuta shule hiyo ya mchepuo wa kilimo kuna mashamba, kumbe watoto wanapata fursa ya kwenda kujifunza namna ya kujitegemea, namna ya kulima. Hata katika shule za ufundi kama pale Mbeya, shule za Iyunga na pale Mwanza shule ya sekondari ya Bwiru Boys, nadhani ni shule za ufundi na shule zingine zilizopo kwenye Mikoa yetu. Kwa hiyo, unakuta pana vifaa pale, wanafunzi wanafanya *practical* kabisa ya masuala ya ufundi. Kumbe, hata wakitoka pale wanakuwa wamepata hiyo kada ya ufundi katika maisha ya kujitegemea huko nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mbunge wa Chakechake angependa kujua, Serikali ina mpango ani wa kuanzisha shule za michezo ili kupata wachezaji wenye vipaji watakaosaidia kuongeza kipato na kutoa ajira kwa vijana hasa mpira wa miguu. Majibu ni kwamba, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa, imeagiza kila kanda ya elimu ijenge shule mbili za michezo; moja kwa shule za msingi na nyingine kwa shule za sekondari. Nawapongeza sana Kanda ya Kati, Dodoma, tayari shule ya msingi Unyankuni na Shule ya Sekondari Mandewa zinaendelezwa kufundisha masuala ya michezo. Mfadhili tayari amepatikana na ametoa shilingi milioni 60 za kuanzia. Tuwapongeze sana Kanda ya Kati kwa kuanza programu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeamsha ari ya michezo shuleni na hivi sasa mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA yanafanyika. Wote ni mashahidi kwamba tayari mwezi huu wa Julai mwanzoni nadhani mliona pale Kibaha pana mashindno ya UMISETA na UMITASHUMTA kwa shule za msingi na sekondari. Kwa hiyo, sera hii tunaitekeleza, mambo yanakwenda vizuri sana. Aidha, sekta binafsi zinajenga shule za michezo kama vile *Baden Powell* kwa kutoa msaada wa kuendeleza michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mbunge wa Morogoro Mjini. Yeye anapenda kujua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa nini haijaruhusu elimu ya uzazi wa mpango kwa wanafunzi wa shule za msingi. Elimu ya afya hufundishwa kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi vyuo vya ualimu. Kwa ngazi ya elimu ya msingi, elimu hii inafundishwa katika somo la sayansi kuanzia darasa la tano.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kutoa ufafanuzi kwamba Elimu ya Msingi ni kuanzia Elimu ya Darasa la Kwanza mpaka la Saba lakini kwa somo hili la Uzazi wa Mpango tusingeweza kuanzisha kwenye Darasa la Kwanza, Darasa la Pili, Darasa la Tatu mpaka la Nne kwa sababu wale vijana wanakuwa bado ni wadogo, tunakuwa tunawapotezea akili fulani angalau kijana wa Darasa la Tano anaweza akaanza kupata utambuzi fulani, na vijana wengine wa Darasa la Tano wanakuwa angalau wamevunja ungo, kwa hiyo wanaweza wakapata elimu hii vizuri sana. Kwa hiyo, huwa tunaanzia kwenye Darasa la Tano, la Sita na la Saba na hata kule Sekondari kuna Masomo ya Bailojia na mengine wanajifunza elimu ya uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum Mbeya, angependa kujua Serikali ina mpango gani kudhibiti ada katika shule za watu binafsi. Serikali ilikwishatoa Waraka Na.19 wa mwaka 2002 unaoweka ukomo wa ada katika shule zisizo za Serikali ili kudhibiti gharama za uendeshaji wa shule hizo. Kwa kuwa gharama za maisha sasa zinapanda, Wizara iko kwenye mchakato wa kutoa Waraka mwingine ambao utazingatia gharama ya kila mwanafunzi *(unit cost).* Waraka utakapokamilika, utasambazwa kwa wadau wote nchini. Nataka tu kusema kwamba sasa ni miaka yapata 11 toka shule zisizo za Serikali zilipopangiwa kulipa ada 150,000/= kwa shule za *day* na 350,000/= kwa shule za bweni lakini mpaka sasa na ndiyo maana unakuta kuna uholela, kila mtu sasa anaweza ku-*charge*. Serikali imeliona hilo, imeingilia kati na iko kwenye mchakato sasa wa kuweka viwango maalum kwa ajili ya ulipaji ada kwa shule hizo baada ya kupata *unit cost* kwamba chakula ni gharama hii kutokana na maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, yeye ameongelea uhaba mkubwa wa vitabu vya kiada na tofauti kati ya shule na shule. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia *EMAC* ilitoa orodha ya vitabu vya kiada viwili vilivyopendekezwa kutumika ili kuwepo na uwiano. Lengo ni kuwa na vitabu vya kiada vinavyoweza kutumika katika shule zote kwa usawa. Maana hapo kwanza tulikuwa na vitabu vingi sana, lakini tunamshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizara ya Elimu, akatoa ushauri wake kwamba angalau tungekuwa na kitabu kimoja au viwili vya kiada. Vitabu vya ziada vinaweza vikawa vingi tu, lakini vya kiada, vya Mwalimu kufundishia darasani basi angalau kiwe kimoja au viwili, basi ikaamuliwa kwamba angalau viwe viwili. Kwa hiyo, zoezi hilo linaendelea kwa baadhi ya madarasa kama Darasa la Sita na la Saba.

Mheshimiwa Lucy Mahenga, Mbunge wa Viti Maalum angependa kujua shule za msingi na sekondari katika baadhi ya Halmashauri kuitwa majina ya baadhi ya viongozi au baadhi ya watu ambao wanakuwa wanatoa misaada kwenye shule hizo na kutaka au

kulazimisha shule hizo ziitwe kwa majina yao. Hapa, Mheshimiwa Lucy ana maana kwamba, kwa mfano, mimi kule kwetu Chunya nakwenda, naweza nikatoa msaada wa mifuko 100 ya *cement* katika shule fulani, basi Kata au Halmashauri wakataka kunienzi wakaiita Mulugo *Sekondary School* au mtu mwingine kwa sababu labda mimi yawezekana ni Naibu Waziri wa Elimu, lakini kwa wadau wengine, hapa Mheshimiwa Lucy angependa kupata tu ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka tu niseme kwamba tulichukue, sisi kama Serikali tukaone namna gani Halmashauri wanatumia vigezo gani vya kuangalia. Mfano tukienda pale Dar es salaam kuna shule zinaitwa Reginald Mengi Shule ya Msingi, yawezekana kwa namna moja au nyingine labda ni mdau au ni Mwenyekiti wa Bodi au alichangia sana katika ile shule mpaka kuwepo lakini vilevile tumelichukua, tuangalie tuzishauri Halmashauri kwamba wanatumia vigezo gani labda mpaka kubatiza majina fulani hasa shule zetu za Kata, zimekuwa na majina ya watu binafsi zaidi. Tungependa kutokuua uzalendo wetu, basi majina yale ya Kata au Kijiji, mimi binafsi ningependa iwe hivyo kwamba shule inaitwa, kama ni Kata ya Kapalala, unasema Kapalala *Secondary School*, Igunga, tunasema *Igunga Secondary School*, *Monsa Secondary School*, kuliko labda kutumia majina binafsi lakini hatutaacha kuwaenzi viongozi wetu wakubwa, Marais, Mawaziri Wakuu, Makamu wa Rais na wengine ambao wanaweza wakawa na mchango mkubwa katika Taifa letu, akina Kawawa, akina Nyerere, akina Mzee Warioba. Wapo sasa hivi akina Mzee Pinda hapa, hatuwezi kuacha kuita Pinda *Secondary School*, tutaendelea kuwaenzi viongozi wa namna hii na hasa wanapofanya kazi za Serikali vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu hoja kubwa ambayo inategemewa sana na Wabunge na hata wananchi kwa ujumla kwamba ni namna gani migomo inakuwepo Vyuo Vikuu na namna gani Serikali imejikita kumaliza migomo hii. Watu wanaposika kwamba vijana wamegoma Vyuo Vikuu daima tunapata picha moja kwa moja kwamba labda tatizo ni Bodi ya Mikopo, lakini mpaka mgomo unatokea au kasoro yoyote inatokea katika uendeshaji wa Vyuo Vikuu, kuna vitu fulani vipo katikati kutegemeana na Taasisi husika. Vitu hivyo ni pamoja na makosa ya wanafunzi katika ujazaji wa fomu, kuna vyuo vyenyewe katika utaratibu wa kutoa matokeo, Bodi ya Mikopo yenyewe, Hazina na *TCU*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vipengele muhimu, Wabunge kama 18 waliuliza kwamba sababu gani Serikali inaruhusu au kitu gani kinatokea kwenye Bodi ya Mikopo mpaka watoto wanagoma. Hizo ni changamoto za kiutendaji, napenda tu kuzitaja kwa harakaharaka. Kuna ucheleweshaji wa kujaza fomu za maombi na kuziwasilisha Bodi kwa wanafunzi wetu. Hapa nataka tu kutoa wito kwa Wabunge na wengine wote wanaonisikiliza kwamba tukirudi Majimboni, wale vijana ambao wameshafanya mitihani ya Kidato cha Sita, wanasubiri kwenda kujaza fomu, basi sisi ambao tunaweza kuwa tunaufahamu utaratibu wa kujaza fomu tuwaelekeze, kwa sababu wapo vijana wengine hata kutumia *internet* bado hawajui kwa vile shule zingine zipo vijijini, lakini tunatoa kwenye magazeti, kwenye mabango mbalimbali hata kwenye *internet* utaratibu wa namna ya kujaza fomu. Angalau mwaka huu tumeboresha kwamba wanafunzi wanajaza fomu kwa kutumia *Central Admission*, ni muundo mzuri sana, mwisho ilikuwa tarehe 30

Juni, 2011. Nawahakikishia Wabunge kwamba mwaka huu hatujapata matatizo hayo. Vijana wetu wengi waliokuwa wamefaulu na wanasifa za kwenda Vyuo Vikuu wameshajaza fomu, nadhani hawawezi kujitokeza tena wenye tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingine ya ujazaji holela wa fomu za maombi ya mikopo kwa wanafunzi. Vigezo vya mtu kupata mkopo kwenye Bodi ya Mikopo vinaeleweka, kama ni mwanafunzi amefaulu kwa kiwango cha *Division One* na *Division Two*, nawaelezea utaratibu ulivyokuwa nyuma japo sasa hivi kuna vigezo vingine vimebadilika ambavyo nadhani muda si mrefu, kama Tume ya Rais iliyoundwa, Wabunge mtakuja kupata taarifa ni namna gani mwaka huu tumetumia vigezo vya kutoa mikopo. Huko nyuma ilikuwa kwamba *Division One* na *Division Two* wanapata mkopo hata kama anasoma *faculty* yoyote, lakini kwa wanaopata *Division Three,* tunaangalia wale wanaokwenda kusoma Ualimu ama Sayansi. Unakuta mtu amepata *Division Four* au *Division Three* naye pia anajaza fomu, anaomba mkopo, kwa hii kidogo ilikuwa inaleta matatizo kwa vijana kutokuelewa lakini tuliwashauri watu wa Bodi kwamba sasa hivi waweke mfumo angalau vijana hawa wanapokuwa Kidato cha Sita, waweze kupata semina na maelekezo fulani, tutume kwa Wakuu wa shule kabla vijana hawajaenda Vyuo Vikuu basi wapate uelewa wa mambo haya, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile wanafunzi kukataa au kuchelewa kusaini *returns* za fedha zinapotumwa Vyuoni, hii imejitokeza hata wiki iliyopita pale chuo cha *DUCE*. Vijana wanasema hatuwezi kusaini fomu kwa sababu hatujaziona fedha. Ni wanafunzi wengi sana ama wanakataa, ama wanachelewa kusaini zile *returns* wanazokopeshwa kupitia Vyuo vya Ualimu. Ada inayotolewa na Bodi ya Mikopo inakwenda kwenye Akaunti ya Chuo, lakini zile fedha zingine za chakula na malazi ndiyo zinakwenda kwenye akaunti ya mwanafunzi. Naipongeza Serikali kwamba mwaka huu imetukubalia ombi la kuongeza kiasi cha fedha kutoka shilingi elfu tano hadi kufikia shilingi elfu saba, sasa hizi fedha ndizo zitakazoingia kwenye akaunti ya mwanafunzi lakini pesa ya ada haiwezi kuingia kwenye akaunti ya mwanafunzi, inaingia kwenye Akaunti ya Chuo. Kwa hiyo, naomba wanafunzi wawe na imani na Vyuo, wanapowaletea zile karatasi za kusaini, ni lazima wazisaini, kwa sababu Mdhibiti na Mkaguzi wa Fedha anataka kuona kwamba hizi fedha zimefika kweli kwenye akaunti na wanafunzi wameridhika kwamba wamepata, ndiyo maana ni lazima wasaini.

Mheshimiwa Spika, inawezekana huko nyuma fedha zilikuwa zinaingia kwenye Akaunti ya Vyuo halafu matumizi yake yanabadilika na wanafunzi wanafukuzwa kwamba labda hawajalipa ada, kwa hiyo tunaomba wanafunzi watuamini. Pale Chuo cha Ualimu Chang'ombe kulikuwa na mgomo lakini tulipowaelewesha, wakaelewa na wakaridhika. Ndiyo maana sasa hivi tunasema kwamba tutakuwa na mafunzo elekezi.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri, mengine yaliyobaki mtayaandika.

## T A A R I F A

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri akiendelea kuhitimisha hoja, amesema kwamba kiwango cha pesa kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu kimebadilika kutoka shilingi elfu tano kwenda shilingi elfu saba. Jana ilitamkwa kwamba ni shilingi elfu saba na mia tano, naomba kujua msimamo wa Wizara.

**SPIKA**: Mheshimiwa Mbunge ni shilingi elfu saba na mia tano *it is a slip of the tongue,* tunaendelea na mtoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa jinsi ambavyo umesimamia vizuri majadiliano ya Bajeti ya Wizara yangu, hekima busara na upeo wako mkubwa wa kiuongozi ambao umeutumia katika kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano haya, umeonesha jinsi gani Chama cha Mapinduzi kilivyo na hazina kubwa ya viongozi katika ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu pia kwa Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mwenyekiti wa Bunge ambaye amesimamia majadiliano ya hoja yangu jana kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa, yote yanalenga katika kuinua ubora wa utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi nchini.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya Hotuba ya Serikali na ya Ofisi ya Waziri Mkuu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 105 walitoa michango yao kuhusiana na sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wakati wa majadiliano ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 43 walitoa maoni yao kwa mdomo na kwa maandishi na wakati wa majadiliano ya Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Wabunge 62 walichangia kwa mdomo na kwa maandishi. Maoni hayo yalihusu maeneo mbalimbali kuhusu namna bora ya kuendeleza na kuendesha sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa bajeti hizi kuhusu Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yalihusu maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, michango hiyo ilihusu eneo la Elimu ya Juu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Elimu ya Msingi na Sekondari na pia Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nitatoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo yaliyojitokeza wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao waliyoitoa kwa maandishi na kuchangia kwa mdomo hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Michango hii mizuri iliyojaa busara itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii pamoja na kuboresha Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Wabunge waliochangia hoja ya bajeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Nyambali Nyangwine, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Munde Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Dokta Lucy Nkya, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mheshimiwa Seleman Jafo, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Amos Makala, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Josephat Kandege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia katika hotuba ya Waziri Mkuu ni hawa wafuatao, naomba niwatambue. Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Dokta Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Suzan J. Lyimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa January Yusuph Makamba, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mheshimiwa

Said Suleiman Said, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Moshi Kasoko na Mheshimiwa Neema M. Hamid. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Kurthum Jumanne Mchuchuli, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Rita Kabati, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu, Mheshimiwa Agnes Hokororo na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuwatambua Wabunge waliochangia hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuzungumza ambao ni 31 na kwa maandishi Wabunge 161 kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Anthony Mbassa, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Prof. Peter Msolwa, Mheshimiwa Riziki Juma, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Margreth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Said Bwanamdogo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa na Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, orodha ya Wabunge waliochangia katika hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Maandishi, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Omar Nundu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Capt. Damian Komba, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Joseph Chagula, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Eng. Athuman Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Nasib Suleman Omar, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Amos Makala, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Margraret S. Sitta, Mheshimiwa Fatuma A.

Mikidadi, Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Aggrey Mwanry, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga, Mheshimiwa Suleiman Said Jafo, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye, Mheshimiwa Munde Tambwe, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Daina Chilolo, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Juma Sululu Juma, Mheshimiwa Kombo K. Kombo, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, Mheshimiwa Hussein Mzee, Mheshimiwa Mch. Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Naomi Kaihula. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Thuwayba Mohammed, Mheshimiwa Salim Khamis, Mheshimiwa Ali Seif, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa Rajab Mohamed, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Sylvester Koka, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Mwanamrisho Abama na Mheshimiwa Rita Kabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Kurthum Mchuchuli, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Waride B. Jabu, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Seleiman Zedi, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Prof. Peter Msola, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu na Mheshimiwa Fakharia Shomar.

Mheshimiwa Suzan A. Lyimo, Mheshimiwa Dr. Titus Kamani, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu, Mheshimiwa Dokta Augustino Mrema, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Raya Khamis, Mheshimiwa Agripina Buyogera,

Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Moza Saidy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Dokta Abdulla Juma Saadalla, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Dokta Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa Hamad Mohamed, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Betty Machangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina taarifa ya Waheshimiwa Wabunge ambao nimewasahau kuwatambua na huyu ambaye amechangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu naye ni Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. Naomba nichukue nafasi hii pia kwa ridhaa yako kuomba radhi wale wote kwa namna moja au nyingine nimekosea kutamka majina yao kwa sababu naona maandishi hayakwenda sawa na wakati mwingine nimetamka vile ambavyo imeandikwa, naomba radhi sana.

**SPIKA:** Saa moja inaanza sasa hivi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua wachangiaji hao naomba sasa kuzungumza yafuatayo kwa kuanza na maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii. Naomba sasa nianze kutoa maelezo ya maoni hayo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Margaret S. Sitta. Maoni ya Kamati yamezingatiwa na naomba nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuimarisha Elimu ya Watu Wazima nchini. Naomba kutoa ufafanuzi kwamba Serikali imechukua hatua za makusudi za kuimarisha elimu ya watu wazima nchini kwa kurejesha Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya mfumo rasmi katika Mfumo wa Wizara tangu mwaka 2008, sasa tuna idara nzima Wizarani.

Mheshimiwa Spika, pili, kuanza kutekeleza mpango wa Mradi wa Ndio Ninaweza kwa lengo la kufuta ujinga kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba. Mpango huu unaanza kutekelezwa rasmi katika mwaka huu wa fedha. Kwa kupitia mpango huo tunataka tuupige vita kabisa ujinga nchini mwetu ili tuondokane kabisa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunapanua na kuimarisha mpango wa elimu ya msingi kwa waliokosa elimu hiyo ama MEMKWA. Hili tutalitilia mkazo sana katika kipindi cha

mwaka huu wa fedha ili kwa pamoja na mipango mingine tuhakikishe kwamba, ujinga tumeutokomeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nne, pia tunapanua mpango wa elimu masafa na elimu ya ana kwa ana ili kutoa fursa ya kupata elimu ya sekondari kwa vijana walio nje ya shule. Mpango huu unatekelezwa kupitia taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ya Kamati kwamba, Serikali irudishe posho maalum kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Serikali imekamilisha rasimu ya sera ya malipo ya mishahara na motisha katika utumishi wa umma ambayo itazingatia pamoja na mambo mengine kuboresha maslahi ya watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu kama vituo katika maeneo ya kazi. Aidha, katika MMES awamu ya pili, chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, Serikali imepanga kutoa *settling allowance* au posho ya kujikimu ya jumla ya shilingi 500,000 kwa wale watakaopelekwa kufanya kazi katika maeneo ambayo yataainishwa kuwa ni maeneo yenye mazingira magumu kuanzia mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuanzia mwaka huu wa fedha, walimu wote ambao tutawapeleka katika maeneo yale ambayo tutayaainisha kwamba, yana changamoto maalum kama ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezitaja hapa. Tutafanya utaratibu maalum kati ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunatambua maeneo halisi yale yenye changamoto maalum ili walimu wanaokwenda katika maeneo yale tuhakikishe kwamba *settling* yao inakuwa ni *settling* ambayo imesaidiwa. Fedha zipo tumezitenga tutazisimamia tuhakikishe kwamba zinalipwa bila ya bugudha na bila ya matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, chini ya mpango huo kwa kuanzia nyumba za walimu 1200 zimepangwa kujengwa katika maeneo hayo. Nyumba 1200 tunataka tuzijenge katika maeneo hayo ili walimu watakapokwenda katika maeneo hayo waweze kufikia angalau katika nyumba ambazo zina heshima waweze kukaa katika nyumba hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizifafanue nyumba hizi 1200, ni kwa mtindo ule wa *duplex* yaani nyumba moja kwa nyumba mbili. Kwa hiyo, kwa maana nyingine tunajenga nyumba za familia 2400 kwa kuanzia. Aidha, naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri kuweka utaratibu ambao utawawekea mazingira ya kuvutia walimu ambao watapelekwa katika maeneo hayo. Hizi ni hatua za mwanzo za Serikali na za nia thabiti, lakini haziwezi kushinda nia na juhudi thabiti za Halmashauri zenyewe kuhakikisha kwamba zinafanya kila ambalo liko katika uwezo wao kuhakikisha kwamba mazingira yale yanaboreshwa yawe mazuri zaidi na ya kuvutia kwa ajili ya walimu ambao wanakuja kuishi katika changamoto hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ya Kamati, ni ugatuaji wa Elimu ya Sekondari. Utaratibu wa ugatuaji wa Shule za Sekondari ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, mwaka 2009. Ugatuaji uliofanyika ulihusisha usimamizi na uendeshaji wa kila siku wa shule za sekondari katika ngazi za Halmashauri. Usimamiaji wa shughuli za

siku hadi siku wa shule hizi unasimamiwa katika ngazi ya Halmashauri. Aidha, rasilimali zinazohusiana na uendeshaji na usimamizi wa shule hizo ikiwemo rasilimali fedha na rasilimali watu zinakasimiwa katika bajeti za Halmashauri. Kamati ya pamoja ya Serikali ambayo ina wajumbe kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina iliundwa kusimamia shughuli za Ugatuaji. Kamati hii itaendelea kuwepo katika kipindi hiki cha mpito hadi pale ambapo Ugatuaji huu wa uendeshaji wa elimu ya sekondari utakapofikia mahali ambapo hauna kitendawili, inafahamika kabisa shughuli gani ni za TAMISEMI na Shughuli zipi ambazo zitasimamiwa na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ya Kamati ni kukamilisha zoezi la ujenzi wa Vyuo vya *VETA*, katika ngazi ya Wilaya. Kamati ilihoji kwamba utaratibu gani na lini tutakamilisha ujenzi wa Vyuo vya *VETA* katika ngazi ya Wilaya. Mwaka huu wa fedha Serikali inatarajia kupata mkopo wa kiasi cha Dola za Kimarekani takriban dola milioni 600 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) katika *circle ADF 12*.

Mheshimiwa Spika, sasa fedha hizi za mkopo dola milioni 600 zitakopwa na Serikali kwa ajili ya sekta tatu, moja ni Miundombinu na pili Sekta ya Afya na tatu Sekta ya Elimu. Tumejipanga kwamba fungu lile la elimu liende katika ujenzi wa vyuo vyetu hivi vya *VETA*. Kwa hiyo, kwa upande wa elimu fedha hizo zitatumika katika Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya. Ujenzi wa Vyuo hivyo utafanyika kwa awamu na kwa kuanzia vyuo 28 katika Wilaya ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi ambazo zimefanyiwa utambuzi stadi ndio zitaanza kujengewa vyuo hivyo. Awamu ya kwanza vyuo 28, lakini awamu ya pili itahusisha Vyuo vya Ufundi Stadi 55. Napo tumesema kwamba tumeainisha vyuo 28 kwa maana ya kwamba tumeangalia maeneo yale, ama Wilaya zile ambazo hazina Chuo cha Ufundi Stadi, kabisa. Iwe Chuo cha Serikali au Chuo cha binafsi. Maana yake kuna Wilaya zingine ambazo zina Vyuo vya Ufundi Stadi, lakini siyo vya Serikali. Tunasema hizo basi, *Alhamdulillah* angalau zinavyo, lakini zingine hazina kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka tuanzie kule ambako hamna kabisa, halafu tunakwenda kwa namna hiyo katika awamu ya pili kwa kuchukua vyuo vingine. Kama nilivyosema kwamba, tutafuata taratibu, tutahakikisha kwamba tunafanya utambuzi wa maeneo yale ama taaluma au stadi zile ambazo zinahitajika kwa ajili ya Wilaya husika. Haitakuwa Mkululo kwamba kila Wilaya stadi ni zile zile zinazofundishwa hazitilii maanani yale mambo muhimu ambayo yanahitajika katika Wilaya hiyo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ya Kamati inahusu wahitimu wa Vyuo vya *VETA* kujiendeleza kitaaluma na kufikia ngazi ya juu ya ufundi ikiwemo stashahada, shahada na kuendelea. Naomba kutoa maelezo yafuatayo: Wizara kupitia *NECTA* na *VETA* imeandaa mfumo wa tuzo za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi unaowezesha wahitimu wa Ufundi Stadi kujiendeleza kitaaluma katika ngazi za ufundi sanifu. Mitaala ya *program* unganishi (*bridging course)* katika fani ya umeme na mitambo imekamilika na imeanza kutumika mwaka huu.

Tuzo hizo ama *NTA system* zimefanikishwa, zimeandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa fani hizo na tayari mitaala katika ngazi. Samahani hii imejirudia hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ukichukua fani hii ya ufundi stadi utakuwa umekwama huwezi, kupanda ngazi tena, huwezi kwenda kuchukua shahada au stashahada ama huwezi kwenda kuchukua shahada za uzamili au uzamivu, hapana, mitaala yetu imeandaliwa katika hali ambayo unaweza ukahama kutoka Mfumo mmoja wa elimu ukaenda katika mfumo mwingine bila ya matatizo yoyote kwa maana ya kwamba vyuo tayari vimejipanga na zimepangwa *courses* ambazo zina-*bridge* kuweza kuhamia katika fani nyingine. Kwa hiyo, nawasihi tu vijana wetu Watanzania na wananchi kwa ujumla kwamba wala wasione wakiingia kupitia *VETA* basi watakuwa wameishia *VETA*, hawatafika kwenye *technical colleges* au hawatafika katika Vyuo Vikuu kwa maana utaratibu kamili umeandaliwa na uko tayari kwa ajili ya utekelezaji na umeshaanza kutekelezwa ambao unaruhusu mtu kwenda katika ngazi hizo mbalimbali mpaka upeo wa kima cha uwezo wake mwanafunzi mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita ni ukaguzi wa utoaji wa elimu, Serikali imepokea na itafanyia kazi ushauri wa kuifanya idara ya Ukaguzi kuwa Mamlaka au Wakala itakayojitegemea ili kuboresha utendaji wa idara hiyo, tumepokea ushauri huo. Kwa bahati tulikuwa tumeshaanza kufikiria Wizarani, tumeujadili sana Wizarani, tumeanza kuchukua hatua za mwanzo. Kwa hiyo, ushauri huu ambao umetolewa na Kamati ya Huduma za Jamii, naomba nikiri kwamba tunaupokea kwa mikono miwili na tutaendelea katika taratibu hizo ili tuhakikishe kwamba tunafanya kazi hiyo kama ilivyoelekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya saba ni taaluma ya ualimu ama uhadhiri nchini. Serikali imepokea ushauri wa kuunda chombo mahususi cha kusajili walimu ambacho kitakuwa na dhana ya kusimamia taaluma na maadili ya fani ya ualimu. Maeneo mengine au kwa wakati mwingine tumeita *teacher professional board* kwamba wahandisi wana bodi yao ambao wanasimamia taaluma yao, wanasimamia nidhamu, wanasimamia *registration* lakini walimu wamelalamika kwamba hawana chombo chao ambacho kinawasimamia wenyewe na wangependa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imepokea ushauri huo na itaufanyia kazi. Lakini pia naomba niseme kwamba muda wa mafunzo kwa vitendo kwa walimu (*BTP*) yanayoendeshwa katika Vyuo vyetu vya Ualimu yamepewa uzito wa kurejesha muda wa mafunzo kutoka wiki nne za sasa kuwa wiki nane kama ambavyo tumetakiwa. Kwa hiyo, kilio kile cha Kamati tumekisikia na tutakifanyia kazi na tunarudisha tena mafunzo haya kuwa wiki nane. Aidha, posho ya kujikimu kwa kipindi cha mafunzo kwa vitendo kwa hawa walimu, awali ilikuwa shilingi 800 kwa siku kwa mwanafunzi na sasa Serikali imepandisha kima hicho kuwa shilingi 2000 kwa siku kwa mwanafunzi. (*Makofi*)

Serikali itajitahidi kuendelea kuboresha kima hiki kwa kadri bajeti itakavyoweza kuruhusu. Najua siyo kima kikubwa sana lakini tumekiongeza karibu mara tatu ya ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane ya Kamati inahusu hatma ya Tume ama Kamati iliyoundwa kushughulikia uoanishi wa *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ama *FDC* ili kuongeza uwezo wa utoaji wa Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Ningependa kusema kwamba mwaka 2010 Serikali iliunda Kamati iliyopewa jukumu la kushauri namna bora ya kuwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC*), jumla yake viko 55 vilivyopo nchini kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi. Mapendekezo ya Kamati yameainisha utekelezaji wa mpango kwa awamu. Katika awamu ya kwanza *FDC* 25 zimependekezwa kuboreshewa miundombinu na rasilimali watu ili ziwe na sifa ya kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo hivyo. Kiasi kitakachohitajika katika awamu ya kwanza ni takriban 67,400,799,662. Kwa hiyo, mpango huu uko tayari katika utekelezaji na tutaanza katika awamu na tutaanza na vyuo hivi vya *FDC* 25.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tisa ya Kamati ni mbinu mbadala ya kupata fedha za kuinua uwezo wa kutoa mikopo ili Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iweze kuwa na uwezo zaidi wa kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Rais, iliyoundwa kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wa utoaji mikopo, imekamilisha kazi yake na ripoti imewasilishwa tayari Serikalini. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo hayo. Ikiwa ni pamoja na kubainisha mbinu mbadala ya kuongeza mapato, kuweka vigezo ambavyo vitawatambua walengwa wenye uhitaji na kuimarisha utaratibu wa urejeshwaji wa mikopo. Aidha, ushauri uliotolewa na Kamati utazingatiwa ukihusisha maeneo yafuatayo: Matumizi ya vitambulisho vya Kitaifa, utaratibu wa kutoa taarifa kwa wanafunzi, uimarishaji wa dawati la malalamiko, uimarishaji wa uhusiano wa wadau na udhibiti wa ongezeko la karo za Vyuo Vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba utekelezaji wa yale yote yaliyoainishwa na Tume hii ya Mheshimiwa Rais, utachukua muda lakini kuna maeneo ambayo lazima yatekelezwa mara moja na kwa haraka. Kwa kuzingatia kwamba katika kero kuu hatutaweza kuzingoja hizi zitekelezwe katika kipindi cha masomo cha mwaka ujao wa masomo lazima baadhi ya vipengele viwe vimetekelezwa hasa utambuaji wa wale wahitaji wa mikopo hiyo.

Kwa hiyo katika yale yaliyopendekezwa, kuna yale ambayo tutachukua muda, lakini yale ya muhimu sana ya kero kubwa yatatekelezwa na hivi sasa Wizara yangu iko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba inayafanyia kazi ili wanafunzi watakapoanza muhula mpya mwezi Septemba 2011, maeneo hayo yawe tayari yameshafanyiwa kazi na kero hizo zimeondolewa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi ni utulivu katika maeneo ya Vyuo Vikuu nchini, Sheria na.7 ya mwaka 2005 iliyoanzisha Vyuo Vikuu na hati idhini na kanuni zake na sheria ndogo ndogo ama *by-laws* hati idhini nikimaanisha hati idhini zile za Vyuo Vikuu vyenyewe na pia Katiba za Serikali za wanafunzi wa vyuo husika, zinakataza uendeshaji wa shughuli za siasa ndani ya vyuo ngazi zote, Sheria kuu na. 7 ya mwaka 2005 na hasa aya ya 51 bayana kabisa inakataza, lakini pia kila chuo kina chata ama hati

idhini na ndani ya idhini ya kila chuo, imebainishwa kinaga ubaga kwamba harakati ama shughuli za siasa ndani ya vyuo haziruhusiwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia katika kila chama cha wanafunzi katika vyuo, kina katiba yake ama *constitution* kipengele hiki kimo, sasa basi ni matarajio yetu sisi Serikalini kwamba, vyama vya siasa, wanafunzi, wahadhiri na wana jumuiya wote katika vyuo watazingatia sheria na kanuni hizi ili maeneo yale ya Vyuo Vikuu yawe vitivo vya kutafuta elimu sio kuwa vitivo vya mapambano ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na moja ni miundombinu ya Vyuo Vikuu. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) hivi sasa umekamilika. Mpango huu ni mpango wa miaka mitano na mpango huu unalenga kutekelezwa katika awamu ya kwanza ya mwaka 2010 mpaka 2015, kuendeleza rasilimali watu. Wizara tayari imeshaanza kutekeleza hili, kwa mfano, kila mwaka tutapeleka wahadhiri wasaidizi 20 nchini Ujerumani kwa mafunzo ya *Masters* na *PhD* chini ya ufadhili wa Serikali ya Ujerumani. Aidha, Serikali kwa miaka mitatu iliyopita imekuwa ikitenga shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kusomesha wahadhiri kwenye Vyuo Vikuu vya ndani ya nchi na kupitia mradi unaofadhiliwa na benki ya dunia, wahadhiri wapatao 170 wanasoma shahada za uzamili na uzamivu nje ya nchi. Lakini pia mpango huu unalenga kuimarisha uimarishaji wa miundombinu ikiwa ni pamoja na kukarabati na kujenga miundombinu mingine. Kuongeza upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na pia matumizi ya TEHAMA kwenye kufundishia na kujifunzia. Pia utafiti na usambazaji wa matokeo yake, aidha, makisio ya mahitaji kwa awamu hii ya kwanza yanayotarajiwa kuwa jumla ya sh. 500,000,000,000/=. Tutahakikisha kwamba tunausimamia Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Juu kama vile ambavyo Serikali imesimamia kwa umakini Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEMM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), tutasimamia mpango huu ili kuhakikisha kwamba vyuo vyetu vikuu ambavyo vina miundombinu mibovu, basi tuweze kuitengeneza katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na mbili ya Kamati ni kuhusu kurejesha mafunzo ya jeshi la kujenga Taifa. Naomba kusema kwamba kama alivyotangaza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Serikali imeshaamua kurejesha mafunzo ya JKT na yanatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2012/2013. (*Makofi*)

Hoja ya malipo ya uzeeni ama pensheni kwa wahadhiri, ningependa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshalitolea maamuzi, suala hili na kwa sasa taratibu za jinsi ya kulitekeleza zinaandaliwa. Kwamba pensheni ya wahadhiri imefanyiwa mapitio na kwamba sasa imeboreshwa, hii pensheni kwa kutumia kikokotoo kipya ili malipo yale ambayo wanalipwa wahadhiri kupitia Mfuko wao wa *PPF* yafanane na yale ambayo yanalipwa na mifuko mingine ya hifadhi na kikokotoo hiki kimeanza Machi, 2011. Lakini pia kulikuwa na wahadhiri ambao walikuwa katika mfumo mwingine ambao unaitwa *Senior Staff Superannuation Scheme* (*SSSS*). Hawa mafao yao yalikuwa duni sana na waliomba wahamishiwe katika Mfuko wa *PPF*, sasa Serikali

imekubali kufanya hivyo na wahadhiri 36 wako katika mfumo huo tangu mwezi Machi, 2011. Serikali itagharamika katika hilo kwa maana ya kulipa stahiki zile zote kwa *PPF*, zilipwe kwa ajili ya watumishi hawa ambao hawakulipiwa ili iwezeshe sasa wao kuingia katika mfuko huu mpya na Serikali imekubali kubeba mzigo huo.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani. Naomba sasa nitoe maelezo kuhusu maoni yaliyotokana na Kambi ya Upinzani yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda kama ifuatavyo:- Moja inahusu malimbikizo ya madai ya Walimu, Chama cha Walimu Tanzania kimewasilisha barua ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa na madai ya malimbikizo ya stahili mbalimbali za Walimu kwa Mkuu wa Utumishi Serikalini, kipindi cha mwezi Mei hadi Juni, 2009, Wizara ilikusanya na kuhakiki madai mbalimbali ya Walimu na ya watumishi wasio Walimu kama ifuatavyo. Madai ya watumishi 25,440 yenye thamani ya sh. 22,772,602,062/= na kwa kipindi hicho madai hayo yalihakikiwa na *CAG* ama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa awamu tatu na yakalipwa pia kwa awamu tatu mwishoni mwa mwaka 2009 kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza ilihusisha madai 5030 ambayo jumla yake ni sh. 1,412,244,876.70 na awamu ya pili ilihusisha madai 5147 ambayo jumla yake ni sh. 1,521,966,160/= na awamu ya tatu ilihusisha madai 4758 ambayo thamani yake ilikuwa jumla ya sh. 2,531,702,371.81. Baadhi ya madai haya yalikataliwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kukosekana kwa viambatanisho muhimu, hivyo Wizara ilitoa tangazo la kuwataka watumishi wote ambao madai yao yalikataliwa wakate rufaa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Novemba 2009 hadi Juni 2011 Wizara iliendelea kushughulikia madai mbalimbali ya watumishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya mishahara yaliyochambuliwa na kuhakikiwa na kuwasilishwa Hazina kwa malipo ambayo jumla yake ilikuwa sh. 998, 384,382.87 kati ya madai hayo sh. 612,327,727.65 zimelipwa. Pia madai mengine yalilipwa katika kipindi cha Julai 2010 hadi Juni 2011 yamebainishwa kama ifuatavyo: Madai ya uhamisho ya kiasi cha jumla ya sh. 108,249,324.60, madai ya wastaafu sh. 26,385,500, madai ya mazishi sh. 1,638,500/=, likizo sh. 37,095,572, matibu sh. 17,273,819/=, ada sh. 807,000, kujikimu sh. 227,254,500 na madai ya usafiri jumla ya sh. 192,677,000/=, jumla ni sh. 611,381,215.60.

Mheshimiwa Spika, madai mengine yanayoendelea kuchambuliwa hadi sasa ni madai ya likizo, posho ya masaa ya ziada, uhamisho, posho ya kujikimu, posho ya vitabu, posho ya mavazi, posho ya usumbufu, fedha za matibabu, kodi ya pango na mazishi, jumla yake ni sh. 1,029,651, 338.47. Aidha, Wizara yangu inaendelea kupokea na kuhakiki madai mbalimbali ya Walimu pamoja na watumishi wengine na kuyalipa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha katika Serikali. Ili kuepukana na malimbikizo ya madeni, Wizara yangu imeweka mikakati ifuatayo:-

1. Kurekebisha mishahara ya watumishi mara wanapopandishwa vyeo na madaraja.

2. Kutokutoa uhamisho bila ya kuwa na fedha kutoka *OC* kwa ajili ya uhamisho. Uhamisho wote utafanywa pale tu ambapo pana hela katika *OC*.

3. Kukamilisha taratibu ya ajira mpya mapema mara baada ya mtumishi kuripoti na kuanza kazi katika kituo alichopangiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu tunalifahamu, tatizo la walimu tunalijali sana. Madeni haya ya walimu tunayajali sana, kazi ya uhakiki imefanywa na malipo yamefanywa katika awamu mbalimbali kwa kumtumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kama takwimu ambazo tumezitoa. Lakini pia tumehakikisha kwamba haya ambayo tunayahakiki sasa, tutahakikisha tunayafanyia kazi kwa umahiri na kwa haraka ili mara tu yatakapokuwa yamehakikiwa pesa ziweze kutolewa, pesa tumezitenga kwa kutambua kwamba bila mwalimu kuweza kutimiziwa mahitaji yake na matakwa yake na madeni yake, hamna elimu ambayo itaweza kupatikana. Si jambo ambalo sisi tunaliona kama ni la faraja kwa Serikali hii kusikia kilio cha Walimu mara kwa mara. Tunajipanga kuhakikisha kwamba kilio cha Walimu tunakimaliza na malipo haya tutayafanya mapema iwezekanavyo kama ambavyo tumeainisha na Walimu niwahakikishie tu kwamba jambo hili sio muda mrefu tutaliweka katika historia.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni hoja ya mafanikio ya shule za Kata. Ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao: Mafanikio ya shule zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi ni pamoja na ongezeko na upatikanaji wa elimu ya sekondari. Aidha, wanafunzi wote wanaofaulu darasa la saba wanapata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari katika shule za sekondari za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila yule anayefaulu darasa la saba anapata fursa ya kuendelea katika shule ya sekondari, sio sawa sawa na hapo mwanzo ambapo wengine wamefaulu lakini hawapati nafasi ya kuendelea, tunasema kwamba ni uchaguzi, kwamba mmefanya mtihani lakini hawa ndiyo waliochaguliwa, sasa tunasema kwamba tumepanua wigo huo kufikia hali ambayo wale wote ambao wanafaulu wanaendelea kupata elimu ya shule ya sekondari. Shule zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo upungufu wa Walimu, miundombinu na samani. Ili kukabiliana na changamoto hizo, MMES awamu ya pili imeweka mkakati wa kupunguza changamoto hizi kwa kutoa kipaumbele katika kukamilisha majengo ambayo hayajakamilika na kutoa fedha za ruzuku kwa ajili ya kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kujenga maabara na nyumba za Walimu ili kuongeza ufaulu zaidi katika shule hizi. Aidha, Serikali inafuatilia kwa karibu zaidi ugawaji wa Walimu ili zile shule zilizoko kwenye mazingira magumu, nazo zipate Walimu wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi zina mchango mkubwa katika kuendeleza elimu ya sekondari. Kwa mfano mwaka 2009 asilimia 50.1 ya wanafunzi wote waliofaulu daraja la kwanza hadi la tatu ambao wana sifa ya kuingia kidato cha tano walitoka katika shule za sekondari za Kata.

Aidha, mwaka 2010, asilimia 49.3 ya wanafunzi wote walioendelea kidato cha tano wametoka katika shule za Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari imepanuka ukilinganisha na mwaka 2005 mpaka mwaka jana 2010 ambako 2005 kulikuwa na jumla ya idadi ya wanafunzi wa sekondari 524,000 na mpaka mwaka jana 2010 kuna jumla ya wanafunzi 1,638,000. Mafanikio hayo ni makubwa, mafanikio haya ni ya uhakika, kila safari ina mahali pa kuanzia, safari ya maili 1000 inaanziwa na hatua moja, tumejenga shule ambazo hazikuwepo, sasa tuna shule ambazo jumla yake ni 4,266 za Serikali nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeongeza upatikanaji wa elimu ya sekondari, naomba sasa wananchi wa Tanzania waiangalie Serikali ya Awamu ya Nne chini ya MMES II inasimamia kuboresha shule hizi, kuzifanya ni shule mahiri ambazo zitaweza kutoa wataalam mahiri. Shule za yebo yebo mwaka 2015 zitakuwa historia na waliosema watatafuta kitu kingine cha kuzungumza wakati huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ningependa kuitolea ufafanuzi ya Kambi ya Upinzani inahusu kuboresha elimu ya juu. Naomba nitoe ufafanuzi ufuatao, kwamba, katika elimu ya juu mambo yafuatayo yamefanyiwa uboreshaji, moja imeanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu, aah! Samahani hii sio hoja yenyewe. Naomba nifute hapo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumziwa ni hoja ya maboresho ya elimu ya awali. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, kila shule ya msingi inapaswa kuwa na darasa la elimu ya awali ili kufikia lengo hilo Halmashauri zinahimizwa kushirikisha Serikali za Mitaa na ugatuaji umehusisha pia kupeleka rasilimali zinazohusiana na uendeshaji wa shule kwenye Halmashauri ikiwemo fedha za kuendeshea shule hizi za awali. Katika shule za msingi Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ambayo inazingatia mabadiliko mbalimbali ya kijamii na ya kiuchumi yaliyotokea na yanayoendelea kutokea ndani na nje ya nchi na rasimu ya Sera hiyo ipo na inajadiliwa na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya sekondari, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga Utaifa kupitia shule za bweni, zinazochukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini, aidha, kwa mwaka 2011 kuna jumla ya shule 201 zinazochukua wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali nchini kwa lengo la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kukuza utamaduni wa kujisomea. Katika kukuza utamaduni wa kusoma miongoni mwa Watanzania, Bodi ya huduma za maktaba Tanzania inaendelea kuimarisha huduma za maktaba katika ngazi za Mkoa na Wilaya, hadi mwaka huu Bodi ya huduma za maktaba Tanzania imetoa huduma katika Mikoa 21 na Wilaya 14. Jitihada zinafanywa ili kuanzisha huduma za maktaba katika Mikoa na Wilaya zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, niingie katika hoja ya uhuru wa Vyuo kujiendesha vyenyewe. Kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Vyuo Vikuu na hati idhini ya Vyuo vyenyewe, Vyuo Vikuu vina uhuru wa kujiendesha, dhamana ya uendeshaji wa Vyuo Vikuu ni ya Vyuo vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, hapa ningependa kutoa ufafanuzi kwamba wala Serikali haiingilii Vyuo Vikuu katika kujiendesha, utaratibu mzima upo wa namna ya kuviendesha Vyuo hivyo vikawa na Mabaraza mahsusi ama ngazi maalum za nidhamu na za kuendesha Vyuo hivi zipo, kwa hivyo, Serikali inawapa fursa maalum na kuwapa uhuru Vyuo hivi kutekeleza taratibu zao za kujiendesha bila ya kuviingilia.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni baadhi ya watu walihoji kwamba kwa nini Serikali imefukuza wanafunzi *UDOM*. Si kweli, *UDOM* wamefukuza wenyewe kwa vikao vyao na taratibu zao za kujiendesha bila ya kuingiliwa. Bodi za *Colleges* zimekaa na maamuzi ya Bodi ya *Colleges* yamepelekwa mbele katika ngazi mbalimbali mpaka *Council* ya chuo imeidhinisha na taratibu za nidhamu kupitia Kamati ya Nidhamu zitafuata mkondo wake kwa maana ya Kamati ya Nidhamu itakaa na kufuata taratibu zile ambazo zinahusika ya namna ya kurudisha wanafunzi wale ambao wamekosa nidhamu na kufanya fujo katika vyuo hivyo. Hakuna mkono wa Waziri wala hakuna mkono wa Serikali. Waziri atafanya kazi katika vyuo vingapi katika nchi hii ikiwa inabidi aendeshe kila chuo nchini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya malimbilikizo ya pango ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya umma na kuboresha mafao ya uzeeni. Maboresho ya mafao ya uzeeni nimeyazungumza, lakini nizungumzie hili la posho ya pango kwa Wahadhiri. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imepokea jumla ya shilingi bilioni 9.3 ya posho ya nyumba ya Wahadhiri wa Vyuo vikuu, ambayo ilikuwa ni deni la pango la nyumba kwa Wahadhiri kwa mwaka 2009 na 2010. Pesa hizi tayari zimeshapokelewa, pesa hizi zitalipwa kwa Wahadhiri ambao walikuwa wanazingoja kwa muda mrefu. Posho hizi za malimbikizo hadi tarehe 30 Juni mwaka huu 2011, zilikuwa zimeshaingia na Wizara sasa inafanya taratibu za kuhakikisha kwamba inazipeleka katika vyuo ili Wahadhiri waweze kulipwa kama ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo ya sayansi, hisabati na *English.* Serikali inatambua umuhimu wa ufundishaji wa masomo ya sayansi, hisabati na *English,* Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)* na *JICA* inatekeleza mkakati wa mafunzo ya ualimu kazini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa ufundishaji wa masomo hayo kwa umahiri. Mpaka sasa jumla ya walimu 2,462 wamenufaika na mafunzo haya. Mafunzo haya yameanza mwaka huu na yataendelea, yatawahusisha walimu wote wale ambao wanaofundisha masomo ya sayansi, hisabati na *English* ili kuhakikisha kwamba uwezo wao na kiwango chao cha kuweza kufundisha masomo hayo, kinapanda ili tuweze kupandisha ufaulu katika masomo hayo. Ni masomo muhimili muhimu ambayo yanawawekea misingi mizuri wanafunzi kwa ajili ya masomo yao baadaye.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Kwanza, ni Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Pili, naomba nitoe shukrani zangu kwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kunipa ushirikiano mkubwa na miongozo safi iliyoniweza kutekeleza majukumu yangu kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tatu, nitoe shukrani zangu za pekee kwako wewe mwenyewe kwa kuendesha Bunge kwa busara, kwa hekima na kwa uvumilivu mkubwa. Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunipa maoni ambayo mara zote yamekuwa ni ya msaada mkubwa. Siyo tu kwa Wizara yangu bali pia ni kwa Taifa letu kwa ujumla. Kwenu nyote nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo langu la uchaguzi la Bagamoyo kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi chote ambacho nimekuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Kwa pamoja tumefanya kazi kubwa za kimaendeleo na kwao naendelea kuwaahidi ushirikiano na kuwatumikia kama ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda pia kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu nyingi za dhati kwa mke wangu na familia yangu kwa kunipa moyo na ushirikiano na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mbalimbali ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna hoja ambazo hatukuweza kuzijibu za Mheshimiwa Mbunge kwa Mbunge. Hoja hizi zote tutazitolea ufafanuzi ama majibu au kwa maandishi na kitabu hiki cha majibu ya hoja za Wabunge, tutakisambaza kabla Bunge hili halijamalizika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja hii imeungwa mkono. Kabla sijaingia hatua nyingine, napenda kuwatambua wageni tulio nao wageni maalum tulionao katika Ukumbi wetu. Kwanza kabisa tunao wageni 32 wanachama cha *Tanzania Albimo Society* wakiongozwa na Ndugu Ernest Kimaya, ndiyo Mwenyekiti wao. Halafu na wengine wote wasimame pale walipo. Ahsante. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Makofi hayo maana yake mnakaribishwa sana na tumefurahi kuwaoneni na ni wageni ambao wamefanyiwa utaratibu na Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu tuna wanafunzi wetu, ni wanafunzi Madaktari, wanatoka Chuo Kikuu cha Bugando wako 15. Wako wapi wanafunzi wa Bugando. Ahaa ahsante sana. Hawa wanatoka Chuo Kikuu cha Bugando na wamekaribishwa na mwenyeji wao Mheshimiwa

Ezekia Wenje. Ahsante sana. Karibuni sana tunawatakieni msome kwa bidii ili muweze kutuhudumia kesho, mambo mengine yasiyokuwa na msingi tumieni busara kuyamaliza na siyo vinginevyo. Karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na hatua inayofuata. *(Makofi)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 46 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Kif. 1001–*Admin. and General*..............Sh. 27,108,633,186/=

**MWENYEKITI:** Wengine mmeshajibiwa mnataka tena kusimama. Tunaanza, leo nianze na huku, Mheshimiwa Salim nimeshamwandika. Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Mrema, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa majina mengine ya huko magumu kuyatamka. Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Mhonga, Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Mtinda, Mheshimiwa Rose Kamili, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Christina, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mikidadi, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Dokta Kigwangalla, Mheshimiwa Chambiri, Mheshimiwa Njwayo.

Wengine ni Mheshimiwa Mipata, Mheshimiwa Alhaj Missanga, Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Mchemba, Mheshimiwa Mkanga nimekuona. Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Dokta Tizeba, Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mheshimiwa Hewa, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Obama, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge, Mheshimiwa Kamani, Mheshimiwa Mtanda, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Makalla. Hapo ndiyo hamwezi kukataa *Guillotine* itafika tu. Tuanze na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ili kuokoa muda nisipoteze kwa kutaja tena vifungu vinajulikana ni hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Usitaje, wanaita mshahara wa Waziri na Naibu wake na Katibu Mkuu. *(Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nachangia hoja yangu katika Wizara hii kwa maandishi nilibainisha tatizo kubwa sana ambalo linazikumba shule zetu za kutokuwa na walimu wa kutosha. Kwa hali ilivyo sasa uwiano wa walimu katika kuwagawa kwenye maeneo yetu unategemea idadi ya wanafunzi. Lakini kitu hicho kwa wakati tulionao na baada ya kufungua shule nyingi kwenye Kata ni kitu ambacho hakiwezekaniki kwa sababu walimu hao wengi

wamekuwa wakibakia maeneo ya mijini kwa sababu nyingine ambazo hazizuiliki. Utakuta wengine wana matatizo ya kiafya mahususi, wengine wameolewa na waume zao na hizo ni sababu za kimsingi kabisa huwezi kuvunja ndoa za watu.

Kwa hiyo ziko sababu nyingi sana. Sasa naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi ni lini tutabadilisha Sera ya mgao wa walimu kwa uwiano wa wanafunzi na tukaongeza vipengele vingine vitakavyosaidia shule zile za vijijini ambazo mpaka sasa hatujaanzisha motisha kwa walimu kwenda kule vijijini zikapata walimu ili kusaidia na maeneo ya vijijini yakawa na walimu kwenye shule za sekondari na za msingi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tunatumia kwa ajili ya kugawa walimu kwenda shule za sekondari hasa katika mwaka huu, walimu ambao tumewagawanya mwezi wa kwanza tumetumia kigezo cha upungufu wa walimu katika shule husika. Kwa hiyo, tumeangalia shule zote kwa ujumla, tukaangalia mapungufu yako kiasi gani na tumepeleka walimu huko kufuatana na mapungufu ya walimu katika shule hizo. Nadhani hicho ni kigezo kikubwa kwa sababu tukiweza kuwa na walimu wa kutosha katika shule au ambao kidogo wana nafuu katika kila shule basi hiyo itatuwezesha sisi kuweza kuboresha mazingira katika shule zetu. Changamoto ambayo Mheshimiwa Jenista Mhagama ameisema ni kweli ipo pamoja na kwamba tumepeleka hivyo lakini kuna ambao hawakuripoti katika maeneo yao. Tutaangalia taratibu zingine ambazo zitawezesha kuboresha upatikanaji wa walimu katika shule hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa mujibu wa kanuni zetu m-*note* kama swali lako limeulizwa na mwingine wewe hutaruhusiwa. Maana yake tena asije mtu mwingine akazungumzia walimu, walimu, suala la walimu ndiyo limeshajibiwa hivyo. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Naulizia shule zilizo katika mtandao wa *UNESCO* ambazo kwa kushirikiana na asasi za Serikali na ambazo si za Serikali Tanzania Bara na Visiwani. Je, mnatumia vigezo gani kuzipata shule hizo na mtandao huu unafanya kazi vipi?

**MWENYEKITI:** Tunaomba Mheshimiwa Hemed rudia tena.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizia juu ya shule ambazo zimo katika mtandao wa *UNESCO*.

**MWENYEKITI:** Wewe unajua kwa mfano moja ipi hiyo? Kwa mfano shule gani?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Zimo katika kitabu chake.

**MWENYEKITI:** Haya! Malizia swali lako basi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Sasa shule hizo zinashirikiana na asasi za Serikali na zile ambazo si za Serikali, Tanzania Bara na Visiwani. Sasa nauliza je, zinapatikanaje shule hizo? Mnatumia vigezo gani katika kuziteua shule hizo na zinafanya kazi vipi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Shirika la *TANESCO*, samahani *UNESCO*. *(Makofi/Kicheko)*

*UNESCO* na siyo *TANESCO*. Suala la shirika la *UNESCO* ni kweli ni la Kimuungano na ukienda pale Shirika la *UNESCO* Dar es Salaam pana fomu maalum bila kujali shule ya *private* au ya Serikali unajaza vile vigezo vyao ukishajaza unaingia kwenye mtandao, wanaanza kukupa ile misaada ambayo unaweza kuipata. Kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge waziarifu Halmashauri zao kwenye shule zao wakajaze fomu hizo.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu kwenye Hotuba hii, nilizungumzia juu ya maslahi ya walimu, hasa hasa matatizo yanayotokana na walimu kutokulipwa mishahara na marupurupu wanayostahili pamoja na matatizo ya kutopata nyumba wanazostahili, kama ambavyo imeelezwa vilevile na Mheshimiwa Waziri, katika Hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi na aliambie Bunge hili Tukufu, aiambie Kamati yako, kwa vile tatizo sio kwamba hakuna fedha! Tatizo ni kwamba fedha zinazotengwa na Bunge hili hazitumiki, kama nilivyoonesha jana! Mabilioni yanayotengwa kwa ajili ya nyumba hayatumiki! Mabilioni yanayotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shule hayatumiki! Sasa Mheshimiwa Waziri, atufafanulie ni kwa nini walimu wetu wanapata shida wakati fedha zinazotengwa hazitumiki? Pili, atuambie kwa mwaka huu wametenga fedha kiasi gani za kutatua matatizo haya ya walimu kutokuwa na nyumba, walimu kuwa na *arrears* za mishahara na marupurupu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa hapa kwamba, nitaondoa shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa unajibiwa habari ya nyumba, sio tena *arrears*, wapi. Mheshimiwa Naibu Waziri, *TAMISEMI*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, hakuwepo wakati natoa mchango wangu. Niliweza kutoa ufafanuzi wa kina juu ya hoja zote alizozieleza. Labda kama utaniruhusu nirudie tena kwa manufaa yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo unatakiwa ujibu. Haya jibu tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA- ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge, ametaka kufahamu maeneo haya mawili; kwanza mishahara nimetoa ufafanuzi wa kina.

**MWENYEKITI:** Nimesema moja tu la nyumba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nyumba tumeshatenga fedha na mwaka huu wa 2011/2012, tumeshatenga fedha za kujenga nyumba 1,200 zitakazomudu kukaliwa na familia 2,400. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kwamba kuna Kampuni inaitwa *Bayport* na imewatapeli walimu wengi sana kwenye Jimbo langu na Majimbo mengine, karibu nchi nzima. Walimu hao unakuta mtu anasaini mkataba wa 300,000/=, wanamwekea 3,000,000/=! Kwa hiyo, hawapati mshahara wowote! Sasa ningependa kujua Waziri anaichukulia hatua gani za haraka hii Kampuni? Maana watu hawapati shilingi hata moja huko!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Kampuni zote ambazo zinatoa mikopo ambayo sisi tunaitambua, huwa tunazipa kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mara baada ya kusikia hiyo kwamba, kuna watumishi ambao wamekopeshwa kinyume cha taratibu, baadhi ya taasisi tulisimamisha kukata yale madai yao na pia tukawaandikia waajiri wote, wahakikishe kwamba mtumishi hakopeshwi zaidi ya theluthi moja ya mshahara wake na tulimtaka kila Mkurugenzi ambaye amemkopesha mtumishi zaidi ya hivyo aelezee ni kwa nini alifanya hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwaombe tu walimu kwamba, wanapokwenda kukopa ni lazima wahakikishe kwamba makubaliano yawe ni mwajiri na yule anayetoa mkopo. Wanavyoingia wao wenyewe kule, inakuwa ni ngumu sasa Serikali kuingilia kati.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba, katika Jimbo langu la Manyovu, vijana wengi wanamaliza shule na wanaomba vyuo vya kujiunga na ualimu na wengi wamekuwa hawapati nafasi hizo. Niliiomba Wizara je, inaweza ikaweka utaratibu kwamba *selections* zikawa zinafanyika mikoani au Wilayani kulingana na *ceiling* mtakayotupa katika Mkoa au Wilaya ili vijana wangu wa Jimbo langu la Manyovu, waweze kupata nafasi za ualimu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Obama kwamba, kwa ombi ambalo amelifanya, linafanana sana na utaratibu ambao tumeutumia

safari hii katika kuchagua walimu wanafunzi au wanafunzi ambao wataingia katika mafunzo ya ualimu katika vyuo vyetu. Kwa kawaida tunaangalia ufaulu na kima cha chini kabisa ni *point* 28 kwa wale wanaomaliza Kidato cha IV, lakini kuwaorodhesha hawa mpaka idadi ya nafasi katika vyuo vyetu vilivyopo, kuna baadhi ya mikoa unaweza ukaiacha kabisa kama vile Kigoma, Mkoa wa Mheshimiwa. Lakini Wizara imetumia busara ya kuhakikisha kwamba inachagua wanafunzi kuingia kwenye mafunzo ya ualimu kufuatana na mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna yule ambaye amepata nafasi akiwa Mkoa wa Pwani, anaweza akakawa na ufaulu ambao uko tofauti na yule ambaye anatoka Mkoa wa Lindi. Nafasi hizi tumezigawa kwa namna hiyo ili kila Mkoa uweze kushiriki katika mafunzo ya ualimu na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba kuna uwiano mzuri wa mafunzo haya ya ualimu. Changamoto kubwa, nafasi ni chache sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam ni kielelezo cha mafanikio ya elimu kwa miaka hii 50 ya Uhuru na mimi niki-*declare interest* ni Mjumbe wa *Council* ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, katika Taarifa yake ukurasa wa 39, Kifungu (j), amesema kwamba Chuo kimeamua kujenga Kituo cha Wanafunzi na hivyo kinachangisha pesa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo. Je, Waziri haoni kama ni fursa nzuri kwake kuomba mchango kwa Waheshimiwa Wabunge, ambao wengi wanakiri kwamba wanapata posho ambayo inaweza kusaidia pia kuchangia Kituo hiki ambacho kimetuzalishia wanafunzi wengi?

**MWENYEKITI:** Kama hamniombi mimi, basi hamna namna! *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi labda na yeye aweke mkazo hapo. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, kwa kutoa pendekezo hilo na mimi ombi hilo nimelikubali na naomba sasa rasmi kwa Bunge lako Tukufu, kwamba nitakuja kwenu kwa ajili ya…

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge, walifanya minong'ono)*

**MWENYEKITI:** Aah, sisi tuna…

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge, kupitia kwako Spika, kutoa mchango wenu kupitia posho, kuchangia maendeleo ya Chuo Kikuu. Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, tumesikia, lakini sisi tuna utaratibu wetu. Mtu anaomba, anasema ukafungue na benki fulani ile ndio zipelekwe zile hela, hivi

inawezekana kweli? Utatutafutia wapi ili uchukue! Hapana, haiwezekani. Sasa tutatumia utaratibu wetu na huwa tunatumia Kamati zetu, wakikubali watakubali, kama wakikataa watakataa. Kama wanakubali, kiasi gani, watasema wao! *(Makofi/Kicheko)*

Dokta Mahenge!

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia niliieleza Serikali mazingira magumu ya shule zilizoko kwenye Wilaya za Njombe, Ludewa na Makete, ambazo zinakumbwa na matatizo makubwa ya UKIMWI na jiografia ngumu na hivyo kufanya walimu wengi kufika na kuripoti na baadaye kuondoka, hasa baada ya kukosa nyumba za kulala. Sasa Mheshimiwa Waziri, amesema kuna nyumba 1,200 ambazo zitajengwa, nataka kumwomba awathibitishie wananchi hawa wa Wilaya za Ludewa, Makete, Njombe, kama watakuwa ni mojawapo wa kupewa kipaumbele kwenye mgao huu wa nyumba 1,200?

**MWENYEKITI:** Enhee na mimi pia nina-*declare interest.* Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kwamba tutayaangalia kwa makini sana maeneo yale ambayo yana mazingira magumu. Lakini kama alivyosema kwamba machakato tutaufanya kati ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI ili kuwa na uhakika kwamba, eneo tunalolibainisha, ni kweli kwamba ni eneo ambalo lina mazingira magumu, sio kwa upendeleo na huko ndiko ambako tutahakikisha kwamba tuna-*settling allowance* ya 500,000/= kwa mwalimu anayeripoti, lakini pia nyumba zile 1,200 tutaanzia katika maeneo hayo.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, katika Jimbo langu na nafikiri ni Jimbo langu tu, labda la Jirani yangu Misungwi, kwamba hakuna *High School* hata moja hizi za Tarafa! Sasa Waziri, ana mpango gani kuhakikisha kwamba Busega na Misungwi, zinapata sekondari za *A–Level*?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NAMAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Halmashauri au Wilaya kuwa na *A–Level*, huwa ninalijibu kila siku hapa kwenye Bunge lako Tukufu. Mwongozo ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge, namshauri arudi kwenye Halmashauri, wateuwe shule moja ndani ya shule zao zile za Kata, waweze kuipa hadhi, watuandikie barua Wizara ya Elimu, sisi tutatuma Wakaguzi kuja kukagua. Kama shule hiyo itakidhi vigezo vya kiukaguzi, sisi tutaipandisha shule moja kuwa na *A–Level. (Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati wa mchango wangu wa kimaandishi, nilizungumzia juu ya suala la

Serikali kutoa *guarantee* kwa mifuko ile ya hifadhi ya jamii ili iweze kukamilisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* kwa 50% iliyobaki, ili kuweza kukidhi haja ya kuwa na *colleges* mbili zaidi zitakazoweza kuchukua wanafunzi 20,000. Naomba Mheshimiwa Waziri, alifahamishe Bunge hili ni lini *Government Guarantee* kwa mashirika hayo itatolewa ili ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, uweze kutekelezeka kwa 100% badala ya 50% ya hivi sasa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufafanua hoja ya Mheshimiwa Said Mtanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wote kabisa, umefanywa kwa fedha ambazo zimetokana na mifuko ya hifadhi nchini mwetu, ni hela ya humuhumu Tanzania. Tumefanya hivyo kwa Serikali, kupitia Hazina, kutoa *guarantee* kwa pesa zile ambazo zimetumika. Kitu ambacho kimefanywa, ujenzi huu unakwenda awamu kwa awamu. Serikali, ime-*guarantee* awamu ya kwanza, sasa tunakwenda katika awamu nyingine ya ujenzi kama vile ambavyo tumefanya kwenye awamu ya kwanza. Hatuna njia nyingine ya kufanya bali ni kuhakikisha kwamba tunatoa *guarantee* tena ili ujenzi huu uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna taratibu maalum ambazo zinafuatwa na kuna Masharti na Kanuni ambazo inabidi zitekelezwe. Hicho ndicho ambacho kinaendelea hivi sasa mpaka pale tutakapofikia Serikali kuweza kutoa *guarantee* hii kwa Mifuko hii. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niiulize Serikali kwamba, inatoa kauli gani kuhusu utafiti uliofanyika nchi nzima kwa wale wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa masomoni. Lakini bado pia, Mheshimiwa Waziri, ametueleza mambo mazuri kwa mfano, posho za walimu za kujikimu katika mazingira magumu, kwamba zitaanza mapema. Je, ameshawasiliana na Hazina, kwamba ile tabia yao ya kucheleweshа pesa, watatoa haraka ili utekelezaji uanze?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata, sasa ni wajawazito au nini? Maana sijaelewa sasa?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunganisha mawili.

**MWENYEKITI:** Aaah! Moja tu, la wajawazito; naomba ujibu hilo. La wajawazito, nani anajibu? Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumjibu Mheshimiwa Martha Mlata, suala la ujauzito kwa watoto wa shule. Hili lipo kwenye Sera ya Elimu ya mwaka 1995 na litahuishwa kwenye Sera Mpya ya Elimu, hii ambayo nadhani tutaileta hapa,. Kwamba, tumeshaangalia matatizo yanayojitokeza hasa huko vijijini, Sera ya Elimu inasema kwamba, tutaanza kuruhusu vijana hawa kurudia masomo, lakini kwa utaratibu maalum ambao tumeuweka. *(Makofi)*

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia kuhusu Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa watu wenye ulemavu, vyuo hivi vipo saba na katika hivyo saba, viwili tu ndio vinavyofanya kazi na pia kwa kusuasua. Athari inayowapata watu wenye ulemavu ni kuzagaa mitaani kwa sababu, hawana la kufanya. Wanazagaa mitaani, hawana lakufanya, maisha magumu! Sasa Mheshimiwa Waziri, ananiambiaje kuhusu ufufuaji wa vyuo hivi ili kuwasaidia watu wenye ulemavu, waweze kupata mafunzo na wao waweze kujikimu kimaisha?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Al-Shaymar Kwegyir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina wathamini na kuwaenzi wananchi wake wenye ulemavu. Kama ambavyo imekuwa ada katika miaka kadhaa ya hivi karibuni, kila mwaka tumetenga pesa kwa ajili ya kuimarisha elimu kwa ajili ya wananchi hawa ambao wana ulemavu. Najua changamoto bado zipo na kwa vyuo hivi saba vya walemavu, Serikali imeweka nia thabiti ya kuviangalia, namna ya kuviboresha kwa kadri ambavyo tutakuwa tumepata pesa.

**MHE. AMOS G. MAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na mambo mengine, nilitaka kujua tatizo la kutokusajiliwa kwa Sekondari ya Wazazi Muhonda. Ni miaka mitano sasa tumekuwa tukifuatilia na Mkaguzi wa Kanda ya Mashariki alishafika, tukatekeleza yale yote ambayo walikuwa wameyasema pamoja na kujenga vyoo, madarasa na jengo la utawala, mpaka sasa, shule hiyo haijasajiliwa. Niliongea na Naibu Waziri, nilifikiri kwamba katika majumuisho yake atanijibu! Kwa hiyo, nataka kujua ni tatizo gani hasa linalosababisha Shule ya Wazazi ya Sekondari pale Muhonda kuwa haijasajiliwa mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Shule ya Wazazi ya Muhonda anayoizungumzia Mheshimiwa Makala, hata pale Wizarani tulilijadili mwezi wa Nne. Wakaguzi walivyotupa maelekezo ni kwamba, suala hili lina utata kidogo wa umiliki; maana ukienda unakuta wanasema Shule ya Wazazi Muhonda, ukienda siku nyingine wanabadilisha jina wanaita jina fulani. Kwa hiyo, ni kama ilikuwa ni *centre* zamani ambayo sasa wanabadilisha majina. Kwa hiyo, suala la vigezo vya kusajili shule linataka tuwe na umiliki, eneo lile la yule mmiliki na jina la shule lionekane kwamba ndilo hili na ndilo lenye umiliki wenye viwanja vile vyenye hati, sasa kidogo pale Muhonda panasumbua. Labda nitamwomba tu Mheshimiwa Makala, hata kesho au keshokutwa, tuonane tuweze kuliweka sawa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi, niliomba kujua kama kuna *Regulatory Board* au chombo cha Serikali, kinachosimamia upangaji wa ada kwa shule za binafsi, kuanzia shule za awali hadi Vyuo Vikuu. Kwa hali halisi ilivyo sasa, kila mmiliki wa shule anajipangia ada za shule au *fees*,

kadiri atakavyoona inafaa. Je, kama chombo hicho hakipo, Serikali ina mpango gani wa kuunda chombo hicho, kusimamia ada za shule za binafsi? Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna chombo hicho kwa sasa, lakini kwa upande wa Vyuo, Tume ya Rais ambayo imeangalia matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, moja katika mambo ambayo wameyatolea mapendekezo ni eneo hili la chombo ambacho kitadhibiti ada katika Vyuo Vikuu. Naomba tu nilihakikishie Bunge lako kwamba, kwa ngazi ya shule za sekondari, tutajitahidi tulifanyie kazi sambamba na ngazi ya Chuo Kikuu, ili tuweze kuwa na usuluhishi wa jambo hili ama kuunda chombo au kukiteua chombo ambacho kitafanya kazi hiyo ambayo tunaihitaji.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipochangia hoja hii kwa maandishi, nilisema kwamba walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu, Serikali haiwajali walimu, haiwapi hata motisha ili wapate moyo wa kufanya kazi zao vizuri. Nilitaka Serikali iwakopeshe angalau pikipiki ili ziweze kuwarahisisishia usafiri wa kufika katika shule wanazofundisha kwa sababu, wengi wao wako mbali na shule wanazofundisha, hasa kule vijijini. Kwa hiyo, je, Mheshimiwa Waziri, Serikali inatoa tamko gani hapa Bungeni leo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Rukia. Pamoja kwamba walimu kama watumishi wa umma wana ruhusa ya kukopa, kupitia taratibu ambazo sekta hiyo imejiwekea, lakini kwa hili ombi maalum la Mheshimiwa Rukia, tutaangalia na kutathimini taratibu hizi ambazo zimetumika hivi sasa na namna gani ambavyo Serikali itaweza ikaziboresha ili kufanya urahisi zaidi kwa hao walimu kuliko ambavyo ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yako kwa kuwa elimu siyo *static* ni *dynamic*, na elimu inatakiwa itatue changamoto tunazokabiliana nazo, na kwa bahati mbaya katika nchi yetu toka tumepata Uhuru hatujawahi kufanya mabadiliko makubwa ya kielimu inayoweza kukabiliana na changamoto tunazozipata, kama Taifa tuna changamoto za *unemployment* na changamoto kadha wa kadha. *(Makofi)*

Je, Waziri unaweza kunithibitishia *future* yetu inakuwaje ili kuwa na elimu ambayo inakabiliana na changamoto tunazozikuta, kwa sababu elimu tuliyonayo sasa hivi kidogo haiendani na *challenge* tunazozipata kwa sababu wanafunzi tunawaandaa kuajiriwa wakati kimsingi ajira hazipo ili tubadilishe mtindo wa elimu wawe ni watu ambao wanapata *skills* na kuwa *creative? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemuelewa vizuri,

lakini nataka nimhakikishie kwamba mabadiliko yapo, Wizara ya Elimu imepanga kufufua Vyuo vya Ufundi kwenye ngazi ya wilaya na katika Bajeti yetu mwaka huu imeonyesha, lakini tuna vyuo vya *VETA* ambavyo pia vijana hawa wakiondoka hawajaandaliwa tu wakaajiriwe tu kwenye makampuni bali wana uwezo wa kujiajiri wenyewe kwenye sekta zao binafsi. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mie mchango wangu wa maandishi nilizungumzia umuhimu wa Serikali kupanua vyuo vyetu vikuu hapa nchini liende sambamba na ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa kila mwaka na nilikuwa *specific*, ningependa Serikali ilieleze Bunge kwamba kwa kuwa mwaka huu tumekuja na suala la kuboresha kilimo na nchi yetu kilimo ni uti wa mgongo. Chuo cha Sokoine ambacho ndiyo chuo pekee Tanzania kinachotoa *degree* zote za kilimo, Serikali ina mpango gani mahususi sambamba na Kilimo Kwanza kuweza kuboresha chuo hiki kwa maana ya miundombinu kwamba madarasa, mabweni, maktaba, maabara, kwa sababu ongezeko limekuwa kubwa lakini miundombinu ni ile ile. Kuna mpango gani maalum kwa ajili ya chuo hiki cha Sokoine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya majumuisho kwamba Serikali imeunda mpango maalum ambao ni mpango wa maendeleo wa elimu ya juu na ndani ya mpango huo tutaangalia maboresho na upanuzi wa vyuo vyetu ili kuweza kukidhi haja na mahitaji yetu ya sasa katika maeneo yetu ya vipaumbele. Kwa hivyo, Chuo cha Kilimo cha Sokoine kitafanyiwa maboresho na miundombinu na rasilimali watu kufuatana na azma yetu ya Kilimo Kwanza. Lakini kipindi hiki pia Serikali imejipanga kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chuo kingine cha kilimo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, lakini pia Serikali inasaidiana na sekta binafsi katika ujenzi wa chuo kingine cha kilimo katika mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda niishukuru Serikali kwa kuweka sera ya kuweka Bodi ya Mikopo ya Vyuo Vikuu ili kusukuma mbele gurudumu la elimu. Sasa katika mchango wangu wa maandishi nilijikita katika suala la mikopo. Kuhusu mikopo inayotolewa idadi kubwa ya wadau wetu wanaopata nafasi ya kuingia Vyuo Vikuu ni maskini. Lakini katika mchango wangu nilielekeza sana katika kuishauri Serikali, mikopo hiyo ibadili mpango wake wa awali wa kutoa mikopo kwa viwango, badala yake mikopo hii itolewe sawa kwa wale wote waliopata fursa ya kupewa mikopo hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri atalieleza nini Bunge letu hili hapa tulipo sasa hivi kuhusiana na suala hili kutoa mikopo kwa usawa?

*(Hapa kengele ililia)*

**MWENYEKITI:** Sawa hiyo kengele tayari, usawa kwa usawa au usawa kutegemeana na umaskini zaidi au vipi, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Rashid Ali

Omar kama nilivyozungumza katika hotuba ya majumuisho kuwa Tume ya Mheshimiwa Rais iliyoundwa kwa ajili ya kuangalia matatizo ya mfumo wetu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu umefanya mapendekezo na naomba niseme kwamba tupo katika mchakato wa kupendekeza mapendekezo yale, mategemeo yetu ni kwamba yanatoa ufumbuzi wa matatizo tuliyokuwa tumekumbana nayo katika miaka ya nyuma tangu bodi hii imeundwa mwaka 2005. Sasa nilihakikishie tu Bunge lako Tukufu kwamba vigezo vipya vitahakikisha kwamba vinajikita katika ufanisi wa zoezi hili la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi na pia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu nilikumbusha matatizo matatu ya walimu wa Halmashauri ya Moshi. Kwanza kulikuwa na walimu wapya 130 ambao walikuwa wanadai shilingi milioni 390 na walikuwa hawajalipwa ingawa waliingia pale Moshi kuanzia Januari mpaka Juni, wakati Waziri Mkuu anasoma hotuba yake. Hili nakumbushia shilingi milioni 67 za walimu wanadai toka mwaka 2008 na tatu kuna walimu wamenifuata hapa zaidi ya kumi waliajiriwa kwa muda wamemaliza kazi yao wamefanya vizuri mpaka leo hawajalipwa. Kwa hiyo, namuomba Waziri kama anaweza kunihakikishia hayo yote niliyoomba wakati wa Waziri Mkuu je, yatakuwa yamefuatiliwa, yatakuwa yametekelezwa, kama bado yatatekelezwa lini?

**MWENYEKITI:** Anaulizia *arrears* kwa walimu wapya na kwamba mtalipa lini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi huu ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza katika hotuba yangu ya majumuisho kwamba tunapokea madeni haya kutoka kwa walimu na tumeweka nia thabiti ya kuhakikisha kwamba tunayahakiki kwa muda muafaka na yale yote ambayo yatakuwa yamehakikiwa na kukubaliwa kwamba ni madai halali basi yataweza kulipwa mara moja. Lakini kama kuna walimu ambao tangu wameripoti mwezi Januari hawajalipwa mpaka leo naomba hao waripoti haraka sana TAMISEMI ili mishahara kuweza kulipwa mara moja. *(Makofi)*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi niligusia tatizo moja kubwa linalowagusa Watanzania walioko shule Maalum ya Mazoezi pale Kabanga ya walemavu wakiwemo walemavu wa ngozi. Tutakumbuka wote kwamba kuna tatizo liliikumba nchi yetu la mauaji ya kikatili mwaka 2009 ambapo kwa mkoa wa Kigoma, wale wote waliokuwa wanakimbia vijijini kuogopa wasiuwawe, walianzisha kituo pale Shule ya Mazoezi Kabanga.

Mheshimwia Mwenyekiti, ninaomba tamko la Serikali kwa kuwa kuna watu wazima wengi waliopo kwenye Shule ya Mazoezi Kabanga ambayo shule ile inahudumia walemavu wa aina mbalimbali. Hao watu wazima ambao ni wazazi wa walemavu wa ngozi hawasomi pale lakini kwa kuwa hawana sehemu ya kwenda kukaa wamelazimika

kuhifadhiwa pale, ninaomba tamko la Serikali, ni juhudi gani za haraka na za makusudi za kuandaa makazi ya Watanzania hao ambao hatujapata sehemu ya kwenda kuwasitiri asanteni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, nani anajibu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Agripina kama ifuatavyo, ni hoja ambayo sikuitambua kabla kwa bahati hoja za maandishi zilikuwa nyingi sana kwa hivyo zingine tumeshindwa kuzijua hoja zake ni zipi. Naomba nilipokee suala hili na kwa ushirikiano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tuone namna ambavyo tutatoa ufumbuzi mzuri kwa tatizo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni suala mahususi kwa hiyo linaweza kushughulikiwa, Mheshimiwa Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, ni kweli kwamba Serikali inafanya jitihada nyingi za kuhakikisha kwamba walimu wanakuwepo kwenye maeneo mbalimbali. Lakini pamoja na hayo bado walimu hawatoshi katika maeneo mengi hususan vijijini ambapo ni kweli kwamba walimu wanapangwa kwenda kule lakini wengine hawaendi na hii sasa inafanya tunakosa walimu maeneo mengi. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kutoa marupurupu ya mazingira maalum yaani *hardship allowance* kwa walimu wanaopangiwa maeneo ya vijijini ili waweze kwenda kule wanakopangiwa, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Alisema laki tano zinatolewa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa suala la Mheshimiwa Wenje kuwa kwenye hotuba yetu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma tulisema kwamba mwaka jana tumepitisha sera ya malipo na motisha na kwamba tayari tumekamilisha mkakati wake ambao utaanza kufanya kazi na kutumika mwaka huu wa fedha 2011/2012 na suala la mazingira magumu limezingatiwa katika sera hii. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante katika mchango wangu wa kuzungumza hapa na wa maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu kitengo cha elimu ya watu wazima. Tarehe 27 Januari, 2009 Katibu Mkuu ndugu Hamis Dihenga, alitoa barua kwa Makatibu Tawala kwamba kitengo hiki sasa kitakuwa idara kamili. Lakini mpaka sasa ni miaka miwili hakuna kinachoendelea, bado Elimu ya Watu Wazima inaendelea kuwa chini ya idara ya elimu. Sasa napenda kujua huu utaratibu mzuri ambao Katibu Mkuu alitoa tamko rasmi umefikia wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kuhusu hoja ya Mheshimiwa Diana

Chilolo kwamba Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni Idara kamili ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na yenyewe ndiyo inasimamia sekta hii au sekta hii ndogo kwa nchi nzima na inapokea katika Halmashauri, katika idara mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kama nilivyokuwa nimechangia katika mchango wangu wa maandishi, baada ya mgomo wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho pia uliwashirikisha na walimu wa chuo hicho. Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mtoa hoja walikwenda chuoni pale kuongea na menejimenti, pamoja na wahusika na moja ya sababu ambazo walikuwa wanasema kuchangia kutoshughulikiwa kero zao kwa haraka ni pamoja na urasimu ambao upo kwenye menejimenti na moja ya mapendekezo waliyoyatoa, mamlaka yashuke katika *college* husika na Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari alishatoa agizo, sasa ningependa kufahamu agizo hilo limefikia wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo; ni kweli kwamba katika ziara ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliifanya Chuo Kikuu cha Dodoma mwezi Januari, hoja hii ilijitokeza na pia ushauri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuwa kwamba chuo kiangalie sasa namna ambayo itateremsha wata-*decentralize* utawala ule katika chuo. Ili vyuo navyo ndani ya Chuo Kikuu viwe na mamlaka ya kiutawala na kiuendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba hatua za mwanzo zimeshachukuliwa na kwa maana kwamba kuna ngazi za uendeshaji na utawala ambao tayari imekabidhiwa vyuo husika, hivi sasa mchakato unaendelea kwa awamu pili ambayo itakamilisha zoezi zima la *decentralization* katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kitawezesha sasa vyuo mbalimbali vya Chuo Kikuu kile kuwa na mamlaka mahsusi ya uendeshaji na utawala katika vyuo.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliongelea umuhimu wa mabweni kwa shule za kata zilizoko vijijini, mbali na umbali wa baadhi ya vijiji kwenda kwenye kata hususan vijijini ni tofauti na mijini. Nikiangalia kama umbali wa kutoka Luono kwenda Kidalu, umbali wa kutoka Ujungu kwenda Mtekente ilipo sekondari, umbali wa kutoka Mlandala kwenda Ulugu, umbali wa kutoka Ng'anguli kwenda Kinampanda ilipo sekondari ni mbali sana. Lakini vilevile kwetu kule vijijini utamaduni wa kujenga nyumba za kupangisha haupo, kwa hiyo, unakuta vijana hata kama wangeamua kupanga, wanapanga kwenye matembe, madaftari yanavujiwa na wale wanaotaka kurudi majumbani kwao wakati mwingine wa mvua wananyeshewa mvua njiani na wamekuwa wakitumia baiskeli. Je, Serikali inatoa tamko gani sasa kuweka msisitizo kwenye kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi hasa wa vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu linalotaka kujua mpango wa Serikali wa ujenzi wa mabweni kwa

matatizo yanayopatikana kwa watoto wetu. Kwa msimu huu wa mwaka 2011/2012 kupitia mpango wa maendeleo ya sekondari (MMES), tumepanga kujenga mabweni kwenye shule zetu yapatayo 500. Utaratibu tunaotumia ni kutoa mgao kwa mikoa, halafu mikoa inafikisha kwenye Halmashauri na pale ambako kuna ugumu ambao unaikabili na ni mzito zaidi ndiko ambako unapeleka *priority*.

Kwa hiyo, Halmashauri zenyewe zinaona ni shule gani ipo mbali sana na vijiji vyake ili kupeleka ile *priority* ya kujenga lile bweni na wewe mwenyewe kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ni mmoja kati ya wadau kwenye Halmashauri ile kama Diwani mwenza una nafasi pia kushawishi kwa kuangalia mazingira haya. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nilikuwa tu napenda kufahamu ni lini kituo cha kutengenezea vitabu vya nukta nundu kilichopo pale Uhuru Mchanganyiko kitafanya kazi kwa uwezo wake wote ili kuondoa tatizo lilipo kwenye shule maalum na vitengo maalum vya watoto wasioona hapa nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Margareth Mkanga, naomba nilipokee hili kama tatizo maalum la kituo hiki na Wizara yangu itafuatilia kwa karibu ili tuweze kuwaondoshea adha wananchi wenzetu hawa. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa vile baadhi ya shule za sekondari wazazi wamejitahidi kujenga nyumba kwa ajili ya walimu hasa hizi shule zetu za kata, lakini kwa bahati mbaya sana zile nyumba hazina ubora wa kutosha, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutoa ushirikiano kwa wananchi wale ili kukamilisha shule hizo ziweze kuwa na kiwango na kufanya walimu waishi kufurahia kuwepo shuleni hasa Mbarali tumejenga nyumba nyingi ambazo zinahitaji msaada tu wa kuwaunga mkono wale wananchi ili ziweze kuwa bora, wale walimu waweze kuzifurahia. Na vilevile…

**MWENYEKITI:** Inatosha yaani anasema kumalizia nyumba zilizoanza.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili ambayo tumeanza kuitekeleza mwaka 2010, tuna mpango mahususi wa kuhakikisha kwamba tunazikamilisha shule za sekondari za wananchi au baadhi ya shule hizi za wananchi hasa zile ambazo zipo katika hali ambayo siyo nzuri ili ziende katika *stage* ambayo tunaita *fully functional secondary schools.* Kwa hiyo, zile ambazo madarasa yake hayajakamilika tutakamilisha, nyumba za walimu tutaangalia tuzikamilishe na miundombinu mingine kama maabara na maktaba tukamilishe ili utoaji wa elimu katika shule hizo uwe ni ule ambao una tija kwa wanafunzi ambao wanasoma katika shule hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Tizeba!

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Katika michango yangu mbalimbali nimekuwa nazungumzia suala la *skills development levy* ambayo imekuwa haitoshi kufikia azma ya Taifa ya kujenga angalau Vyuo vya Ufundi Stadi yaani *VETA* katika kila Wilaya. Tozo hii ilipunguzwa katika Bajeti ya Wizara ya Fedha na tukawa tumeomba Serikali itafute utaratibu wa kuiongeza ili kila Wilaya angalau tuweze kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi yaani *VETA.* Jambo hili sikulisikia linatolewa majibu na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri majibu! Mimi lakini nilisikia. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa majibu yafuatayo kwa hoja ya Mheshimiwa Dkt. Tizeba kuwa, ni kwamba Serikali imeweka utaratibu ambao utaiwezesha kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya na tuliainisha katika hotuba ya majumuisho kwamba kwa sasa hivi tumetaja pesa za mkopo, tunakopa pesa kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika jumla ya dola milioni 600 ambapo sehemu ya pesa hizo zitakuja kwenye sekta ya elimu na tutatumia pesa hizo kwa ajili ya kujenga vyuo hivi kwa awamu tukianzia na vyuo 28 na tutegemee kwamba tutamudu kwenda huko. Thamani ni kama bilioni tatu mpaka sita kwa kila chuo, nadhani tukitumia pesa hizi tutapiga hatua nzuri tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa!

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu la msingi ambalo niliwasilisha kimaandishi, mojawapo niliomba ufafanuzi kwamba sasa tunahitaji elimu katika *secondary school* yenye *emphasis* ya *science* na katika hilo nilipendekeza mikakati kadhaa ambayo ingekuwa vizuri ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kutambua hilo Bunge lako Tukufu mwaka jana liliidhinisha shilingi bilioni 19.6 zitumike kwa ajili ya kutegemeza *science and technology* katika taasisi zetu za elimu ya juu ambayo mpaka miezi miwili iliyopita zilikuwa hazijapelekwa hata senti moja.

Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini juu ya ahadi kwamba sasa Wizara itaimarisha shule zote za sekondari na hazitaitwa *yeboyebo* kama ilivyokuwa mpaka sasa tulikuwa hatujapeleka hata senti moja katika fedha iliyoidhinishwa katika kipindi hiki cha fedha? Sasa hiyo nguvu itatoka wapi?

**MWENYEKITI:** Mnapojenga maswali yenu jengeni ya kutosha muda uliopangwa. Mheshimiwa Waziri majibu! *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mgimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ambazo zimetengwa katika mwaka huu wa fedha Bunge lako likiidhinisha chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili, naomba nilihakikishie Bunge kwamba pesa hizo zitatumika kikamilifu kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya sekondari na tutaweka mkazo katika sayansi kama ambavyo kila siku tumekuwa tunafanya kwa sababu haya ndiyo maeneo ambayo yatatuwezesha kupiga hatua za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu kwamba pesa hizo zitatumika kwa ajili ya maendeleo ya shule za sekondari.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maria Hewa! *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa kuzungumza Bungeni nilizungumzia suala la uanzishwaji wa Vyuo Vishiriki vya Elimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikiwemo cha kuanzisha Chuo cha Butimba ambacho kimelengwa kwa upande wa Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi lakini sikupata jibu. Naomba kupata majibu kutoka kwa Waziri, wamefikia hatua gani ili na sisi tuweze kukiona hicho chuo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala hili niseme kwamba tunalipokea kwa ajili ya kulifanyia kazi Wizarani yaani tutalifanyia tathmini, tutaangalia uwezo wa Serikali na tuangalie mazingira yalivyo kwa pesa zilizokuwepo hasa katika mipango yetu tuliyokuwa nayo ya maendeleo ya elimu ya juu tutakavyoweza kukiingiza katika mwaka huu wa fedha ama kukiingiza katika miaka inayofuata lakini tutalifanyia mkakati ili tuweze kupata suluhisho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mariam Mfaki!

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nataka kujua katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la mtaji kwa ajili ya vijana ambao watajifunza katika vyuo ambavyo vitajengwa. Je, Serikali imejiandaa vipi kuwaandalia mfuko ambao wakimaliza mafunzo hayo wapate kukopa ama kwa kudhamini angalau hata vyeti vyao ili ufundi huo watakaoupata wakaweze kujiajiri moja kwa moja watakapomaliza chuo. Napenda kujua, je, Wizara imejiandaaje na hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umemuelewa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mariam Mfaki kama ifuatavyo; katika hivi vyuo ambavyo tutavijenga yaani Vyuo vya Ufundi Stadi, jambo muhimu ambalo tutakuwa tunalifanya ni kubainisha stadi ambazo zinafaa kufundishwa katika vyuo hivyo kwa maana kwamba viendane na mazingira na mahitaji ya Wilaya hiyo. Kama Wilaya hiyo ina migodi maana yake ni kwamba stadi zile zitaendana sana na kazi ambazo zipo katika Wilaya hiyo. Mategemeo yetu ni kubainisha stadi zile zenye umuhimu katika Wilaya husika. *(Makofi)*

Lakini pia kwa kutumia mifumo ya ufundishaji ambayo tunaijenga kwa kushirikiana na Vyuo vya Jamii vya Canada ambavyo mfumo wake ni mafunzo yenye kuzingatia umahiri kwa maana ya *competence base curriculum.* Mafunzo haya tunayategemea kwamba yatawawezesha baadhi ya waliopata ajira na wasiopata ajira kuweza kujitengenezea wao wenyewe ajira kwa kujiajiri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa mamlaka niliyonayo kufuatana na kifungu cha 104 naongeza dakika 30 kuanzia saa mbili kasoro robo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Susan Kiwanga karibu!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye hotuba ya Waziri ya mwaka 2011/2012 amezungumzia kuhusu kuimarisha Idara ya Sekondari hasa katika matumizi ya *TEHAMA* na amesema kwamba wataboresha, watakwenda katika sekondari kuanzia sekondari 30 lakini kwa majaribio. Lakini katika hotuba ya mwaka 2009/2010 katika Idara ya Shule za Sekondari walisema kwamba watakuwa na uboreshaji wa kuimarisha ufundishaji wa *TEHAMA* katika shule 500. Sasa hapo ndiyo inanishangaza, mwaka uliopita ni shule 500 zipi? Na mwaka huu shule 30 vipi? Ni kweli mnakwenda mbele au mnarudi nyumba? Naomba ufafanuzi! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Susan Kiwanga, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuliweka nia thabiti ya kubadilisha mfumo wetu wa ufundishaji ili uweze kutumika zaidi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ama *TEHAMA.* Lakini katika mpango huu kuna mradi ambao tumeuita *Tanzania Beyond Tomorrow*. Katika utekelezaji wake tumebaini ama kugundua kwamba mahitaji yake ya kifedha ni makubwa zaidi kuliko vile ambavyo tulikuwa tukitarajia au tukifikiri. Kwa hiyo, imebidi katika utekelezaji wa mpango huu tuweze ku-*scale down* kwa sababu uwezo wetu wa kifedha hautaweza kufikia kiwango kile ambacho tulikuwa tukidhani. Sina uhakika kama tuliainisha shule 500 za sekondari lakini kama tulifanya hivyo niseme tu kwamba hatuna uwezo wa kuweza kufanya hivyo na tumejipanga ili tuweze kulifanya jambo hili kwa awamu badala ya kuchukua hatua kubwa sana ambazo hatuziwezi kifedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Susan Lyimo! Msiwe mnakaa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni ukweli usiopingika kwamba ubora wa elimu hapa Tanzania umeporomoka na kigezo kikubwa tunachokiangalia ni matokeo ya mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ubora huu siyo tu kwamba umeporomoka katika shule za msingi na sekondari lakini umekwenda mpaka katika Vyuo vya Elimu ya Juu na niseme kwamba nakumbuka mwaka juzi Waziri wa Elimu alikuja na kusema kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekuwa chuo cha 13 bora katika Afrika kati ya vyuo mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ndiyo kioo cha vyuo vyetu vikuu kimeshika nafasi ya 34. Sasa naomba kwa sababu Mheshimiwa Waziri ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na alikuwa Mhadhiri pale, anaweza kutueleza tatizo ni nini na wana mkakati gani ili kuhakikisha kwamba tunarejesha hadhi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam? Ama tatizo ni *management* kwa sababu natambua kwamba wakati alipokuwa Profesa Luhanga chuo kile kilikuwa kinakwenda vizuri. Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao kuhusu hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika na hizi takwimu ambazo amezitaja kwamba tumeanguka mpaka nafasi ya 34 katika Afrika lakini niseme tu kwamba tunaendelea kuvifuatilia vyuo vyetu na kuwekeza katika vyuo hivi ili viendelee kung'ara katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Katika *exchange program* kati yetu na Uganda na kati yetu na Msumbiji nimetoa taarifa hapa katika Bunge lako Tukufu kwamba tuna wanafunzi wengi zaidi wa Uganda na Msumbiji ambao wametaka kuja kusoma hapa kuliko wale wa Tanzania ambao wamekubali kwenda kusoma katika nchi hizo. Kwa kuonyesha kwamba wanapata elimu nzuri zaidi hapa kuliko kule lakini naona elimu hii hasa katika Vyuo Vikuu itaboresha zaidi pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wengine watakapoacha taratibu za kugeuza vyuo vile kuwa sehemu za kufundishia siasa kuliko elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na kinachotakiwa ni zile Sheria ulizosema zikazwe basi! Zile Sheria ulizosema zipo basi zisimamiwe kama ni Sheria, nadhani ndivyo ilivyo! Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi!

**MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilisema kwamba Sera ya Taifa ya UPE ya mwaka 1974 mpaka 1977 iliingiza watoto wengi sana katika shule za msingi na baadaye wakawa watoto wengi sana hawana ajira baada ya kumaliza shule za msingi. Kwa hiyo, tuliomba shule za ufundi zifufuliwe na Waziri amejibu hapa kwamba wana mpango wa kufufua Shule za Msingi za Ufundi. Lakini mimi nasema ni shule zipi, katika Mkoa upi au Wilaya zipi? Mimi niliomba sana suala hili liangaliwe katika mikoa ya pembezoni kufufua Shule za Msingi za Ufundi zilizopo katika mikoa ya pembezoni na hasa katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi kwa vile mpaka sasa *VETA* bado haijawa tayari na ni miaka mitano sasa, tunaomba tuanzie na Mkoa wa Lindi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, unafufua Shule za Msingi za Ufundi au unataka Shule za Ufundi?

**MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI:** Kufufua Shule za Msingi za Ufundi zilizopo mikoani ili kuendeleza watoto ili waweze kupata ajira.

**MWENYEKITI:** Haya basi tumekuelewa, Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Fatuma Mikidadi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngazi ya shule za msingi ziko hivyo kama shule za msingi na juhudi ambazo Serikali imefanya ni kuhakikisha kwamba udahili wa watoto wote wa rika lengwa wanajiandikisha katika shule za msingi na tumefanikiwa na sasa hivi tunadahili zaidi ya 95% ya watoto wa rika lengwa kwa Tanzania nzima na tunaelekea katika 100%. Shule zile ambazo zina fani tofauti ya ufundi, kilimo, biashara na kadhalika hizi ni shule za sekondari ambazo mkakati na utaratibu wake ni tofauti, tutaendelea kuziimarisha na hizi zimetokana na maendeleo ya elimu kuziondosha shule za sekondari katika mpango wa *general secondary education* na kuziwekea mikondo au mitaala mbalimbali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante,Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeelezea juu ya uchakavu wa shule za msingi hasa katika shule za msingi za Mwese, Katuma, Kabungu, Ikola na Karema. Je, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ana maelezo yapi juu ya ukarabati wa shule hizo?

**MWENYEKITI:** Shule maalum hizi? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya ukarabati wa shule za msingi ni mipango ambayo inafanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa tukianza na Serikali zenyewe za vijiji ambako kuna Kamati za shule wanabaini mahitaji ya ukarabati lakini pia kwa ngazi hiyo inapowazidi uwezo wanaingiza kwenye Halmashauri ya Wilaya kupitia Baraza la Madiwani na Halmashauri itafanya mawasiliano au kupitia fedha ambazo TAMISEMI inatuma kwenye Halmashauri kwa ajili ya maendeleo, Afisa Elimu anaweza kujua ana matatizo ya shule ngapi ili aweze ku-*allocate funds* kwa ajili ya ukarabati. Wakati mwingine Halmashauri zenyewe kupitia *own source* zao wanaweza pia kuongeza nguvu kukarabati shule zilizopo ili kuweza kuondoa tatizo hilo. Hilo nalizungumzia hasa kwa shule za msingi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliongelea kuhusu jitihada za Serikali katika ku-*foster equity* kati ya walio nacho na wasio nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimependekeza na kutoa ushauri kwa Serikali ili kuweza kupunguza tofauti iliyopo kati ya walio nacho na wasio nacho ni lazima walimu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu wapewe motisha maalum ambazo zinaweza zikawa *calculated* kijiografia au kwa vigezo vingine ambavyo vinatokana na tafiti mbalimbali. *(Makofi)*

Je, Serikali imejipanga vipi katika kutoa motisha kwa walimu wanaoishi katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na nyumba, mikopo ya vyombo vya usafiri na posho za *hardship* katika kazi zao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Dkt. Kigwangalla nadhani limejibiwa hili sijui ulikuwa umetoka. Mheshimiwa Chambiri!

**MHE. DKT. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zote tulizonazo ndani ya Jimbo la Babati Mjini yaani shule za Serikali ni za kata. Hizi shule hazina maabara na ukiangalia *perfomance* ya shule za Babati Mjini ilikuwa mbaya sana kwani shule moja inapitisha wanafunzi wawili na hao wawili wote ni *division four*. Sasa namuuliza Waziri wa Elimu kwamba ili kuweza kunusuru Babati Mjini tunahitaji tupate maabara ndani ya shule zetu na sababu Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi kwamba katika kila shule ya kata tutapata maabara, naomba sasa nielewe ndani ya Jimbo la Babati Mjini hizo maabara zitajengwa lini ili tuweze kuwanusu wanafunzi wa Babati Mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Atajibu kuhusiana na sera, hataweza kusema Babati. Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mkakati maalum kuhakikisha kwamba tunaziboresha shule zetu hizi za sekondari na kwa upande wa sayansi, tunachukua kila hatua inayowezekana ili kuhakikisha kwamba maabara zinajengwa katika shule zote zenye mikondo ya sayansi. Hakika tutaenda awamu kwa awamu na kama nilivyosema awali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, awamu ya pili, tutaangalia maeneo yale ambayo yana changamoto kubwa ili tuweze kuanza kujengea miundombinu yake kukamilisha shule hizi ili ziweze kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za awali nina imani vivunge hivi vya *UNESCO* ambavyo tulipata hivi karibuni vita-*target* shule za Babati ili kuweza kupata msaada wa awali kabla hatujaweza kupata maabara katika shule hizi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Chuo cha Ualimu cha kawaida cha Mtwara kina mazingira mazuri kabisa yanayofaa kuanzishwa kuwa Chuo Kikuu Kiambata. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 - 2010 ilibainisha wazi kwamba katika miaka mitano ijayo chuo hicho kingekuwa Chuo Kikuu Kiambata chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Serikali kupitia aliyekuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, aliliambia Bunge hapa kwamba jambo hili lilikuwa kwenye mchakato na lilikuwa linakaribia kuisha, lakini hadi leo hatujaelezwa chochote, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaambia wananchi wa Mtwara na mikoa yote ya Kusini jambo la mchakato limefikia wapi na lini chuo hicho cha kawaida cha Ualimu cha Mtwara sasa kitakuwa Chuo Kikuu Kiambata, chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hata mimi nakumbuka, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Juma Njwayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uhaba huu wa walimu, Serikali inafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa vyuo vya kuweza kuzalisha walimu. Tupo kwenye mchakato, matatizo ya utekelezaji na ukamilishaji wa michakato ili tuwe na vyuo vingi zaidi kwa ajili ya kuzalisha walimu wengi zaidi. Bahati mbaya kwa chuo hiki imechukua muda, sina jibu kamili sasa hivi la kusema kwamba lini tutakibadilisha kuwa Chuo Kikuu Kishiriki, lakini naomba tu nimuombe Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane baada ya Bunge hili ili niweze kumpa kwa uhakika taratibu ambazo tumefikia, nini tutafanya na tutajitahidi kuharakisha kwa nia yetu ile ile ya kuweza kuzalisha walimu wengi zaidi ili kupunguza tatizo la walimu nchini.

**MWENYEKITI:** Vyuo hivyo vilikuwa ni Mkwawa, Chang'ombe na Mtwara. Mheshimiwa Gaudentia Kabaka! Hatukusikii, hama hapo.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee tu kwenye majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ni kwamba kuwa Chuo Kikuu Kiambata ina maana chuo hicho kiendelee kuwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tofauti na Chuo Kikuu Kishiriki ambacho kinaenda moja kwa moja wakati ule ilikuwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa sheria zilizoanzisha hizi taasisi ni mbili tofauti, kilichokuwa kinaendelea ni kuhakikisha sheria hizi sasa zinabadilishwa ili ziweze kukubaliana katika kuhakikisha hiki chuo kinakuwa Chuo Kikuu Kiambata na ndiyo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sheria hii bado inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya mgawanyo wa rasilimali za Taifa kwa usawa na nikazungumzia juu ya mgawanyo wa masuala ya elimu kwamba Mkoa wa Rukwa ambao upo pembezoni hauna Chuo Kikuu chochote na wala Chuo cha ufundi, je, Serikali ina mpango gani ili kuuwezesha mkoa huu kupata Chuo Kikuu au Chuo cha Ufundi ukiachia kule Katavi ambako kuna Chuo cha *VETA?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni maswali yanayojirudia lakini naomba ujibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Desderius Mipata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mikakati kwa Mkoa wa Rukwa ambayo ni pamoja na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya, lakini pia tuna ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Katavi. Kwa hivyo, tutauangalia mkoa huu kwa namna ambayo Mheshimiwa Mbunge angependa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba kuna Idara kamili ya Elimu ya Watu Wazima pamoja na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kwamba walimu wa MEMKWA wanafanyakazi nzuri kule vijijini hasa ninakotoka mimi, lakini wana malalamiko makubwa kwamba malipo yao, posho zao, stahili zao hawazijui, hawazipati na hawana vitambulisho na hawajui ni nani anawalipa.

Sasa ningependa ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hivi ni nani hasa anayestahili kulipa malipo au posho za hawa walimu wa MEMKWA kati ya Kijiji, Halmashauri ya Wilaya au Serikali Kuu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Mohamed Missanga linalohusu walimu wanaofundisha programu ya MEMKWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wale ni mpango wa ndani ya Halmashauri na wanalipwa na Halmashauri zenyewe kupitia Idara ya Elimu. Kwa hiyo, kama kunakuwa na udhaifu wa ulipaji ni pale kwenye Halmashauri yenyewe. Sasa kwa sababu tumepata taarifa basi tutaanza kufanya ufuatiliaji wa programu hiyo kwa sababu ni programu ambayo kwa kweli inaleta manufaa makubwa kwa sababu vijana hawa ambao walikosa nafasi ya kwenda shule za msingi kwa umri uliotakiwa, wameonjeshwa matumaini makubwa sana na kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha sekta hiyo ili tuweze kupata mafanikio makubwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sisi Wabunge na watumishi wengine wa umma na kwenye sekta binafsi tunapata fursa ya kuchagua mishahara yetu tuipate kwenye taasisi gani au kwenye benki gani na baadhi ya waajiri hata hutoa pesa taslimu. Lakini kwa walimu, wao wanalazimika kupokea kwenye benki moja tu *NMB* bila kujali umbali wa wanakotoka. Kule kwangu kuna mahali ambapo unasafiri saa nne ili kuweza kufika benki na pale benki mwisho wa mwezi walimu wanapanga msati mrefu. Sasa Serikali iseme ni lini itafanya uamuzi, mwalimu nae awe na *choice* kwamba mshahara wake aupokelee wapi, asilazimike kuchukua mshahara kupitia benki moja na vilevile Serikali iseme kama kweli siyo uonevu kwamba unakuta shule haina mwalimu hata mmoja wa hesabu lakini mtihani wa somo la hesabu unakuja katika mitihani ya *form four*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tayari umeshasema, inatosha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa January Makamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba walimu, lakini siyo walimu pekee, ni watumishi wote wa Serikali ndiyo wanaopokea mishahara yao kupitia benki ya *NMB*, na sababu ambazo ziliipelekea Serikali kufanya mkataba na *NMB* ni kwa sababu ya mtandao wake ambao umefika mpaka maeneo ya vijijini, lakini bado tumefanya mawasiliano na *NMB* kuweza kuanzisha *mobile bank* na tumeshaanza kuona magari yao ili utaratibu huu uweze kuwafikia watumishi wetu, walimu na sekta nyingine kwenye maeneo yao ya vijiji. Tunaendelea kufanya mazungumzo na *NMB* ili waongeze *mobile banks* zile ziweze kutembea maeneo yote ili walimu waweze kukutwa kule na waweze kutumia *ATM cards* zao waweze kupata mishahara yao kwenye maeneo yao. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuuliza hoja moja. Katika mchango wangu nilizungumzia suala la *TSD* kuwa na hali mbaya kwa sababu tunajua kwamba hii ni Idara muhimu ambayo inashughulika na masuala ya ku-*promote* walimu hususan katika miundo ya madaraja yao; lakini kumekuwa na taarifa hasa nichukue *case study* kwa Wilaya ya Kasulu, ofisi ya *TSD* imeweza kuthibitisha kwamba haijapokea fedha ambazo

zingetumika kwa ajili ya kukaa vikao ili kuweza kupandisha madaraja ya walimu ambao ni wengi kwa Wilaya ya Kasulu, wengine wamesoma wamefikia viwango vya Shahada, wengine Stashahada na wengine kwa kigezo cha umri kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi ya Umma, waieleze Kamati yako ni kwa nini mpaka leo hii tunapozungumza kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ofisi inasema kwamba iliweza kukaa kikao kimoja na wakati ni *quarter system* na walipaswa kukaa vikao vinne ili kuweza kufanya *promotions* za walimu ambao hawajawa *promoted?* Tatizo ni nini na kwa nini fedha hizo hazijaenda?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja ambayo Mheshimiwa Moses Machali ameitoa ya *TSD* kuwa na hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika kipindi cha katikati *TSD* iliyumba kutokana na uchache wa watumishi, pia kulikuwa na matatizo ya kifedha. Kuanzia mwaka jana na mwaka huu tumewaombea maombi maalum, tumewapelekea watumishi wa kutosha na mwaka huu katika Bajeti yetu tumeonesha kwamba tutawawezesha kielimu pamoja na vifaa. Ningependa tu niseme hilo suala la kwamba watu hawajawa *promoted* kwa sababu pesa tulizopeleka ni chache nadhani kidogo nina wasiwasi nalo. Ninahisi kuna matatizo ya ziada sana katika *TSD* ya Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kwamba aniachie na tutalifuatilia kuona tatizo ni nini lakini pia kuhakikisha kwamba wanafanyakazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa hivi nchi yetu ina uhaba mkubwa sana wa madaktari ambapo kwa maeneo ya vijijini daktari mmoja anahudumia hadi wagonjwa 100,000 kwa mfano, Lindi Vijijini hiyo imeonekana katika ripoti. Pia katika Mkoa wa Rukwa, daktari mmoja anahudumia hadi wagonjwa 200,000, vilevile na Kigoma. Kwa kawaida daktari mmoja anatakiwa angalau ahudumie wagonjwa 25,000. Mheshimiwa Rais ameliona hili na ameona kwamba ni vyema nchi yetu ikazalisha madaktari 1,000 kwa mwaka. Kwa utaratibu wa sasa hivi ukiomba kujiunga nachuo, *Tanzania Council of Universities (TCU)* ndiyo ina *select* wapi mwanafunzi aende. Wapo wanafunzi wengine ambao wanapangiwa Muhimbili na wengine wanapelekwa *IMTU.* Tatizo la *IMTU* ni kwamba wanafunzi wanatakiwa walipe ada kwa dola na kwa mwaka ada ni dola 4,500 na Serikali inatoa *full sponsorship* ya *only* shilingi milioni 2.6 kwa wanafunzi wote wanaosoma udaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuongea na mmiliki wa chuo ili aweze kuruhusu wanafunzi walipe ada kwa shilingi kwa sababu mwanafunzi akipewa shilingi milioni 2.6 na Serikali, zinazobaki ina maama mzazi anatakiwa alipe, hakuna mtiririko mzuri wa ulipaji wa ile ada kwa sababu inategemea na *exchange rate*. Je, Serikali inasemaje juu ya hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wakiwa ni *IMTU* unalipa kwa dola, haya.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba tunalipokea suala hilo kwa ajili ya kulifanyia kazi na vyuo vyetu vya *private* ambavyo vinatoza tofauti na shilingi ya Tanzania, lakini namba mbili pia ni kwamba Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaosomea udaktari wa binadamu, meno na mifugo kama ambavyo imekuwa ikifanya katika miaka iliyopita na mwaka huu tunaazimia kutoa ufadhili kwa wanafunzi 1,700 katika vyuo vyetu vikuu. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nchi yetu sasa hivi inakaribia kukumbwa na janga lingine la Kitaifa la kuwa na watoto mambumbumbu. Ninazungumza hili kutokana na matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana ambapo asilimia 88 walipata *zero* na *division four* na asilimia 11.8 ndiyo walipata *division one* sababu kubwa iliyosababisha kufeli huko ni upungufu wa walimu wa sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka Bunge lililopita tulipitisha Itifaki ya Afrika Mashariki ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa inaruhusu *movement* ya walimu kutoka nchi moja kwenda nyingine, lakini kitu ambacho kinatubana kama nchi tumejifunga mpaka mwaka 2015. *(Makofi)*

Kwa kuzingatia unyeti wa suala hili je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufungua hicho kizingiti tulichokiweka mpaka mwaka 2015 wakati tunazalisha walimu wetu wa ndani kuweza kupata walimu wengine kwa mkataba wa muda mfupi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge tayari, mnapouliza maswali muwe *brief*.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati katika shule zetu za sekondari, tofauti na ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezungumza, tayari tumesaini mkataba na nchi za Afrika Mashariki kwamba katika maeneo ambayo Tanzania imefungua ajira kwa ajili ya wananchi wa nchi nyingine nne za Afrika Mashariki ni pamoja na walimu wa sayansi na hisabati, kuweza kufundisha katika nchi yetu ya Tanzania. Walimu wameanza kuja na lakini nchi hizo na wao wana matatizo yao, Kenya wametangaza na wenyewe wana uhaba wa walimu, Uganda wana walimu wachache lakini kuja kwao si kwa wingi kame vile ambavyo tulitarajia. Vifungu hivi chini ya Mkataba wa Afrika Mashariki, tumevifungua na walimu kwa upande huo wanakubaliwa kuja nchi, *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Japo nilikuwa na hoja tatu, mbili zimeshafilisiwa sasa naomba nizungumzie moja kuhusu elimu ya awali katika shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aweze kunipa maelezo ya kutosheleza kwamba sera mpya ya elimu sasa hivi inataka shule za msingi wawe na darasa la awali, lakini ukiangalia katika mazingira ya kawaida shule zilizopo sasa hivi ni za *private* ambazo zina-*charge* fedha nyingi. Mfano, pale Babati kuna Debora na *Lift Valley* ambao wana-*charge* shilingi 800,000/= ambazo wananchi wengi hawamudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atwambie ni lini hayo madarasa ya shule za awali yataanza katika shule za msingi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul linalohusu shule za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya Serikali za Mitaa na mpango mzima wa elimu ikiwemo Wizara ya Elimu, tumeamua kila palipo na shule ya msingi kuwe na darasa maalumu la elimu ya awali. Kwa hiyo, kila Mtanzania ana nafasi ya kumpeleka mtoto wake kwenye shule yoyote ile ya msingi ambako kuna darasa la awali. Hizo shule za *private* ambazo umezizungumza ni mahitaji ya mtu mwenyewe kama anaamua kwenda kwenye shule hizo, ingawa siwezi kujibu hapa sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshatoa ufafanuzi sana juu ya ada mbalimbali na mkakati wa Serikali wa kudhibiti malipo haya yanayotozwa na watu wa shule za binafsi nyingi. Lakini mwananchi yeyote wa kawaida mahali alipo tayari madarasa ya elimu ya awali yako katika kila shule ya msingi nchini Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nawasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani kama Msemaji Mkuu, nilihoji ni vyuo vingapi vinavyofundisha walimu wanaokwenda kufundisha shule za awali, kwa sababu walimu wote tunafahamu kwamba mwanafunzi wa shule ya awali anatakiwa afundishwe na mwalimu ambaye amesomea kozi maalum kwa ajili ya watoto hawa na walimu wote tunafuata mwongozo wa mwanasaiokolojia mashuhuri Maria Montessori kwa sababu yeye…

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Christowaja inatosha, huyo mwanasaikolojia tumempata, ni shule ngapi zinafundisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyuo.

**MWENYEKITI:** Haya nitaomba Mheshimiwa Waziri ujibu hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu vyuo vinavyofundisha elimu ya awali ni kwamba sasa hivi Vyuo vyetu vya Ualimu *Grade A,* maana yake *syllabus* imewekwa

kwamba pamoja na masomo haya ya kufundisha darasa la kwanza hadi darasa la saba na *form one* mpaka *form four*, lakini hata mtaala wa elimu ya awali umeingizwa ili mwalimu yeyote aweze kuwa na ufahamu wa kufundisha masomo ya awali. *(Makofi)*

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi swali langu naomba nijikite kwenye suala la upungufu wa Bajeti ya mwaka huu kwenye miradi ya maendeleo, kwani kwenye randama hawakuonesha miradi halisi ambayo ni ya maabara, hosteli na madarasa, bali wameonesha habari ya elimu na kufuatilia na kuendesha shughuli za sayansi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri, ana tamko gani kuhusu miradi ya maendeleo ndani ya nchi hii kwa sababu tuna upungufu mkubwa wa maabara, hosteli, madarasa na madawati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la maabara, mabweni kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la awali lipo kwenye mipango yetu ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES). Hiyo ni ile nyongeza ambayo itaingia kwenye Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) ili kuweza kuboresha zaidi huduma hii ya ujenzi wa madarasa, mabweni na maabara kwenye shule zetu za sekondari. Kwa hiyo, tutakapoanza kutekeleza tutatoa migao kwenye Halmashauri za Wilaya ili ziweze kujenga na ndipo ambapo sasa tunaweza tukawa tumeweza kuona mafanikio yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa hiyo zipo kule kwenye TAMISEMI.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utaratibu wa kuchapa watoto viboko mashuleni unaaibisha, unadhalilisha Taifa letu mbele ya Mataifa mengine, na kwa kuwa haki ya mtoto ni haki ya binadamu vilevile. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu aibu hii maana tunafanya vitendo ambavyo vinapigwa vita na dunia nzima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, viboko mnafanya navyo nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leticia Nyerere ameomba kujua adhabu hii.

**MWENYEKITI:** Wewe jibu tu viboko mnafanya navyo nini? *Don't repeat the question.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Sawa, ipo sheria ya mwanafunzi kwa mwalimu yeyote yule anapotaka kutoa adhabu ya viboko sharti aombe kibali kwa Mwalimu Mkuu.

Kwa hiyo, viboko haviko holela shuleni na kwa hiyo adhabu hiyo ni mara chache sana kutokea kwa sababu ipo sheria inayomzuia mwalimu kumchapa mwanafunzi mpaka apate kibali kwa Mwalimu Mkuu na Mwalimu Mkuu ataona umuhimu wa adhabu hiyo kama inastahili kumpiga mtoto huyo yaani kutolewa kwa mtoto huyo. Kama jambo hilo ni lazima, basi mwisho ni viboko vine, hiyo kama ni lazima. *(Makofi)*

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuwa na dhamira…

**MWENYEKITI**: Achana nayo, acha pongezi sema unachotaka kusema. *(Makofi)*

**MHE. REGIA E. MTEMA*:*** *Okay*. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Bajeti ya mwaka jana Serikali ilitenga shilingi 986,400,000/= kwa ajili ya vifaa maalum kwa watu wenye ulemavu. Lakini vilevile kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha fedha hizi ni kwamba zilinunua vifaa kwenye shule za msingi 317, shule za sekondari 30 tu pamoja na vyuo vya ualimu saba. Lakini kwenye Bajeti ya mwaka huu ni shilingi 800,000,000/= pekee ndio zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa maalum kwa watu wenye ulemavu.

Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ninahitaji kupata *commitment* ya Serikali kwamba iandae *special fund raising* kwa ajili ya kusaidia fungu hili ili kuwasaidia watu wenye ulemavu wapate vifaa. *(Makofi)*
*(Hapa kengele ililia)*

**MWENYEKITI:** Kengele imegongwa shilingi 800,000,000/= zitatumikaje?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Regia Mtema kuwa ni kweli kufuatana na ufinyu wa Bajeti tulilazimika kutenga pesa chache zaidi. Lakini tutazitumia kwa ajili ya kununua vifaa kama tulivyofanya mwaka jana. Lakini tutaongeza juhudi kuhamasisha wadau mbalimbali, wahisani pamoja na wananchi kwa ujumla ili kuona jambo hili ni la kwetu wote ili tuweze kulichangia na wananchi walemavu waweze kupata elimu bora. Mashirika kadhaa wamejitahidi wamefanya kazi hiyo, *TIGO, NMB* na kadhalika nawashukuru sana na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawahamasisha. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilihoji juu ya Waraka wa Serikali wa mwaka 2009 unaowataka walimu wanaomaliza Shahada ya Kwanza kuanza na ngazi ya mshahara ya *TGTS D.* Waraka ambao unawalazimisha walimu wanaoenda kujiendeleza hata kama walivuka daraja hilo wakimaliza Shahada ya Kwanza warudishwe chini. Naomba Waziri anipe majibu juu ya waraka ambao unawavunja moyo walimu kujiendeleza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la waraka ule ni suala tu la kuwapanga walimu katika muundo. Ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na Bunge

lako Tukufu kwamba kwanza hatupunguzi mshahara wa mwalimu yule. Tunachofanya kwa sababu kabla hajaenda kuchukua hiyo shahada yake alikuwa labda ni mwalimu au Afisa Elimu Msaidizi. Si ajabu alikuwa Mwalimu Mwandamizi au Afisa Elimu Msaidizi Mwandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anavyokuja hawezi tena akawa Afisa Elimu Mwandamizi kwa sababu hakuwa afisa wakati anakwenda kusoma. Kwa hiyo, anavyokuja tunamwanzisha sasa kwenye muundo wa maafisa kwa maana daraja D, lakini mshahara wake unabaki vilevile. Hiyo yote ni kuhakikisha kwamba walioenda Chuo Kikuu kabla yake hawazidi kwa sababu si ajabu alimaliza miaka minne kabla yake lakini bado ni Maafisa Elimu Daraja la Pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunafanya hivyo si kwa walimu ni kwa kada zote na lengo ni kuhakikisha tunawapanga kwa kadri ya umri wao, *seniority list. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Aah!!! Muda hautoshi naendelea na *guillotine time* hakuna hoja wala Mwongozo wala chochote. Katibu endelea.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*…………………Shs. 679,952,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*…………………..Shs. 2,613,324,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……………………..Shs. 244,262,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*…..Shs. 374,472,000
Kifungu 1006 - *Information, Edu. & Comm.*…………Shs. 215,035,000
Kifungu 1007 - *Legal Unit*..........................................Shs. 31,336,040,186
Kifungu 2001 - *Commissioner for Education*……..Shs. 8,496,312,000
Kifungu 2002 – *Inspectorate*………………………Shs. 17,705,663,656
Kifungu 3001 - *Basic Education*……………………….Shs. 1,355,204,000
Kifungu 3002 - *Adult Education & Non Formal Edu.*…..Shs. 816,628,000
Kifungu 4001 - *Secondary Education*……………….Shs. 1,119,925,000
Kifungu 5001 - *Teacher Education*…………………..Shs. 34,722,873,000
Kifungu 7001 - *Higher Education*………………….Shs. 418,917,062,758
Kifungu 7002 - *Tech. & Vocational Training Div.*.…Shs. 9,309,057,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

## FUNGU 46 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Kifungu 1001 - *Administration and General*…………Shs. 200,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*…………………..Shs. 4,193,692,000

Kifungu 2001 - *Commissioner for Education*…………Shs. 975,299,000
Kifungu 2002 **–** *Inspectorate*…………............……….Shs. 100,000,000
Kifungu 3001 - *Basic Education*……………...………Shs. 1,304,400,000
Kifungu 4001 - *Secondary Education*……….....……..Shs. 533,368,000
Kifungu 5001 - *Teacher Education*……………..……..Shs. 635,340,000
Kifungu 7001 - *Higher Education*…………………….Shs. 29,117,801,000
Kifungu 7002 - *Tech. & Vocational Training Div.*......Shs. 4,173,974,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mlichokosea sasa ni wakati siwa inawekwa ninyi wote mlikuwa mnaongea. Huo sio utaratibu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika, naomba Mwongozo wa Spika kuhusiana na namna ambavyo uamuzi wa kupitisha hoja hii umefikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo ninaoumba unahusu Kanuni ya 103(2); “Vilevile Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote cha fungu hilo.”

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupitisha hoja vifungu kwa vifungu unaruhusu Wabunge kuondoa shilingi na mimi nilisimama kutaka kuondoa shilingi, lakini Mheshimiwa Spika umenizuia. Sasa Mwongozo ninaouomba ni kama huu uamuzi wa

kupitisha mafungu yote haya bila kuruhusu Wabunge kuondoa shilingi kuonyesha kutokubaliana na hoja, napend kujua kama umefutwa na umefutwa kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu soma vizuri. Kifungu 104 kinasema hivi; "Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kumaliza muda ulioongezwa chini ya fasili 104(1) ya Kanuni hii, Kamati bado haijamaliza kufikia mafungu yote yanayohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote yanayoendelea na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo." Ndiyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tundu Lissu Kanuni ya *guillotine* ikibakia dakika kumi tu yote yanapitishwa hivyo hivyo. Hatuupendi huu utaratibu, lakini wingi wetu unatubidi tufikie hapo, huwezi kutoa shilingi kwenye *guillotine. There is no way you can do that. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sisi hatuna matangazo mengine, ningependa kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.13 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 21 Julai, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*